Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Arobaini - Tarehe 4 Agosti, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza, kuna watu wengi kutoka nchi za nje wanaopenda kutembelea Bunge letu kuona jinsi demokrasia ya Kibunge inavyofanya kazi. Kwa hiyo, leo napenda kumtambulisha mgeni ambaye ni *Political Analyist* katika *United States Department of State. I wish to recogonize the presence of the Political Analysit from the United States, Department of State. (Makofi)*

Kikao cha arobaini cha Mkutano wa Bajeti, kinaanza. Katibu, *agenda* inayofuata.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hazi zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* kwa mwaka 2001/2002 *(The Annual Report and Accounts of the Business Registration and Licensing Agency (BRELA) for the Year 2001/2002).*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji) kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji) na Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 375

### Ujenzi wa Vituo vya Afya

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa vituo vya afya?

(b) Kwa kuwa, Wilaya ya Kyela ina wakazi karibu 180,000 lakini ina kituo kimoja tu cha afya kilichoko kwenye Mji Mdogo wa Ipinda; na kwa kuwa Wananchi wa Kyela kwa kipindi kirefu wamekuwa wakiiomba Serikali yao iwapatie kituo cha afya cha pili katika Tarafa ya Unyakyusa; je, Serikali itakuwa tayari sasa kuigeuza Zahanati ya Kilasilo iliyopo kwenye kata ya Ikolo ili iwe kituo cha afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali hivi sasa ni kuimarisha na kuboresha kiwango cha huduma kinachotolewa kwa Wananchi na Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo nchini. Hatua hii inachukuliwa kwa kukarabati majengo yaliyopo, kununua vifaa mbalimbali na kuongeza watumishi kadri wanavyopatikana. Hata hivyo, endapo uongozi wa Halmashauri unaona kwamba kuna haja ya kuongeza Vituo vya Afya, basi maamuzi haya yafanywe na Halmashauri husika kwa kuwashirikisha Wananchi na wadau wengine hata Wizara ya Afya. Serikali itaunga mkono jitihada hizi kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia ya kuongeza vituo vya afya ili uwiano unaokubalika kulingana na Sera ya Afya ufikiwe. Ili kutekeleza azma hii, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela inao mpango wa kujenga Kituo cha Afya katika Kijiji cha Njisi mpakani mwa Tanzania na Malawi katika Tarafa ya Unyakyusa. Mpango huu ni wa muda mrefu uliobuniwa tangu mwaka 2002 na haujaanza kutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha. Endapo Mheshimiwa Mbunge, anaona kuwa ni muhimu kuibadili

Zahanati ya Kilasilo iliyopo katika Kata ya Ikolo ili iwe Kituo cha Afya, badala ya mpango wa kujenga kituo cha Afya katika Kijiji cha Njisi, basi ninamshauri alipeleke wazo hili katika Kikao cha Baraza la Madiwani ambapo yeye ni Mjumbe vilevile ili waweze kujadiliana na kukubaliana kuhusu kuchukua hatua zinazostahili kuchukuliwa.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri sana. Ningependa kumweleweshа kwamba, Njisi na Kilaseno ni kijiji hicho hicho. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwamba, Njisi itabadilishwa kuwa Kituo cha Afya. Je, hatua hizo za kukibadilisha hicho kituo itaanza lini kwa sababu hivi sasa kituo cha Njisi kiko katika Mji Mdogo wa Kasubulu ambao unakua sana na Wananchi wanapata tabu sana kwenda Kyela Mjini, kitaanza lini kujengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni lini hasa utaratibu wa kubadili zahanati hiyo kuwa Kituo cha Afya unaweza ukaanza, mimi naomba tu nimwombe yeye ashauriane na Halmashauri yake, uamuzi ufanywe, muanze. Kwa sababu kinachohitajika kwa kweli kama ni matofali ya kuchoma, muanze kutengeneza. Juhudi za Wananchi zionekane zimeanza kabla ya Serikali haijafikia uamuzi wa kuweza kuwasaidia. Sisi tutakuwa tayari kushirikiana na Halmashauri yako.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza kwamba, Wilaya kama Kyela ingestahili kuwa na Vituo vya Afya siyo chini ya sita na Wilaya kama hizo ni nyingi na kinachotokea ni kwamba, madhehebu na mashirika ya dini yamekuwa yakitoa huduma zaidi ya asilimia 60 katika ngazi ya vituo vya Afya. Serikali itakubali kuitengea fedha madhehebu haya ambayo hutoa huduma ya afya kwa asilimia 60 katika ngazi ya Vituo vya Afya na *Dispensary?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli na Serikali imekuwa ikikiri kwamba, kwa sasa bado hatujafikia uwiano unaotakiwa katika utoaji wa huduma za afya. Maeneo mengi ambayo yanastahili kuwa na Vituo Afya bado hatuna vituo vya afya lakini tatizo kubwa limekuwa kama ambavyo nimekuwa nikisema ni uwezo mdogo wa fedha. Lakini juhudi zipo na zinaendelea.

Kuhusu uwezekano wa kusaidia hivi vituo vya afya vinavyoendeshwa na madhehebu ya dini. Jambo hili tumekuwa tunalieleza mara kwa mara kwamba, kwa utaratibu ulivyo hivi sasa, msaada unatolewa katika ngazi za hospitali ambazo ni teule kwa sasa. Lakini jambo hili linafikiriwa na Serikali ili tuweze kuona namna gani tunaweza vilevile tukashirikisha hadi ngazi ya Kata kutegemea na uwezo kama utapatikana.

Na. 376

**Sheria iliyoanzisha Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam**

**MHE. HADIJA K. KUSAGA (k.n.y. MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swali langu la nyongeza tarehe 31 Januari, 2002 Bungeni iliahidi kuchunguza na kuangalia upya sheria iliyoidhinisha kuanzishwa kwa Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri za Manispaa Tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni, ili kuondoa kasoro zilizojitokeza za kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo Jijini Dar es Salaam:-

(a) Je, Serikali baada ya utafiti wao imeona kasoro, migongano na migogoro gani ya usimamizi na uratibu kutokana na kuwepo kwa Halmashauri ya Jiji na zile Manispaa tatu?

(b) Je, ni hatua gani za kisheria zitakazochukuliwa na Serikali za kurekebisha hali hiyo kama ipo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kujibu swali Na. 16 la Mheshimiwa Margreth Bwana, Mbunge wa Viti Maluum, tarehe 31 Januari, 2002, nilijibu pia swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mbunge wa Ukonga, ambaye alihoji kuhusu masuala mawili yafuatayo:-

Kwanza, Mheshimiwa Mbunge aliona kuwa ufanisi wa Halmashauri nne za Mkoa wa Dar es Salam bado unaathiriwa kidogo na matatizo yanayotokana na Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji Na. 8 ya mwaka 1982 inayotoa *autonomy* kwa Halmashauri zote nne.

Pili, Mheshimiwa Mbunge aliona kwamba, kutoonekana vizuri kwa *role* ya *co-ordination* ya Halmashauri ya Jiji, kunaleta kidogo matatizo katika utendaji kazi wa Halmashauri hizi. Aliitaka Serikali ichukue hatua za kuiweka Sheria hiyo vizuri ili *co-ordination role* ya Halmashauri ya Jiji kwenye Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke, iwe wazi na isilete migongano.

Mheshimiwa Spika, niliahidi kuendelea kutathmini kuhusu rai zake mbili na kushauri ipasavyo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi yangu iliunda timu iliyojumuisha Wanasheria kutoka Ofisi yangu na Wanasheria wa Manispaa za Ilala,

Kinondoni na Temeke na baada ya uchunguzi wa kina, Serikali haikuona kasoro, migogoro wala migongano ya usimamizi na uratibu wa shughuli za maendeleo baina ya Jiji na Manispaa zake tatu inayotokana na Sheria Na. 8 ya mwaka 1982. Majukumu ya Halmashauri za Manispaa yameainishwa vizuri chini ya Kifungu cha 54 na yale ya Halmashauri ya Jiji yameelezwa katika kifungu cha 69 (a) cha Sheria hiyo na vifungu hivi havina migongano iliyo wazi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika sehemu (a) hapo juu kwamba, hakuna kasoro zilizobainishwa, hivyo, kwa sasa hakuna hatua zitakazochukuliwa kuhusiana na muundo na majukumu ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke.

Hata hivyo, iwapo Mheshimiwa Mbunge, anaona kwamba ipo migongano anayoiona yeye katika utendaji wa Halmashauri hizi inayosababishwa na Sheria Na. 8 ya 1982, basi Ofisi yangu ipo tayari kabisa kupokea maoni yake au ushauri wake na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuboresha utendaji wa Halmashauri hizi kwani lengo letu wote ni kutoa huduma bora kwa Wananchi.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sifa za kuwa Halmashauri za Jiji katika Manispaa hizi tatu zimefikiwa. Sifa mojawapo ikiwa ni ongezeko la watu na Wilaya ya Kinondoni na Temeke zinaongoza kwa kuwa na ongezeko la watu na kuwa na vitendea kazi vinavyostahili kufanya ziwe Majiji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni sasa ni muda muafaka wa kuweza kufanya hivyo ili Wananchi waweze kunufaika na Jiji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa vigezo vile vya msingi vinaweza kuwa vimefikiwa siyo katika Manispaa ya Temeke tu, lakini hata Kinondoni, hata Ilala lakini ninachotaka kusema tu ni kwamba, utaratibu ulivyo sasa ni huu ambao tunao ambapo kunakuwa na Jiji moja linalo-*co-ordinate* shughuli fulani fulani katika Manispaa tatu. Haiyumkiniki kwamba, tunaweza tukawa na majiji matatu ndani ya Mkoa ule wa Dar es Salaam na mkategemea kwamba, tutaweza ku-*function* vizuri na kidogo itakuwa ni *situation* ambayo ni *unique* lakini tuko tayari kujaribu kulitazama katika *angle* tofauti na siyo ya kuifanya kuwa miji mitatu au kama anavyoshauri miji miwili.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda tu kuuliza kwamba, kwa kuwa Jiji la Mwanza limeshakuwa Jiji na lina hadhi ya Jiji. Je, Serikali ina mpango gani wa kulifanya Jiji la Mwanza likawa na Halmashauri ya Nyamagana na Ilemela, sambamba kama ilivyo Temeke, Ilala na Kinondoni?

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya, liletwe katika taratibu za kawaida. *(Kicheko)*

Na. 377

**Miradi iliyowekezwa kwenye *EPZ***

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

(a) Je, tangu sheria ya uanzishwaji wa *(EPZ)* ipitishwe, ni miradi mingapi imewekezwa ndani yake na imeombewa kibali na nani kutoka wapi na kwa ajili ya kuzalisha nini?

(b) Je, kati ya miradi hiyo, ni mingapi imepitishwa kwa ajili ya utekelezaji na itatekelezwa lini na wapi na ni ya thamani gani *(Investment Value)?*

(c) Je, kwa wastani huchukua muda gani tangu maombi yanapoletwa na kibali kutolewa hadi utekelezaji kuanza?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Sheria ya *EPZ* iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Aprili, 2002, ili ianze kutumika kuanzia mwezi Julai, 2002. Hata hivyo, utekelezaji wake ulianza rasmi mwezi Aprili, 2003, baada ya kukamilisha kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa forodha katika maeneo ya *EPZ.*

Baada ya maelezo haya, sasa napenda nijibu swali la Mheshimiwa Mbise kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya *EPZ* inatambua matabaka matatu ya wawekezaji: Wajenzi na miundombinu *(Developers),* Wazalishaji *(Operators)* na Watoa huduma za msingi *(Service Providers).* Tangu Sheria ya *EPZ* ipitishwe ni miradi mitano imewekezwa ndani ya *EPZ.* Miradi hiyo ni *NIDA Textile Mill,* iliyopo Tabata. *Millennium Business Park,* iliyoko Ubungo, *Star Apparels* ambayo pia iko Ubungo na *Reclaimed Appliances* nayo iko Ubungo na *African Pride Textile Mill* nayo iko Ubungo. Mradi wa *NIDA Textile Mill* umeombewa kibali na wamiliki wanaotoka Pakistani na Omani na ni mradi kwa ajili ya kutengeneza shuka na foronya. Hadi sasa kimeshauza nje bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani 5.8 milioni.

Mradi wa *Millennium Business Park* umeombewa kibali na wamiliki wanaotoka Uingereza na Tanzania na ni mradi uliojenga miundombinu ya *EPZ* na wanawakodishia wazalishaji.

Mradi wa *African Pride Textile Mill* nao unatoka Sri-Lanka, huu bado haujakamilika. Lakini utatengeneza nguo *(garments)* na vilevile shuka.

Mradi wa tano ni ule wa *Reclaimed Appliances,* umeombewa kibali na raia wa Uingereza na unazalisha bidhaa za umeme *(Electric Appliances)*.

Mpaka sasa hakuna kampuni au mtu binafsi anayetaka kutoa huduma aliyesajiliwa, kwa sababu hatujapokea maombi ya aina hii.

(b) Miradi yote iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Baraza la *EPZ* baada ya kushauriwa hivyo na Wakala wa Serikali wanaosimamia *EPZ* ambaye ni *NDC.* Utekelezaji wake unaendelea vizuri. Jumla ya thamani ya uwekezaji katika miradi yote hii ni dola za Kimarekani 19.86 milioni.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa *EPZ,* muda wa maombi hadi kujibiwa kutolewa leseni ni siku zisizozidi 14. Hata hivyo, imebainika kwamba, kwa maombi ambayo yanakuwa yamekidhi masharti ya *EPZ* bila kutakiwa kufanya marekebisho, utoaji wa leseni unaweza kuchukua wastani wa siku tatu.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Kuna mpango wowote wa *EPZ* kwa ajili ya madini yetu ya Mererani, madini ya *Tanzanite?*

**SPIKA:** Swali zuri fupi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo kuna mpango wa *EPZ* kwa ajili ya Mererani. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu ya Waziri inavyoonekana miradi yote hii imeanzishwa katika sehemu ya Dar es Salaam. Je, anaweza akalithibitishia Bunge mikoa mingine ambayo imeteuliwa kuwepo katika *EPZ* na ambayo kwa hakika hata *infrastructures* ni shida kama Kigoma itapata lini wawekezaji?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali ina mpango wa kuwezesha ujenzi wa *EPZ* katika maeneo mengine ikiwemo Kigoma, Tanga, Mtwara, Kibaha na Arusha. *(Kicheko)*

Na. 378

**Upatikanaji wa Malighafi kwa Kiwanda Kipya**

**MHE. NJELU E.M. KASAKA (k.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa miongoni mwa mambo yanayozingatiwa sana katika uzalishaji wa kiwanda kipya ni pamoja na upatikanaji wa malighafi kwa kuzingatia umbali na gharama za usafirishaji. Je, kiwanda cha nguo cha Mbeya ambacho malighafi yake ni pamba inatoka wapi hadi sasa?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Benson Mpesya kwamba, upatikanaji wa malighafi kwa wingi na kwa urahisi ni moja ya sababu zinazochangia uamuzi wa kujenga kiwanda katika sehemu husika. Sababu zingine ni upatikanaji wa nishati, miundombinu na sera ya nchi kuhusiana na ujenzi wa viwanda kwa wakati huo.

Kiwanda cha nguo cha Mbeya kilijengwa Mbeya kikikusudiwa kutumia pamba iliyokuwa inalimwa Chunya katika Mkoa wa Mbeya. Kutokana na ushauri wa wataalam wa kilimo, zao la pamba katika miaka ya hivi karibuni limezuiliwa kulimwa Mbeya. Kiwanda kinanunua pamba kutoka mikoa mingine inayolima pamba.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha nguo cha *New Mbeya Textile Mill Limited* kwa miaka minne iliyopita kimenunua pamba kwa ajili ya utengenezaji nguo kutoka sehemu mbalimbali na vilevile Zimbabwe kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 1999 kiwanda kilinunua pamba marobota 726 kutoka Mwanza, marobota 355 kutoka Chunya, marobota 331 na marobota 40 kutoka Iringa.

(ii) Mwaka 2000 kiwanda kilinunua jumla ya marobota 1,742. Kati ya marobota hayo, marobota 708 ni kutoka Mwanza na marobota 1,034 ni kutoka Shinyanga.

(iii) Mwaka 2001 kiwanda kilinunua pamba marobota 4,142 ambapo marobota 3,377 yalinunuliwa kutoka Mwanza na marobota 770 yalinunuliwa kutoka *Ubungo Spinning Mill Limited.* Pamba iliyonunuliwa kutoka *Ubungo Spinning* ilitokana na *stock* iliyokuwepo baada ya kiwanda hicho kusimamisha uzalishaji.

(iv) Mwaka 2002 kiwanda kilinunua marobota 2,524 ambapo marobota 2,475 yalinunuliwa kutoka Mwanza na marobota 49 kutoka *Ubungo Spinning Mill Limited.*

(v) Katika mwaka 2003 kiwanda kilinunua pamba toka Mwanza marobota 2,629, *Ubungo Spinning Mill* marobota 176 na Zimbabwe marobota 234.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004, kiwanda kinatarajiwa kununua pamba toka Mwanza na Shinyanga ambako ndiko kwa sasa pamba nyingi inalimwa na kupatikana.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa lengo la swali hili kwa kweli ilikuwa ni kutaka kupata kauli ya Serikali lini pamba itaruhusiwa kulimwa Wilaya ya Chunya na Mkoa wa Mbeya kwa ujumla, kwa mazingira yaliyoko sasa inaonyesha kwamba pamba ile italimwa bila athari kubwa yoyote kwa uchumi wa nchi?

(ii) Kwa kuwa mwekezaji alifanya maamuzi kwa kuzingatia sera za Serikali zilizokuwepo wakati ule na alijua kwamba pamba ataipata Chunya ambapo ni karibu; na kwa kuwa sasa anapata pamba kutoka Mwanza, Shinyanga na sehemu nyingine za mbali; je, Serikali itampa manufaa gani kufidia gharama zake ambazo sasa anatarajia kupata pamba kutoka mbali zaidi kuliko alivyokusudia hapo mwanzoni?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyotoa maelezo katika jibu la msingi kwamba, upatikanaji wa malighafi ndiyo moja ya sababu ya kuamua kiwanda kijengwe mahali hapo. Hili jambo limetokea nje ya shughuli za viwanda. Kwa hiyo, kitu tunachofanya sasa ni nini? Kwanza, tunawahimiza watu wa Morogoro. Watu wa Morogoro wanalima pamba safi sana, ambayo ni *long step,* lakini katika miaka ya karibuni kutokana na ununuzi wa ovyo na hasa Ulanga pia. Kwa hiyo, tunafanya kampeni ya kufufua zao la pamba na mwaka huu hali ni nzuri katika Wilaya ya Ulanga na Kilombero. Mimi nina matumaini ya kwamba, baada ya muda si mrefu, pamba inayotakiwa kwa ajili ya kiwanda cha *Mbeya Textile Mill* itatoka Ulanga na Kilombero. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa majibu yake mazuri yanayotuhakikishia kwamba, tutapata pamba kutoka Ulanga na pia niwapongeze na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, kwa jitihada wanazofanya ili kuhakikisha zao hili linalimwa katika Mkoa wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Jumapili tulifanya kikao na Waheshimiwa Wabunge, wanaotoka maeneo yote yanayolima pamba nchini na tulifikia makubaliano kwamba, kwa sasa itakuwa ni hatari sana kuruhusu kilimo cha pamba kwenye eneo la Chunya kwa sababu ya mdudu anayeitwa *Red Boll,* anayekula vitumba vya pamba na wakaagiza kwamba, Wizara ama Serikali ifanye utafiti kuona nini kifanyike mapema iwezekanavyo ili pamba iweze kulimwa katika eneo hilo.

Kwa hiyo, naomba tusubiri Serikali ifanye huo utafiti ndipo tutakaporudia kulima. Hata hivyo, ni kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika Mkoa wa Morogoro, kilimo cha pamba kinakua kwa kasi kubwa sana na kwa hiyo, kiwanda cha *Mbeya Textiles* tunaomba kichukue pamba kutoka Morogoro na kwingineko nchini.

Na. 379

**Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma**

**MHE. HADIJA K. KUSAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika kujibu swali Na. 47 la Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mbunge wa Ukonga, kuhusu marekebisho ya Sheria ya *PPF* Na. 25/2001 iligundua kwamba, Sheria hiyo baada ya kutungwa imeonekana haiwatendei haki baadhi ya wafanyakazi na waliostaafu kabla ya kufikia umri uliopendekezwa na Sheria hiyo; na kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali langu la nyongeza juu ya swali hilo la msingi iliahidi kulitafakari na kulifanyia kazi suala hilo:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika tafakari yake na kulifanyia kazi suala hilo?

(b) Kama Serikali itakuwa tayari imeshalifanyia kazi na ikiwa imekubaliana na hoja iliyotolewa ya kuileta Sheria hiyo Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho, je, ni lini sasa sheria hiyo italetwa Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hadija Kasola Kusaga, Mbunge wa Temeke, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu sehemu ya maelezo ya awali ya swali hilo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuweka kumbukumbu sahihi, wakati ninajibu swali Na. 47 la Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mbunge wa Ukonga, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu, kuhusu marekebisho ya Sheria ya *PPF* Na. 25/2001, sikusema kuwa Serikali imegundua kwamba, Sheria hiyo baada ya kutungwa imeonekana haiwatendei haki baadhi ya wafanyakazi na waliostaafu kabla ya kufikia umri uliopendekezwa ndani ya sheria hiyo. Hata hivyo, wakati ninajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mbunge wa Temeke, niliahidi kwamba, tutalitafakari na kulifanyia kazi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hadija Kusaga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari na kulifanyia kazi suala hili, Serikali imeona kwamba, marekebisho ya Sheria Na. 25 ya mwaka 2001, yalizingatia kanuni na taratibu za mafao ya uzeeni (pensheni) hapa nchini na duniani kote. Aidha, ibara ya 11(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatamka kwamba na nanukuu: "Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu".

Kwa sababu hiyo, Serikali haikusudii kuleta hapa Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 26(2) cha Sheria hiyo.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, niipongeze sana Serikali mara baada ya swali hili waliweza kukaa na kutafakari na kulifanyia kazi, kwa hiyo,

nawapongeza sana. Swali la nyongeza sasa, tatizo lipo pamoja na Serikali kukaa, naomba iendelee kukaa tena ili tuweze kulifanyia kazi. Je, wapo tayari kuendelea kukaa kwa sababu tatizo bado lipo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Serikali haiko tayari kuendelea kukaa juu ya jambo ambalo jibu lipo. Serikali itaendelea kukaa kufikiria mambo mapya, kwa mfano, namna ya kuboresha Mifuko ya Akiba ili kusudi iweze kuwaletea manufaa zaidi wanachama. Suala kubwa ni namna ya kufanya Mifuko hii kuwafaa zaidi wanachama na kama tukiingia kwenye utaratibu, bila hata Katiba, wa kusema kila anayeondoka bila kujali umri, achukue chake, Mifuko hii itafilisika na hakuna hata mmoja atakayekuwa na manufaa yoyote, wakati tunatakiwa Mifuko hii tuitunze kwa ajili ya wazee sio vijana au watu ambao kwa sababu moja au nyingine, imebidi waache kazi kabla ya kuzeeka. *(Makofi)*

Na. 380

**Soko kwa Ajili ya Korosho Ghafi**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la bei ndogo ya korosho ghafi linasababishwa na kuwepo kwa mnunuzi mmoja tu (India) na hivyo kulifanya zao hilo kukosa ushindani kabisa na kwa kuwa mwaka 2000/2001 viongozi kadhaa wa Wizara ya Ushirika na Masoko na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara wa wakati huo, Mheshimiwa Nsa Kaisi, waliwahi kufanya ziara kwenye nchi kadhaa kutafuta soko la ziada kwa zao hilo. Je, ni yapi matokeo ya ziara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la bei ndogo ya korosho ghafi lilitokana na kutegemea soko moja tu la India kama mnunuzi wa korosho zetu ghafi katika miaka ya hivi karibuni, ambapo viwanda vyetu vya kubangua korosho vilikuwa vimeacha kufanya kazi. Katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, mwaka 2000/2001, viongozi kadhaa wa Bodi ya Korosho na Serikali wakiwemo wa Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Kilimo na Chakula, pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Nsa Kaisi, walifanya ziara kwenye nchi kadhaa zikiwemo Vietnam na Singapore, kutafuta masoko ya ziada ya zao la korosho kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara hizo, Serikali za Tanzania na Vietnam, zilitiliana saini makubaliano *(Memorandum of Understanding)* ya kuendeleza biashara ya zao la korosho kati ya nchi mbili hizo. Kutokana na makubaliano hayo, wawekezaji kutoka Vietnam walikuja Tanzania mwezi Machi na mwezi Novemba, 2002 ili kutathmini uwezekano wa kuwekeza katika viwanda vya sekta ya korosho hasa katika

kuanzisha mashamba makubwa ya korosho na kuwekeza katika ubanguaji. Katika mwezi Novemba, 2002, wawakilishi wa kampuni ya *Vietnam National Agricultural Produce and Foodstuffs Import and Export Corporation (VINAFIMEX),* kutoka Vietnam, walikuja Tanzania na kupata fursa ya kufanya mazungumzo zaidi na Serikali ya Tanzania. Aidha, wawakilishi wa Kampuni hiyo walitembelea viwanda vya kubangua korosho vya Kibaha, Mbagala, Masasi, Tunduru na Lindi, kwa lengo la kuangalia na kubaini viwanda ambavyo wangeweza kuwekeza. Vilevile wanunuzi maarufu wa korosho na kahawa za Tanzania kutoka Singapore, wajulikanao kwa jina la *Olam Tanzania Limited,* walifanya uamuzi wa kuwekeza katika viwanda vinne vya kubangua korosho Tanzania na tayari kiwanda kimoja kati ya hivyo kimekwisha jengwa na kinafanya kazi. Kiwanda hicho kilichopo Mjini Mtwara, kinajulikana kwa jina la *Olam Tanzania Limited* na kina uwezo wa kubangua tani 4,800 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakubaliana nami kuwa, uamuzi wa kuwekeza unatakiwa kufanywa kwa makini na mara nyingine huchukuwa muda mrefu kukamilika. Hivyo, ni matarajio yangu kuwa, jitihada zetu za kuvutia wawekezaji katika sekta ya korosho zitafanikiwa ili kuondoa utegemezi wa kuuza korosho ghafi kwa kuwa korosho zilizobanguliwa zina soko la uhakika zaidi.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ila nina maswali mawili tu ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa suala la bei ya korosho kuwa chini ni kero kwetu na kwa kuwa upo utaratibu wa Bodi ya Korosho kutoa mwelekeo wa bei kwa mfano Sh. 700/= kwa kilo na wanunuzi hununua kwa Sh. 150/= mpaka Sh. 200/= na Serikali inaona. Je, Serikali ipo tayari kutoa tamko hapa kwamba, bei inayotamkwa na Bodi ya Korosho hainunuliwi chini ya hapo?

(ii) Kwa kuwa bei ya korosho inakuwa chini kulingana na gharama kubwa za uzalishaji kwa mfano mwaka huu *sulphur* tumenunua Sh. 20,000/= badala ya Sh. 9,000/=. Je, Serikali ipo tayari kutuwekea kiwanda cha *sulphur* Mtwara ama kutuongezea *agents* wa kuleta *sulphur* ili gharama za uzalishaji ziwe chini kulingana na bei? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, suala la bei ya dira kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, bei ya dira kama inavyojieleza ni ya mwelekeo tu si bei ambayo inaweza ikachukuliwa kwamba ndio bei halisi kwa sababu inawekwa ili kuweza kuweka mwelekeo ambao unaweza kukabiliana na hii. Kwa hiyo, itakuwa si busara wala si sahihi kwa Serikali kutamka kwamba, bei ya dira ikishawekwa basi itumike hiyo hiyo kwa sababu hiyo ni ya mwelekeo tu na inawezekana ikapanda au ikateremka.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusiana na kuweka kiwanda cha *sulphur* kule Mtwara, sasa hivi tusingeweza kutoa ahadi ya moja kwa moja kwamba, Serikali itaweka kiwanda cha *sulphur* kule Mtwara isipokuwa tutakachokifanya ni kwamba, tutaendelea kuwasiliana au kufanya utaratibu wa kuwezesha wafanyabiashara au watu wengine

wanaohusika na upelekaji wa *sulphur* katika maeneo haya kuweza kupeleka *sulphur* kule Mtwara na kuhakikisha kwamba, inapelekwa kwa bei nafuu zaidi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa soko la zao la korosho liko India na kwa kuwa nchi ya India ndio soko pekee la zao la dengu ambalo linalimwa sana katika Mkoa wa Singida. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atawaambia nini Wananchi wa Singida ambao wanahangaika na kupata soko la kudumu la dengu wanazolima kwa wingi sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu korosho, kwa hiyo, dengu lije swali lake maalum litajibiwa. Korosho Mheshimiwa Lydia Boma.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa zao la korosho nchini ni la pili kwa kusaidia Pato la Taifa hili. Sasa hivi hapa wakulima wa Mkoa wa Mtwara hawana *sulphur,* je, Serikali inalijua tatizo hilo na kama inalijua itawasaidiaje? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba, upungufu wa *sulphur* katika nchi hii na hatupendekezi sana matumizi ya *sulphur* kwa sababu *sulphur* inaongeza tindikali katika udongo. Kwa hiyo, tunapendekeza matumizi ya madawa mbadala ikiwemo *bithiodan* na kuna dawa nyingine.

Kwa sasa hivi pale Mtwara kuna tani 100 za madawa mbadala na Serikali imeamua kulipa ruzuku ili bei ya madawa haya ipungue na yaweze kutumiwa. Tunashirikiana na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala kuhakikisha kwamba, kazi hiyo inafanyika mapema iwezekanavyo. Naomba wakubali kutumia haya madawa mengine kwa sababu ni mazuri kuliko *sulphur.* Namshukuru sana Mheshimiwa Lydia Boma, kwa jinsi anavyoshirikiana na sisi katika kazi hii. *(Makofi)*

Na. 381

**Ubomoaji wa Nyumba Pembezoni mwa Barabara**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza:-

Kwa kuwa majibu ya Serikali yaliyotolewa Bungeni tarehe 13 Aprili, 2004 na Naibu Waziri wa Ujenzi juu ya suala la kubomoa nyumba zilizojengwa pembezoni mwa barabara yalisema kuwa hakutakuwa na fidia au malipo yoyote yatakayotolewa ikiwa mwananchi husika hana hati halali ya nyumba husika na kwamba watakaolipwa kutokana na kubomolewa kwa nyumba zao ni wale tu wenye hati halali; na kwa kuwa Waziri alikiri kabisa kwamba kuna nyumba zilizojengwa zamani kabla barabara husika haijajengwa; na kwa kuwa nyumba hizo hazina hati halali hivyo zitavunjwa bila fidia:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kumnyima fidia mtu aliyejenga kabla ya kuwepo kwa barabara na kwamba kwa kufanya hivyo inamdhulumu na kumnyima mtu haki yake na huko ni kukiuka haki za binadamu?

(b) Je, Serikali inatambua kwamba ardhi yote Tanzania kama haina hati miliki ni mali ya Kijiji na Kijiji ni Serikali kamili yenye uwezo wa kumtambua mmiliki na akakubalika kisheria?

(c) Je, Serikali iliweka mawe *(beacons)* kwenye mipango yake ili mwananchi/mwanakijji husika aweze kuifuata ili asikosee juu ya eneo linalohusu ujenzi wa nyumba yake au maeneo husika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikiendesha zoezi la uwekaji wa alama ya X kwenye nyumba zote ambazo zipo ndani ya eneo la barabara *(Road Reserve),* kwa lengo la kuzitambua na kisha kuwataka wahusika wazibomoe il kutota nafasi kwa mipango mbalimbali ya upanuzi wa barabara. Aidha, wakati Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akiwasilisha Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, alitoa maelezo kwenye kitabu chake kuhusu suala la hifadhi ya barabara na kitabu hicho, nina hakika alipewa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Kwa kuwa suala hili ni la kisheria, hatutegemei kuwepo kwa utata wowote wa tafsiri yake toka kwa wahusika halali wa nyumba na mashamba yaliyomo ndani ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeazimia kuweka mawe ya mipaka *(beacons)* kwenye mipango yake ya ujenzi na upanuzi wa barabara ili kuzuia hili tatizo la Wananchi kujenga na kulima ndani ya hifadhi ya barabara. Ili kutekeleza azma hii, Wizara yangu imeanza kuweka mawe hayo katika miradi yote mipya inayoendelea na ile itakayotekelezwa siku za usoni. Lakini hii haina maana barabara ambazo hazina *beacons* zivamiwe. Namshauri Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ashirikiane na Serikali katika kuwaelimisha Wananchi wa Jimbo lake kuhusu Sheria ya Hifadhi ya Barabara pamoja na Wabunge wengine wote.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Swali langu la msingi lilihusu majibu tofauti ya Mawaziri kwamba, tarehe 13 Waziri wa Mawasiliano alisema kwamba na hapa nanukuu kidogo: "Pia napenda niwaarifu rasmi kuwa msimamo wa Serikali kwa wale waliojenga katika *road reserve* upo pale pale kwamba, hakutakuwa na fidia". Siku hiyo hiyo Naibu Waziri wa Ujenzi, alituambia hapa kwamba, kama hakuna hati halali hawatalipwa fidia. Hayo ni majibu na hii ni *Hansard* ninayo hapa. Kwa hiyo, ningependa nijibiwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, pili, nataka kuuliza kwamba, kwa kuwa malalamiko ya hizo X ni mengi na ni Tanzania nzima, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuileta hiyo sheria tuiangalie upya ili sisi wadau tuweze kuelewana na Serikali kwa pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, matamko ya Serikali hayana tofauti wala hayagongani. Ni tafsiri ya msikilizaji, nini mtu amezungumza na naomba niweke wazi, Sheria ya *Road Reserve* imetungwa mwaka 1932, kama yupo mtu mwenye hati ya mwaka 1931 atalipwa, huyo ana haki maana yake amekuwepo hapo kabla ya sheria kutungwa. Hicho ndicho tunachosema, mtu akiwa na hati halali. Hati halali ni ile ya kabla ya sheria kutungwa. Sisi tuna hati ya barabara *(Road Reserve)* mwaka 1932, ikaja kusahihishwa Bungeni mwaka 1947, ikasahihishwa tena na Bunge hili hili Tukufu mwaka 1967 na bado imetamka *road reserve* na umbali gani kutoka katika barabara mpaka mwisho. Kwa hiyo, masuala ya Serikali kutofautiana matamko si sahihi, maana alichosema Mheshimiwa Maua Daftari kwamba, watu hawatalipwa ni sawa kabisa kwa sababu anajua watu hawana hati halali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malalamiko kwamba yapo mengi, malalamiko haya yapo mengi, kwa bahati mbaya ni kwa sababu sheria zipo nyingi tu ambazo hazitekelezwi bado. Lakini unapokuwa ndio unaitekeleza sheria, ukiona wanalalamika, kwanza, wanajua sheria ipo, la pili, wanathamini hicho kitu kinachotendeka, hilo watataka marekebisho na Waheshimiwa Wabunge ni haki yenu kuleta hapa masahihisho yoyote ya Sheria, Mheshimiwa Spika atayapokea na kuyaweka hapa hadharani, tutayajadili, lakini sheria iliyokuwepo sasa hivi ndiyo inayotekelezwa. *(Makofi)*

Na. 382

**Ujenzi wa Matuta Katika Barabara ya Muhutwe - Kagoma**

**MHE. OMAR S. CHUBI (k.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga matuta katika barabara ya lami ya Mhutwe - Kagoma ili kupunguza kasi ya magari na ajali za barabarani na kwa kuwa kazi ya ujenzi huo inaendelea vizuri sana:-

(a) Je, Serikali bado inakumbuka ahadi hiyo na kwamba ni muhimu kuitekeleza?

(b) Je, Serikali inaonaje kama ikitoa somo la usalama barabarani kwa shule zote zilizo kandokando ya barabara hiyo na Wananchi wa maeneo hayo kwa ujumla ili kupunguza ajali za barabarani?

(c) Je, ni adhabu gani hutolewa kwa dereva aliyegonga mtu barabarani hasa katika eneo la wavukaji wa miguu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Masifiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara yoyote inayotambuliwa kuwa barabara kuu chini ya nyongeza ya Sheria ya Barabara kama ilivyotamka kwenye Tangazo la Serikali Namba 165 la tarehe 5 Mei, 1967 inajengwa kwa makusudi ya kutumia mwendo wa kasi unaokubalika kwa watumiao magari, kwa sisi hapa Tanzania ni kilomita 80. Aidha, barabara kuu zote zinalenga pia kuwapunguzia wenye magari gharama za usafirishaji zinazojumuisha mafuta, matairi, breki na muda wa safari, kwani barabara hizi hutumia pia na magari ya masafa marefu.

Mheshimiwa Spika, uwekaji wa matuta kwenye barabara kuu si utaratibu sahihi kwani matuta husababisha magari kutembea kati yakilomita 10 na 50 kwa saa hata kama hakuna watumiaji wengine wa barabara. Mwendo huu ambao ni wastani wa kilomita 30 ni kinyume na madhumuni ya kujengwa kwa barabara hizi, ambayo pamoja na mambo mengine, ni kurahisisha usafiri kwa kupunguza muda wa usafiri. Matuta hujengwa kwenye barabara za Mjini kwenye makazi na msongamano wa watu wengi ili kuwalazimisha madereva kupunguza mwendo na kutohatarisha maisha ya watumiaji wa barabara. Aidha, ujenzi wa matuta hufanywa mara tu baada ya kushindikana kwa njiia nyingine zote.

Mfano, ni barabara kuu kutoka Dar es Salaam kupitia Dodoma, Singida, Shinyanga na Mwanza, ambapo kama tutaamua kuweka matuta barabara yote kusudi la barabara kuu kupunguza gharama za usafirishaji litakosa maana iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu haina kumbukumbu yoyote inayoonyesha kuwa, kuna Kiongozi wa Serikali aliyewahi kutoa ahadi hiyo ya kujenga matuta katika barabara ya Muhutwe - Kagoma iliyowekewa lami hivi karibuni. Kutokana na maelezo ya awali si uamuzi sahihi kuweka matuta katika barabara kuu na hasa ukizingatia kwamba, Vijiji kwenye sehemu hizi vinachukua umbali mkubwa kiasi kwamba, matuta mengi yatahitajika kila baada ya hatua chache. Hivyo, Serikali itajitahidi kuweka alama za barabarani kwenye barabara zote zinazojengwa na tunategemea madereva wote na watumiaji wengine wa barabara wataziheshimu na kuzifuata.

Pia Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kutoa vipeperushi kwa Wananchi wakiwemo wa maeneo ya Vijiji vilivyopo kandokando ya barabara ya Muhuwe - Kagoma, juu ya utumiaji salama wa barabara zetu. Hii ni pamoja na kuwashirikisha Polisi wa Usalama Barabarani ili kuwadhibiti madereva wasiofuata sheria za usalama barabarani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, ikishirikina na Wizara ya Ujenzi, imeshaandaa mitaala ya kufundishia elimu ya usalama barabarani kwa

shule za msingi, sekondari na Vyuo vya Ualimu Tanzania Bara. Mitaala hiyo bado ipo kwenye majaribio katika Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro. Baada ya majaribio na kupatikana fedha za kuandaa vitabu vya kutosha kwa ajili ya somo hili, Serikali itasambaza elimu hiyo katika Mikoa yote ukiwemo Mkoa wa Kagera. Kama mpango huu utachelewa kuanza, Wizara yangu itafanya mpango wa kutumia watalam wake kutoa elimu ya usalama barabarani katika shule zilizopo kandokando ya barabara ya Muhutwe - Kagoma.

(c) Mheshimiwa Spika, dereva anapopatikana na kosa la kumgonga mtu barabarani hasa katika eneo la wavukaji wa miguu *(Zebra Crossing),* hupewa adhabu ya kifungo cha kati ya miaka miwili na mitano na wakati mwingine kutozwa faini na Mahakama kulingana na Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya Mwaka 1973, Kifungu Na. 40 na Kifungu Na. 63, kifungu kidogo 2(a).

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Sambamba na utaratibu wa usalama barabarani, kumezuka mtindo wa askari hawa wa usalama barabarani wanaokuwa na vidhibiti mwendo kujificha na ukiendesha ghafla wanajitokeza ili wakutoze kwamba, umekwenda spidi kali. Sasa kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, hii nayo ipo kwenye mitaala kwa sababu ni mambo ya hatari ambayo yanaweza kusababisha ajali barabarani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, swali hili tumewahi kulijibu humu ndani ya Bunge na tulieleza sababu kwamba madereva mara nyingi wanakuwa wanaashiriana wanapoona askari. Kwa hiyo, wanaendelea kufanya makosa bila askari kujua, kwa hiyo, ndio maana wanafanya hizo mbinu ili kuwakamata. Lakini nataka nikiri kwamba, huo si utaratibu mzuri, tutaendelea kuhakikisha uadilifu katika utendaji wa askari wetu wa trafiki ili kuepuka huu mtindo wa kuvizia.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na naomba kuuliza swali la nyongeza. Katika hii barabara husika iliyotajwa hasa huanzia Mutukula - Muhitwe mpaka Kagoma ina Vijiji vikubwa na barabara ndogo ndogo zinazokwenda Vijijini, lakini zimepitishwa *drainage* ambazo siyo kwamba ni *open,* ambazo zinazuia watu kuingia kwa urahisi katika barabara hizi za Vijijini, inabidi kwenda kwa muda mrefu mpaka wapate mahali pa kuingilia na kusababisha msongamano katika barabara. Je, Waziri mhusika ana habari hiyo na atafanya nini kuwaambia wakandarasi kusudi waweze kuweka barabara za kuingia huko Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hiki ni kitu ambacho nimekipata sasa hivi na bahati nzuri sasa hivi ninaelekea huko huko. Kwa hiyo, nitakwenda kuona mwenyewe na kuwasiliana na mkandarasi tuone tatizo hilo likoje.

Na. 383

**Kilimo cha Umwagiliaji - Bonde la Mto Bubu**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. KHALID S. SURU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Bonde la Mto Bubu lililoko Kondoa ni muhimu kwa shughuli za Kilimo cha umwagiliaji ambacho kinasaidia kuinua uchumi, kuondoa umaskini na kuongeza ajira kwa vijana; na kwa kuwa Bonde la Mto huo limepitia kwenye Vijii vya Berabera, Kikilo Kati, Kwahengwa, Sakami, Thawi, Kwamadebe, Changaa, Munguri, Mongoloma, Serya, Chemchem, Iyoli, Kingale, Tampori na kadhalika na kwamba Wananchi hususan vijana wameamua kupambana na umaskini kupitia kilimo hicho:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje Wananchi hao katika kuanzisha miradi mikubwa ya umwagiliaji maji kwenye mashamba kwa njia rahisi na za kisasa ili kuinua kipato chao?

(b) Je, Serikali katika *master plan* ya umwagiliaji ya Kitaifa ambayo shabaha zake ni kuyatumia mabonde kama hayo kukuza kilimo na kuondoa njaa na umaskini, imetembelea maeneo hayo?

(c) Je, Serikali itaanza lini kutekeleza ahadi zake za kuwasaidia Wananchi wa Bonde la Mto Kisese kwenye shughuli za umwagiliaji maji mashamba kwa njia ya kisayansi kwenye Vijiji vya Mapinduzi, Unjeji, Sauna, Dissa na Madisa hadi Atta pamoja na kutoa pikipiki mbili kwa ajili ya kufuatilia shughuli hizo kama Serikali ilivyoahidi kwa Wilaya ya Kondoa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Chini ya Mpango Kamambe wa Kilimo Cha Umwagiliaji Maji Mashambani, skimu ishirini na moja za umwagiliaji maji zenye jumla ya hekta 12,890 katika Wilaya ya Kondoa, zimeainishwa na baadhi yake zimeanza kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Skimu zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni miongoni mwa skimu zilizoainishwa katika mpango huo.

Katika mwaka wa 2003/2004, wataalam kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, waliendelea kuwasaidia wakulima kuchambua skimu za umwagiliaji zilizoainishwa katika Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Aidha, wataalam wanaendelea kuandaa maandiko ya kuwezesha skimu hizo kuingizwa katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya ya Kondoa kwa lengo la kuombewa fedha Serikalini na kutoka vyanzo

vingine vya fedha. Tayari, skimu za Chang'aa na Berabera zimefanyiwa uchambauzi wa kitaalam na maandiko yamekamilika.

Aidha, zipo kazi ambazo zimekwishafanywa kuendeleza skimu za umwagiliaji katika Wilaya ya Kondoa na nyingine bado zinaendelea kufanywa. Maelezo ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kati ya mwaka wa 1977/78 na 1981/82, Serikali kwa kupitia programu ya nguvukazi iliyojulikana kwa jina la *Special Labour Intensive Public Works Programme,* ambayo iligharamiwa na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* ilijenga skimu za umwagiliaji maji mashambani za Berabera zenye ukubwa wa hekta 60, Mnenia hekta 80 na Kikore hekta 400 kwa gharama ya Sh. 331m/=.

- Kati ya mwaka wa 1998/99 na 2003/2004, Serikali kupitia *Kondoa Integrated Rural Development Programme* na *Tanzania Social Action Fund (TASAF),* ilikarabati skimu za Berabera za Kwamadebe zenye ukubwa wa hekta 60 kila moja ambazo zilikuwa zimeharibiwa na mvua za *Elnino.* Ukarabati wa skimu zote mbili uligharimu jumla ya Sh. 58m/=.

(b) Wakati wa maandalizi ya Mpango Kamambe wa Kitaifa wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, wataalam kutoka Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji ya Tabora, kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, walitembelea Bonde la Mto Bubu kati ya mwezi wa Desemba, 2001 na Januari, 2002.

(c) Kaitka mwaka wa 2003/2004, Serikali ilianza kufanya ukarabati wa skimu ya umwagiliaji maji ya Kisese kwa gharama ya Sh. 25m/= na hivi sasa kazi inaendelea. Aidha, Serikali haikutoa ahadi ya kutoa pikipiki mbili kwa Wilaya ya Kondoa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Dodoma una mabonde mengi likiwemo Bonde hili la Mto Bubu, Bonde la Lumuma, Bonde la Matomondo, Bonde la Bahi na kadhalika. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba, kama Serikali itasimamia kilimo cha umwagiliaji kwenye mabonde haya itapunguza tatizo la upungufu wa chakula katika Mkoa wetu wa Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli miradi hii ikiendelezwa tatizo la njaa litapungua. Napenda kumthibitishia kwamba, tunafanya hivyo. Kwa Lumuma nimefika mwenyewe nikiwa hapa hapa mwezi uliopita, nimeona mambo mazuri yanaendelea, nilikwenda na Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, ambaye yupo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bahi pia tunafanya hivyo. Nimeshafika kwa miaka miwili mfululizo, mambo yanaendelea na kadhalika. Sasa ninachosema ni kuwa, fedha

zilizotengwa zinakwenda kwa awamu, tatizo ni ufinyu wa bajeti. Tungependa kueneza miradi ya umwagiliaji nchi nzima, lakini tatizo ni fedha. *(Makofi)*

Na. 384

**Mabonde na Mito Ifaayo kwa Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Wilaya ya Mbinga ipo mito mingi na mabonde yafaayo kwa kilimo cha umwagiliaji kama vile Bonde la Mitomoni, Kata ya Liparamba, Bonde la Lundo, Kata ya Lipingo, Bonde la Lituhi, Kata ya Lituhi, Bonde la Kihagala katika Kata ya Litumbandyosi na mengine mengi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wadogo wadogo waishio katika maeneo hayo ili waweze kuyatumia mabonde hayo kikamilifu kwa kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napedna kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ya mwaka 2002, ambayo pamoja na mambo mengine, inakipa kipaumbele kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Aidha, katika mwaka wa 2002/2003, Serikali iliandaa Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, ambao umekwishasambazwa kwa Halmashauri za Wilaya zote. Mpango huo umeainisha skimu sita zenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika Wilaya ya Mbinga. Skimu hizo ni Lituhi yenye ukubwa wa hekta 4,000, Lundo hekta 1,500, Chiulu hekta 300, Kihagala hekta 350, Mitomoni hekta 500 na Litumbandyosi hekta 300.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula, ilifanya uchunguzi wa kitaalam na makadirio ya kuendeleza skimu za uwmagiliaji za Lundo, Litumbandyosi na Lituhi na kukabidhi maandiko hayo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imekwisha jumuisha skimu hizo pamoja na skimu ndogo za Kigonsela hekta 15 na Makoko hekta 60, katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya wa mwaka 2004/2005.

Aidha, katika mwaka huu Serikali imetenga Sh. 20m/= kwa ajili ya kuanza kuendeleza skimu ya Lundo.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa hatua iliyochukua Serikali kutenga shilingi milioni 20 kwa

ajili ya Bonde la Lundo ni hatua nzuri naipongeza Serikali. Ningeomba kufahamu, je, kwa mabonde yaliyobaki kama Lituhi, Chulu, Mitomoni na Kihagala, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha kwa ajili ya hayo mabonde?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunashukuru kwa pongezi, zinatuimarisha na kutupa ari ya kufanya kazi nzuri zaidi.

Kuhusu mabonde yaliyobaki tunamwomba tu awe na subira ndiyo yamewasilishwa sasa wala haikuwa siku nyingi. Kwa hiyo, tumeanza na Lundo na tunaendelea kwa awamu, tatizo letu ni ufinyu wa fedha zikiwa nyingi tutafanya yote kwa mkupuo, lakini kwa sasa tunafanya kwa awamu. Limepokelewa tunaomba awe na subira.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote ya msingi yamejibiwa. Sasa tunaendelea na matangazo ya vikao vya Kamati kwa leo ni Kamati mbili tu zimejipangia vikao vyake.

Kamati ya kwanza ni ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti wake, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane mara baada ya hotuba za Mawaziri kumalizika katika chumba namba 133 ghorofa ya kwanza. Kamati ya pili ni ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 219 ghorofa ya pili.

Chama cha Hiari cha Wabunge cha Idadi ya Watu na Maendeleo, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Paul Kimiti, anawaarifu kwamba kutakuwa na Mkutano na Semina kwa Wanachama wa Chama hicho katika ukumbi wa Chuo cha Ufundi *VETA* kuanzia saa 7.00 mchana leo tarehe 4 Agosti, 2004. Mwisho wa matangazo ya vikao.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kuhusu ratiba ya leo, mtakumbuka ilibidi turekebishe ratiba yetu kutokana na kazi ya Mungu, isiyokuwa na makosa. Sasa marekebisho hayo matokeo yake ndiyo leo kwamba, Wizara mbili zitawasilisha hoja zao siku hii ya leo na zitajadiliwa kwa pamoja ili kusudi tusitoke nje ya ratiba ya awali iliyopitishwa na Kamati ya Uongozi. Kwa ajili hiyo, hatutakuwa na nafasi ya kutosha Waheshimiwa Wabunge wote walioomba kuchangia ambao wako 23 haitawezekana na tutakwenda kwa utaratibu wetu ule ule, ambaye hajachangia atapewa nafasi ya kwanza, waliochangia mara moja watapewa nafasi inayofuata, waliochangia mara mbili na kuendelea, nadhani wangejitahidi wachangie kwa maandishi tu sidhani kama watapata nafasi ya kuchangia kwa mdomo.

Sasa baada ya maelezo hayo, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa mwaka 2004/2005, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ikiongozwa na Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa mchango mkubwa ilioutoa wakati ikijadili na hatimaye kuyapitisha Makadirio haya. Aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa uvumilivu na umakini wenu wakati wa kupitia, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti za Wizara mbalimbali tangu kuanza kwa kipindi hiki cha Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani zangu kwa Wakurugenzi, Viongozi wa Asasi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu, Dr. Enos Bukuku na Naibu Katibu Mkuu, Bwana Omar Bendera, kwa kufanikisha maandalizi ya Makadirio haya na ushirikiano wao katika kutekeleza malengo tuliyokuwa tumejiwekea mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko, nachukua nafasi hii, kwa niaba ya Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na kwa niaba yangu mwenyewe, kutoa rambirambi zetu kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa familia, jamaa na marafiki, kwa misiba ya Wabunge waliotutoka, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, pamoja na Marehem Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, ni pamoja na kuishauri Serikali katika masuala ya kiuchumi na kijamii, kutayarisha mipango ya maendeleo, kuandaa miongozo ya mpango na bajeti pamoja na taarifa mbalimbali za hali ya uchumi na jamii. Katika kufanikisha majukumu haya kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, idara na asasi zilizoko chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji zilishirikiana katika kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

- Uchambuzi na maandalizi ya sera na mikakati ya uchumi jumla na ya kisekta;

- Uchambuzi wa sera na mikakati ya kuendeleza sekta za jamii na maendeleo ya rasilimali watu;

- Usimamizi wa uchumi jumla;

- Utayarishaji na uratibu wa mipango ya maendeleo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi;

- Urekebishaji na ubinafsishaji wa mashirika ya umma;

- Uimarishaji wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu;

- Uendelezaji wa taaluma ya ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu;

- Utoaji wa mafunzo, utafiti na ushauri kuhusu masuala ya mipango ya maendeleo vijijini;

- Kuratibu uendeshaji wa Tovuti ya Taifa;

- Ukuzaji na uendelezaji wa uwekezaji wa rasilimali nchini;

- Uandaaji wa miongozo ya shughuli za sekta ya nje na kuratibu matumizi ya misaada kutoka nje;

- Uimarishaji wa tija;

- Utayarishaji wa taarifa na nyaraka mbalimbali za Kiserikali; na

- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na sera na mikakati mbalimbali ya kiuchumi na kijamii kwa lengo la kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa tathmini halisi ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na asasi zake kwa mwaka 2003/2004, pamoja na maelezo ya malengo ya mpango wa maendeleo na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Kujenga mazingira bora ya utendaji kazi na uwezo wa kuendeleza utafiti na uchambuzi wa masuala ya kiuchumi na kijamii

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika mwaka 2003/2004, iliajiri wachumi na maafisa mipango 44 na kuwapangia vituo vya kazi katika Wizara na Mikoa mbali mbali. Aidha, watumishi 30 walio kazini walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ndani na nje ya nchi. Wakati huo huo jumla ya wachumi sita, afisa utawala mmoja na mhasibu mmoja wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ya shahada za uzamili.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ofisi iliendelea na ukarabati wa awamu ya pili wa jengo la Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Vile vile, awamu ya kwanza ya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Taifa ya Takwimu ulikamilika na awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma pia ulikamilika na kuzinduliwa rasmi tarehe 8 Desemba, 2003 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Frederick T. Sumaye.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuhakikisha kwamba ofisi zinapatiwa nyenzo, vitendea kazi na mahitaji muhimu ya kiofisi. Aidha, itaendesha mafunzo ya wafanyakazi juu ya utawala bora, hususan, mapambano dhidi ya rushwa na maadili kazini. Pia, itaendelea na ukarabati wa majengo ya Ofisi ili kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ilifanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Muda wa Kati kwa lengo la kuhuisha malengo, dira, madhumuni, taratibu na shabaha za Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Baada ya kukamilisha mapitio hayo, pia, Ofisi imefanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja ili uende sambamba na yaliyobainishwa kwenye Mpango Mkakati na utakapokamilika utasambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itaendelea na utekelezaji wa malengo yaliyomo kwenye Mpango Mkakati na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na kuendeleza teknolojia ya maendeleo ya habari na mawasiliano na kuhakikisha kwamba Tovuti ya Taifa *(National Website),* inaboreshwa na kufanya kazi ya kutoa taarifa mbalimbali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na asasi zake iliendelea kuboresha ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu na taarifa mbalimbali za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na hali ya uchumi katika mwaka 2002 na mfumo wa sera za jumla za uchumi na maendeleo ya jamii 2003/2004 - 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea kukusanya na kuimarisha ubora wa takwimu pia ilifanya mapitio ya kigezo cha fahirisi ya bei kwa kuhuisha idadi ya bidhaa na huduma zinazofanyiwa utafiti wa bei kila mwezi ikiwa ni pamoja na umuhimu wa makundi ya bidhaa na huduma hizo kwenye matumizi ya kaya kulingana na matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi uliyofanyika mwaka 2000/2001. Aidha, Ofisi ilifanya tafiti za Ajira na Mapato, Hali ya Utalii, Kilimo na Mifugo, Uzalishaji wa Sekta ya Viwanda kwa mwaka na robo mwaka, pamoja na utafiti wa Biashara *(Business Survey).* Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea kusambaza matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na yale ya Tafiti za Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi na Ajira kwa Watoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi iliendelea na mradi wa kufanya mapitio ya kigezo cha Pato la Taifa kwa kutumia tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi, Kilimo, Sensa ya Watu na Makazi; Viwanda, Ajira na Mapato na Sensa ya Biashara. Ni mategemeo yetu kuwa, kitabu cha Hali ya Uchumi cha mwaka 2004 kitakachowasilishwa katika Bunge la Bajeti mwaka 2005 kitaonyesha kigezo cha Pato la Taifa kulingana na mabadiliko yatakayofanywa pamoja na Fahirisi ya Bei mpya.

Mheshimiwa Spika, kama wakala wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanikiwa kupata kazi *(Commissioned Work)* zifuatazo: Utafiti wa viashirio vya UKIMWI Tanzania *(Tanzania HIV/AIDS Indicator Survey),* Utafiti wa kutathmini uwezo wa halmashauri mbalimbali wa kutoa huduma kwa kutumia wadau, Uchambuzi wa maoni ya wananchi kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini pamoja na Utafiti wa Kijamii juu ya Uhusiano wa Watoto na Maradhi ya UKIMWI katika Wilaya ya Moshi Mjini kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Tiba cha Havard cha Marekani.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kushughulikia tafiti za kawaida za viashiria vya kila mwezi, robo mwaka na kila mwaka. Vilevile, itafanya Utafiti wa Hali ya Uhai na Afya 2004 *(Tanzania Demographic and Health Survey 2004)* ili kuboresha takwimu za viashirio vya umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi ya Taifa ya Takwimu pia itaendelea na uchambuzi na usambazaji wa takwimu zilizotokana na tafiti za kilimo na ya viashirio vya UKIMWI na pia itaendelea kukamilisha utafiti wa shughuli za kiuchumi Tanzania na kusambaza matokeo yake kwa wadau mara uchambuzi utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea na utekelezaji wa mradi unaofadhiliwa na Shirika la Japani la Ushirikiano Kimataifa *(Japan International Cooperation - JICA),* wenye lengo la kujenga uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika eneo la teknolojia ya habari na mawasiliano. Baadhi ya kazi zinazotarajiwa kufanyika ni pamoja na kuanzisha kitengo cha uchambuzi wa taarifa za habari na masoko; kutayarisha mfumo wenye uwiano kati ya mtandao wa utunzaji taarifa za kijamii na kiuchumi *(Tanzania Socio-economic Database - TSED),* upatikanaji wa vifaa muhimu vya mtandao, kutoa mafunzo yahusuyo teknolojia ya habari na mawasiliano kwa watumishi; kuimarisha maktaba ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na kuchapisha majarida mbalimbali ya taarifa za kitakwimu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa kushirikiana na mikoa husika, imekamilisha vitabu vya taarifa za Hali ya Maendeleo ya Uchumi na Kijamii kwa Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Kagera, Mara na Kilimanjaro. Aidha, kazi ya kutayarisha vitabu vya mikoa ya Singida, Rukwa, Tabora na Arusha inaendelea. Kazi ya kukusanya takwimu kwa mikoa ya Pwani, Tanga, Iringa Ruvuma na Manyara inaendelea pia.

Aidha, Ofisi itaendelea na uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa kutokana na utafiti wa Kilimo na Mifugo pamoja na kuzichanganua na kuchapisha taarifa mbalimbali

na kuzisambaza. Uchambuzi wa takwimu za Utafiti wa Biashara utaendelea, pamoja na kuchanganua, kuchapisha taarifa na kuzisambaza kwa wadau. Vilevile, kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na mikoa husika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itaendelea kuandaa Taarifa ya Hali ya Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Mkoa *(Regional Socio-Economic Profile)* na kuzisambaza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, kazi ya kuchambua na kusambaza takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 iliendelea. Kazi iliyofanyika ni pamoja na kutoa takwimu zilizochambuliwa za ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji. Takwimu muhimu zinazoendelea kutolewa kwa watumiaji ni pamoja na zinazohusu umri, elimu, afya, hali ya makazi, ajira, uhamiaji, hali ya ulemavu, hali ya ndoa, vizazi na vifo pamoja na mahusiano ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Ofisi pia iliendelea kuchambua takwimu za Sensa kwa madhumuni ya kukamilisha vigezo vya msingi. Kati ya vigezo hivyo ni pamoja na matarajio ya kuishi *(Expectation of Life at Birth)*. Kigezo hiki kimebadilika toka miaka 50 mwaka 1988 hadi miaka 51 mwaka 2002. Ongezeko hilo linatokana na jitihada za Serikali katika kuboresha huduma za afya na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Vizazi, matokeo ya sensa yameonyesha kuwa kwa kila mwanamke mwenye umri wa kuzaa (miaka 15 hadi 49) huzaa wastani wa watoto 6.3, kulinganisha na wastani wa watoto 6.5 kwa kila mwanamke mwaka 1988. Takwimu hizo zinaonyesha kuwa kiwango cha uzaaji bado ni cha juu ingawaje kinaonyesha mwelekeo wa kupungua. Kwa upande wa viashirio vya umaskini, matokeo ya sensa ya mwaka 2002 pamoja na maeneo mengine, yanaonyesha yafuatayo: Asilimia 91 ya kaya zote wana vyoo, asilimia 23 ya kaya zote hutumia nishati ambayo siyo ya kuni au mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia, asilimia 34 ya kaya zote chanzo kikuu cha maji ya kunywa ni maji ya bomba na asilimia 36 ya kaya zote chanzo kikuu cha nishati ya kuonea usiku sio kibatari

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi Kuu ya Sensa itaendelea kutayarisha na kusambaza taarifa mbali mbali zitokanazo na uchambuzi wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi na baadhi ya taarifa zinazotarajiwa kutolewa ni pamoja na hali za kiuchumi na kijamii za Wilaya/Mikoa na Taifa, uchambuzi wa Sensa, uendeshaji wa mfumo wa ramani na mipaka pamoja na makadirio ya idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ilikamilisha kazi ya kutayarisha Mpango wa Muda wa Kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini 2004/2005 - 2006/2007. Lengo la Mpango huu ni kubainisha programu za kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuunganisha nguvu za wananchi na rasilimali za Taifa ili kukuza uchumi na hatimaye kupunguza umaskini

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi itaendelea na majukumu ya kutayarisha na kusambaza Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2005/2006 - 2007/2008 na pia kwa kushirikiana na wadau, itatayarisha programu za kutekeleza

Mpango wa Muda wa Kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 - 2007/2008. Aidha, Ofisi itaandaa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu za maendeleo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Tovuti ya Taifa iliendelea kuboreshwa kwa kuwekewa taarifa nyingi na zinazotolewa kwa wakati. Uboreshaji huo umeenda sambamba na kuiunganisha na tovuti nyingine za wizara na idara za serikali pamoja na asasi zake kwa lengo la kuwa na mseto wa taarifa ili kuwavutia watumiaji wengi zaidi na wa nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Tovuti ya Taifa itaendelea kuboreshwa zaidi kwa kuongeza upatikanaji wa taarifa muhimu na kwa wakati. Aidha, muonekano na mpangilio wa taarifa utarekebishwa ili uwe wa kisasa zaidi na rahisi kutumiwa. Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inatarajia pia kuajiri wataalamu wa kompyuta na mambo ya usimamizi wa *Website* ili kuongeza ufanisi katika kitengo cha Tovuti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika kiliendelea kuboresha taaluma ya ukusanyaji na utunzaji takwimu nchini kwa kuendelea kutoa mafunzo ya cheti na Stashahada. Katika mwaka 2003/2004, Chuo kilikuwa na jumla ya wanafuzi 40 wa cheti na 24 wa Stashahada. Katika kujenga uwezo wa kukusanya na kuchambua takwimu katika ngazi ya Serikali za Mitaa, jumla ya wanafunzi 21 ambao ni waajiriwa wa Serikali za Mitaa walifadhiliwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika chuo hicho. Wanafunzi wengine walitoka taasisi nyingine nchini na nchi za Botswana, Kenya, Malawi, Namibia na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Chuo kinatarajia kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya tafiti na kutoa ushauri kwa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali na wadau wengine. Aidha, Chuo kitaendelea kuboreshwa kwa kuajiri walimu zaidi wenye ujuzi, kuimarisha mazingira ya Chuo na kuhamasisha mafunzo kwa walio kazini.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza fani ya mipango ya maendeleo nchini, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, kimeendelea kutoa mafunzo yanayolenga kutayarisha na kuendeleza ujuzi na stadi za mipango ya maendeleo kwa viongozi na maafisa watendaji wa Serikali za Mitaa Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya na wadau mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo kimetoa mafunzo ya Cheti katika Mipango ya Maendeleo Vijijini, Stashahada ya Juu katika Mipango ya Mikoa, Stashahada ya Juu katika Mipango ya Mazingira, Stashahada ya Uzamili katika Mipango ya Mikoa na Stashahada ya Uzamili katika Mipango ya Mazingira. Kwa mwaka 2003/2004, jumla ya wanafunzi 67 walihudhuria mafunzo ya Cheti, 277 mafunzo ya Stashahada ya Juu na 45 mafunzo ya Stashahada ya Uzamili. Aidha, Mafunzo ya muda mfupi kwa walengwa mbalimbali yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Chuo kitaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya utafiti, na kutoa ushauri na uelelezi kwa wadau wote wa maendeleo. Upanuzi na uboreshaji wa miundombinu utaendelea kutekelezwa ili kukabiliana na ongezeko kubwa la wahitaji mbalimbali wa huduma za Chuo. Aidha, ujenzi wa jengo la bweni la Frederick Sumaye utakamilishwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ilishiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za maandalizi ya kukamilisha Itifaki ya Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia ngazi ya wataalamu, Makatibu Wakuu pamoja na Mawaziri. Aidha, Itifaki iliwekwa sahihi na wakuu wa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda tarehe 2 Machi, 2004 na itaanza kutekelezwa baada ya kuridhiwa na nchi wanachama. Maeneo muhimu yaliyomo kwenye itifaki hiyo ni pamoja na kuondoa ushuru wa bidhaa kwa biashara za ndani na utaratibu wa kuhakiki uasili wa bidhaa na uanzishaji wa mfumo mmoja wa ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilikamilisha rasimu ya kubaini fursa na athari za ushiriki wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la zoezi hili ni kuweka mikakati ya kupunguza athari na kutumia vizuri fursa tulizonazo katika ushirikiano. Aidha, katika kuendeleza miradi ya pamoja nchi wanachama zilikubaliana kutoa kipaumbele kwa sekta za barabara, nishati na uendelezaji wa Bonde la Ziwa Victoria. Kwa mwaka 2004/2005, Ofisi itaendelea na juhudi za kubaini fursa ambazo zitatumiwa ili Tanzania iweze kufaidika na Ushirikiano wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji iliendelea na kuratibu Mpango wa *NEPAD* kwa kuunda Kamati za kisekta na kutayarisha programu na miradi ya Kitaifa itakayotekelezwa chini ya mpango huo. Serikali imekwisha jiunga na mfumo wa kupima na kutathmini utekelezaji wa malengo na vigezo vya Utawala Bora na uendeshaji uchumi *(African Peer Review Mechanism - APRM).* Mfumo huu unalenga kuweka utaratibu rasmi wa nchi shiriki kujitathmini na kujipima zenyewe kuhusiana na utekelezaji wa vigezo muhimu vya *NEPAD.* Maeneo yatakayofanyiwa tathmini ni utawala bora wa kisiasa, utawala wa sheria, ushirikishwaji, migogoro ya kisiasa, uendeshaji wa uchumi, hususan sera za fedha na utendaji wa asasi zinazosimamia mabenki na fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itaendelea kutathmini fursa na vikwazo vitokanavyo na ushiriki wa Tanzania katika taasisi za ushirikiano Kimataifa na katika biashara ya nje chini ya asasi na programu kama *EAC, SADC, NEPAD, WTO, AGOA, TICAD* na *EU/ACP.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji iliendelea kuratibu Ushirikiano wa Kiufundi baina ya Nchi Zinazoendelea kwa kugharamia mafunzo ya muda mfupi ya wataalamu katika fani mbalimbali na kuendesha semina kwa wadau ili kuhamasisha na kuendeleza shughuli za *TCDC* kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP).* Vilevile, zoezi la

kutathmini ufuatiliaji wa maamuzi ya mikutano ya Umoja wa Mataifa na asasi zake lilianza kwa lengo la kuiwezesha Tanzania kutekeleza malengo na maamuzi yaliyokubaliwa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Ofisi itaendelea kuratibu majadiliano ya mikataba ya kukuza na kulinda rasilimali kati ya Serikali na nchi nyingine kwa lengo la kuendeleza uwekezaji rasilimali nchini, pamoja na kuendeleza Ushirikiano wa Kiufundi baina ya Nchi zinazoendelea *(TCDC).*

Mheshimiwa Spika, Programu hii inalenga katika kutoa msukumo zaidi wa kuendeleza sekta binafsi kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini, hususan, uboreshaji wa sera, sheria, taratibu, utawala bora na kuimarisha vyombo na taasisi mbali mbali kama *TIC, BRELA* na Mahakama ya Biashara. Katika mwaka 2003/2004, maandalizi ya kuanzisha Kitengo cha Kusimamia Mazingira Bora ya Kibiashara *(Better Regulation Unit - BRU)* yamefanyika ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ofisi, ununuzi wa samani na vitendea kazi na kuajiri wafanyakazi wa muda. Taratibu za kumwajiri Mkuu wa Kitengo zipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2004/2005, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itaendelea na utekelezaji wa mradi chini ya Programu ya Kujenga Mazingira Bora ya Sheria na Taratibu za Kibiashara *(Business Environment Strengthening for Tanzania - BEST).* Maeneo ya urekebishaji yaliyobainishwa na yatakayopewa kipaumbele ni: marekebisho ya kodi za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, marekebisho ya sheria za uajiri, utatuzi wa migogoro ya kibiashara, usajili na utoaji wa leseni za biashara, sheria ya ardhi, ugawaji na uendelezaji wa viwanja na maandalizi ya mkakati wa kuendeleza sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, katika azma ya kuleta msukumo mpya wa kuongeza ukuaji wa pato la taifa, kupunguza umaskini, kuongeza ajira na mauzo ya bidhaa nje, Ofisi itaratibu maandalizi ya mkakati mpya utakaoliwezesha Taifa kufikia azma ya haraka chini ya Mpango wa Kuongeza Kasi ya Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo Tanzania *(Tanzania Mini - Tiger Plan 2020)*. Lengo la mpango huu ni kubuni mbinu mpya kwa kuzingatia uzoefu wa nchi za Asia Mashariki. Mpaka sasa wataalamu wetu wakishirikiana na wataalamu wa taasisi ya *Japan Development Institute (JDI),* wamekwisha kutembelea baadhi ya mikoa hapa nchini ili kubaini fursa mbalimbali zilizopo na kuanzisha maeneo maalumu ya kuendelezwa kwa ajili ya kuvutia uwekezaji rasilimali wa ndani na nje ya nchi *(Special Economic Zones).*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma iliyoanza kazi rasmi zaidi ya miaka 12 iliyopita imefanikiwa kurekebisha jumla ya mashirika/makampuni na mali zisizokuwa muhimu *(non-core assets)* 737 ikijumuisha mashirika/makampuni 366 na mali zisizokuwa muhimu 371. Katika kipindi cha mwaka 2003 pekee, ubinafsishaji ulikuwa ni makampuni/mashirika 26 na mali zisizokuwa muhimu 75 ikiwa ni pamoja na ukodishaji wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka *(DAWASA),* ubinafsishaji wa Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo *(SPM)* na Kampuni za Hoteli za *TAHI.* Mashirika haya yamebinafsishwa kwa Watanzania na wawekezaji

kutoka nje, na mengine kwa njia ya ubia. Mengi ya mashirika hayo yanafanya kazi kwa ufanisi na kuiingizia Serikali mapato kwa njia ya kodi, kutoa nafasi za ajira na kuwezesha upatikanaji wa manejimenti na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kubinafsisha mashirika ya miundombinu na huduma imeandaliwa. Tafiti mbili zimefanyika kwa ajili ya kuligawa Shirika la Umeme *(TANESCO)* kuwa kampuni tatu na kuunda mfumo mpya wa utendaji wa soko la nishati ya umeme. Kwa upande wa Shirika la Reli *(TRC),* wawekezaji walioonyesha nia wamealikwa kuleta zabuni zao kwa ajili ya kukodisha miundombinu ya shirika. Utekelezaji wa mkakati wa ubinafsishaji vitengo vya kibiashara vya Mamlaka ya Bandari, Shirika la Bima na Benki ya *NMB* upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mazingira mazuri ya kupata wawekezaji na kulinda maslahi ya Serikali na walaji, Serikali imeazimia kuunda mamlaka za udhibiti ambapo mamlaka mbili zimekwishaundwa ambazo ni *Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA)* na *Tanzania Communications Regulatory Authority (TCRA).* Mamlaka nyingine zinazotarajiwa kuundwa ni *Surface and Marine Transportation Regulatory Authority (SUMATRA), Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), Fair Competition Commission (FCC)* na *Fair Competition Tribunal (FCT).*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ubinafsishaji wa mashamba makubwa ya kilimo na mifugo, juhudi zimeelekezwa katika kuainisha mashamba yatakayobinafsishwa kwa shughuli za ukulima na ufugaji wa kisasa kwa wawekezaji wenye nia na uwezo. Aidha, katika sehemu zenye uhaba wa ardhi baadhi ya mashamba yatapimwa na kukabidhiwa kwa wananchi wa mikoa husika ili wayaendeleze kwa kilimo. Kwa upande wa ranchi za taifa, baadhi zitabinafsishwa bila kumegwa kwa ajili ya kuendelezwa kama ranchi za mfano. Maeneo ya ranchi nyingine yatagawanywa katika maeneo madogo ili wamilikishwe Watanzania wenye nia ya kufuga kibiashara. Ranchi za Kongwa na Ruvu hazitabinafsishwa kutokana na umuhimu wake katika maendeleo ya sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufuatiliaji wa mashirika yaliyo binafsishwa, pamoja na kwamba jukumu hilo lipo chini ya vitengo vya ufuatiliaji vilivyo chini ya wizara zenye dhamana ya mashirika hayo, bado Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inalo jukumu la kufanya tathmini ya kila mwaka juu ya ufanisi wa mashirika na viwanda vilivyobinafsishwa. Wizara husika huwasilisha taarifa za mwenendo wa uendeshaji wa mashirika hayo Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa ajili ya uchambuzi na kutoa mapendekezo kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Kituo cha Uwekezaji Rasilimali *(TIC)* kiliendelea na hatua mbalimbali zinazolenga katika kukuza uwekezaji rasilimali nchini. Jitihada hizi zimewezesha kituo kusajili miradi 372 yenye thamani ya sh. bilioni 1669.4, miradi 229 ikiwa mipya na 143 ikiwa ni ya upanuzi na ukarabati. Kati ya miradi hiyo, 155 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 109 ya wawekezaji wa nje na miradi 108 ilikuwa ya ubia. Aidha, mitaji ya kigeni ya moja kwa moja iliongezeka kufikia dola milioni 300 kutoka dola milioni 240.4.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Kituo kitaendelea na jitahada za kutangaza na kuwaunganisha wawekezaji wa ndani na nje wenye mitaji, teknolojia, mbinu za masoko na fedha ili kuweza kuendeleza miradi mbalimbali. Aidha, Kituo kitaendelea kutoa na kusambaza taarifa juu ya fursa za uwekezaji, faida na vivutio vilivyopo pamoja na kuendelea kuainisha na kuchambua maeneo ya ardhi yanayofaa kuingizwa katika Benki ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kueneza huduma za uwekezaji nchini, Kituo kitafungua ofisi za Kanda mjini Moshi na Mwanza. Ofisi ya Moshi itahudumia Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Singida na Manyara. Ofisi ya Mwanza itahudumia Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Kigoma na Tabora. Hii inalenga katika kutoa huduma karibu zaidi na wananchi. Sambamba na uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani kituo kitafanya semina katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Iringa na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Baraza la Taifa la Biashara Tanzania *(TNBC)* lilishiriki katika mapitio ya sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973 na kutoa ushauri kuhusu sheria mpya ya kodi ya mapato iliyopitishwa na Bunge hili Tukufu mwezi Aprili 2004, ili iendane na hali ya sasa ya biashara. Vilevile, Baraza limeendelea kutoa ushauri kuhusu marekebisho ya sheria ya leseni za biashara kwa nia ya kuondoa urasimu na kero katika taratibu za kupata leseni za biashara. Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha mapato na matumizi ya Serikali alizingatia ushauri uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Baraza litaendelea kuratibu mawasiliano kati ya Serikali na sekta binafsi katika juhudi za kuimarisha mazingira na taratibu za uwekezaji ili kuweza kuvutia wawekezaji wengi zaidi hasa kwa kuanzisha midahalo ijulikanayo kama *Smart Partnership Dialogue,* baina ya sekta za umma na binafsi. Serikali pia itaendelea na mchakato wa kutayarisha sera ya kukuza na kuendeleza sekta binafsi ambayo itawawezesha wananchi walio wengi kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji imeendelea na kazi ya kuratibu utekelezaji wa Sera ya Idadi ya Watu ikiwa ni pamoja na kukamilisha uhuishwaji wa sera yenyewe, kuendeleza taaluma ya kuoanisha masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo ya kisekta na kiwilaya na kuandaa warsha kwa Wabunge zenye lengo la kupanua uelewa wao juu ya masuala ya idadi ya watu. Aidha, uratibu uliendelezwa katika utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Idadi ya Watu inayojumuisha utetezi wa masuala ya jinsia na haki za wanawake *(Advocacy and Gender),* afya ya uzazi *(Reproductive Health)* na mikakati ya maendeleo ya idadi ya watu *(Population Development Strategies).*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ikishirikiana na taasisi zisizo za kiserikali za kimataifa *UNFPA, PATH* na *PATH Finder International* kwa pamoja wamesimamia utekelezaji wa mradi wa vijana wa *African Youth Alliance ( AYA),* unaotekelezwa na wadau mbalimbali hasa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba sheria iliyoanzisha lililokuwa Baraza la Tija Tanzania ilifutwa rasmi na Bunge katika kikao chake tarehe 12 Februari, 2004. Zoezi la kuhamishia shughuli pamoja na waliokuwa watumishi wa Baraza katika Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji linaendelea kufanywa na ni matarajio yetu kulikamilisha zoezi hili katika mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utekelezaji wa mwaka 2003/2004 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2004/2005, sasa napenda kuchukua nafasi hii kuainisha kwa muhtasari masuala ambayo Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na asasi zilizo chini yake itayapa kipaumbele katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, kama ifuatavyo:-

- Kuboresha mazingira ya utendaji kazi na upatikanaji wa nyenzo za kazi pamoja na kuboresha na kupata wataalamu wa uchumi na takwimu kwa ajili ya kuimarisha utafiti na uchambuzi wa sera na masuala ya kiuchumi na kijamii;

- Kuendeleza juhudi za kuelimisha wananchi kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuandaa programu za kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini 2004/2005 - 2006/2007;

- Kubuni na kuchambua fursa za kukuza uchumi katika sekta mbalimbali kwa lengo la kupendekeza vipaumbele katika matumizi ya rasilimali za Taifa;

- Kubaini na kuainisha fursa na vivutio katika Mikoa kwa lengo la kuvutia na kuendeleza uwekezaji;

- Kuendeleza ufuatiliaji wa karibu wa utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa ili kubaini mafanikio na matatizo wanayopata wawekezaji katika mashirika hayo na kutoa ushauri;

- Kuendelea kuchambua, kuchapisha na kusambaza taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002. Aidha, programu za kuendeleza taaluma ya uoanishaji wa masuala ya Idadi ya Watu katika sera na mipango ya kisekta na Wilaya itatekelezwa;

- Kuendelea kusimamia ubinafsishaji wa mashirika yaliyobaki;

- Kuendeleza sekta binafsi kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini;

- Kuendeleza ushirikiano wa kikanda na Kimataifa kwa manufaa ya Taifa;

- Kuratibu uendeshaji wa Tovuti ya Taifa;

- Kuhakikisha kwamba malengo ya Mpango Mkakati yanatekelezwa kwa wakati pamoja na kuzingatia mkataba wa huduma kwa wateja;

- Kuimarisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu ili kutathmini mwenendo wa uchumi na kuwezesha utayarishaji wa sera, mikakati na mipango ya maendeleo; na

- Kuboresha mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera na programu za Mpango wa Muda wa Kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya shilingi 22,651,031,100/= kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa mwaka 2004/2005 kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 14,698,297,800/= ambazo kati ya hizo shilingi 600,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 14,098,297,800/= ni fedha za nje.

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni Sh. 7,952,733,300/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,010,459,642/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,942,273,658/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005**
**Wizara ya Fedha**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, iliyowasilishwa hapa Bungeni leo asubuhi, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa masikitiko na majonzi makubwa, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wote wanaohusika kutokana na kuwapoteza Wabunge wenzetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi. *Amina.*

Aidha, ninawapa pole sana Waheshimiwa Wabunge waliopata matatizo ya ajali na ya kushambuliwa na majambazi wakati wakiwa safarini kuja Dodoma kwa ajili ya Kikao cha Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge wa Jimbo la Tunduru, kwa jinsi mlivyoendesha kwa ufanisi mijadala ya bajeti ya mwaka

2004/2005, tangu majadiliano yalipoanza tarehe 14 Juni, 2004. Aidha, ninashukuru sana kwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati zote za Kudumu za Bunge katika kuchambua mapendekezo ya bajeti za Wizara, Idara na Mikoa. Shukrani za pekee ninazitoa kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kwa ushauri na mapendekezo waliyotoa kwa Wizara yangu. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali inathamini sana michango yao na tutayafanyia kazi ipasavyo maagizo na mapendekezo yaliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya Wizara yangu ambayo ni kusimamia masuala yote ya fedha na mali za umma, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa ujumla hali ya utekelezaji imekuwa ni ya kuridhisha licha ya ukame uliotokea mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya wizara yangu ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2003/2004 na malengo yetu kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuimarisha mfumo wa kuandaa Bajeti unaozingatia Mpango wa Upeo wa Miaka Mitatu unaoitwa *"Medium Term Expenditure Framework - MTEF"*. Mafunzo juu ya utumiaji wa mfumo huu yaliyotolewa kwa Mikoa na Halmashauri za Wilaya yaliwawezesha kutayarisha bajeti zao kwa ufanisi zaidi. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa wadau wote kwa lengo la kuimarisha mfumo huu ambao una ufanisi mkubwa katika kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeweka mkakati wa kufuatilia utekelezaji kuhakikisha kwamba mipango, malengo na matarajio yaliyoidhinishwa na Bunge yanafanikishwa. Katika mwaka 2004/2005, mbali na kusimamia nidhamu katika makusanyo ya mapato, matumizi ya fedha na madeni, Wizara yangu pia imedhamiria kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti. Ufuatiliaji makini na uhakiki wa mara kwa mara wa utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye Bajeti *(Expenditure Tracking)* utafanyika kwa lengo la kuhakikisha matumizi ya fedha yanaleta matokeo yaliyokusudiwa na yanafikiwa kwa ubora uliotarajiwa *(value for money).* Wizara yangu itaimarisha na kutumia Kitengo chake cha Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi *(Technical Audit Unit)* kwa lengo hilo. Wizara yangu itaendelea pia kuimarisha uwezo wa Watumishi wote wanaohusika na utekelezaji wa mkakati huu kwa kuwapa mafunzo ya kuongeza ujuzi wa kinadharia na vitendo katika nyanja za ufuatiliaji miradi, ukaguzi, mawasiliano ya tekinolojia na usimamizi wa masuala ya Zabuni za vifaa na ujenzi.

Wizara yangu inao mwanzo mzuri wa kuimarisha mkakati wa *Expenditure Tracking,* ambapo Kitengo hicho cha Ukaguzi wa Miradi kwa mwaka 2003/2004, kimefanya ukaguzi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Umma kwenye Halmashauri za Wilaya 24, Ofisi za Tawala za Mikoa sita na ukaguzi wa kina kwenye miradi mitatu ya barabara katika Mkoa wa Lindi. Baadhi ya matatizo ya utekelezaji yaliyoainishwa ni pamoja na:

- Utekelezaji wa kazi kutozingatia ratiba iliyopangwa;

- Gharama za miradi kuongezeka sana ukilinganishwa na gharama za miradi wakati wa kuanza;

- Upungufu au ukosefu wa vitendea kazi, kama magari, kwa ajili ya usimamizi wa miradi;

- Ubora wa kazi kuwa hafifu; na

- Kutofuata na kutokuelewa vizuri taratibu za zabuni, hivyo kuchelewa kumpata mzabuni kwa wakati.

Kutokana na taarifa za ukaguzi, Halmashauri za Wilaya na Tawala za Mikoa wameshauriwa na kuelekezwa kuhusu maeneo ambayo yanatakiwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kazi za kufuatilia matumizi zitaimarishwa mwaka 2004/2005. Katika jukumu la kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Wizara imeweka mkazo katika kuhakikisha kwamba sera na malengo yanayoridhiwa na Bunge lako kuhusu mapato, matumizi na madeni yanafanikishwa kwa kiwango kilichotarajiwa. Katika mwaka 2004/2005 Wizara ya Fedha imetenga bajeti ya kutosha kufuatilia utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba yangu ya Bajeti ya Serikali ya mwaka huu, nililitaarifu Bunge lako tukufu kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani katika mwaka 2003/2004, uliridhisha na tumeweza kuvuka malengo kila mwezi. Wastani wa mapato yaliyokusanywa ilikuwa Sh. bilioni 121.6 kwa mwezi mwaka 2003/2004 ikilinganishwa na Sh. bilioni 101.5 mwaka 2002/2003. Takwimu za awali zinaonyesha kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani hadi Juni, 2004 yalifikia shilingi bilioni 1,459.3 ambapo tumevuka lengo lililorekebishwa la shilingi bilioni 1,400.6 kwa asilimia nne. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza sana wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kazi nzuri wanayofanya. Serikali itaendelea kuimarisha juhudi za kusimamia mikakati ya kuongeza mapato ya ndani kwa lengo la kupunguza kiwango cha utegemezi wa Bajeti kwa misaada na mikopo kutoka nje. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vyote kwa ufanisi na kwa kuzingatia sheria na mikakati niliyoieleza katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Mamlaka ya Mapato Tanzania kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani zinaendelea chini ya Mpango wake wa Miaka Mitano *(Corporate Plan).* Kama nilivyoeleza kwenye Hotuba yangu mwaka jana, ofisi zote za Mamlaka za Wilaya zimeanza kutoa huduma zote za kodi isipokuwa za forodha, kuanzia Januari 2004. Idadi ya walipa kodi wakubwa imeongezwa na kufikia 200 kuanzia Julai, 2004. Aidha, sheria zote za kodi zimehuishwa na tunategemea kuwasilisha marekebisho yaliyoainishwa katika kikao cha Bunge lijalo. Utaratibu wa kisasa unaomwezesha mlipa kodi kulipa kodi moja kwa moja kwenye akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania *(Tanzania Intersettlement System)* umeanza kutumika kwa walipa kodi wakubwa kuanzia Aprili,

2004. Utaratibu huu unaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kuondoa usumbufu kwa walipa kodi, kwa kuwawezesha kuhamisha fedha kutoka akaunti zao moja kwa moja kwenda kwenye akaunti ya Benki ya Tanzania. Wakati huo huo, baadhi ya hatua za mapato nilizotangaza mwezi Juni, 2004 katika Hotuba ya Bajeti zimeanza kutekelezwa kama ifuatavyo:-

- Sheria ya Kodi ya Mapato Namba 11 ya 2004 ambayo inaanzisha utaratibu wa walipa kodi kujikadiria kodi *(Self Assessment System)* imeanza kutumika kwa walipa kodi wakubwa kuanzia Julai mosi, 2004. Tayari wafanyakazi 236 wa Mamlaka ya Mapato wamepata mafunzo kuhusu matumizi ya sheria mpya.

- Ukaguzi wa mizigo baada ya kuwasili nchini *(Destination Inspection),* pamoja na matumizi ya chombo kiitwacho *scanner,* chenye kuweza kupiga picha za mizigo ndani ya kontena umeanza Julai 1, 2004. Mizigo yote ya kontena imetengwa katika makundi ya rangi tatu yaani nyekundu, njano na kijani. Mizigo ya kundi la rangi nyekundu itakaguliwa kwa *scanner* pamoja na kufunguliwa *(Physical Verification)*, rangi ya njano itakaguliwa kwa kutumia *scanner* na ya kundi la rangi ya kijani itaachiwa mara moja baada ya kulipia kodi zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani chini ya Mpango wa Miaka Mitano wa Mamlaka ya Mapato kwa mwaka 2004/2005 ni pamoja na:-

- Kuendelea kuboresha na kuimarisha usimamizi wa forodha *(modernization of customs administration);*

- Kutoa mafunzo kwa walipa kodi;

- Kukamilisha mkataba wa huduma kwa walipa kodi;

- Kuboresha na kurahisisha sheria za kodi; na

- Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi wa Malamlaka kwa kutoa mafunzo, vifaa na kuboresha mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2003/2004, Bodi ya Rufaa za Kodi ilipokea rufaa 63 zilizohusu kodi ya Mapato, Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na Ushuru wa Forodha. Rufaa 42 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Kwa upande wa Baraza la Rufaa za Kodi kwa mwaka 2003/2004, rufaa 21 zilitolewa maamuzi. Katika mwaka 2004/2005, Bodi na Baraza zitaendelea kusikiliza na kutoa maamuzi kwa malalamiko mapya yatakayopokelewa. Wakati huo huo, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzisha utaratibu wa kukutana na walipa kodi kwa lengo la kujenga maelewano na mahusiano mazuri.

Mkutano wa kwanza ulifanyika tarehe 19 Machi, 2004 na ulishirikisha wadau kutoka sekta za madini, kilimo, fedha, viwanda, mafuta, pamoja na asasi za uhasibu, mashirika yasiyo ya kiserikali, na Kituo cha Uwekezaji *(TIC).* Mkutano huu unafanyika

mara mbili kwa mwaka kwa wajumbe wote na mara nne kwa mwaka kwa wajumbe wa kamati ya utendaji. Aidha, Mamlaka imeanzisha kamati za maadili makao makuu na ofisi za mikoani ambazo zinafuatilia malalamiko ya walipa kodi na kutoa taarifa za utekelezaji kila mwezi kwenye Ofisi ya Rais, Kitengo cha Utawala Bora. Mwaka 2004/2005, Mamlaka imepanga kuanzisha kituo kimoja *(One Stop Centre)* chenye kupokea na kushughulikia malalamiko yote ya walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Bodi na Baraza zitaendelea na zoezi la kutoa elimu kwa wadau wa kodi husika kuhusu taratibu na sheria zinazohusu ufunguaji na uendeshaji wa rufaa za kodi katika Bodi na Baraza hadi Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Wizara itaimarisha uwezo wa watumishi wa Bodi na Baraza kwa mafunzo mbalimbali ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mapato ya nje, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu ililenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kusimamia Misaada kwa Tanzania *(Tanzania Assistance Strategy - TAS)* kwa kuweka mkazo katika kuwianisha mifumo ya wahisani ya kutoa misaada *(Aid Harmonization),* pamoja na kuongeza uhakika wa kupata misaada yenyewe *(Aid Predictability);*

(b) Kuboresha na kuimarisha kumbukumbu za misaada ili kupata takwimu sahihi za misaada na kuongeza kiwango cha misaada inayohasibiwa kwa kutumia mfumo wa Serikali;

(c) Kulipa kwa wakati michango ya Serikali kwenye Mashirika ya Kimataifa ambako Tanzania ni mwanachama; na

(d) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi katika kusimamia na kuratibu misaada na mikopo nafuu na katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu kutoka nje ya nchi kwa kutekeleza Mkakati wa Misaada Tanzania ambao unalenga kupunguza urasimu na gharama zisizo za lazima katika utoaji wa misaada na pia kutoa nafasi kwa Serikali kusimamia matumizi ya mikopo hiyo. Majadiliano kati ya Wafadhili na Serikali kuhusu utaratibu huo umeonyesha mafanikio kwa kuimarisha zaidi imani ya Wafadhili kwa Serikali ya Tanzania. Matokeo ya mafanikio hayo ni pamoja na kuvukwa kwa malengo ya upatikanaji wa fedha walizochangia Wafadhili hasa kwenye Bajeti *(General Budget Support)* ambapo kiasi kikubwa kilipatikana katika nusu ya mwanzo ya mwaka 2003/2004. Malengo ya mwaka 2004/2005, ni pamoja na kuendelea na majadiliano na Wafadhili kuhakikisha kuwa Serikali inamiliki kwa uhakika zaidi maendeleo ya nchi yetu kwa kuelekeza misaada na mikopo kwenye miradi na programu za kipaumbele, ili kuchangia katika kukuza uwezo wetu wa kuboresha uchumi, kuendelea kuwashawishi wafadhili kufuata taratibu zilizoainishwa katika Mkakati wa Misaada Tanzania *(TAS),* pamoja na kuanza kuandaa mkakati wa pamoja wa misaada *(Joint Assistance Strategy)* badala ya kila mfadhili kuwa na mpango wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika hatua zote za kukamilisha Hati ya kuanzisha Umoja wa Forodha *(Protocol for the Establishment of Customs Union)* kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hati hiyo ilisainiwa na Wakuu wa nchi hizo tarehe 2 Machi, 2004 Mjini Arusha. Kwa mujibu wa Hati hiyo, kutakuwa na viwango sawa vya ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoagizwa toka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali kadhalika, ushuru wa bidhaa kutoka Kenya kuingia Tanzania utaondolewa polepole hadi kufikia kiwango cha asilimia sifuri ndani ya miaka mitano, kuanzia wakati Hati hiyo itakapoanza kutumika mapema mwaka ujao. Hata hivyo, biashara baina ya Tanzania na Uganda itakuwa kwa kiwango cha asilimia sifuri mara Hati itakapoanza kutumika. Inatarajiwa kwamba, matokeo ya ushirikiano huu yatawezesha kupanua soko la bidhaa za Tanzania, kuongeza biashara pamoja na kuvutia uwekezaji na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kuchochea maendeleo katika upunguzaji wa umaskini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Wizara zingine, Wizara yangu itaimarisha ushiriki wake katika mikutano yote ya kikanda na kimataifa hususan katika masuala ya fedha pamoja na kufanya tathmini za pamoja kati ya Serikali na Wafadhili kwa lengo la kuboresha ufanisi na manufaa ya ushirikiano kati ya Serikali, Nchi Wafadhili na Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kutumia utaratibu wa *Cash Budget* katika kudhibiti matumizi ya Serikali, na kuhakikisha fedha zinazopatikana zinatumika tu kwa kazi zilizokusudiwa kwenye *MTEF.* Utaratibu huu, umechangia sana kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha kwa ujumla kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha, kulingana na Bajeti iliyopitishwa na Bunge. Hata hivyo, kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani na wafadhili kutoa sehemu kubwa ya misaada yao mapema, Sekta za kipaumbele katika kupunguza umaskini zimekuwa zikitengewa fedha kwa mahitaji ya kila robo mwaka kulingana na taarifa za utekelezaji kwa robo iliyopita.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imeendelea kuimarisha na kueneza utumiaji wa mtandao wa kompyuta wa kutayarisha bajeti na kufanya malipo *(IFMS).* Mtandao huo unahakikisha kwamba matumizi yanazingatia Bajeti iliyopitishwa na Bunge na kwamba, ubadhirifu unabainishwa kwa haraka na uhakika zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya mtandao huo. Kwa mfano, matukio ya wizi yaliyotokea Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara ya Magereza yalibainishwa kwenye mtandao. Aidha, kuna matukio kadhaa ambayo yamebainishwa na kudhibitiwa kabla ya fedha kuibwa. Baada ya kuweka mtandao huu kwa Maafisa Wahasibu wote wa Wizara na Idara zinazojitegemea, Wizara yangu sasa imeweka mtandao huo katika kila Ofisi za Katibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara. Katika mwaka wa 2004/2005, Wizara yangu itaimarisha mtandao huo kwa kufunga vifaa vitakavyotumika kwa tahadhari pindi mtandao uliopo ukipata matatizo *(Disaster Recovery Site).* Lengo ni kunusuru kumbukumbu na shughuli za malipo na usimamizi wa fedha za Serikali zisikwame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa madeni katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara yangu ilianza kutekeleza marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 yaliyopitishwa na Bunge lako katika kikao chake cha Aprili, 2003. Katika mwaka 2003/2004, Kamati ya Kusimamia Mikopo, Dhamana na Misaada imechambua mapendekezo 31 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,154.08 na kupendekeza mikopo 12 yenye thamani ya shilingi bilioni 154.6. Mikopo hii ni kwa ajili ya miradi kwenye sekta za mawasiliano na usafirishaji, nishati, elimu na maji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Mwaka 1974 ikijumuisha:-

(a) Kutafuta mikopo kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu na kuielekeza kwenye maeneo muhimu ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini;

(b) Kuendelea kusitisha udhamini wa Serikali kwa mikopo toka nje na kuweka mamlaka pekee ya kukopa kwa Waziri wa Fedha, baada ya kushauriwa na Kamati ya Kusimamia Madeni; na

(c) Kuendelea kufanya mazungumzo na nchi za kundi la Paris na zile zisizo katika kundi la Paris ili kupata misamaha ya madeni chini ya mpango wa Msamaha wa Madeni kwa Nchi Masikini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoliarifu Bunge wakati wa Bajeti ya Serikali ya mwaka uliopita, Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission - JFC)* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tume hii imeanza kazi na imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na utekelezaji wa Masuala ya Muungano, na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mgawanyo kwa kila mojawapo ya Serikali hizo;

(b) Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za kifedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano wa mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili; na

(c) Kutekeleza majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, kati ya kazi za uanzishaji wa Tume zilizoshughulikiwa ni pamoja na kupata Ofisi za Tume, vifaa na vitendea kazi kwa Tanzania Bara na Zanzibar, kutayarisha muundo wa utumishi na kukamilisha mipango ya kuazima watumishi toka Utumishi wa Umma. Hivi sasa Tume inaandaa Kanuni za Utumishi *(Staff Regulations)* na Kanuni za Fedha *(Financial Regulations)*. Inatarajiwa Tume itaanza kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa matakwa ya sheria mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, wizara yangu imeendelea kusimamia na kuendeleza mafunzo ya Sheria ya Fedha za umma ya mwaka 2001. Mafunzo yametolewa kwa Watendaji mbalimbali walioko chini ya Maafisa Wahasibu nchini. Aidha, katika mwaka huo Wizara yangu iliandaa na kukamilisha miongozo ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani *(Accounting and Internal Audit Manuals).* Vilevile, katika jitihada za kuongeza usimamizi na utawala bora katika sekta ya Fedha, Wizara yangu ilielekeza Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa iunde na iwasilishe Hazina, Kamati za Ukaguzi *(Audit Committees)* kama inavyotamka Sheria ya Fedha ya mwaka 2001. Tunafurahi kueleza kuwa karibu Wizara, Idara na Mikoa yote imetimiza sharti hilo na hii ni dalili nzuri kuelekea kwenye usimamizi bora wa fedha za umma. Tunatarajia kuendesha mafunzo kuhusu Mwongozo wa Uhasibu kwa wadau 1,300. Wadau 700 watapatiwa mafunzo kuhusu Mwongozo wa ukaguzi wa ndani. Aidha, Wajumbe wa Kamati za Ukaguzi pamoja na wadau 700 watapewa mafunzo juu ya uendeshaji wa shughuli za Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inawajibika kusimamia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2001. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Halmashauri Kuu ya Zabuni iliidhinisha Zabuni 84 zenye thamani ya shilingi milioni 123,892.2.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kurekebisha Sheria ya Ununuzi wa Umma na kutunga sheria mpya ili kujibu malalamiko yaliyojitokeza, kuongeza ufanisi katika manunuzi ya umma, kuimarisha uwajibikaji wa moja kwa moja wa Maafisa Wahasibu kwa kazi za manunuzi, pamoja na kuiachia Halmashauri Kuu ya Zabuni utekelezaji kwa ukamilifu wa jukumu la kusimamia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi. Kwa mwaka huu wa fedha, Wizara yangu inatarajia kufanya yafuatayo:-

(a) Kurekebisha Kanuni za Ununuzi za Mwaka 2001 ili ziwiane na marekebisho ya Sheria;

(b) Kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili kubainisha mkakati wa kudhibiti na kuziba mianya ya rushwa katika ununuzi wa umma;

(c) Kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuanzisha kada ya wataalam wa ununuzi serikalini *(Procurement Cadre);*

(d) Kuandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watumishi wanaoshughulikia ununuzi wa umma, pamoja na watumishi mbali mbali kutoka Taasisi ya Kuzuia Rushwa na ofisi ya Ukaguzi wa Taifa;

(e) Kuajiri wataalam wa kutosha na wenye sifa mwafaka ili kutekeleza majukumu yake; na

(f) Kubuni, kuandaa na kuweka mfumo wa taarifa katika mtandao kwa ajili ya Usimamizi na Uchambuzi wa Zabuni.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kuanzisha Mamlaka ya Rufaa za Zabuni *(Public Procurement Appeals Authority)* ilikamilika mwezi Februari, 2004 kwa uteuzi wa Mwenyekiti wake ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu. Mamlaka hiyo itaanza kazi zake rasmi wakati wowote kuanzia sasa. Majukumu ya Mamlaka hiyo yanajumuisha yafuatayo:-

(a) Kupokea malalamiko dhidi ya maamuzi ya Halmashauri Kuu ya Zabuni na Bodi za Zabuni za Wizara, Mikoa, Wilaya na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji ambazo sasa zitakuwa sehemu ya sheria mpya;

(b) Kusuluhisha migogoro ya zabuni;

(c) Kupokea maoni ya Wazabuni kuhusu taratibu za ununuzi na utoaji wa Zabuni; na

(d) Kuishauri Halmashauri Kuu ya Zabuni kuhusu maeneo ya kufanyia marekebisho ili kupunguza malalamiko ya Wazabuni na ununuzi wa umma kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka inatakiwa kisheria kuchunguza malalamiko na kuyatolea maamuzi katika muda wa siku 30 tangu siku ya kuyapokea. Ni matumaini ya Serikali kuwa kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo kutapunguza malalamiko na mianya ya rushwa katika ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuhakiki Bohari 440 za Serikali ambapo taarifa zake zilipelekwa kwa Maafisa Wahasibu husika na kutoa hoja za Uhakikimali 356 zenye thamani ya shilingi milioni 5,989.3 ambazo zimejumuishwa kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2003;

(b) Kusimamia uundwaji wa Bodi za Ukaguzi 50 *(Boards of Survey)* katika Wizara 22, Idara 9 na Mikoa 19 na hivyo kuidhinisha, kufuta vifaa chakavu na sinzia vyenye thamani ya shilingi milioni 98.2;

(c) Kuidhinisha kufuta na kuuza vifaa chakavu vya Serikali vipatavyo 675 na kukusanya kiasi cha shilingi milioni 406.6 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Pwani, Mtwara, Lindi na Iringa;

(d) Kufanya maandalizi ya kuuza vyombo 1,249 vilivyopo katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mwanza, Shinyanga, Tabora na Tanga. Zoezi la kufuta liliendelea kwa Mikoa iliyosalia; na

(e) Kuendelea na zoezi la kuthamini mali za Serikali katika Wizara nane zikijumuisha Wizara ya Fedha, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Sheria na

Mambo ya Katiba, Ofisi ya Rais - Mipango na Ubinafsishaji, Mambo ya Ndani, Maliasili na Utalii, Elimu na Utamaduni pamoja na Afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara inalenga kufanya yafuatayo:-

(a) Kuhakiki bohari 500 za Wizara, Idara na Mikoa;

(b) Kushauri na kusimamia ufutaji, uondoshaji (kuuzwa/kuharibiwa) mali za Serikali ambazo ni chakavu, sinzia na ziada kwa mahitaji ya Serikali;

(c) Kuthamini mali za Serikali katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Ujenzi, Kilimo na Chakula, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;

(d) Kuteua Bodi za Ukaguzi wa Bohari, kukagua na kuhesabu mali katika Bohari zote za Serikali; na

(e) Kukamilisha utekelezaji wa maamuzi yaliyotokana na taarifa za Bodi za ukaguzi zilizoteuliwa Mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ya Fedha iliendelea kusimamia hisa za Serikali katika mashirika mbalimbali pamoja na taasisi za umma kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 418 *(Treasury Registrar Ordinance - Cap 418)* na Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992. Katika mwaka huo wa fedha, Serikali ilitarajia kupata gawio la shilingi bilioni 10.27 kutoka katika mashirika ambayo bado kuna hisa za Serikali pamoja na marejesho ya mikopo na mapato mengine ya shilingi bilioni 18.4. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2004, mapato yatokanayo na gawio ya kiasi cha shilingi bilioni 8.77 yalipokelewa kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Kampuni ya Bia, Kampuni ya Sigara, *National Bank of Commerce Limited, Mbinga Coffee Curing, Tanzania Central Freight Bureau, Tanganyika Planting Company Limited, Tanzania Development Finance Limited,* Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya Saruji Wazo.

Katika mwaka 2004/2005, mapato kutokana na gawio yanatarajiwa kupungua kutokana na kuendelea kubinafsishwa kwa baadhi ya makampuni. Hata hivyo, kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kunufaika na mapato yatokanayo na kodi zinazolipwa na makampuni mbalimbali yakiwemo yale yaliyobinafsishwa. Kwa mfano, katika mwaka 2003/2004, Serikali imepata kodi kiasi cha shilingi billioni 45.66 kutoka Kampuni ya Sigara Tanzania; shilingi bilioni 96.9 kutoka Kampuni ya Bia Tanzania, shillingi billioni 3.13 kutoka Kampuni ya Saruji Tanzania na shilingi bilioni 7.61 kutoka *National Bank of Commerce.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma

na Wizara mama za mashirika mbalimbali itashiriki kikamilifu katika zoezi la ubinafsishaji wa Sekta ya umma. Lengo, ni kuhakikisha kuwa mashirika hayo hayaendelei kuwa mzigo kwa Serikali na badala yake yanaingiza mapato Serikalini kwa njia ya kodi, gawio na mapato mengine na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi na ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekagua hesabu 47 za Wizara na Idara za Serikali, Mikoa 21, Halmashauri 117 na Ofisi 15 za Ubalozi za Tanzania. Kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi hii imepanga kukagua hesabu 47 za Wizara na Idara za Serikali, Mikoa 21, Halmashauri za Wilaya na Miji 125 na Ofisi za Balozi 15.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha utaalamu wa ukaguzi na udhibiti wa hesabu za Serikali mwaka 2003/2004, mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu yametolewa kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Jumla ya Wakaguzi 333 wamepata mafunzo hayo. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kudhamini watumishi wake wanaochukua mafunzo katika vyuo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi, na kuendesha mafunzo ya ndani kwa watumishi wa ngazi mbalimbali ili kuboresha utendaji wao wa kazi. Aidha, katika juhudi za kuimarisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Serikali imepata ufadhili wa shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya kuimarisha utendaji. Msaada huu utatumika katika kutoa mafunzo na vifaa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliajiri watumishi 70, wakiwemo wahasibu 28. Aidha, watumishi 88 walithibitishwa kazini na 226 walipandishwa vyeo. Wizara itaendelea kuajiri, kuthibitisha kazini na kupandisha vyeo watumishi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi na Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 14 wa mwaka 2002 ambao umeanza kutumika Julai, 2003. Hadi kufikia mwaka 2003/2004, watumishi waliopelekwa kusoma shahada, stashahada za Uhasibu na Utunzaji Bohari ni 734. Kati ya hao, watumishi 290 wanatoka Serikali za Mitaa na 444 wanatoka Serikali Kuu. Watumishi wengine wa Serikali Kuu 292 waliweza kuongeza ujuzi katika kazi zao kwa kuhudhuria kozi za aina mbalimbali zikiwemo Shahada ya Falsafa, Uzamili, Stashahada ya Uzamili na mafunzo ya muda mfupi, kwa lengo la kujiendeleza. Wizara yangu itaendelea na jitihada ya kuboresha mazingira ya fani za Uhasibu na Taaluma ya Matumizi ya Kompyuta *(IT)* ili kuvutia zaidi ajira ya fani hizi serikalini na asasi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM),* Chuo cha Uhasibu Arusha *(IAA)* na Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* vilivyo chini ya Wizara yangu, vimeendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wanaofadhiliwa na Serikali, Waajiri mbali mbali na wanaojilipia wenyewe. Katika mwaka wa 2003/2004, Vyuo hivi vimetoa wahitimu katika fani mbalimbali wapatao 1,449. Pia vinatarajiwa kutoa wahitimu 2,076, mwaka 2004/2005 na wahitimu 3,155 katika mwaka 2005/2006. Ni matarajio yangu kuwa, utendaji kazi Serikalini, hususan katika fani za uhasibu na uboharia utaimarika kufuatia kuhitimu kwa watumishi hao. Aidha, Wizara yangu inayo matumaini kuwa asasi za serikali, Halmashauri za Jiji, Miji na Wilaya na Mashirika ya Umma na binafsi

zitaweza kuwaajiri wahitimu hao wenye sifa zinazotakiwa hususan Watarajali *(Pre-Service).* Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilitoa udhamini kwa wanafunzi 1,233 ambao kati yao 814 walikuwa watarajali. Wizara imepanga kudhamini wanafunzi 1,787 mwaka 2004/2005. Aidha, mwaka 2004/2005, Wizara itachukua hatua ya kuviimarisha vyuo ili vipanue nafasi za wanafunzi wapya na kuboresha wahitimu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi bora na sahihi ya kompyuta ni muhimu katika kuendeleza na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu, na utoaji taarifa mbalimbali kwa wakati muafaka. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau wengine iliendeleza Sera ya Taifa kuhusu Teknolojia ya Mtandao wa Habari na Mawasiliano, kwa kuanzisha mtandao ili kurahisisha mawasiliano ndani na nje ya Wizara na Idara za Serikali. Aidha, Wizara iliendelea kuweka kumbukumbu na kusahihisha taarifa za watumishi wa Serikali na kuboresha mfumo wa malipo kwa kupitia mtandao. Mfumo huu umesaidia kuboresha malipo ya Serikali.

Wizara kwa kutambua mchango mkubwa wa teknolojia ya kompyuta, katika mwaka wa fedha 2004/2005, itahakikisha ubora na usalama wa njia hii ya mawasiliano na utunzaji kumbukumbu ili kuweza kupata taarifa kwa wakati kwa nia ya kufanya chambuzi za kiuchumi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA),* inayo majukumu ya kukuza, kusimamia na kuendeleza fani ya Uhasibu hapa nchini. Katika mwaka 2003/2004, malengo ya Bodi yalijumuisha yafuatayo: -

(a) Kutoa ushauri serikalini kuhusu mfumo wa kodi na kuendesha semina na warsha kwa wananchi kuhusu masuala ya kodi;

(b) Kuhakikisha utoaji wa miongozo mbalimbali kwa wanataaluma; na

(c) Kuendeleza ushirikiano na vyombo vingine vya Kimataifa kuhusu masuala ya kileo ya kihasibu na ukaguzi wa hesabu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Bodi iliendelea kutoa kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu utunzaji na ukaguzi wa mahesabu. Bodi itaendelea kufanya utafiti wa kina mara kwa mara ili kwenda na wakati sambamba na mabadiliko ya teknolojia. Aidha, Bodi imeamua kuridhia miongozo ya kiuhasibu na ukaguzi hesabu katika viwango vya kimataifa kama nchi nyingine zinavyofanya ikiwa ni pamoja na Kenya na Uganda kwa lengo la kuiwezesha taaluma nchini iendane na utandawazi na kuweka misingi ya utawala bora. Bodi imeendelea kuimarisha ushirikiano wake na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu *(IFAC)* na Shirikisho la Muungano wa Kihasibu linalojumuisha Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika *(ECSAFA)* pamoja na kuwa mjumbe wa Shirikisho hilo na Baraza la Uongozi wa *IFAC.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Bodi itaendelea na majukumu hayo pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la Kitengo cha Mafunzo ya Uhasibu *(The*

*Accountancy Education Centre)* ili kuongeza ufanisi na tija katika usimamizi wa uhasibu na ukaguzi wa mahesabu.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kudhibiti malipo ya mishahara ya Watumishi wa Serikali, Waraka wa Hazina Na. 12 wa mwaka 2004 umetolewa kwa Maafisa Wahasibu wote ili kusisitiza zaidi majukumu yao, na kuwakumbusha kuhusu wajibu wao wa kusimamia masuala yote yanayohusiana na marekebisho ya mishahara ya Watumishi na kushughulikia marekebisho hayo kwa wakati. Lengo la Waraka huu ni kuhakikisha malipo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali yanafanyika ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi kama ilivyopangwa na Serikali na wakati huo huo kuhakikisha kuwa mianya ya ubadhilifu katika mishahara inadhibitiwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti mbinu za wizi kupitia malipo ya mishahara ya Watumishi, Serikali imeweka utaratibu mpya utakaotumika kushughulikia marekebisho na madeni ya mishahara ya Watumishi wake. Utaratibu huo mpya ambao pia umeelezwa katika Waraka wa Hazina Na. 12 wa mwaka 2004, unawataka Maafisa Wahasibu wenyewe kuhusika na jukumu la kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi na kisha kuwasilisha madai hayo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ambayo inawajibika kuyawasilisha Hazina kwa malipo.

Mheshimiwa Spika, Baadhi ya watumishi wa Serikali wameendelea kupokea mishahara yao kupitia Benki. Mpaka sasa Wizara 24 na Idara 17, Mikoa minne na Halmashauri 41 zinahusishwa. Tathmini iliyofanyika kuhusu utaratibu huu imedhihirisha kwamba, watumishi wa serikali wameanza kujenga mazoea ya kuweka akiba benki. Katika mwaka 2004/2005 Wizara ina lengo la kuendeleza utaratibu huu kwa Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri zilizosalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa la watumishi wapya kutolipwa mishahara mapema hali ambayo imeleta kero kubwa ya madeni ya mishahara na hasa kwa upande wa walimu. Ili kutatua tatizo la malimbikizo ya mishahara, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetoa Waraka wa Hazina Na. 12 wa mwaka 2004. Lengo la Waraka huu ni kuimarisha udhibiti, uwajibikaji na kuhakikisha kwamba wenye madai halali tu ndiyo wanalipwa, madai ya watumishi yanashughulikiwa haraka na Waajiri wenyewe kwenye vituo vyao vya kazi kwa kujaza Fomu za madai zinazohusika. Hatua hiyo itawezesha Waajiri kupata madai ya Walimu na watumishi wengine kwa haraka zaidi na kuyawasilisha madai hayo mapema katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na hatimaye Hazina kwa malipo. Ili kurahisisha utekelezaji wa waraka huu maofisa toka Wizara ya Fedha na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Elimu wameanza kuendesha semina za kikanda kwa Maafisa wa Seirikali Kuu na wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Aidha, kwa upande wa madai yasiyo ya mishahara, tumeweka mkakati wa kukusanya na kuhakiki madai yote ya Waalimu na watumishi wengine wa Serikali, ili yaweze kulipwa. Mkakati utakaotumika utahusisha timu ya wataalam toka Wizarani na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambayo itaungana na

wataalam wa Halmashauri za Wilaya na Miji. Tunatarajia kwamba zoezi hili la kukusanya na kuhakiki madeni yaliyolimbikizwa litakamilika katika muda wa miezi miwili kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Kero ya Rushwa katika Wizara yangu *(Sector Specific Anti-Corruption Strategy and Action Plan)* kama sehemu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Kero ya Rushwa *(National Anti-Corruption Strategy and Action Plans - NACSAP).* Mapambano hayo yameelekezwa katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato *(Tax Administration)*, usimamizi wa matumizi *(Expenditure Management and Control),* uratibu wa misaada kutoka nje *(Aid Co-ordination),* pamoja na ununuzi wa umma *(Public Procurement).*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inayo wafanyakazi 960. Wanawake Viongozi ni 15 ambao ni sawa na asilimia 37.5 ya viongozi wote 40 walioko Makao Makuu. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imeendelea na jitihada za kuzingatia masuala ya jinsia *(Gender Mainstreaming)* katika utayarishaji wa sera na bajeti ya Serikali. Kazi maalum ya kuainisha njia za uchambuzi inaendelea katika Sekta ya Afya na Elimu ambayo matokeo yake yatasaidia kutayarisha mwongozo juu ya uainishaji wa masuala ya jinsia katika kutayarisha bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imeendelea na jitihada za kuhamasisha wafanyakazi juu ya athari ya ugonjwa wa UKIMWI Semina zilifanyika ili kuleta uelewa zaidi juu ya ugonjwa huu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *UNDP* na *TACAIDS* imefanya tathmini kuainisha mazingira ya kujua mambo yanayosababisha maambukizi ya ugonjwa huu kwa wafanyakazi na hatua ambazo zitapaswa kuchukuliwa katika kudhibiti, kutibu na kuwasaidia wale walioathirika na ugonjwa huu. Katika mwaka wa 2004/2005, hatua zitachukuliwa kutekeleza mapendekezo ya tathimini hii. Vile vile, hatua za dhati zitachukuliwa kuwapatia wafanyakazi uelewa zaidi wa kujikinga na ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kutoa semina na kuwasaidia walioathirika kwa kuwapatia huduma muhimu zikiwa ni pamoja na dawa za kurefusha maisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kuimarisha huduma ya pensheni kwa wastaafu na kulipa mirathi. Jitihada zimefanywa ili kuboresha zaidi uwekaji wa kumbukumbu za wastaafu hasa katika kufanya maandalizi na mikakati ya kuhakikisha tatizo hili linapata ufumbuzi wa kudumu, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi, hasa kompyuta, kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi.

Hatua nyingine iliyochukuliwa ni ushirikishwaji zaidi wa wadau mbali mbali hususan Taasisi za Walimu, na Asasi za Ulinzi na Usalama katika ufuatiliaji wa kumbukumbu za utayarishaji wa malipo kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu imelipa mafao kwa wastaafu 1,423 yenye thamani ya shilingi bilioni 23.8. Wizara pia imelipa madai ya mirathi 1,168 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.7. Aidha, wastaafu 33,719

wamelipwa pensheni zao za mwezi zenye thamani ya shilingi bilioni 9.3 kwa utaratibu wa malipo ya kila baada ya miezi sita. Wizara yangu itaendelea na jitihada za uboreshaji wa huduma kwa wastaafu katika mwaka wa fedha 2004/2005. Uboreshaji huo utalenga kupunguza kero zinazowakabili wastaafu katika kufuatilia mafao yao. Waajiri wao ndiyo watakaowajibika kufuatilia mafao badala ya wastaafu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Januari, 2005, Serikali itaanza kulipa pensheni kwa wastaafu waliolipwa pensheni zao miaka ya nyuma kwa mkupuo. Uamuzi huu unawahusu wale wastaafu ambao wamefikisha miaka kumi kutoka siku walipostaafu. Vile vile, uamuzi huu unawahusu watumishi wa Serikali waliostaafishwa kwa manufaa ya umma, lakini pensheni yao ilikuwa haizidi shilingi 36,000/= kwa mwaka. Wastaafu wa kundi hili walilipwa pensheni yao yote wakati wanapewa barua za kustaafishwa na ambao wakati wanastaafishwa walikuwa kwenye masharti ya ajira ya kudumu *(Permanent and Pensionable)* na walikuwa wametimiza miaka kumi au zaidi kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, urejeshwaji kwenye daftari utategemea ni lini mstaafu alistaafu kazi na kwa maana hiyo watakaorejeshwa mwaka huu ni wale waliostaafu mwaka 1993/94 na kurudi nyuma. Aidha, wale waliostaafu 1994/95 watarejeshwa mwaka wa fedha ujao na kuendelea hivyo hivyo. Kwa mara ya mwisho Serikali ililipa malipo ya pensheni kwa mkupuo mwaka 2001/2002. Utaratibu huu wa kuwarudisha wastaafu kwenye daftari utaendelea hadi mwaka wa fedha 2010/2011 ambapo wale wote waliowahi kuchukua mkupuo watakuwa wamerejeshwa kwenye daftari la malipo ya wastaafu, kwa utaratibu “wa kwanza, kwanza na wa mwisho, mwisho”.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwarejesha wastaafu kwenye daftari, imebidi tufanye utaratibu wa kuwahakiki na kuwatambua wale wote ambao walijiandikisha. Malipo ya kwanza ya wastaafu hawa yanategemewa kufanyika Januari, 2005 ikiwa ni majumuisho ya miezi sita, kama utaratibu ulivyo hivi sasa. Utaratibu huu wa malipo ya pensheni ya miezi sita uliwekwa baada ya kupata malalamiko mengi kutoka kwa wastaafu kwamba gharama ya kufuatilia pensheni ya kila mwezi ilikuwa kubwa kuliko pensheni yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF),* ulianzishwa chini ya Sheria ya Akiba ya Wafanyakazi Serikalini Sura ya 51 ya mwaka 1942 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria Namba 52 ya mwaka 1965 kwa ajili ya wafanyakazi wa Serikali ambao Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma haiwahusu. Wafanyakazi hao ni pamoja na watumishi wa ngazi ya chini *(Operational Service Staff),* watumishi wanaofanyakazi kwa mikataba na askari polisi na magereza walio chini ya cheo cha Inspekta Msaidizi na wale ambao hawajafanya kazi kwa zaidi ya miaka 12. Tangu uanzishwe, Mfuko umekuwa chini ya Idara ya Pensheni Hazina na baadaye chini ya uangalizi wa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma *(PSPF)* hadi mwezi Julai, 2004 ambapo menejimenti ya Mfuko ilipoteuliwa na kuanza kazi. Kuanzia Julai, 2004, *GEPF* inafanya kazi kama Mfuko unaojitegemea chini ya Bodi ya Wakurugenzi. Kazi za Mfuko ni pamoja na kukusanya michango ya wanachama, kuziwekeza katika dhamana za Serikali na vyanzo vingine vinavyotoa riba kubwa, kutoa mikopo nafuu kwa wanachama

na kuwalipa wanachama mafao yao pale wanapostaafu, kufukuzwa au kumaliza mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, michango ya mfuko ilikadiriwa kufikia shilingi bilioni 14.232. Hata hivyo, kiasi kilichofikiwa ni shilingi bilioni 14.054 ikiwa ni sawa na asilimia 98.8 ya malengo. Mapato yatokanayo na uwekezaji yalikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi milioni 490.0 ambapo mapato halisi yalifikia shilingi milioni 712.0 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 45 ya malengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, thamani ya Mfuko inakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 16.317 sawa na ongezeko la asilimia 16 ikilinganishwa na mwaka 2003/2004. Kwa upande wa mapato yanayotokana na uwekezaji, lengo ni kufikia shilingi billioni 1.0902 sawa na ongezeko la asilimia 53 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Pamoja na mambo mengine, katika mwaka 2004/2005, Mfuko unatarajia kujiimarisha chini ya Menejimenti mpya kwa kuandaa Mpango wa Muda Mrefu, Sera ya Uwekezaji na kukamilisha miongozo ya utawala na fedha.

Mfuko huu ambao ni mkongwe kuliko Mifuko yote ya hifadhi ya jamii, umekuwa haufahamiki hata ndani ya Serikali Kuu yenyewe Mambo muhimu ambayo mfuko umekuwa ukifanya kwa sasa ni pamoja na:-

(a) Kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanachama wake ili kulipia gharama muhimu kama vile matibabu, elimu, mazishi, na kuanzisha miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za kuishi; na

(b) Kuwalipa wachangiaji riba kila mwaka kulingana na mapato ya Mfuko.

Kwa kipindi cha mwaka 2004/2005, Mfuko umetenga kiasi cha shilingi milioni 200.0 kwa ajili ya mikopo hiyo. Kiasi hiki cha pesa kitaongezeka kila mwaka kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma uliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusajili, kuhifadhi kumbukumbu sahihi za wanachama wake, kukusanya michango na kuiwekeza. Aidha, Mfuko umetoa vitambulisho maalum kwa wastaafu ambavyo vinatarajiwa kupunguza uwezekano wa kugushi malipo ya pensheni. Vitambulisho hivi vinamtambua mstaafu kwa alama ya dole gumba, picha, pamoja na sahihi yake. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Mfuko ulikusanya kiasi cha shilingi bilioni 62.079 na kufanya jumla ya michango yote iliyokusanywa tangu kuanzishwa kwake kuwa shilingi bilioni 238.05.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu wa nyaraka zinazotakiwa kwa ajili ya usajili na kumbukumbu nyingine muhimu bado limeendelea kujitokeza lakini Mfuko umeendelea kuwasiliana na waajiri ili kutatua tatizo hili, hasa kwa kuhifadhi kumbukumbu zote za wanachama wake katika mfumo wa kompyuta.

Mheshimiwa Spika, Mfuko, kisheria unatakiwa kuanza kulipa mafao kwa wastaafu kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 ambapo wanachama 1,995 wanatarajiwa kustaafu na kulipwa mafao yao kiasi cha shilingi bilioni 34. Maandalizi yanayohitajika yamekwisha kamilika. Aidha, Mfuko umeteua benki za *NMB, CRDB, Standard Chartered* na Shirika la Posta kama wakala wa kulipa pensheni za wastaafu za kila mwezi. Hatua hii imechukuliwa ili kurahisisha ulipaji wa mafao na kuwawezesha wastaafu kupata fedha zao karibu na huko waliko.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 44.3 mwaka uliopita ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi bilioni 45.1 kwa mwaka 2002. Upungufu huu wa asilimia mbili unatokana na kupungua kwa michango ya wanachama kutokana na zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yameongezeka kwa asilimia 13 kutoka shilingi bilioni 9.4 kwa mwaka 2002 hadi shilingi bilioni 10.6 katika mwaka 2003. Ongezeko hili katika mapato limewezesha Mfuko kulipa mafao kiasi cha shilingi bilioni 16.7 katika mwaka wa 2003 ikilinganishwa na shilingi bilioni.14.3 zilizolipwa mwaka 2002 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.8.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 15.5 kutoka shilingi bilioni 128.0 hadi shilingi bilioni 147.8 mwishoni mwa mwaka 2003. Katika kuboresha utoaji wa huduma, Mfuko umefungua ofisi katika kanda nne yaani - Mbeya, Mwanza, Arusha na Dar es Salaam. Katika mwaka 2004, Mfuko utaendelea kutekeleza mpango wake wa miaka mitano (2003 - 2007) wa kuandikisha wanachama zaidi kutoka katika sekta isiyo rasmi, kuongeza wigo wa uwekezaji wenye manufaa zaidi kwa wanachama wake na kuimarisha mafao yenye kukidhi haja za wanachama.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera ya uwazi na ukweli Wizara yangu mwaka uliopita ilianzisha kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ili kuelimisha umma kwa njia ya habari zinazohusu sera na majukumu ya Wizara. Katika mwaka 2003/2004, Kitengo kilifanikisha uandaaji wa mikutano ya Wizara na vyombo vya habari iliyohusu ufafanuzi wa mambo mbali mbali ndani ya sekta ya fedha. Aidha, kilisambaza nyaraka muhimu kwa wadau zilizoelezea matukio muhimu katika sekta ya fedha na kufuatilia katika vyombo vya habari kero zilizojitokeza. Katika hatua za kuboresha mawasiliano na umma, Wizara imezindua Tovuti *(Website)* ya Wizara *www.mof.go.tz* tarehe 29 Julai, 2004. Kwa hiyo, hotuba yangu inapatikana kwenye tovuti hii. Aidha, tutaanzisha Jarida *(News Letter)* la Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kutumia utaratibu wa kutoa taarifa katika vyombo vya habari kila robo mwaka zikibainisha fedha zilivyotolewa kwa ajili ya matumizi ya Serikali kulingana na Bajeti. Utaratibu huu, umewawezesha wananchi kujua kiasi cha fedha kilichotolewa katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo ongezeko la benki na maduka ya fedha za kigeni. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2003, sekta ya benki ilijumuisha benki za biashara 23 na taasisi nane zisizo za kibenki. Katika kipindi hicho, Benki ya Wananchi

wa Dar es Salaam *(Dar es Salaam Community Bank Limited)* imekuwa benki kamili ya biashara, wakati Benki ya Wananchi wa Mbinga *(Mbinga Community Bank Limited)* ilianza shughuli zake. Katika kipindi hicho hicho, Benki ya *Federal Bank of the Middle East Limited* ya Cyprus iliichukua Benki ya Delphis *(Delphis Bank (T) Limited* iliyokuwa chini ya ufilisi. Aidha, Benki ya Baroda ya India imepewa leseni na inatarajiwa kuanza kazi wakati wowote. Kutokana na maendeleo hayo, idadi ya benki zilizokuwa zinafanya kazi ziliongezeka kutoka 21 hadi 23 na taasisi za fedha zisizo za kibenki zilipungua kutoka tisa hadi nane. Kuhusu maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, hadi sasa Benki Kuu imekwisha toa leseni kwa maduka 92 yanayofanya kazi sehemu mbalimbali nchini. Katika kuboresha huduma, baadhi ya benki zimeanzisha huduma ambayo humwezesha mteja kupata fedha kwa uharaka zaidi wakati wowote kutoka vituo maalum.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2004, rasilimali za ndani za mabenki ziliongezeka kutoka shilingi billioni 710.3 hadi shilingi bilioni 910.0. Hali hii ilichangiwa na kukua kwa mikopo ya mabenki kwa sekta binafsi kwa asilimia 35.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 24.5, lililowekwa. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa mabenki ya biashara katika kutoa mikopo, pamoja na juhudi za serikali za kuboresha mfumo mzima wa miundo mbinu katika uchumi. Katika mwaka wa fedha uliomalizika, riba za mikopo kwa ujumla zilishuka kutoka asilimia 14.1 mwezi Juni, 2003 hadi kufikia asilimia 13.9 mwezi Mei, 2004, wakati riba za amana kwa muda maalum zilipanda kutoka asilimia 3.5 na kufikia asilimia 4.2. Hali hii imechangiwa na jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya kibiashara kwa kupunguza riba ili kuhamasisha ongezeko la mikopo toka kwenye benki kwa ajili ya sekta binafsi, hususan wafanyabiashara ndogo ndogo na kati ambao ni mhimili wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Desemba, 2003, jumla ya rasilimali *(Total Assets)* katika sekta hii ilifikia shilingi bilioni 2,775, ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,269 mwaka 2002. Hili ni ongezeko la asilimia 22. Jumla ya amana *(deposits)* iliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,928 mwaka 2002 hadi shilingi bilioni 2,329 mwaka 2003, ambalo ni ongezeko la asilimia 21. Mtaji uliolipiwa *(paid up capital)* katika sekta hii, pia uliongezeka kutoka shilingi bilioni 108 mwaka 2002 hadi shilingi bilioni 159 mwaka 2003 sawa na ongezeko la asilimia 47. Mabadiliko haya, yanaonyesha jinsi ambavyo mwamko wa Wananchi kutumia huduma za benki ulivyoongezeka, sambamba na kuanzishwa kwa benki mpya pamoja na kupanua mitaji kwa baadhi ya benki zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweka kipaumbele katika kuimarisha *SACCAS, SACCOS,* Benki za Wananchi na Mfuko wa Udhamini Mikopo ya biashara ndogo na za kati *(SMEs)*. Aidha, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mikopo inawafikia wananchi. Hatua hizi ni pamoja na:-

(a) Kutoa kanuni za kusimamia mikopo midogo midogo;

(b) Kupitisha sheria na kanuni za kuanzishwa kwa asasi ndogondogo za kifedha *(MFI)* za ushirika au binafsi ikiwa ni pamoja na zile ambazo zitapewa leseni na kusimamiwa na Benki Kuu na ambazo zitatoa mikopo bila kudai dhamana;

(c) Kurekebisha Sheria ya Ardhi ambayo itawawezesha Wananchi kutumia ardhi kama dhamana; na

(d) Kuanzisha mfuko wa udhamini wa mikopo kwa wakopaji wadogo na wa kati *(SMEs)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu urekebishaji wa benki za umma, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki Kuu na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma inaendelea na utaratibu wa kurekebisha benki za umma nne zilizobaki yaani *TIB, TPB,* Twiga na *PBZ* ya Zanzibar. Kupitia Mpango wa Pili wa Kuendeleza Taasisi za Fedha *(Financial Institutions Development Project),* ripoti zinakamilishwa ili kuwasilishwa Serikalini kwa uamuzi. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa asasi hizi zinaimarishwa na kuwezeshwa kutoa mikopo ya muda mfupi, kati na mrefu ili kuchangia kasi ya ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kubinafsisha *National Microfinance Bank (NMB)* yapo katika hatua nzuri. Kufuatia matangazo ya kukaribisha wawekezaji kiongozi *(Strategic Investors)* kununua asilimia 49 ya hisa za *NMB,* maombi manne yamepokelewa na kufanyiwa uchambuzi wa awali *(pre-qualification)*. Aidha, taratibu za kukamilisha rasimu ya Mkataba *(Shareholders Agreement)* na *Information Memorandum* na taarifa nyingine zimekamilika na zinatarajiwa kugawanywa kwa walioonyesha nia mnamo mwezi Agosti, 2004.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB),* imeendelea kutoa mikopo ya muda mfupi na wa kati kwa wateja wake. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2003, benki iliidhinisha mikopo ya shilingi bilioni 10.87. Benki pia imeendelea kusimamia mifuko ya *Commodity Import Support (CIS)* na Mradi wa Urekebishaji Sekta ya Mafuta *(Petroleum Sector Rehabilitation Project).* Benki hii, imeendelea kukusanya madeni ya benki zilizo chini ya ufilisi zikiwemo *THB* na *Greenland Bank.* Benki imepata faida ya shilingi milioni 252.0 kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2003, ikilinganishwa na shilingi milioni 110.0 kwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2004/2005, Benki hiyo inanuia kuwa mshiriki mkubwa katika kuinua maendeleo ya kiuchumi kwa kutoa huduma katika miradi ya biashara kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza mikopo kwa asilimia 100 kutoka shilingi milioni 9,889 mwaka 2003 hadi shilingi milioni 19,308 mwaka 2004. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 60 itaelekezwa katika sekta ya kilimo; na

(b) Mikopo kwa wakopaji wadogo wadogo pia inatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 40 kutoka shilingi milioni 2,544 mwaka 2003 hadi shilingi milioni 3,561 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, amana za wateja wa Benki ya Posta Tanzania *(TPB),* ziliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 49.57 kutoka shilingi bilioni 45.13 za mwaka 2002. Vitega uchumi vya benki katika dhamana za Serikali za muda mfupi na mrefu zilifikia shilingi bilioni 43.15 ikilinganishwa na shilingi bilioni 41.66 kwa kipindi hicho hicho. Katika kipindi kinachoishia Desemba, 2003, Benki ilitoa mikopo mipya ya shilingi bilioni 8.93 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.23 mwisho wa mwaka 2002. Aidha, huduma ya Usafirishaji wa Fedha *(Western Union Money Transfer)* iliingiza pato la shilingi bilioni 1.67 katika mwaka 2003. Katika mwaka 2004, Benki imelenga kuboresha huduma zake na kupanua wigo wa ukopeshaji mikopo midogo midogo kwa vikundi, kuingia mikataba na waajiri zaidi ili kuwapatia wafanyakazi mikopo, kuimarisha huduma ya utumaji fedha na kufungua matawi mawili mikoani.

Mheshimiwa Spika, asasi iliyokuwa *National Bureau de Change (NBDC),* sasa imejiita *Twiga Bankcorp Ltd*. Katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2003 mtaji wa Benki ulikuwa shilingi milioni 801.4. Aidha, amana za wateja katika Benki ziliongezeka kutoka shilingi milioni 8,022.3 mwaka 2002 hadi kufikia shilingi milioni 11,262.5 katika kipindi hicho ikiwa ni ongezeko la shilingi milioni 3,240.2 sawa na asilimia 40.9. Benki hiyo, katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2003 ilipata mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 2.32 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.39 zilizokusanywa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, *CRDB Bank Ltd*. ni mojawapo ya benki za kizalendo iliyo na mafanikio mazuri na ya kujivunia. Benki hii ambayo Serikali imekwishajitoa kikamilifu ina matawi 32 katika Mikoa ya Tanzania na imekuwa inapata faida na kulipa gawio kwa Wanahisa wake mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2003, Benki hiyo ilitoa mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 60.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 43.0 mwaka 2002 ikiwa ni ongezeko la asilimia 40. Aidha, mapato yanayotokana na riba yaliongezeka kwa asilimia 32.4 kutoka shilingi bilioni 13.9 katika mwaka 2002 hadi shilingi bilioni 18.4 mwaka 2003. Katika mwaka 2004, *CRDB Bank Ltd.* pamoja na kuendelea kutekeleza mpango wake wa maendeleo wa miaka mitano unaoweka mkazo kwenye biashara rejareja ya kibenki, itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja hasa katika sekta ya kilimo, ili kuchangia vilivyo katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti biashara ya fedha haramu nchini, Wizara imefanya mapitio ya sheria mbalimbali zihusuzo masuala hayo na kuandaa Rasimu ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria husika ili kuwa na muundo madhubuti wa kisheria *(Regulatory Framework)* utakaowezesha udhibiti wa fedha haramu pamoja na vitendo haramu vinavyoambatana na fedha hizo. Aidha, rasimu hiyo imewasilishwa kwa wadau mbali mbali zikiwemo Wizara na Asasi mbalimbali ili kupata maoni yao kabla ya kuwasilisha Serikalini kwa hatua zaidi. Aidha, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa kundi la nchi za *SADC* na Afrika Mashariki zinazoshirikiana kudhibiti kuenea kwa matumizi ya fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, Biashara ya Bima katika mwaka wa fedha 2003/2004, iliongezeka kutoka shilingi bilioni 53.76 hadi shilingi bilioni 70.61 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.34. Ongezeko hili limetokana na kuendelea kupanuka kwa huduma za makampuni binafsi ya bima kwenye baadhi ya mikoa na kuanza kueleweka kwa aina mpya ya Bima ya Matibabu (Medical Insurance). Idadi ya Kampuni za Bima ziliongezeka kutoka 11 hadi 12 mwaka 2003/2004. Huduma ya Bima ya Mtawanyo *(Tanzania Reinsurance)* ilianza rasmi Januari 2004 kufuatia kuandikishwa kwa kampuni hii na kuanza biashara. Madalali wa bima waliongezeka toka 38 hadi 43, mawakala wa bima waliongezeka kutoka 308 hadi 333 na Wakadiriaji wa hasara waliongezeka kutoka 24 hadi 29. Ulipaji wa madai ya bima umeongezeka kutoka shilingi bilioni 17.1 mwaka 2002/2003 hadi shilingi bilioni 18.71 katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, pato la shughuli za bima linatarajiwa kukua kwa asilimia 10 kutokana na kuendelea kupanuka kwa shughuli za bima mikoani, kuendelea kuimarika kwa bima za mtawanyo na kuanza kwa bima ya kinga ya majanga ya kisiasa (political risks) pamoja na bima za mikopo *(Credit Risk Insurance)* inayotolewa na *Africa Trade Insurance Agency.* Bima hii inatarajiwa kuwezesha bidhaa za Kitanzania kuvutia waagizaji walioko nje.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa linakabiliwa na madai mengi ya muda mrefu na yenye kero kubwa. Wizara kwa kushirikiana na PSRC na Idara ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imeendelea kuuza baadhi ya mali za Shirika zisizokuwa muhimu kwa shughuli za bima *(non-core assets)* hasa majengo, ili kuendelea kulipa madai yaliyothibitishwa. Katika mwaka 2003, *NIC* ilikuwa na madai yaliyothibitika ya shilingi milioni 7,612.9 ambapo hadi kufikia Desemba, 2003, jumla ya madai ya bima zisizo za maisha yaliyolipwa na Shirika yanafikia kiasi cha shilingi milioni 1,562.81. Katika mwaka 2004/2005, Shirika linatarajia kulipa madai ya bima zisizo za maisha yanayokadiriwa kuwa shilingi milioni 2,459.2 baada ya kuyathibitisha. Kati ya Januari 2003 na Machi, 2004, Shirika lililipa madai ya bima zisizo za maisha ya kiasi cha shilingi bilioni 3.942, na madai ya bima za maisha yanayofikia shilingi bilioni 4.79. Madai yaliyobaki yanafikia shilingi bilioni 9.564 kwa bima zisizo za maisha na kiasi cha shilingi bilioni 4.938 kwa bima za maisha. Aidha, Shirika la *NIC* limeendelea kuwa chini ya usimamizi wa *PSRC* ambapo mikakati inaendelea ili liweze kubinafsishwa katika mwaka wa 2004/2005 na kulipa madeni yote.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uorodheshwaji wa hisa na hatifungani katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam *(DSE).* Mamlaka ilikamilisha kutoa elimu kwa umma nchi nzima kuhusu masoko ya mitaji baada ya kuendesha semina kwa wilaya zote za mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Zanzibar. Matokeo ya semina kwa viongozi wa juu wa Manispaa za Dar es Salaam ni maombi ya kwanza ya hatifungani za Manispaa za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali, hatifungani 4 za muda tofauti wa kuiva *(Maturity Date)* zenye thamani ya shilingi bilioni 119.6 zimeorodheshwa na kuongeza thamani ya hatifungani za Serikali kufikia shilingi bilioni 289.3 Aprili, 2004.

Kwa ujumla, hatifungani zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa zimefikia thamani ya shilingi bilioni 330.3 wakati thamani ya hisa zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa zimefikia shilingi bilioni 654.18.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Mamlaka ni kutoa leseni kwa washiriki *(operators)* katika sekta na soko la mitaji na dhamana. Washiriki hao ni pamoja na Washauri wa uwekezaji, Wakala, Madalali na asasi za kuendesha uwekezaji wa pamoja *(Collective Investment Schemes).* Aidha, Mamlaka imepokea maombi ya Shirika la Ndege la Kenya ya kuorodhesha hisa zake katika *DSE* baada ya Serikali kuidhinisha mpango wa mashirika na makampuni ya nje kuorodhesha hisa zao hapa nchini. Serikali inaangalia uwezekano wa kuruhusu makampuni yake nayo kuanza kuorodhesha hisa zao nje ya nchi *(Cross Listing).*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 juni 2004, Soko la Hisa la Dar es Salaam limeorodhesha hisa za makampuni kadhaa yakiwamo Kampuni ya Bia, Kampuni ya Sigara, Kampuni ya Majani ya Chai *(TATEPA)*, Kampuni ya Oksijeni *(TOL)*, Kampuni ya Saruji Tanga na Kampuni ya Kuhudumia Mizigo Viwanja vya Ndege *(DAHACO).* Soko pia limeorodhesha hatifungani za makampuni matatu yanayojumuisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, Benki ya *PTA* zenye thamani ya shilingi bilioni 15 pamoja na kampuni binafsi inayowekeza hapa nchini ya *BIDCO Oil and Soap Limited* shilingi bilioni 190. Ununuzi wa hatifungani hizi umevuka viwango *(Over Subscribed)* kwa asilimia 2 na 40. Soko la Hisa la Dar es Salaam limeendelea kukua na inatarajiwa kuwa hatifungani za Serikali za Mitaa *(Municipal Bonds)* zitasajiliwa kwenye soko hili. Inatarajiwa pia kuwa makampuni ya kigeni yatajiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni 2004, hatifungani za Serikali katika soko la Hisa zilifikia thamani ya shilingi bilioni 405.8 kufuatia hatifungani za Benki ya *PTA* na *BIDCO Oil Soap Limited* kuorodheshwa. Kwa upande wa hisa, hapakuwa na kampuni mpya iliyoorodheshwa kwa mwaka huo. Kwa mwaka 2004/2005, Soko la Hisa litaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu faida ya masoko ya mitaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Asasi ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania *(Unit Trust of Tanzania - UTT),* ilianzishwa rasmi tarehe 19 Juni, 2003 chini ya Sheria ya Udhamini Sura ya 375. Majukumu ya asasi hiyo ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuchukua na kuhodhi hisa za makampuni yaliyobinafsishwa zilizokuwa chini ya dhamana ya *Privatization Trust* na nyingine ambazo Serikali itaamua kuwekeza kwenye Dhamana hii;

(b) Kuhakikisha kwamba hisa zilizopo kwenye Dhamana zinatawanywa kwa Watanzania kwenye wigo mpana kwa njia itakayohakikisha kwamba Watanzania wengi wanapata nafasi na tabia ya kujiwekea akiba ili waweze kumiliki sehemu ya mashirika yaliyobinafsishwa na kuongeza ushiriki wao kwenye masoko ya mitaji; na

(c) Kuanzisha Mpango wa Uwekezaji wa Pamoja *(Collective Investment Schemes).* Chini ya mpango huo, Mfuko utakaoitwa "Mfuko wa Umoja *(Umoja Fund)"* utaanzishwa. Matayarisho ya kuanzisha Mfuko huo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, dhana ya uwekezaji wa pamoja *(Collective Investment Scheme)* ni mpya hapa nchini. Ili kufanikisha uanzishwaji na uendelezaji wake, *UTT* itaajiri wataalam kutoka India watakaosaidia kujenga uwezo wa soko, miundombinu, elimu kwa umma na kuboresha uhodhi wa hisa kwa manufaa ya Mfuko. Wizara imeruhusu chombo hiki kumiliki sehemu ya hisa zake katika makampuni ya Bia *(TBL)* asilimia mbili sawa na shilingi bilioni 8.7 na Sigara *(TCC)* asilimia moja, sawa na shilingi bilioni 1.72 kuwa mtaji wa awali *(Seed Capital)* wa kuanzisha na kuendeleza asasi hii. Wizara pia, imeidhinisha kutoa punguzo la bei ya ununuzi wa *units* zitakazouzwa awali *(Initial Public Offering - IPO)* na kutoa unafuu wa kodi kwa bidhaa ya kwanza kwa lengo la kuhamasisha wananchi kuwekeza katika mpango huu mpya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Mfuko wa Udhamini wa Mikopo na Madeni *(LART)* unaoshughulikia madeni sugu umeendelea kupokea madeni kutoka benki na asasi za kifedha kama Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, Benki ya Posta, *Federal Bank of Middle East Limited,* pamoja na kupokea kazi za ufilisi kutoka *PSRC* zinazotokana na zoezi la ubinafsishaji. Katika mwaka ulioishia 2003/2004, *LART* iliweza kukusanya madeni ya wadaiwa saba wa awamu ya kwanza yenye thamani ya shilingi bilioni 1.44, kufunga akaunti saba za madeni ya awamu ya kwanza na 6 za madeni ya awamu ya pili pamoja na kukusanya jumla ya shilingi milioni 27.8 hivyo kufikia makusanyo ya shilingi bilioni 2.35 za awamu ya pili. Shughuli za ufilisi ziliingiza jumla ya shilingi bilioni 2.84.

Mheshimiwa Spika, *LART* ambayo Bunge linaloendelea sasa limeongezea muda wake kwa kipindi cha hadi miaka miwili kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 inatarajiwa kukamilisha uuzaji wa mali za wadaiwa wanane zenye thamani ya shilingi bilioni 2.10, kuuza mali za mashirika na kukusanya madeni yenye thamani ya shilingi bilioni 2.80, kukusanya shilingi bilioni 2.6 kutokana na mashirika ya umma na kuendelea kusimamia kesi za madai 56 zilizopo mahakamani na mpya zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *Consolidated Holdings Corporation* ilikusanya shilingi bilioni 7.03 katika mwaka wa 2003 sawa na asilimia 156 ya lengo kutokana na uuzaji wa majengo, magari, vifaa, ukusanyaji wa madeni, utoaji wa huduma mbalimbali na gawio kutoka *NBC Ltd.* Aidha, Shirika liliweza kuwasilisha Hazina ziada ya shilingi bilioni 2.66 kwa mwaka 2003. Tatizo kubwa limeendelea kuwa kesi za madai zinazofikia shilingi bilioni 140. Mwaka 2003 Shirika limelipa shilingi milioni 881 kutokana na maamuzi ya Mahakama *(Court Decrees)* dhidi yake. Katika mwaka 2004/2005, Shirika linatarajia kukusanya shilingi bilioni 2.88. Fedha hizo zitatokana na madeni ya shilingi bilioni 1.70, uuzaji wa majengo shilingi milioni 904 na mapato kutoka vyanzo vingine shilingi milioni 276. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Board of Tanzania)* ilianza kazi ya kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa biashara za

michezo ya kubahatisha hapa nchini tarehe 1 Julai, 2003. Hadi sasa, Bodi imetoa leseni sita za kuendesha Casino na 219 za michezo ya mashine *(Slot Machines)* katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Moshi, Shinyanga, Morogoro na Songea. Aidha, Bodi imetoa leseni moja kwa ajili ya kuendesha michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa, Lotto na Papo Hapo *(Instant Lotteries)*. Shughuli hizi zimeingiza shilingi bilioni 1.05 katika mwaka 2003/04.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Bodi imedhamiria kuhakikisha kuwa biashara za michezo yote ya kubahatisha inaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa kisheria. Aidha, pamoja na uchanga wetu mwezi Oktoba, 2004, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Bodi za Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha katika Afrika *(Annual Conference of the Gaming Regulators Africa Forum).* Bodi inatarajia kuchangia shilingi milioni 110.0 kwa ajili ya maendeleo ya michezo kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu ambayo nimekwisha yaeleza na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu inaomba Bunge lako liidhinishe:-

(a) Kwa Fungu 50 Jumla ya shilingi 163,035,551,100 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 146,514,731,100.00/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 16,520,820,000.00/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(ii) Katika matumizi ya kawaida Shilingi 1,335,119,000.00/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara, Shilingi 48,169,831,400.00/= kwa ajili ya Asasi chini ya Wizara, Shilingi 61,065,302,300.00/= kwa ajili ya Matumizi Maalum na Shilingi 35,944,478,400.00/= kwa ajili ya kuendesha Idara ikiwa ni pamoja na mafunzo, tathmini ya mali za Serikali, ada za uanachama kwenye Mashirika ya Kimataifa, ulipaji wa madeni dhidi ya Serikali na madai yanayotokana na urekebishaji wa Mashirika.

(iii) Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, shilingi 14,160,820,000.00/= ni misaada na mikopo nafuu kutoka nje na shilingi 2,360,000,000.00/= ni fedha za ndani.

(b) Fungu 22 linaombewa shilingi 477,011,533,500.00/= kwa ajili ya Deni la Taifa. Kati ya kiasi hicho shilingi 908,426,400.00/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 476,103,107,100.00/= ni kwa ajili ya matumizi mengine.

(c) Fungu 23 l inaombewa jumla ya Shilingi 82,582,598,400.00/=. Kati ya fedha hizo, Shilingi 71,282,749,400.00/= ni Matumizi ya Kawaida na Shilingi 11,299,849,000.00/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(i) Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida: Shilingi 1,882,636,300.00/= ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, Shilingi 32,018,194,800.00/= kwa ajili ya Malipo ya Kodi kwa Taasisi zinazolipiwa kodi na Serikali *(Treasury Voucher System),* Shilingi

10,116,000,000.00/= kwa ajili ya Bima ya Afya, Shilingi 9,000,000,000.00/= kwa ajili ya Gharama za Benki kwa malipo ya Serikali na Shilingi 18,265,918,300.00/= ni kwa ajili ya kuendesha Ofisi, ikiwa ni pamoja na kuboresha Mtandao wa Kompyuta *(IFMS)* na Mafunzo kwa Wahasibu walio kazini *(In-service)*.

(ii) Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Shilingi 218,949,000.00/= ni Fedha za Ndani na Shilingi 11,080,900,000.00/= ni misaada na mikopo nafuu kutoka nje.

(d) Fungu 45 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, inaombewa jumla ya Shilingi 6,761,174,700.00/=. Kati ya hizo:-

(i) Shilingi 5,143,270,000.00/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, zikiwemo Shilingi 1,143,783,200.00/= za Mishahara.

(ii) Shilingi 1,617,904,700.00/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, zikiwemo misaada na mikopo nafuu kutoka nje Shilingi 1,408,606,600.00/= na za ndani Shilingi 209,298,100.00/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ilipitia Makadirio ya Wizara ya Fedha, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Deni la Taifa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya mwaka 2004/2005 na kuyakubali. Naliomba Bunge lako sasa likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Deni la Taifa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Manaibu Waziri, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mbunge wa Makunduchi na Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wote wa maandalizi ya makadirio haya. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha chini ya Makatibu Wakuu, Bw. Gray S. Mgonja na Bw. Peniel M. Lyimo, Manaibu Katibu Wakuu, Bw. Ramadhani M. Khijjah na Bw. Wilfred L. Nyachia, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Benki Kuu ya Tanzania na Asasi nyingine zote zilizofanikisha maandalizi ya Hotuba hii. Nawaomba ushirikiano huo udumishwe ili kuhakikisha kuwa mapendekezo yaliyopitishwa na Bunge lako yanatekelezwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. NJELU E.M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 81(1) ya Kanuni za Bunge

Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu Taarifa na maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa mwaka wa Fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea napenda kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijiji kwa kifo cha Mbunge wao Marehemu Yete Sintemule Mwalyego, aliyefariki dunia hapa Dodoma tarehe 24/06/2004. Aidha, napenda kuwapa pole familia na wananchi wa Jimbo la Mahenge Masharikì kwa kifo cha Mbunge wao Marehemu Theodos Kasapira aliyefariki dunia usiku wa kuamkia tarehe 22 Julai, 2004 hapa Dodoma. Ninamwomba Mwenyezi Mungu azipokee roho zao na kuwapa pumziko la milele.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji walifikisha mbele ya Kamati na sisi kama Kamati tulipitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo na kuchambulia kama ifuatavyo:-

Hapa ningependa napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliohusika. Mimi mwenyewe Njelu Kasaka kama Mwenyekiti; Mheshimiwa Lephy Gembe, alikuwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, MheshimiwaIddi Simba, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Abdillatif Esmail, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, na Mheshimiwa Stanley Kolimba.

Mheshimiwa Spika, Wengine ni Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Hasnain Murji, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Issa Salim, Mheshimiwa Rostam Aziz na Katibu wetu James Warburg. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka wa Fedha uliomalizika Juni 2004 na kubaini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio, Wizara ya Fedha iliandaa na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Kodi ya Mapato wa 2004. Muswada huu hatimaye ulipitishwa na Bunge. Pili, Wizara iliandaa na kuwasilisha Bungeni marekebisho ya Sheria iliyounda *National Microfinance Bank* na hatimaye kupitishwa na Bunge; tatu, makusanyo ya mapato yaliongezeka na kufikia wastani wa zaidi ya Sh.100 bilioni kwa mwezi hivi sasa. Nne, mfumko wa bei umebaki chini ya asilimia tano kwa kipindi chote. Tano, usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali kwa kutumia Mfumo wa *IFMS* uliimarishwa na kuboreshwa na ufanisi katika usimamizi wa fedha umeongezeka. Sita, upelekaji wa fedha kwenye Wizara, Mikoa na Wilaya ulikuwa bora zaidi kuliko vipindi vya nyuma. Saba, baadhi ya Ofisi za Wizara na baadhi ya majengo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hizi ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Uhasibu iliyoko Kurasini pamoja na Kituo cha

Uwekezaji kilichoko pale Dar es Salaam, yote yalikarabatiwa. Nane, idadi ya Benki za kibiashara na Taasisi za fedha hapa nchini zimeongezeka; tisa, kiwango cha riba cha mikopo ya mabenki kimeendelea kushuka ingawa bado hakiridhishi. Hivi sasa ni kati ya asilimia 13 na 15. Kumi, kiwango cha utegemezi wa Bajeti kwa misaada ya nje kimepungua kutoka asilimia 45 mwaka 2002/2003 na kufikia asilimia 41 mwaka 2004/05. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Wizara imeongeza idadi ya wanafunzi inaowadhamini katika vyuo na Taasisi za Uhasibu kama alivyoeleza Waziri hapa. Hatua hii imeongeza idadi ya wahitimu wa fani ya Uhasibu kila mwaka. Wizara imeanzisha ukaguzi wa migodi mikubwa ya dhahabu ili kujiridhisha kama kiasi gani cha dhahabu kinapatikana na kiasi gani cha kodi kinalipwa Serikalini. Wizara iliandaa na kuwasilisha Bungeni na kupitishwa na Bunge Azimio la Kuongeza Uhai wa *LART* yaani *Loans and Advances Realization Trust* na pia kuliletwa Azimio lingine la Kuongeza Uhai wa *PSRC* ambayo ilipitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi mpana imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi cha mwaka wa fedha uliomalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na matatizo katika Wizara hizo. Kwanza, bado kuna ukwepaji mkubwa wa kulipa kodi kwa baadhi ya Wafanyabiashara wakubwa na Wafanyabiashara wadogo wadogo. Wigo wa kuwapata walipa kodi zaidi bado haujapanuliwa vya kutosha. Kuna shughuli nyingi za kibiashara bado hazijaingizwa kwenye wigo wa kodi; Sekta ya Mafuta ya Petroli haijasimamiwa vya kutosha kuhakikisha kodi zote zinakusanywa bila udanganyifu; Wizara haijafanikiwa vya kutosha kusimamia matumizi ya fedha za Serikali zikishafika Mikoani, Wilayani na kwenye Idara zinazojitegemea na kuona uwiano wa hali ya fedha iliyotumika na kazi iliyofanyika yaani *value for money. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Ofisi nyingi za Serikali ngazi ya Wilaya hazina vitendea kazi vya kisasa kama vile kompyuta, *fax machines* na *photocopier.* Hakuna Benki maalum za viwanda, kilimo na nyumba. Inaeleweka duniani pote kuwa Benki za kibiashara hazikidhi mahitaji ya uwekezaji katika viwanda, kilimo na ujenzi wa nyumba. Riba inayolipwa kwa amana ni ndogo sana, ni kati ya asilimia 1.4 hadi asilimia 3. Wakati huo huo riba kwa mikopo ni kubwa kama nilivyoeleza pale awali, zaidi ya asilimia kati ya 13 na 15. Mabenki mengi na Taasisi za Fedha zimerundikana katika Miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Mabenki yana fedha nyingi lakini hayatoi mikopo ya kutosha ili kujipatia mapato kwa njia ya riba. Badala yake yameanzisha gharama nyingi mbalimbali kwa wenye akaunti za wateja ili Mabenki yasipate hasara na sasa yanapata faida kubwa kwa njia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara inakabiliwa na tatizo la kukosa Wahasibu wenye sifa zinazotakiwa kutokana na kutokuwa na utaratibu mzuri wa kuwaajiri wahitimu na kuwaondoa wasio na sifa na uwezo. Wizara imeshindwa kukiwezesha Chuo cha Uhasibu Kurasini kuajiri Walimu wanaohitajika. Kwa kweli tulipofika pale ilionekana kwamba ni mabo ya urasimu tu; Wizara bado kulipa baadhi ya madeni ya

ndani. Kwa mfano wafanyakazi wa Serikali za Mitaa wanadai zaidi ya Shilingi bilioni 3.5 ikiwa ni malimbikizo ya madeni yao. Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 bado kulipwa mafao yao; wafanyakazi wanatozwa kodi kubwa mno, hivyo kuna haja ya kuliangalia tena jambo hili na pia Makampuni zaidi ya kumi yaliyobinafsishwa hayajaanza kufanya kazi na hapa tunaiomba Wizara inayohusika iendelee kuyashughulikia Mashirika haya ili yaanze kufanya kazi au yachukuliwe na kupewa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasikiliza Mawaziri na kuchambua Bajeti zao na kuangalia makusudio ya Bajeti ya 2004/2005, Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao:-

- Wizara iboreshe na kuimarisha utaratibu wa kukusanya mapato ya Serikali, Wizara ihakikishe wote wanaostahili kulipa kodi wanalipa na kusiwe na mwanya wa kukwepa kulipa kodi. Misamahama ya Kodi itolewe kwa uangalifu na Kamati ya Fedha na Uchumi ijulishwe nani wamesamehewa na kwa kiwango gani au kwa sababu gani.

- Taarifa ya ukaguzi wa migodi ya dhahabu ambayo Waziri ameshateua ukaguzi wake iletwe Bungeni ili kuona ni jinsi gani nchi yetu inafaidika na utajiri wa maliasili iliyo nayo.

- Mapendekezo yaliyotolewa na Makampuni ya Mafuta ya Petroli yatekelezwe kwa madhumuni ya kuziba mianya ya kukwepa kulipa kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu. Mafuta yanayopelekwa nchi jirani yafuatiliwe kuepuka udanganyifu.

- Wigo wa kodi upanuliwe kwa kufanya utafiti namna gani biashara ndogo zitaingizwa kwenye wigo ili zichangie Pato la Taifa. Lengo liwe ni kuongeza mchango wa kodi kwenye Pato la Taifa kufikia angalau asilimia 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha asilimia 20 cha *VAT* kinachotozwa Tanzania ni cha juu mno ukilinganisha na Wanachama wengine wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Kenya na Uganda. Ili kuwezesha Makampuni ya Tanzania kushindana katika soko la Afrika Mashariki, Kamati inaishauri Serikali kupunguza *VAT* ili isitofautiane sana na Uganda na Kenya ambako *VAT* ni asilimia 16 na 17 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya Fedha za Serikali yasiishie kwenye uwekaji sahihi wa mahesabu na kuweko kwa vielelezo vya matumizi. Jambo kubwa ni kukamilika kwa shughuli au miradi kwa muda uliopangwa na kwa gharama ndogo. Hali ilivyo sasa sivyo. Shughuli au miradi ya Serikali huchukua muda mrefu kukamilika na aghalabu kwa gharama kubwa. Usimamizi na uwajibikaji ngazi za chini haupo na kila Ofisa Mwandamizi ameachwa ajisimamie mwenyewe. Matokeo yake Maafisa wengi Waandamizi hutumia magari ya Serikali na hata muda wa kazi wa Serikali kufanya shughuli zao binafsi na hakuna anaewauliza. Fedha zinazotengwa kila mwaka zinaweza kuleta mabadiliko makubwa katika maendeleo ya nchi hii kama zikisimamiwa Vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kuimarisha Serikali za Mitaa na kufanya Watumishi wote Wilayani wawajibike kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ni mzuri sana iwapo utasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo. Kuna haja ya kuimarisha Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuteua watu wenye sifa na uwezo wa kuongoza na kusimamia kushika wadhifa wa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.

- Kuajiri Wahasibu na Makarani wenye sifa na uwezo ili kuhakikisha fedha zinazopelekwa Wilayani zinatumika vizuri na kumbukumbu sahihi zinawekwa.

- Kwa kuwa watumishi wote wa Serikali wamewekwa chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Umma, basi watumishi wa Idara zote wawe na sifa zinazofaa na wenye mapungufu wapewe mafunzo ya mara kwa mara.

- Idara ya Mipango katika Halmashauri iimarishwe kwa kupewa watumishi bora, wenye sifa na uwezo wa kazi hiyo na wawe na vifaa vya kufanyia kazi. Uamuzi wa kuzifanya Halmashauri za Wilaya kuwa ndiyo kitovu cha maendeleo ya Wilaya lazima uambatane na uimarishaji wa Halmashauri zenyewe.

- Bajeti zinazopewa Halmashauri za Wilaya iongezwe ili Halmashauri ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

- Ofisi ya Mkuu wa Wilaya nayo iboreshwe na kuwa ya kisasa. Katibu Tawala wa Wilaya anafanya kazi na vifaa vya kizamani kwa kutumia *typewriter* ambazo hutoa nakala zisizosomeka. Vinginevyo asipotumia *typewriter* hiyo, Mkuu wa Wilaya analazimika kuchapa barua zake nje ya Ofisi na hivyo kutoa siri za Serikali. Mfano halisi ni Wilaya yangu ya Chunya ambako *manual typewriter* bado inatumika, lakini najua zipo Wilaya nyingi zenye hali kama hiyo. Tunaiomba Serikali itenge Bajeti ya kutosha, kuzipatia Kompyuta Wilaya zote ambako umeme upo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali iharakishe mpango wa kuunda Benki za Maendeleo ya Viwanda, Kilimo na Ujenzi wa Nyumba. Kamati imekuwa mara kwa mara inaishauri Serikali kuanzisha Benki zilizotajwa ili kuharakisha maendeleo ya Sekta za Viwanda, Kilimo na Ujenzi wa Nyumba.

Mheshimiwa Spika, Benki za Kibiashara hazikuandaliwa kutoa mikopo ya muda mrefu na masharti yake ni ya kibiashara siyo kiuwekezaji. Ili kuwezesha Wawekezaji wa ndani kupata mikopo, kuna umuhimu kuanzisha Benki za aina hiyo. Kuanzishwa kwa Benki ya Nyumba au *Mortgage Bank* kulitokana na agizo la Rais Benjamini Mkapa aliyesema angependa kuona Benki hiyo imeanza kazi kabla hajaondoka madarakani.

Pia Kamati inashauri mkakati unaoendelea wa kubadili Benki ya Raslimali kuwa Benki ya Viwanda uharakishwe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa ina Mabenki na Taasisi nyingi za Fedha lakini upatikanaji wa mikopo kwa Sekta za Uzalishaji ni matatizo, hasa kilimo, viwanda na ujenzi wa nyumba bado ni tatizo kubwa. Mabenki yamejipatia amana nyingi kiasi cha kushusha riba hadi asilimia 1.4. Wakati huo huo riba kwa wanaoomba mikopo bado ni juu zaidi ya asilimia 15. Kamati inaishauri Serikali kuyachagiza Mabenki kupunguza riba ya mikopo na kujenga mazingira yatokayowezesha Mabenki na Taasisi za fedha kutoa mikopo zaidi kwa Sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Tanzania utaimarika na kuwa na nguvu kwa kuongeza na kupanua Sekta za Uzalishaji. Kilimo ni Sekta kiongozi kwa uchumi katika kipindi cha mpito, lakini katika uchumi imara sekta kiongozi ni viwanda. Kamati inashauri Wizara ihakikishe madeni yote ya ndani yanalipwa na hususan haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Serikali za Mitaa; Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, wanaidai Serikali zaidi ya Shilingi bilioni 3.52 ambayo ni madai ya nyakati tofauti yanayotokana na posho za kipindupindu, nauli za likizo, nyongeza za mishahara, kupanda cheo, uhamisho, matibabu, masomo kazini, usafiri kazini, kustaafu, fidia ya kuumia kazini, na kadhalika.

Kwenye mwaka 1995 Serikali ilizitaka Halmashauri kuorodhesha na kuwasilisha madai hayo Wizara ya Fedha. Zoezi hilo lilifanyika na madai kuhakikiwa. Lakini madai hayo bado kulipwa licha ya kukumbusha mara kwa mara. Tunashauri Serikali iwalipe watumishi hawa stahili yao bila kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuwalipa Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika 1977. Wastaafu hawa hawajalipwa mafao yao kwa miaka 27 sasa. Ni jambo la kusikitisha kuona Watanzania hawa waliotumikia Jumuiya ya Afrika Mashariki wamesota kwa miaka yote hiyo bila kupata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, taarifa za kuaminika zinaonyesha kuwa fedha kwa ajili ya kuwalipa Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilitolewa na Serikali ya Uingereza yaani *Crown Agents* na Wastaafu wa Jumuiya kwa upande wa Kenya na Uganda walilipwa, isipokuwa upande wa Tanzania. Tangu wakati huo, wastaafu wa Jumuiya kwa upande wa Tanzania wamekuwa wakifuatilia bila mafanikio. Swali ni je, kwa nini Serikali imesita kuwalipa haki zao wastaafu wa Jumuiya iliyovunjika kwa kipindi chote hiki? Je, kitendo hiki cha Serikali si cha kuwatelekeza Watanzania hawa? Kwa taarifa hii, tunaiomba Serikali itoe tamko itawalipa lini mafao yao wastaafu hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaelewa kuwa suala hili lilipelekwa Mahakamani na Wastaafu kutaka wapate haki yao. Hatua ya kwenda Mahakamani ni kitendo cha kutapatapa baada ya kuona Serikali haionyeshi nia ya kuwalipa. Kesi kuwa Mahakamani kisiwe kizingizio cha kucheleweshа malipo yao. Tunaiomba Serikali ifikie makubaliano na wastaafu hao na malipo yafanywe bila kuingiza suala la Mahakama. Kama kuna kesi Mahakamani ni bora ifutwe na malipo yafanyike.

Mheshimiwa Spika, katika kukubali *NMB* ibinafsishwe, Bunge liliitaka Serikali izingatie mambo manne na ilikubali. Kwanza *Strategic Investor* apewe asilimia 49 ya hisa kwa masharti kwamba atahusisha au kuungana na Kampuni au Makampuni ya Kitanzania.

Pili, Wafanyakazi wa *NMB* washiriki katika umiliki wa Benki kwa kununua hisa watakazoruhusiwa. Tatu, Wananchi wengine nao waruhusiwe kununua hisa kati ya hisa asilimia 21, na Nne, Serikali iendelee kushikilia asilimia 30 ya hisa ambazo kwa wakati muafaka zitauzwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna habari kwamba Serikali inataka kubinafsisha *NMB* bila ya kuzingatia yaliyotamkwa hapa Bungeni na Serikali. Kufanya hivyo itakuwa ni kitendo cha kutoheshimu tunayokubaliana Bungeni na matokeo yake ni kutoaminiana kwa siku zijazo. Ni matumaini ya Kamati kuwa hilo halitatokea na ubinafsishaji utazingatia yaliyokubaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *NMB* hivi sasa ndiyo Benki yenye amana kubwa karibu bilioni 400 kuliko Benki zote hapa nchini. Kwa bahati mbaya Benki hii imewekewa vikwazo na Serikali vinavyoifanya isitumie fedha hizo kukopesha Sekta za Uzalishaji. Vikwazo hivyo ni pamoja kutopewa leseni na kutokuwa na akaunti za hundi. Tunajiuliza lengo la hatua hizi ni nini?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna fedha nyingi katika mfumo wa Benki ambazo hazikopeshwi ili kuendeleza na kukuza uchumi. Imeelezwa kuwa katika Mabenki hapa nchini kuna karibu Shilingi bilioni 960 ambazo zingetumika kukopesha, lakini hazikopeshwi. Nyingi katika fedha hizo ziko *NMB, CRDB,* na *NBC.* Kutokana na kuzuiliwa, *NMB* hutumia fedha za amana kununua hawala za Serikali na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa Mabenki mengine.

Mheshimiwa Spika, *NMB* ni Benki kubwa hapa nchini hivi sasa na ubinafsishaji wake ufanywe kwa uangalifu mkubwa. Ubinafsishwaji wa *NMB* usifanye Benki hiyo ikayumba au kuparaganyika. Ni Benki yenye mtandao mkubwa nchi nzima na kwa kiwango fulani ukubwa wa amana zake unatokana na mtandao wake. *NMB* ikiyumba au kuparaganyika kutavuruga mfumo wa malipo na kuathiri uchumi. Kamati inashauri Serikali kuwalipa nyongeza ya mishahara watumishi wa *NMB* kama stahili yao ilivyo. Kwa sasa watumishi hao hawajapata nyongeza kwa miaka mitano kwa madai kuwa *NMB* itabinafsishwa. *NMB* kuwa katika mkakati wa kubinafsishwa isiwe sababu ya watumishi kunyimwa haki na stahili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuitaka Serikali kuzingatia na kuufanyia kazi ushauri uliotolewa kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, napenda kumshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji Dr. Abdallah Kigoda, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa ushirikiano wao mzuri kwa Kamati yangu na kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Wizara zao na Serikali kwa ujumla. Uchumi umeimarika kutokana na usimamizi na utekelezaji mzuri wa kazi za Wizara hizi. Napenda pia kutumia nafasi

hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa ushirikiano wanaonipa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza wewe mwenyewe na Katibu wa Bunge pamoja na Katibu wa Kamati James Warburg kwa kujituma kwao katika kazi za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inaomba jumla ya Sh.7,952,733,300/= kama matumizi ya kawaida na Sh.4,698,297,800/= kama fedha za maendeleo, ambayo jumla inafanya Sh.22,651,031,100/=. Hili ni Fungu 66.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza shughuli zake, Wizara ya Fedha inaomba fedha kama ifuatavyo:-

Fungu 50, Sh.146,514,731,100/= ikiwa ni matumizi ya kawaida na Sh.16,520,820,000/= Fedha za Maendeleo, Fungu 23, Sh.71,282,749,400/= Matumizi ya Kawaida na Sh.11,299,849,000/= Fedha za Maendeleo, Fungu 22, Sh.477,011,533,500/= kwa ajili ya deni la Taifa na Fungu 45, Sh.5,143,270,000/= Matumizi ya Kawaida na Sh.1,562,749,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaliomba Bunge hili liidhinishe maombi haya. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI NA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukurani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha kwa mwaka 2004 na 2005 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 435(b)(c) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, aidha naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu wao pamoja na Viongozi wa Vitengo na Asasi zilizo chini yao. Wote tunawapongeza kwa kuratibu mipango na mwenendo wa uchumi pamoja na ukusanyaji wa mapato hadi nchi yetu kuweza kujijengea sifa ya kuwa mahali pazuri pa kuwekeza na uvunaji wa raslimali mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuondoa umasikini miongoni mwa Watanzania ndio lengo mahsusi la Dira ya Taifa ya Maendeleo. Mtandao mkubwa wa kiasasi yaani *Institutional Infrastructure* unaosimamiwa na Ofisi hii ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ambao umekusanya Taasisi hii kama zifuatazo:-

Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* Baraza la Taifa *(NPC),* Baraza la Taifa la Biashara *(NBC),* Taasisi ya Taifa ya Takwimu, Chuo cha Afrika ya Mashariki, Chuo cha Mafunzo

ya Takwimu, Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, Chuo cha Mipango ya Maendeleo na Taasisi ya Taifa ya Mambo ya Sensa.

Mheshimiwa Spika, mipango mibovu na sera potofu ni kati ya mambo ambayo yanakwamisha mno maendeleo ya Bara la Afrika na hasa Afrika iliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Wazungu wa Ulaya Magharibi kwa wastani wanaishi miaka 78 badala ya miaka 35 ya Afrika.

Pato la mtu kwa mwaka katika Ulaya ni Dola 30,000 wakati Afrika pato la mtu kwa mwaka ni Dola 470 tu. Matajiri milioni 25 wa Marekani wanadaiwa kuwa na kipato sawa na watu bilioni mbili kwa nchi masikini zilizopo Afrika Kusini Mashariki mwa Bara la Asia na *America* ya Kilatino.

Mheshimiwa Spika, ni matazamio ya Watanzania wengi kwamba mjumuiko wa Taasisi zote hizo unamaanisha kuisha kwa umasikini uliokithiri kuelekea 2025.

Taasisi hizi zinatakiwa kushirikiana kuboresha maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii badala ya kurudufiana shughuli zake na mwisho kusigana na kuhitilafiana. Wingi wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii bado haujaondolea wananchi wa kawaida zigo kubwa la umaskini uliokithiri.

Mpaka sasa ni asilimia 39 tu ya wananchi wanaopata huduma ya maji ya bomba na inafahamika pia kwamba kuna asilimia 44 tu ya kaya zilizopo Tanzania ambazo zinaendelea kutumia maji yasiyo na usalama wowote ule hasa kutokana na visima na chemchem mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Kanuni muhimu ya upangaji mipango ni pamoja na kufanya tathmini za mara kwa mara za mipango husika, kuangalia upya mpango mzima kwa lengo la kuboresha yaani review au hata kutupilia mbali mpango usiotekelezeka. Kujua mipango ambayo inawezekana kutekelezwa, kufuatilia utekelezaji wake na matatizo mapya ya njiani na kuchukua hatua sahihi za kuuboresha au kuacha kabisa ni kukomaa na kutaalamika kimipango na si dalili ya unyonge au ujinga. Ni dalili ya kuimarika kuifanyia maamuzi.

Hivyo tunaishauri Serikali kuwa, kutenda kosa sio kosa ila kosa ni kuendeleza kosa au kurudia kosa ambalo limeshaonekana. Tunaamini kabisa kuna mipango ambayo inalazimishwa kutekelezwa lakini haitekelezeki.

Kutokana na kubadilika kwa sera na mazingira ya nchi yetu, tunaomba kwa manufaa ya nchi yetu u-*turn* ni kitu kinachowezekana na sio cha ajabu katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la ubinafsishaji yapo mafanikio na matatizo. Yapo maeneo Ajira zimeongezeka, yapo maeneo mapato na kodi zimeongezeka. Lakini yapo pia matatizo ambayo ni lazima yachukuliwe hatua, miongoni mwao ni ile miradi ambayo imebinafsishwa lakini Mwekezaji anasuasua. Kwa mfano *TAFICO* ni dhahiri

kuwa Mwekezaji ameshindwa lakini amekuwa akilindwa kana kwamba TAFICO sio mali ya umma. Matokeo yake bahari inaimaliza *TAFICO. (Makofi)*

Aidha, pale *PSRC* inapowajibika kuwalipa watu haki zao au mafao yao kwa mfano *Morogoro General Supplies Limited* ambao wanadai Sh.5,778,360/=, huu ni mwaka wa tano hawajalipwa haki zao na wanaendelea kuzungushwa kila siku.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba ipate maelezo juu ya hatua iliyofikia Serikali baada ya kutuma Tume mbalimbali *TAFICO.* Pamoja na Kamati ya Fedha na Uchumi kwenda kuona mradi huu, ni hatua gani zilizochukuliwa na Serikali juu ya maendeleo ya *TAFICO?* Aidha, Waziri atueleze ni kwa nini hadi leo wadai wa *Morogoro General Supplies* hawajalipwa fedha zao?

Mheshimiwa Spika, tathmini, Kambi ya Upinzani kama tulivyotangulia kusema kuwa kazi yoyote isiyofanyiwa tathmini, kuna tabia ya kuendelea kufanya makosa yale yale kila wakati. Hivyo kambi ya upinzani inaomba kupata taarifa juu ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji ambayo ndiyo ingetupa mwanga wa tunakokwenda kwani sasa tunaingia kwenye kubinafsisha masharika nyeti kama vile *NMB, TRC, TANESCO* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika uuzaji wa hisa za Serikali inaonekana hakuna uwazi wa kutosha. Aidha hakuna mawasiliano baina ya Wizara husika yaani *PSRC* na mmiliki wa hisa za Serikali yaani HAZINA.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze hizi hisa 25 kati ya 50 zilizouzwa za *Williamson Diamonds* zilikuwa za kiasi gani na ni wazabuni wangapi walijitokeza kununua hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, hatuna budi kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuvutia wawekezaji kuja nchini kwetu kuwekeza. Hii sio kazi rahisi hata kidogo. Maana katika dunia hii ya ushindani kila mmoja anavutia kwake.

Mheshimiwa Spika, lakini nilidhani pia tunapofanya hivyo kila wakati tunatanguliza maslahi ya Taifa mbele na zaidi kujiuliza ni kwa wastani gani Watanzania watafaidika na uwekezaji huo. Kwa mfano, tunapompa mwekezaji uhuru wa kukopa bila ya sisi kujua kwa undani masharti ya mkopo. Muda wa malipo na kama kweli kiwango kilichokopwa ndicho kinachohitajika au uhuru wa kununua mitambo ambayo wakati mwingine huwa imekwishatumika au kuongezewa bei marudufu. Au kumpa mwekezaji uwanja wa ndege wa Kilimanjaro kwa dola 1,000 kwa mwezi wakati ndege moja ikitua uwanjani hulipa si chini ya dola 2,000 kwa saa moja.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hali kama hiyo haiwezi kuwa na manufaa kwa Mtanzania. Hivyo Kambi ya Upinzani inaomba kama ile tathmini ya uwekezaji imekwishafanywa Waziri atueleze ili tujue kasoro zetu na mafanikio yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na masuala mengi juu ya uwekezaji wanapouza miradi waliyowekeza kwenda kwa mwekezaji mwingine, hasa kuhusiana na mapato. Kwa mfano mzuri ni *SHERATON* alipotoka na kuingia *Royal Palm.* Pale mwekezaji baada ya kufanya biashara kwa muda wa miaka mitatu au minne anapouza au kubadili jina la mmiliki na hivyo kuingia mkataba mpya na Serikali, kitu ambacho tunataka kuelewa ni je baadhi ya msamaha ya kodi aliyopewa mwekezaji wa kwanza inatolewa kwa mwekezaji wa pili au mkataba na Serikali kuhusiana na ulipaji wa kodi wa Serikali unabaki kama ulivyokuwa mwanzo? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango na maendeleo ya nchi kuwa endelevu utumiaji wa takwimu sahihi ni kitu muhimu sana. Kitengo cha Takwimu, *National Bureau of Statistics* ni muhimu sana. Hivyo kukiimarisha Kitengo hiki ili kiweze kukusanya takwimu sahihi katika sekta zote za huduma na uzalishaji kwa mipango ya maendeleo yetu. *(Makofi)*

Vianzo vya takwimu ni suala la kutilia mkazo. Kwani takwimu zinaweza kuwa sahihi lakini chanzo chake si sahihi kulingana na sekta husika. Hivyo Kambi ya upinzani inasisitiza kuwepo na umakini wa katika kupanga vyanzo vya hizi takwimu ili kuondoa upotoshaji katika upangaji mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja katika jumuiya mbalimbali za kimataifa hivyo, takwimu zetu za maendeleo, uzalishaji na huduma za jamii ni lazima zifanywe ulinganisho na zile za mataifa mengine. Aidha, matumizi yake hayana budi kushabihiana na mipango ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani ina wasi wasi mkubwa kuhusu baadhi ya takwimu zitolewazo hapa nchini, mathalani zile zinazosema mkazo wa Dar es Salaam kuishi kwa siku unahitaji shilingi 350/= zinatosha, wakati za kimataifa zinasema kuwa kwa hali ya kawaida mtu kuishi kwa siku anatakiwa apate angalau wastani wa dola moja. Yaani shilingi 1,150/=.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inaomba ielimishwe ni kwa nini hatutumii vigezo vya kimataifa ambazo zinaelezea hali halisi kuliko hizi takwimu zetu. Takwimu kama zilivyo hata kama zikiwekwa au zikipelekwa mpaka kijijini bado hazitakuwa na maana. Kitu kikubwa ni uchambuzi wa takwimu hizo ili ziweze kueleweka kwa wananchi au katika sekta husika kwa matumizi ya maendeleo ya sekta hiyo. Hivyo kambi ya upinzani inashauri mamlaka husika kutoa uchambuzi wa takwimu hizo na madhara ambayo yanaweza kutokea kutokana na mwelekeo wa takwimu. Kwa njia hiyo tutaweza kuchukua tahadhari mapema au kujipanga vizuri zaidi. Gharama kubwa za mawasiliano katika Serikali. Kuna matumizi makubwa sana ya simu katika Idara za Serikali na ukiangalia ankara za simu zinatisha. Na hii inatokana na ukweli kwamba dunia sasa ni mawasiliano na simu ni mojawapo. Hivyo Serikali haiwezi kufuta hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinachoitwa *Public Automatic Branch Exchange,* Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii ya mawasiliano hili nadhani sio geni kwake.

Hivyo Serikali inaweza kupunguza matumizi yake ya simu kama itawekeza kwenye kuhakikisha Wizara zote za Serikali zinaunganishwa kama ilivyo mtandao wa kompyuta na *internet.* Hili linawezekana kwa kutumia *public automatic branch exchange* kitu kikubwa ni kuangalia nikiwa vipi na ni Wizara gani zinaweza kutumiwa kama *pilot project.* Kambi ya upinzani inaamini kabisa kuwa huko tunakokwenda kutakuwa na matumizi ya *audio* na *video* hivyo tujiandaye katika kuingia ndani ya teknolojia hiyo ambayo itatupunguzia sana gharama za mawasiliano Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu nzuri za mapato na matumizi ya nchi zinategemea ni jinsi gani Wahasibu na Maboharia wake walivyo *qualify.* Kutokana na tatizo la nyanja hiyo ya watendaji katika Idara za Serikali imekuwa tukipoteza mamilioni ya fedha kutokana na uzembe au kutokuelewa kazi kwa Wahasibu ambao hawana sifa au walioko ni wachache kulingana na wingi wa kazi katika Serikali pamoja na uaminifu mdogo wa watendaji.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inaomba kufuta si chini ya bilioni 50 kutokana na kasoro hizo nilizozitaja. Kambi ya upinzani bado inaamini kabisa kwa Tanzania ina Wahasibu na wana Maboharia wengi wenye sifa ambao wamesomeshwa kwa fedha za Serikali. Lakini wameacha kazi na kwenda kufanya kazi kwenye makampuni binafsi kutokana na malipo yatolewayo na Serikali yasiyoridhisha mahitaji yao ya kila siku. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali iajiri Wahasibu na Maboharia wenye sifa na malipo yao yaendane na ya wale walioko kwenye makampuni yasio ya Serikali. Kitu kinachoondoa uwezekano wa kuhama Serikalini na kupandisha ari ya kiutendaji wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hii hata Wakaguzi wa Mahesabu nao malipo yao yanatakiwa yaangaliwe upya ili kuondoa uwezekano wa vishawishi vya kurubuniwa na kutoa taarifa zisizo sahihi. Hivyo ongezeko la malipo yao ni kitu cha muhimu kwa uwajibikaji na utendaji wa Serikali. Pamoja na hali hiyo, Kambi ya upinzani inawapongeza Wahasibu na Wanaboharia wanaochapa kazi pamoja na malipo madogo wanayopata.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia karibu bajeti zote za Serikali utaona kuwa ununuzi wa matengenezo ya vifaa ni matengenezo ya vifaa yanachukua karibu asilimia 80 ya kila mwaka. Lakini kitu cha ajabu na cha kushangaza ni kwamba Serikali inaanangalia na kushughulikia sana upotevu wa fedha wakati upotevu wa vifaa ni mkubwa sana. Tunashauri Serikali iweke watendaji wazuri na wenye sifa katika utunzaji wa vifaa vya Serikali na kudhibiti utoaji holela wa mali za Serikali kwa matumizi ya binafsi.

Mheshimiwa Spika, *CTB* na *MTB*. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha na Manunuzi, *Finance and Procurement Act,* Zabuni za wazi hutangazwa kwenye magazeti, baada ya hapo mwombaji hutuma maombi sehemu husika na baadaye maombi yake kupitiwa kwa maana ya kuchambua na kuona ni nani anayefaa. Uchambuzi huu hufanyika kwa kufuata *tender evaluation government* ambazo ndizo msingi wa kumpata mzabuni baada ya hapo *Central Tender Board* na *Ministerial Tender Board* inatangaza mzabuni au

wazabuni waliochaguliwa kulingana na sifa zilizokuwa zinahitajika. Huu ndio utaratibu wa kuwapata wazabuni, iwapo kuna matatizo Bodi hiyo huarifiwa na kuangalia upya Wazabuni.

Sasa kuna matatizo yanayojitokeza katika *Central Tender Board* kwamba baada ya kutoa maamuzi kwa mzabuni, huwa kunatokea mabadiliko ghafla ambayo yanafanywa nje ya utaratibu wa sheria yaani ile ya *Central Tender Board.* Na hayo maamuzi hutekelezwa iwapo tatizo limejitokeza ni *Central Tender Board* ndiyo inayolaumiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri kuwa wakati umefika kwa Serikali kuwa wazi zaidi hivyo suala la kuingia katika *electron system* kwenye hii *source* ambayo inahusu mlolongo mzima wa kuomba *quotation and evaluation* hii *procurement* ni muhimu sana katika kupunguza urasimu, rushwa na malalamiko. *(Makofi)*

Aidha, kuna faida nyingi kama vile *modernization* kuongeza ufanisi kwa Watendaji, kuongeza mahusiano ya kibiashara na wazalishaji wa bidhaa. Kupunguza gharama za mtu kufanya biashara na Serikali, kitu kitakachoshusha bei ya bidhaa, kuongeza uwezo wa Idara katika kufanya maamuzi kwa haraka na kwa uhakika zaidi. Kama nilivyokwishaeleza kama tutaweza kutumia njia hii Serikali itaweza kupunguza gharama na vile vile wazabuni watakuwa ni wengi zaidi, uwezekano wa kupata *best product and best price* ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika semina iliyofanyika Bagamoyo, mtoa mada kutoka Tejari - Dubai alijitolea kuwafundisha watu wetu *Central Tender Board* na *Ministerial Tender Board* hivyo tunashauri Serikali nafasi hiyo isiiache ikapotea, kwa maendeleo ya nchi yetu huo ni mwanzo mzuri kuingia kwenye *Business* na zaidi kupunguza rushwa.

Mheshimiwa Spika, kitengo cha msajili hazina *(Treasury Registrar)* pamoja na kazi zingine pia hutunza kumbukumbu ya makampuni ambayo Serikali ina hisa. Kitengo hiki ni muhimu sana katika kuhakikisha serikali inapata gawio lake kutokana na kule inakomiliki hisa. Hivyo tunaiomba Seriali ikiimarishe Kitengo hiki ili kifanye kazi iliyokusudiwa. Kambi ya Upinzani kwa manufaa ya Watanzania tunaomba tujulishwe na Mheshimiwa Waziri ni makampuni mangapi mpaka sasa Serikali ina hisa ni hisa ngapi kwa asilimia Serikali inamiliki katika makampuni hayo. Aidha, tunaiomba Serikali ilitaarifu Bunge ni gawio kiasi gani tunalopata kutokana na hisa hizo za Serikali kwenye makampuni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kitabu cha Makadirio ya Mapato kinaonyesha gawio la Serikali kutoka kwa *Other Parastatals* limepungua kutoka sh.4,218,518,186/= mwaka 2002/2003 na kufikia shilingi 1.8 milioni mwaka 2004/2005. Kampuni ya Sigara mwaka 2002/2003 shilingi 1.6 bilioni na sasa hivi inatazamiwa kutoa shilingi 540 milioni mwaka 2004/2005. Kampuni ya bia *(TBL)* ilitoa shilingi 3,486,100,000/= mwaka 2003/2004 mpaka shilingi 1,400,000,000/=.

Kambi ya upinzani inadhani Serikali haiweki watu wa kuangalia na kulinda *interest* zake kwenye makampuni yanayobinafsishwa, kitu kinachowapa mwanya watendaji wakuu ku-*maximize profit on our expense* kwani makampuni mengi hapa ni kama *branch* tu na makao makuu yako nje ya nchi hivyo hesabu zake za faida au hasara zinatunzwa nje ya nchi. Hivyo uwezekano wa Serikali kukosa gawio ni mkubwa mno.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* kwa vipindi viwili mfululizo limeshindwa kutoa gawio kwa Serikali, tunashindwa kuelewa hasa hii inatokana na nini, kwani tunaamini sekta ya bima katika nchi yetu inazidi kutanuka na shirika hilo lina *competitive advantage* kulingana na makampuni mengine yaliyoko kwenye biashara hiyo kutokana na mtandao wake ulioenea nchi nzima. Tunaomba Serikali kwa kusaidiana na sisi Waheshimiwa Wabunge tuliangalie kwa makini Shirika hili, lisije kutolewa bure kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, katika uchangiaji wa hotuba ya Waziri Waheshimiwa Wabunge walitaka kujua na wengine walitoa thamani ya ujenzi wa jengo linalojengwa la benki kuu ya Tanzania kuwa inakadiriwa kuwa zaidi ya 72 bilioni, sasa kitu tunachotaka kuelewa ni je, majengo yote yanayomilikiwa na benki kuu pamoja na jengo hilo jipya yataendelea kuwa chini ya benki au mengine yatakodishwa kwa watu wengine kufanyia biashara? Aidha tunaishauri Serikali iangalie na kubadilisha sheria zake na ianze kumtumia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Auditor General)* afanye kazi za ukaguzi wa mahesabu ya benki kuu badala ya kutumia makampuni ya binafsi, au *Auditor General* awe ana-*verify* mahesabu hayo kutokana na umuhimu na unyeti wa kitengo hicho cha Benki Kuu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa ajili ya kilimo, katika nchi yetu taasisi nyingi bado thamani ya akiba *(deposit)* ni kubwa kuliko thamani ya mikopo *(credit)* kawaida thamani ya mikopo ya benki huwa ni kubwa kuliko thamani ya akiba. Mwaka 2003 ilikuwa mara mili zaidi kuliko mikopo, na ndio maana tukashikilia kuwa ni Serikali peke yake ndio inaweza kuwahudumia wakulima, na ndio maana Serikali ilianzisha *CRDB* ili itoe mikopo vijijini na maalum kwenye nyanja ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, benki zilizoanza kukopesha kwa ajili ya kilimo kama *Standard Chartered Bank,* kambi ya upinzani inashauri:-

Utaratibu wa *Credit Guarantee Scheme* urahisishwe Serikali iuze madeni yake na kutoa ushauri kwa anayetaka kununua aweze kuwekeza kupitia Benki zinazotoa mikopo ya kilimo kama moja ya masharti. Fedha za mradi wa pembejeo zipelekwe kwenye Benki ambazo zina mpango unaoeleweka wa kutoa mikopo kwa ajili ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Serikali ishauri mashirika na asasi zenye fedha za ziada zifungue *account* zao kwenye benki zinazojihusisha na utoaji wa mikopo ya kilimo. Aidha tunaishauri Benki Kuu isaidie kuimarisha utaratibu huo ulioanzishwa na *Standard Charted Bank* wa kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, deni la nchi yetu, la Tanzania inalodaiwa linazidi kuwa kubwa badala ya kupungua, pamoja na makusanyo yetu ya kodi kuongezeka, mpaka mwezi wa Machi 2004, madeni tunayodaiwa ni kama ifuatavyo:-

(i) *Paris Club Group* dola 1,344.23 bilioni;
(ii) *Non-Paris Club Group* dola 918.23 bilioni;
(iii) *Multilateral Instituions* dola 4,576.62 bilioni.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa masharti ya *Paris Club* ni kwamba Serikali inaweza kuuza deni lake kama huyo mdeni atakuwa tayari:-

(a) Kusamehe 2/3 ya deni lake na 1/3 anaweza kuliuza na kukubaliana mdai na mdaiwa.

Mheshimiwa Spika, sharti hili linawezekana kutekelezwa na *Paris Club,* lakini kwa nchi za *Non-Paris Club* sharti hilo ni gumu sana, kwa mfano nchi kama Algeria, Angola na kadhalika siyo rahisi kutusamehe 2/3 ya deni lao. Kambi ya upinzani inashauri kuwa wadai wa *Non-Paris Club* masharti yao yawe tofauti na yale ya *Paris club* ili yatoe nafasi kwa wadaiwa kuweza kusikilizana na wadai.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inauliza kama *co-ordination* katika ukopaji haipo kutachochea ukuaji wa deni la Taifa hivyo *competitive economy* haitafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inashauri kuwa ifanyike tathmini ya kuangalia mahitaji kisekta kwa sasa na baadaye ili pindi Serikali inapokopa basi sekta zote zinazokuwa na mahitaji yanayofanana na kiwango gani cha matumizi kwa sekta, tayari ziwe zimeingizwa katika mpango wa mkopo huo. Aidha, ifanyike tathmini ya kutoka kuhusu *fiber optic backbone, TRC* sasa hivi wana 300 kilomita, mradi uliougharimu Taifa *US dollar 8.2* milioni na mradi uliokamilika na kukabidhiwa kwa *TRC* mwaka 2002. Hivyo Serikali ikishaelewa uwezo wake inaweza kupunguza au kusitisha mpango wa kukopa kwa ajili ya *Institutions* zingine. *(Makofi)*

Kitu kizuri na cha kujivunia ni kwamba sasa hivi Tanzania ina wataalam wengi wa nyanja hizi, na makampuni yenye uwezo wa kufanya kazi hiyo badala ya makampuni ya nje. Mafao ya waliostaafu, ninapenda kutoa pongezi kwa jitihada kubwa zinazofanywa na uongozi wa *PPF* katika uendeshaji wa Mfuko huu. Ubunifu wa mafao ya elimu kwa watoto wa wanachama wanaofariki dunia ni jambo la kujivunia sana. Ubunifu huu, ambao hauna budi kuigwa na mifuko mingine, umekuwa ni faraja kubwa kwa watoto ambao wazazi wao wanafariki na hasa ukitilia maanani ugonjwa wa ukimwi unaolikabili taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ningependa kushauri *PPF* sasa iangalie namna ya kuwasaidia wanachama wake wakiwa bado katika ajira, kwa kuwakopesha ili wanachama waweze kujipatia mahitaji muhimu kama vile nyumba,

mashamba na kadhalika. Pia ni vyema mifuko hii ianze kuweka ndani ya mipango yake namna ya kuwaingiza wakulima ambao ndio wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna watu au waliokuwa watumishi Serikalini na kulingana na sheria za nchi, watu hao walistaafu. Kwa mujibu wa sheria za nchi wastaafu hawa wanapaswa wapate mafao yao mapema iwezekanavyo ili kumudu maisha mapya kama watavyoamua wenyewe. Tuna amini kabisa kuwa Serikali itawalipa wastaafu hao, ila kitu tunachoiomba Serikali ni kuwepo na utaratibu unaoeleweka na wa kudumu *(consistency)* kuhusu lini hasa wanatakiwa kulipwa ili kuondoa usumbufu wa njoo leo njoo kesho na kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi kwa wahusika, kupoteza nauli zao kwenda na kurudi wakati hawarudishiwi hizo pesa ni jambo linalo wazidishia hali mbaya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha, tokea tume ya pamoja ya Fedha ya Muungano kuundwa hadi leo hii hatujapata taarifa yake, hivyo kambi ya upinzani inaomba ipatiwe taarifa ya kujua *formula* itakayotumika katika Serikali mbili kuchangia mfuko wa Serikali ya Muungano kama ilivyoaishwa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar. Kutokana na hali hii tunatoa wito Serikali iangalie na kuyazingatia yale tuliyoyatolea ushauri na pale tulipoona kuna mapungufu na tukataka yarekebishwe, kwani hii ni kwa manufaa ya sisi sote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa tunaingia mjadala wa jumla Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyowaeleza watakaopata nafasi ni wale ambao hawajachangia kabisa na wale waliochangia mara moja tu. Nao ni hawa wafutao:- Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Abdulatif Esmail, Mheshimiwa Emmanuel Kipole na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Naanza na Mheshimiwa Rostam Aziz. *(Makofi)*

**MHE. ROSTAM AZIZ:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Awali ya yote ningependa nitumie nafasi hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Igunga kutoa salam za rambi rambi kwa wananchi wa Ulanga Mashariki na wananchi wa Mbeya Vijijini kwa kufiwa na Waheshimiwa Wabunge wao.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kutumia nafasi hii kumpa pole sana Mheshimiwa Waziri Dr. Kigoda kwa kufiwa na Mzee wake, pole sana. Baada ya kusema hayo, kwa idhini yako ningependa kuendelea kwa kujielekeza katika mchango ambao nimekusudia kuutoa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni katika Wizara hii ya Mipango na Ubinafsishaji. Majukumu makuu ya Ofisi hii au Wizara hii ya Ubinafsishaji na Mipango ni kusimamia uchumi kwa ujumla, uchumi wa nchi yetu. Ninafanya hivyo kwa kufuatilia mwenendo wa bei, kufuatilia ukuaji wa uchumi wetu. Kwa kufuatilia hali ya fedha

nchini, kufuatilia bajeti ya maendeleo kutoka kwa Wizara ya Fedha na pia jukumu la Wizara hii ni kuandaa mpango wa maendeleo.

Jukumu lingine muhimu Mheshimiwa Spika, ni kubuni, kusimamia na kutathmini miradi ya maendeleo. Hayo ndiyo majukumu makuu ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mengine yataongezewa baadaye ya ubinafsishaji na kadhalika. Lakini hayo ndiyo majukumu makuu ya Wizara ambayo tunaijadili hivi sasa. Hali halisi ni kwamba haya majukumu makuu ya Wizara hii hayafanywi ipasavyo. Wizara hii hivi sasa inajishughulisha zaidi na suala la ubinafsishaji na halipo kabisa katika kushughulikia masuala haya muhimu ya mpango wa maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Hiyo ndiyo hali halisi Mheshimiwa Spika, kutoka pale bajeti ya maendeleo ilivyoondoka katika Tume hii ya Mipango basi Wizara hii hivi sasa kazi yake imekuwa ni kukusanya takwimu kutoka Benki Kuu, kutoka Wizara mbalimbali na kuziandika katika vitabu vyake kutuletea hapa Bungeni. Ni kama vile unasoma gazeti vile. Hiyo ndiyo hali ya Wizara hii.

Suala la kuwasiliana na Wizara mbalimbali za kisekta katika kushughulikia masuala ya miradi kipaumbele halipo tena. Sasa ni hatari kwa nchi kama yetu ambayo tunajua matatizo tuliyokuwa nayo. Tuna umaskini uliokithiri, tuna wananchi wanatoka vijijini kuja mijini, hawana kazi.

Tunaingia katika jumuiya mbalimbali pamoja na *East African Community.* Utandawazi lakini hatari ni kwamba hatuna Wizara ambayo inakaa na kupanga jinsi tutakavyokwenda huko tunakokwenda.

Kinachotokea ni kwamba tunababaishababaisha tu na ndiyo maana hata uchumi wetu ambao ulitakiwa kukuwa kwa angalau asilimia 8 kwa mwaka kwa muda mrefu hivi sasa unakuwa ni *roller coster by* 1999 ulikua kwa asilimia 4.7. Mwaka 2000 ulikuwa kwa asilimia 4.9. 2001, 5.7. 2002 ukapanda kidogo 6.2. Mwaka uliopita ukashuka tena 5.6.

Mheshimiwa Spika, huu uchumi haukui ipasavyo na kama tunakuwa hivi basi umaskini utaendelea kuwa ni mkubwa zaidi kuliko hivi sasa. Nchi zote kama si Wizara tunakwenda wapi. Wanakaa wanabuni, wanatengeneza mipango na wanatengeneza *strategies* za kufika huko wanakotaka kwenda.

Sasa kama huna chombo kama hicho katika nchi yetu, hivi nani ana-*co-ordinate* na shughuli hizi za maendeleo nani? Wizara ya Fedha inafanya kazi nzuri sana. Lakini Wizara ya Fedha ina mahusiano na Wizara za Kisekta katika shughuli za mahitaji yao ya fedha tu. Hamna maingiliano ya kusughulikia masuala ya miradi kipaumbele hamna.

Mheshimiwa Spika, kama unakwenda namna hii hatuwezi kufika huko tunakokwenda. Tutakuwa tunababaishababaisha tu hata uchumi huu ulivyokuwa ni zaidi

kwa sababu ya misaada na mikopo ya kutoka nchi za nje. Si kwamba tunatengeneza uchumi hapa ndani ambao utaleta mafanikio ya kukua endelevu, hamna ndiyo maana mnaona hapa unapanda unashuka, unapanda lakini pia haupandi kwa jinsi inavyotakiwa ili kupunguza umaskini. Tunatakiwa angalau tukue kwa asilimia 8 kwa muda kama miaka 10 au 15 ndipo tutakapoona wananchi wetu wanakuwa na hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, hii Wizara ilianzishwa na Sheria iliyoanzisha Wizara hiyo, bado ipo, sasa mimi ningependa Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha atueleze hasa hii Wizara inaelekea wapi. Je, itabakia ni Wizara ya Ubinafsishaji na mwaka kesho ubinafsishaji unakwisha. Je, tunafanya nini baada ya pale? *(Makofi)*

Je, tunarejeshea nguvu zote katika Wizara hii ili iweze kufanya kazi ambayo inapaswa kufanya atueleze. Kwa sababu ubinafsishaji unaendeshwa na *PSRC* wala Wizara siyo muhimu sana katika hilo. Unaweza kuwekwa hata kwenye *Treasury Registrar* kwa sababu hii ni *asset* ya siyo lazima uwe chini ya Wizara ya Mipango. *(Makofi)*

Cha msingi hapa Mheshimiwa Spika, ni Wizara hii kukaa na kuwa na *think tank* ya uhakika ambayo itaandaa mpango wa maendeleo katika nchi hii. Tuna mambo mengi yanatokea ambayo mimi nadhani yanatokea kwa sababu hamna *co-ordination* hana mtu anayeweza kuingilia kati akasema hapa mnakosea. Kwa mfano, hili suala la shilingi, shilingi yetu imeshuka kwa kiasi kikubwa sana katika muda huu mfupi uliopita. *(Makofi)*

Na ukiangalia hupati sababu za msingi kwa nini shilingi imeporomoka namna hiyo. Kwa sababu unapojaribu kuweka thamani ya shilingi unaangalia vitu viwili. Cha kwanza unaangalia urari wa malipo ya nje, *balance of payments,* cha pili unaangalia *inflation rank* yako yaani mfumko wa bei kati ya nchi yako na nchi hiyo ambayo unafanya nayo biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua kwamba urari wa malipo ya nje umeimarika sana. Umeimarika sana kiasi ambacho hivi sasa tuna miezi minane ya mahitaji yetu ya ku-*import* wakati huo huo tunajua mfumko wetu wa bei uko chini sana ukilinganisha na hata nchi tunazofanya nao biashara. Mimi sioni sababu ya msingi kwa nini shilingi inaendelea kuporomoka kama ilivyoporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaoathirika ni wakulima kwa sababu mkulima inabidi aletewe pembejeo kutoka nchi za nje, inabidi matrekta yatolewe nchi za nje na hata majembe ya mkono inabidi yaletwe kutoka nchi za nje. Kwa hiyo analipa pesa zaidi kuliko vile alivyolipa kama thamani ya shilingi ingekuwa imara. Lakini mafuta yamepanda sana, hata usafirishaji umekuwa ghali mno kwa sababu pia thamani ya shilingi ipo chini kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wawekezaji wetu wa ndani wanashindwa kukopa nje leo hii kwa sababu wanaogopa wakikopa nje hii thamani ya shilingi ambayo inaporomoka kila siku watalipa vipi. Sasa tungekuwa na Wizara ambayo inashughulikia masuala ya huko tunakokwenda na imepanga mipango yake vizuri, *strategy* zake vizuri, ingewavuta

shati hawa watu wa Benki Kuu na kusema jamani hii haitoshi. Kama mnadhani kwamba mtakuza mauzo ya nje hamwendi hivyo peke yake, kuna vitu vingine sana vinatakiwa kufanyika. Kuna *intervention* nyingi sana zinatakiwa kufanyika pamoja na kwa mfano, bei ya umeme, bei ya mafuta, mawasiliano yote haya yanatakiwa kuangaliwa wakati huo huo ili kuweza kufanikisha hilo ambalo linapaswa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mimi rai yangu ni kwamba, kama tupo *serious* na tunataka kupiga hatua mbele kimaendeleo na kukuza uchumi wetu kwa angalau asilimia nane na kuendelea basi inabidi tuwe na Wizara *serious* ya Mipango ambayo inafanya kazi kama ilivyokusudia kufanya. Tusipofanya hivyo hatuwezi kufanikisha haya ambayo tunatakiwa kufanikisha na wananchi waliotuchagua hapa. Ningependa kusema kwamba, nitategemea maelezo kamili na ya uhakika ya ama tunaimarisha Wizara hii ya Mipango na kuifanya ifanye kazi ambazo zimekusudiwa au tunasema hii Wizara basi isiwepo tena na tujue tunakwenda vipi katika kuhakikisha kwamba tunafanikisha haya mambo ya kuweka mipango yetu ya maendeleo sahihi na kuwa na *coordination* ya uhakika ili tuweze kwenda mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba siungi hoja mkono na ni kwamba nitasubiri maelezo ya Waziri wakati wa majumuisho na kama sitaridhika na majibu yake, nitakutana naye tena kwenye vifungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa pili katika kuchangia hotuba zote mbili za Wizara ya Mipango pamoja na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutumia nafasi hii kutoa rambirambi kwa familia mbili za Wabunge wenzetu waliotutoka mwezi wa sita na mwezi wa saba. Niombe Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana nikianzia kwenye Wizara ya Mipango Mheshimiwa Dr. Kigoda kwa kazi nzuri ambayo ameionyesha kwa Taifa letu kwa kutupa mikakati ya mipango ya Taifa letu na kuhakikisha kwamba maeneo mengine ambayo kama mashirika ya umma yalikufa hatimaye sasa hivi yanatuwezesha kupata mapato pamoja na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuonyesha matunda yaliyotokana na ubinafsishaji wa mashirika ya umma ukizingatia kwamba mchezo wa tarehe 30/7 wa Wabunge wanawake katika kuonyesha mafanikio ya ubinafsishaji wengine wakawa ni mabwana harusi na wengine ni mabibi harusi kuonyesha wazi kwamba ubinafsishaji umeleta matunda hatimaye wananchi wote sasa wanaelewa. Hapa sasa nikisema hivi, mimi ndiye nilikuwa bwana harusi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Kigoda katika kitabu chake cha hotuba katika cover lake, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri katika kuona umuhimu wa upanuzi wa Chuo cha Mipango kilichopo hapa Dodoma. Ni kweli kimepanuliwa vizuri na kimeonyeshwa hapa, waliona umuhimu wa kuweka bweni kwa kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaochukua masomo toka Mikoani wapate mahali pazuri pa kuweza kujisitiri hatimaye waweze kusoma vizuri, wakitoka darasani waingie bwenini, ukizingatia kwamba walikuwa wanalala Mjini ambao ulikuwa ni usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa kwa kuweka mpango huo wa kuhakikisha kwenye Chuo hiki cha Mipango wameweka bweni ili kuhakikisha kwamba wanafunzi hao wanasoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tujue kwamba Chuo hiki kimoja hakitoshi. Kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri aangalie maeneo mengine maana yake wanafunzi wote wanatoka Mikoa yote ishirini na sita, kutegemea Chuo kimoja tu cha Mipango hakitoshi, basi tumwombe aongeze jitihada zake za kuweka mipango ya upanuzi na huku akiendelea kupanua maeneo haya kwa sababu ana eneo kubwa sasa hivi la kuweka mabweni na madarasa, pia aangalie maeneo mengine kama Mwanza au Kusini ili kijengwe Chuo kingine ili kuwarahisishia wanafunzi kutoka Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, lingine, naomba tu nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri kwa kazi nzuri ya kuonyesha jengo letu la Kilimanjaro hoteli lipo hapa likifanyiwa ukarabati. Ni jengo lililokuwa linatia aibu, ikiwa viongozi wageni wa kutoka nchi za nje wanapita barabara hii wakielekea Ikulu, likiwa limeachwa tu. Lakini sasa inatupa matumaini Watanzania kwamba linatengenezwa, hatimaye Serikali yetu iweze kupata fedha za kodi. Lakini bado nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba, bado kuna jengo moja la *Embassy Hotel.* Serikali inaliangaliaje, lipo katikati ya Mji, linafedhehesha jengo zuri kama lile, sasa hivi hata maua yamenyauka, imekuwa ni vumbi. Kwa kweli naomba basi Mheshimiwa Waziri tulifanyie mikakati ili tuondokane na aibu hiyo. Labda nimwombe Mheshimiwa Waziri anapotoa majumuisho yake basi atusaidie kutueleza hatma ya jengo la *Embassy Hotel* inakuwaje.

Mheshimiwa Spika, pia namwomba Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la ubinafsishaji wa Shirika la Reli. Shirika hili ni shirika ambalo linategemewa sana na wakazi wa Mikoa ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, Mara na Kagera, lakini sasa hivi inasikitisha sana kuona mabehewa ni mabovu, engine ni mbovu, ratiba yote ya usafiri wa reli sasa hivi imevurugika. Nafikiri ni kwa sababu ya kutokana na uchakavu wa reli pamoja na hizi engine. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri wanafanya uharaka gani ili kulikomboa ili shirika kwa kumpa huyu mtu ambaye kwenye taarifa yao wamesema kwamba amepatikana. Naomba atakapokuwa anajumuisha, atueleze ni wazabuni wangapi wameshajitokeza ili waweze kuliweka katika hali nzuri hili shirika letu kwa kulinusuru kutokana na hali lilivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi nyingine kuingia kwenye Wizara ya Fedha. Napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu wawili na Mama mwenzetu

Blandina Nyoni, kwa kazi nzuri sana ambayoamelifanyia Taifa letu, hatimaye tumefika sasa na sisi nchi yetu tunaweza kukusanya mapato yetu ya ndani bila kutegemea misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kuwapa pongezi lakini lazima nije sasa kwenye Mamlaka ya Mapato. Mamlaka hii imetusaidia sana kuona mbele na kutuletea mikakati ambayo kweli sasa hivi tunakubaliana na hawa watu wa Mamlaka ya Mapato kwa kazi nzuri, ubunifu wao mzuri wa kuhakikisha kwamba kazi waliyopewa wameweza kuisimamia vizuri na sisi Tanzania tunatembea kifua mbele. Naomba waendelee na moyo huo wa kumsaidia Waziri Mramba katika Wizara yake kuhakikisha haya mapato ambayo yamewekwa kwenye bajeti ya mwaka huu 2004/2005, yafike lengo na kuvuka kama tulivyozoea sasa kuwa tunaletewa taarifa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba inazidi kiwango cha malengo ambayo mmekisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe pole sana Mheshimiwa Waziri Mramba, Katika Wizara yake yeye anaonekana kwamba anazuia watu wenye tabia ya kutumia fedha ovyo ovyo. Lakini nimwambie lawama zao ni bure, ninamwomba asonge mbele na sisi tupo tayari kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, napenda nipongeze sana utaratibu wa *Cash Budget,* ni mzuri sana japokuwa wengine sasa hivi wanafikia mahali pa kubeza, kwa nini tutumie *Cash Budget? Cash Budget* ni utaratibu ambao unakuwezesha wewe kufanya utaratibu wa kutumia kitu ulicho nacho. Hivyo mimi naunga mkono sana utaratibu huu; kwanza unaongeza ufanisi kwa kuhakikisha kwamba unafanya vitu vyako kwa uhakika kwa sababu huwezi kuweka bajeti ya kitu kwa kutumia msaada kutoka nje kwani mfadhili anaweza akakuahidi, kesho hapa anakuja kukwambia kwamba mimi sina fedha za kukupa. Kwa hiyo, anakudumaza na kuvuruga mategemeo yako.

Lakini sasa utaratibu huu wa kukusanya fedha zetu za ndani ni mzuri, ndiyo maana sasa hivi tunaona utaratibu wa barabara ya Dodoma-Mwanza, makandarasi wapo kazini kutokana na matumizi haya ya *Cash Budget.* Pia Lindi tuna daraja lile, kama tusingeweka ile Bajeti yetu ya kutenga kila mwezi hela yetu ya ndani, mafanikio haya yasingeonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kumweleza Mheshimiwa Mramba kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge tupo tayari kum-*support* kwa hili jambo la kutumia fedha aliyoikusanya na kutumia kwenye matumizi ambayo yeye anaweza kuyapangilia kwa ukamilifu. Mheshimiwa Mramba anaangalia maeneo gani niyape, sasa watu wengine wanabeza wanasema ahaa, sasa huyu anatupangia hivi, anatupa ya mwezi mmoja mmoja, lakini Mheshimiwa Mramba anajua wapi penye kupeleka fedha ya miezi mitatu mitatu na pia wapi pa kupeleka mwezi mmoja mmoja. Hivyo nimwombe tu Mheshimiwa Waziri aendelee na mpango huo kwa kweli sisi tutam-*support* tu na aendelee tu kutekeleza hii Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mramba, kwa kweli kazi kubwa anaifanya ya kukusanya pesa na kuzituma kwenye

Wizara mbalimbali. Katika taarifa yake ya bajeti ya Serikali alisema kwamba hesabu za Serikali ni chafu. Sasa nimwombe Mheshimiwa Mramba sasa aweke mikakati ya kuhakikisha basi anawapa motisha wahasibu kwa sababu tunawasomesha Wahasibu wetu kwenye Vyuo vyetu vya *IFM, TIA* pamoja na cha Arusha, lakini wanapomaliza mafunzo yao wanaondoka Serikalini kwenda kwenye mashirika ambayo kuna mishahara mikubwa. Basi namwomba Mheshimiwa Waziri akae na Waziri wa Utumishi ili kuona jinsi ya kuboresha maisha, mishahara pamoja na marupurupu ya Wahasibu hawa pamoja na hao wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato. Nina uhakika kila mtu anapopewa wajibu wake na huku amepewa motisha yake, ana uhakika kwamba nyumbani anapika nini, atafanya kazi nzuri tu na hawataondoka kwenda kwenye maeneo mengine. Niombe tu turekebishe mishahara yao na tuangalie basi umuhimu wao ni upi ili tuweze kusawazisha mahesabu yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize tu kwamba katika hotuba yake ameeleza kwamba kuna utaratibu mpya umeanza kwa wafanyabiashara kujikadiria mapato yao. Ni elimu gani Mheshimiwa Waziri ameiandaa kuahikikisha imewafikia mapema hawa wafanyabiashara waliopo Vijijini? Kwa mfano, mimi Mkoa wa Mwanza nina Wilaya nane, nina Kata 174, je, hawa wafanyabiashara wanaotoka huko kwenye Kata, elimu wataipata lini kabla ya kuanza kujikadiria mapato yao?

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho, napenda nijaribu kumwomba tu Mheshimiwa Waziri, ni kweli tunakusanya mapato, lakini tunaangalia tunafanyaje kusaidia walengwa ambao wanaingia ndani ya kukatwa hayo makato. Sasa hivi wakati bajeti ya Serikali inapitishwa hapa, gharama ya mafuta ilikuwa Sh. 700/= kwa lita na sisi Waheshimiwa Wabunge katika bajeti yetu nafikiri tulikuwa tumepigia bajeti ya mafuta yetu ya kila mwezi Sh. 700/=. Sasa imefika lita moja Sh. 1000/=, Mheshimiwa Waziri amelizingatia vipi suala hili la kuhakikisha basi ile Sh. 300/= iliyoongezeka itatusaidiaje sisi Waheshimiwa Wabunge tunapoingia basi mwaka 2004/05 ili kuhakikisha tunakwenda sambamba na gharama ya mafuta ilivyokuwa au sijui anatusaidiaje kuhakikisha basi yeye anapata mapato yake lakini na sisi tunakwenda vizuri?

Mheshimiwa Spika, mimi sitaki tena nigongewe kengele ya pili, kwa hiyo niwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wawili kwa mshikamano wao wa kuhakikisha kwamba Serikali yetu wameiweka katika hali isiyokuwa ya kuleta kuomba *Supplementary Budget* hapa kwenye Bunge letu. Ni mara moja tu kati ya mwaka 2000 na natarajia itakuwa mpaka 2005. Kwa hiyo, niwaombe tu basi tunawategemea sana katika kuhakikisha uchumi unapanda na mapato yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hotuba zote mbili na fedha hizo wapewe na waongezewe na zaidi. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF HASSAN ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi kwanza naanza kwa kuwapa pole familia na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki Mkoani Morogoro kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Kasapira. Vile vile nampa pole Mheshimiwa Omar Ali kwa kufiwa na baba yake mzazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba safi kabisa. Urekebishaji na ubinafsishaji wa mashirika ya umma mimi naishauri Wizara i-*privatize all dying state enterprises,* zibinafsisheni zote ambazo zinakufa haya mashirika ambayo ya Serikali. Jaribuni kwenda mwezini mkianguka juu ya nyota pia mshukuru. Kila Mtanzania anamiliki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa jengo la Ofisi ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, mimi naunga mkono sana. Kwa sababu *appearance matters,* jengo halipo katika hali nzuri na kazi yake Wizara hii ni kubwa ya Kimataifa na bora watumie fedha walizokuwa nazo kama mfalme kuliko kuwa mfalme kutumia fedha kama maskini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maandalizi ya mkakati wa kuendeleza sekta binafsi mimi namwambia Waziri kwamba jambo ambalo Serikali imefeli basi sekta binafsi imefanya vizuri zaidi. *I have always believed and I will always believe that private enterprise as the backbone of economic well being of any country in the world. (Makofi)*

Nampongeza Waziri kwa kuzingatia au kwa kuleta ule mkakati wa *smart partnership dialogue* baina ya sekta ya umma na binafsi. Mimi namshauri Waziri kwamba awasikilize yote wanayoyasema, afuate anayoyapenda. Kuendeleza ushirikiano wa Kikanda na wa Kimataifa kwa manufaa ya Taifa, mimi nampongeza Waziri kwa kazi hii hasa ukiangalia kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ina watu takriban milioni themanini na soko la *SADC* bilioni mia tatu. Sisi tukishirikiana wenyewe tutafika mbali, lakini tukitegemea masoko ya Uingereza na nchi za nje hatutafika. Sisi tunataka kuwa ndugu wa mtu mweupe *we want to be the whiteman's brother and not the brother-in-law. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wahenga wanasema ukifeli kupanga basi ujue unapanga kufeli. Tukija katika Wizara ya fedha makusanyo mazuri ya bilioni mia moja na ishirini na moja kwa mwezi mimi naipongeza *TRA* pamoja na Wizara na hii ni kazi ya genius na Mheshimiwa Waziri kwamba *money is the best incentive to make someone do something better. The Ministry should always try to do and improve something somewhere.* Vile vile naipongeza Wizara kwa kuweka mkakati wa kulipa kodi kwa kupitia akaunti za benki, muda ni kitu muhimu sana kwa wafanyabiashara, Waingereza wanasema *time is money.* Vile vile *destination inspection,* ukaguzi wa pale pale bandarini wa bidhaa mimi nafikiri *scanners* ni moja, ni ndogo sana, kutakuwa na msongamano wa makontena, Wizara ingejitahidi kuongeza *scanners* ili kuondoa tatizo hili. Vile vile naipongeza Wizara kwa kuanzisha *green light system* ya kukagua makontena. *The simple job of the Government is to make easier for people to do good and difficult to do bad.* Naipongeza sana Wizara kwa hili.

Mheshimiwa Spika, kuboresha na kurahisisha sheria za kodi mimi naiambia *tax to please and not tax to kill.* Kutokana na udogo wa Zanzibar, *due to the smallness of Zanzibar Island I would like to bring my consideration,* kwamba Wizara izingatie udogo wa Zanzibar na iwekewe *preferential duty rates. Let us never negotiate out of fear but let us never fear to negotiate.* Kuhusu uanzishwaji wa *sub protocol of the establishment*

*of the Custom Union. Custom Union* kuna watu wanaogopa, unaogopa nini? Unaogopa mabadiliko. Cha kuogopa ni kuogopa, *fear fear itself* Waingereza wanasema, watu wengi wanachukia mabadiliko wakati mabadiliko ndio yanayoleta maendeleo nchini. Bila kuvunja nyumba yako mbovu yote utaweza kujenga nyumba mpya pale?

**WABUNGE FULANI:** Huwezi.

**MHE. ABDULLATIF HASSAN ESMAIL:** Marekani wanasema *just do it.* Tusitake kufanya yale waliyofanya mababu zetu. Wakati ule kulikuwa hakuna sayansi na teknolojia, tufanye mapya, tuzingatie ili tupate maendeleo. Utaratibu wa *Cash Budget* mimi naupongeza sana unadhibiti matumizi lakini usitufanye tukashindwa kununua tunachotaka. Utumiaji wa kompyuta, mtandao wa kompyuta katika kutayarisha bajeti na kufanya malipo ni mzuri, lakini wasiwasi wangu, Wizara itakapoomba fedha katika Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri asije akajibu *computer is down.* Wenzetu wana hii *electronic Government, paperless Government.* Kwa hiyo, naipongeza Wizara kuwa na mwelekeo wa kwenda huko na Mwenyezi Mungu ataijalia itaweza. Naomba nizungumzie kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo inaanza kazi yake mwaka huu. Naitakia kila la kheri na ni matumaini yangu kwamba itafanya kazi vizuri, kidiplomasia, ikizingatia faida za pande zote mbili bila kusikiliza watu wa nje. Kuhusu mkakati dhidi ya UKIMWI ambao Wizara imeutaja, Rais Museveni wa Uganda alikwenda hivi karibuni katika Mkutano kule Thailand Bangkok na akasema kwamba utumiaji wa kondom siyo dawa, isipokuwa tujikinge na ngono, tuwe mbali na ngono hasa ngono za haramu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu leseni sita za *Casino* zimetolewa, 219 za *Slot machine* katika Mikoa yote au Miji yote mikubwa ya Taifa letu. Mimi wasiwasi wangu *we should prepare the youth for the future and not make this nation a nation of gamblers. Free speech does not live many hours after free industry and free commerce die. Trade is a plant, which grows where there is a peace, as well as if there is a peace and as long as there is a peace.* Mimi binafsi bila ya kuapa nazipongeza Serikali zote mbili za CCM kwa kuhakikisha kuwepo kwa amani ya kutosha nchini na biashara zinafanyika na shughuli zote zinafanyika na Serikali zetu zinapata mapato kama rekodi ilivyoonyesha ya bilioni 121.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja za Mawaziri wote wawili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba ya bajeti ya hizi Wizara mbili, lakini nitakuwa nalenga zaidi kwenye Wizara moja ya Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia na mimi kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Msalala nitoe salam za rambirambi kwa wananchi wa Majimbo ya Mbeya Vijijini pamoja na Ulanga Mashariki kwa kupotelewa na Wabunge wao katika kipindi cha Bunge hili. Nawapa pole sana na ninawaombea Mwenyezi Mungu awatie roho ya ujasiri na vile vile Marehemu awalaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii ambayo nimesema naichangia ya ubinafsishaji na Mipango. Ninaunga mkono kwa asilimia mia moja japo ninaungana kabisa na maelezo aliyokwishayazungumza hapa Mheshimiwa Rostam Aziz na ambayo yalimfanya asite kuunga mkono. Mimi naunga mkono lakini naunga mkono pia yale yaliyozugumzwa na Mheshimiwa Aziz.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba sasa hivi tupo katika zama za kurekebisha uchumi na hili hakuna anayepinga wala kubisha. Tumekubaliana kubinafsisha na tumekubaliana kurekebisha uchumi wetu. Lakini kwa kweli pia nasikitika kwamba mtazamo wa mwenendo wa njia yetu kwa maoni yangu sioni kama upo sahihi sana. Kama alivyosema Mheshimiwa Aziz kwamba hii Wizara ambayo tunadhani kwamba ingeweza kutusaidia kurekebisha uchumi wa nchi hii na kuweka mipango mizuri tunakokwenda na tunakotoka inafanya mambo mawili la kukusanya takwimu za uchumi na kubinafsisha mashirika ya umma. Sasa imeacha jukumu la msingi kabisa ambalo tunadhani ingeweza kuwa inalifanya na pengine tusingeweza kuwa na maneno mengi ya kuzungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotokea sasa kila mtu ama kila Wizara inabaki pale inafanya mambo yake inavyotaka yenyewe. Ukienda Wizara ya Nishati na Madini na ndiko ninakotaka kuzungumzia, kila mtu anafanya jambo lake anavyotaka mwenyewe, hakuna mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye uchumi wa soko uchumi wa soko. Mimi ninavyojua, sikusoma uchumi, nadhani ni uchumi ambao unamilikiwa na wananchi wa aina zote bila kujali rangi.

Sasa katika uchumi huu nilifikiri kwamba wananchi sasa ndiyo wawezeshwe kujua mambo ya uchumi ikiwa ni pamoja na mikataba mbalimbali ya uchumi inayoingiwa na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza mimi naona tunataka kwenda kwenye uchumi wa wananchi, lakini ninachokiona hapa tunarudi zaidi kwenye uchumi wa *State Controlled Economy* kuliko tunakotaka kwenda. Tunataka kwenda kwenye *Market Economy* na *therefore* kwenye *People Economy.* Lakini vitendo vinaonyesha tunarudi zaidi na zaidi kwenye *State Economy.*

Mheshimiwa Spika, kwa maana gani? Katika mikataba yote hiyo inayofanyika hapa tunaambiwa ni siri, sisi Wabunge tusijue, wananchi wasijue na mikataba hiyo ndiyo mikataba ya kurekebisha uchumi. Sasa tunamrekebishia uchumi nani? Tunamrekebishia uchumi mwekezaji mzungu kutoka nje sisi wenyewe tubaki hatujui chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeleta kilio sana hapa Waheshimiwa Wabunge tunasema jamani mikataba ipitishwe Bungeni tunaambiwa ni siri. Hawataki mikataba sisi tuione na wananchi kwa hiyo wasiifahamu. Mikataba ya migodi yote hatujui ni siri. Kila Wizara inaingia mkataba ni siri, lakini mikataba yote bahati mbaya pengine sisi ama

Waheshimiwa Wabunge wote sijui, sisi ndiyo tuna dosari tunaolalamika kwamba mikataba hii ina matatizo na nyie mnasema haina matatizo it means sisi Waheshimiwa Wabunge tuna dosari hatuelewi. Sasa ndugu zangu hii inanionyesha kwamba badala ya kwenda kwenye uchumi wa watu, sasa tunakwenda kwenye uchumi wa *State* zaidi kwa sababu *State* peke yake ndiyo inataka kujua haya mambo na hii mimi nafikiri si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana mikataba yote ya uchumi wa nchi hii kwa kweli iletwe Bungeni. Nikijaribu kuangalia labda hivi ni kwa nini mikataba hii inafichwa sana, na kwa nini mikataba hii inakuwa na makosa makosa mengi ambayo sisi tunayaona ipo mingi sitaki kuitaja, kila eneo ukitaja kunakuwa na dosari dosari. Mimi nikaanza kujaribu kutafakari labda ni kwa nini mikataba hii inakuwa hivi na kwa nini tunakuwa tunailalamikia sisi. Mimi nikajaribu kuweka sababu zangu hapo kwamba hii mikataba inawezekana kabisa iko katika sura hii kwa sababu ya ujinga na ninaposema ujinga hapa nisieleweke natukana ni kutokuelewa ndiyo tafsiri ya ujinga kwamba hatuelewi tunachokifanya ndiyo maana tunaandika mikataba ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya pili ni nikaona mimi hapa hii mikataba mingine inaelekea inaandikwa kwa sababu za njaa. Nikaanza ku-*qualify* sababu hizi mbili hiyo ya ujinga na hiyo ya njaa. Lakini nimekuta ina-*qualify* zaidi ile ya njaa kuliko ya ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kama ingekuwa pengine wenzetu wanafanya kwa bahati mbaya wangedhani kwamba ushauri wa kuwaambia tushirikiane wote hapa kuibariki na kuikubali ungeweza kusaidia zaidi ili asitokee mmoja wa kulaumiwa wangeleta hapa tukasema hii sawa na hii si sawa rekebisha hivi, fanya hivi tukakubaliana sote. Lakini naona hiyo pengine wenyewe hawaoni kama ni sababu kwa hiyo, hiyo haipo. Ika-*qualify* zaidi hii moja ya njaa kwamba katika mikataba mingi pengine kuna *ten percent* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na pengine naogopewa sasa kwa sababu kama kuna kitu fulani mnaingia mkataba watu wawili mtaweza kugawana vizuri kuliko kufanya umma wote mzima huu hapa itakuwa ngumu. Sasa nikaona pengine hii ndiyo sababu, lakini hata hivyo sisi Waheshimiwa Wabunge kuna yale mambo ya msingi tunaweza tukaletewa hapa tukayabariki yale ya msingi, yale mengine madogo madogo mkafanya huko. Mtaelewana huko.

Lakini yale msingi basi tukakubaliana hapa. Kuna yale mambo ya msingi kama *royalty percentage, three percent* kwetu sisi tunao ni ndogo. Tungekubaliana hapa kwa pamoja tusingemlaumu mtu yeyote, lakini sasa hivi mimi nalaumu hapa sikushirikishwa na wananchi hawakushirikishwa isipokuwa watu wachache katika Wizara ya Nishati na Madini ndiyo wamefanya hayo mambo. Tunadhani kuna matatizo katika utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si nia yangu kulalamika hapa ila nataka kuzungumza tu. Mwanafalsafa mmoja akiitwa Thomas Hopes wa Kiingereza yeye anajua na anaamini

kwamba: “Binadamu katika mazingira yoyote ni wa binafsi.” Binadamu yoyote ukimweka mahali peke yake ata-*attend* kufanya vitendo vya kibinafsi na hii ina *apply* katika mikataba yetu kwa vyo vyote.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka kushauri hapa tunapokwenda kwenye *market economy* na kwa maana hiyo kwa watu kama ninavyotafsiri mimi bila kuwa na utaalam wa kiuchumi ninamaanisha kwa wananchi uwazi uwe mkubwa zaidi na Wizara ya Nishati na Madini itusaidie zaidi kupanga mipango mizuri na waipange hiyo mipango watuletee hapa ndicho ninachoshauri uwazi uwepo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, falsafa ya nchi yetu sasa hivi tunaamini sana katika uwazi na ukweli. Lakini katika suala la uchumi uwazi umekuwa ni dosari hautakiwi why? Huu uwazi tunaousisitiza unaishia kwenye magazeti tu, ndugu zetu wa magazeti nyie sasa hivi mnapata huo uhuru wa *press,* hebu tusaidieni na kuomba huo uhuru wa uwazi kwenye uchumi.

Nyie sasa hivi mnaweza mkaamua mkaniandika mimi nimekula rushwa *nobody asks,* sasa mmeshapata huo uhuru wa kutosha tusaidieni kudai huo uhuru wa uchumi kuwa wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri Serikali ni vyema basi ingeunda chombo maalumu cha kupitia hii mikataba ya kubadilisha uchumi wetu, tunabadilisha kwenye madini. Sipendi kabisa hii kila Wizara inajifanyia jambo lake tu huko, sasa wewe *Engineer* wa madini una ujuzi gani wa kiuchumi au wa kisheria unaokuwezesha kusaini mkataba mwingine wa kufanya biashara. Ninashauri kiundwe chombo ilikuwepo Tume ya Mipango zamani, sijui *PSRC* wana kazi yao ya kurekebisha Mashirika yaliyokufa, lakini pengine kiwepo chombo kingine, *TIC* nao wapo lakini wana shughuli zingine za kutangaza na vivutio na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kiwepo chombo kingine madhubuti kama Negotiation Instrument yaa nchi hii kama alivyosema Rostam Aziz *a think tank of this country* watakaokuwa wanatusaidia kuchambua *issues* hizi na hii lazima ijumuishe kanda mbalimbali Wanasheria wawemo, Wafanyabiashara, Wanauchumi, Wanamazingira, Wanasiasa na kadhalika ndiyo watakaotusaidia kuingia mikataba. Kwa sababu kuna mikataba mingine nasikitika sana kusema muda wenyewe ni mdogo hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali mingine haipiti ofisini kwake au kama inapita pengine sijui kuna mingine tumehoji sisi nayo mingi hafahamu. Sasa kiwepo chombo ambacho kitatusaidia kuingia mikataba na wenzetu wa nchi za nje katika uwekezaji katika nchi hii, lakini *ultimately* maamuzi yao lazima yafikishwe lazima kwenye Bunge hapa tuamue kwa pamoja. Tukiamue kwa pamoja *at the end of the day* hakuna mtu atakayemlaumu mwenzake au sijui wenzangu huko upande wa mbele mnafurahi tunapolalamika, natumaini hamfurahi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini mnataka sisi tuendelee kuwalaumu. Fungueni milango ya uwazi na uwazi uwe mkubwa zaidi ili tuweze kushiriki, na sisi tukipata

*information* sahihi hapa hata wananchi kwa ujumla nchi nzima tutawaelekeza jamani uchumi wetu unaenda hivi. Hata hayo malalamiko wanayotangaza kwa wananchi kwamba uchumi wanasema unakua mbona nyie mnakuwa maskini pengine tungekuwa na majibu. Lakini sasa hivi mimi mwenyewe nashangaa migodi imefunguliwa mingi uchumi unachangia kwa *two point nine percent* kutoka kwenye migodi yote. Nilitegemea pengine tungekuwa na chombo cha namna hii tungeweza kujua pia kwamba baada ya muda gani sekta fulani itachangia kwa kiasi fulani kwenye uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika hoja zilizotolewa leo. Lakini mchango wangu zaidi nitauelekeza katika Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba na mimi uniruhusu nitoe pole na rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki Marehemu Capt. Theodos James Kasapira, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia katika maeneo machache tu. Kwanza nianze na eneo la malipo ya pensheni ya wastaafu. Napenda nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa niaba ya wastaafu wa Wilaya ya Kondoa kwa mambo mawili. La kwanza, ni hatua ambayo imechukuliwa na Serikali kuongeza kiwango cha pensheni ya chini kufikia shilingi 20,000/= kwa mwezi. Napenda kuishukuru Serikali kwa kuwajali wastaafu wake na kuweza kuwaongezea kiwango hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni hii hatua ya Serikali ambayo imechukuliwa katika bajeti ya mwaka huu. Serikali imechukua hatua ya kurejesha wastaafu waliochukua pensheni zao kwa mkupuo kwenye orodha ya wastaafu. Kwa hiyo, napenda kuishukuru sana Serikali pamoja na Wizara ya Fedha kwa hatua hiyo ambayo imechukuliwa. Lakini pia wastaafu wana maombi yao au wana ombi lao. Unakumbuka kwamba huko nyuma wastaafu walikuwa wanalipwa kila mwezi lakini kutokana na kiwango kidogo cha pensheni iliyokuwa inalipwa kila mwezi wastaafu waliomba walipwe kwa kipindi fulani na kwa makubaliano Wizara ya Fedha ilikubali kwamba wastaafu walipwe kwa kipindi cha miezi sita sita na huu ndiyo utaratibu ambayo unafuatwa hadi leo. Sasa kutokana na hatua ya Serikali kuongeza kiwango cha chini cha pensheni wastaafu hasa wa Wilaya ya Kondoa wanaomba Wizara ya Fedha iangalie upya kipindi cha kuwalipa hiyo pensheni yao, hawaombi warejee utaratibu wa zamani, lakini wanaomba ikiwezekana basi hiyo pensheni ilipwe kila baada ya miezi mitatu. Kiwango cha shilingi 60,000/= nafikiri ni kiwango kizuri cha kuweza kuwalipa wastaafu wetu kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa gharama halisi huko nyuma tatizo lilikuwa kiwango kilikuwa ni kidogo sana ndiyo maana wastaafu waliomba kwamba walipwe kwa kipindi kirefu zaidi kwa sababu kiwango cha shilingi 10,000/= kilikuwa ni kidogo mno, lakini sasa kuna kiwango cha shilingi 20,000/= na kwa miezi mitatu zitafika shilingi 60,000/=.

Gharama ya kwenda kuchukua pensheni hiyo kiwango cha juu kabisa ni shilingi 10,000/= kwa hiyo bado watabakiwa na shilingi 50,000/= mfukoni. Kwa hiyo , wanaomba sana ikiwezekana pensheni hiyo ilipwe kwa miezi mitatu mitatu. Hilo ndiyo ombi la wastaafu wa Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ambalo ningependa nilichangie ni matatizo ya Shirika la Bima la Taifa. Nilikuwa mengi ya kuchangia lakini kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana hatua ambazo amechukua hadi leo sina mengi sana ya kuchangia. Nimeona kwamba jitihada zimefanyika kuweza kulipa madeni ya Shirika hili na kwa sasa hivi kama Mheshimiwa Waziri alivyofafanua ni kwamba amekwishaona Shirika hilo kupitia *PSRC* wamejitahidi kulipa madai ya wateja wake kwa kiwango cha shilingi bilioni 8.732. Napenda nilipongeze sana Shirika na pia niipongeze *PSRC* kwa kusimamia vizuri suala la kulipa madeni ya Shirika letu la Bima. Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia katika ukurasa wa 54 hadi 55 utaona bado deni ni kubwa sana. Bado deni la Shirika la Bima kwa wateja wake ni kubwa sana ukijumlisha madeni yote utaona kwamba Shirika hili linadaiwa bado shilingi bilioni 14.502. Kwa hiyo, bado Shirika lina deni kubwa sana. Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu kwa kifupi ni kwamba basi *PSRC* ichukue hatua za haraka za kuweza kuuza mali za Shirika hili na kuweza kulipa madeni ambayo ni ya muda mrefu sana. Mimi katika Jimbo langu na Wilaya ya Kondoa ninao wateja wa Bima ama wateja wa Shirika la Bima la Taifa wapatao zaidi ya 500 ambao Bima zao za maisha zimeiva na hasa ni walimu ambao bima zao zimeiva, lakini kwa zaidi ya miaka mitano mpaka sasa hawajalipwa. Hao watu walipochukua bima hizi walikuwa na malengo ya kusomesha watoto, walikuwa wana malengo ya kujenga nyumba zao, walikuwa na malengo ya kuanzisha miradi lakini sasa wamekwama. Kwa hiyo, naomba *PSRC* ifanye haraka ama ivute kasi ili hao wateja waweze kulipwa katika kipindi cha mwaka huu ili waweze kujifanya shughuli zao na waweze kujiletea maendeleo yao na waweze kufikia malengo ambayo wamejiwekea. Hivi sasa wamekwama, kwa hiyo naomba sana jitihada zifanyike katika suala hili la kufuatilia madeni haya ya Shirika la Bima la Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, ambalo ningependa nilichangie ni hatua ambayo ilichukuliwa na Serikali mwaka jana kufuta kodi za kero katika Halmashauri zetu. Napenda nirejee ama nirudie tena kutoa shukrani za dhati kabisa kwa uamuzi wa Serikali kufuta hizo kodi za kero. Hizo kodi zilikuwa na athari mbalimbali. Watu walikuwa wananyanyaswa, wengine walikuwa wanakamatwa, wengine walikuwa wanawekwa ndani na kadhalika na kadhalika. Hizo kero sasa hivi zimefutika.

Aidha, mwingine walikuwa wananyimwa hata huduma ukienda hospitali unaanza kuambiwa kwanza hutoe stakabidhi ya kodi ya maendeleo ndiyo uhudumiwe hizi kero sasa zimefutika. Kwa hiyo, napenda niishukuru sana Serikali. Lakini hatua hii pia ina athari kwa Halmashauri zetu na mimi kwa sababu sina uzoefu na Halmashauri nyingine nitazungumzia juu ya Halmashauri ya Kondoa kama mfano. Sisi tumeathirika sana kutokana na kufutiwa kodi mbalimbali ambazo zilikuwa ni za kero. Lakini wakati Serikali ilipoamua kufuta kodi hizo pia iliahidi kwamba itafidia, ndiyo suala la msingi ambalo nataka kuzungumza. Serikali iliahidi kwamba itatoa fidia halisi ili Halmashauri zetu zisitetereke katika wajibu wake. Sasa kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya

Kondoa sisi tumeathirika sana kwa sababu hatukupewa fidia halisi, narudia hatukupewa fidia halisi, tumepewa fidia kidogo mno kiasi ambacho kwamba sasa shughuli zetu nyingi zimesimama.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba sisi uwezo wa Halmashauri wa kukusanya mapato kwa wastani nachukua ya miaka minne hivi ilikuwa ni wastani wa shilingi milioni 372 kwa mwaka. Kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka 2003 tulikuwa na uwezo wa kukusanya fedha ama kodi shilingi milioni 372. Kiwango cha vyanzo vya mapato tulivyobakiziwa sasa hivi baada ya Serikali kufuta kodi hizo za kero tumebakiwa na vyanzo ambavyo vinaweza kutupa shilingi milioni 29 tu. Kwa hiyo, upungufu halisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ni shilingi 343.4 ndiyo upungufu. Sasa fidia tunayopata ni kiasi gani, fidia tunayopata hivi leo shilingi milioni 264 kwa mwaka. Kwa hiyo kuna upungufu wa shilingi milioni 80 ambayo hatulipwi ama hatufidiwi. Sasa matokeo yake nini? Athari zake ni kama zifuatazo: -

Kwanza, Halmashauri imeshindwa kulipa mishahara ya watendaji wake hasa watendaji wa Kata na Vijiji. Pili, Halmashauri imeshindwa kuchangia katika mifuko mbalimbali hasa ile ya vijana na wanawake kwa sababu uwezo ni mdogo. Tatu, Halmashauri imeshindwa kuchangia miradi hasa ya wahisani ambayo lazima huchangie kwa kiwango fulani. Nne, Halmashauri imeshindwa kutekeleza miradi yake yenyewe. Tano, Halmashauri imeshindwa kuitisha vikao vya kisheria na mwisho kabisa Halmashauri imeshindwa kulipa posho za Madiwani. Kwa hiyo tatizo hili limekuwa ni kubwa. Kwa hiyo mimi natoa mfano wa Wilaya ya Kondoa lakini inawezekana kuna Halmashauri nyingine lakini ndiyo hali halisi ya Halmashauri zetu. Sasa mimi ombi langu na ushauri wangu ni kwamba Serikali hizi takwimu zipo kwenye kitabu hiki na mimi sikuyatoa kichwani. Orodha ya majedwali yaliyoambatanishwa na hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka huu ukurasa nafikiri wa 43 kila Halmashauri imeorodheshwa. Kwa hiyo, naomba mtumie takwimu hizi wakati kutoa fidia msitoe *figures* vichwani kwa sababu tunaathirika. Naomba hili ombi. Kwa kuwa katika hoja yangu nimesema kwamba tumepata ama tumepunjwa kwa shilingi milioni 80 naomba Wizara ya Fedha itupe hizo shilingi milioni 80 ili tuweze kulipa madeni naomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo. Naomba nizungumzie kidogo mradi mmoja ambao unaitwa *Local Government Support Programme* huo mradi mwaka huu una shilingi bilioni 12.4. Lakini masharti ambayo yametolewa katika mradi huu ni yafuatayo:- Mengine ni magumu kweli kweli kwamba hizi bilioni 12.4 huwezi kuzipata isipokuwa kwa kutekeleza yafuatayo:- Nachukua yale magumu tu, mengine ni ya utaratibu wa kawaida. Moja, hesabu za mwisho zilizokaguliwa zisiwe zimepata hati chafu kwenye Halmashauri. Pili, kusiwe kumegundulika usimamizi mbaya wa fedha tangu ukaguzi wa mwisho wa Halmashauri. Tatu, mikutano ya Halmashauri kufanyika angalau kila baada ya miezi mitatu. Nne, Nafasi ya Mkurugenzi iwe imejazwa. Tano, nafasi ya Mweka Hazina iwe imejazwa hakuna Kukaimu na mwisho nafasi ya Mkaguzi wa Ndani iwe imejazwa katika kila Halmashauri ndiyo utapata hizo fedha. Kama hutekelezi hayo huwezi kupata. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake sasa hivi ni kwamba Halmashauri zilizopata sifa ya kupewa fedha hizo ni Halmashauri 47 tu.

Mheshimiwa Spika, Sasa ukitoa idadi ya Halmashauri ziko ngapi na ngapi zimekosa ama zimenyimwa. Sasa mimi najaribu kuhoji hivi kweli hizi fedha zinazotolewa si kwa ajili ya kuboresha Halmashauri kwa ajili faida ya wananchi? Sasa kwa nini tunawaadhibu wananchi ambao hawana makosa. Hivi mwananchi anaweza kuja kuweka mahesabu sawasawa ama mwananchi ana uwezo wa kuajiri Mkurugenzi, lakini wewe unamwekea kigezo kwamba usipomwajiri Mkurugenzi basi hupati fedha hizo. Kwa kweli hili si sahihi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sijawahi kusikia Wizara hata moja inanyimwa fedha, Wizara ngapi zinapata hati chafu hapa lakini zinapewa fedha. Kama hili ni sharti la Wahisani naomba mwende mkarejee kuzungumza nao, hayo ndiyo amezungumza hapa Mheshimiwa Emmanuel Kipole kwamba tusaini mikataba bila ya kuisoma. Hii ni kati ya mfano mojawapo ambapo mikataba imesainiwa na masharti yameletwa na wafadhili mkakubali. Kwanza, sharti la kuajiri Mkurugenzi sisi hatuna uwezo Halmashauri. Halafu pili, tukisema hatuna Mkurugenzi au hatuna mtumishi fulani wanakwambia mpaka ungoje kibali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalikizika)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetolewa asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa mara nyingine tena ione umuhimu wa kulipa posho kwa Wazee ambao walipigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1939 hadi 1945.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa pensheni kwa wastaafu ni mbaya sana kwani wanaostaafu hupata shida wakati wa kufuatilia hundi zao. Baadhi yao huishiwa hata nauli ya kutoka wanakopanga kwenda Ofisi ya Fedha. Naishauri Serikali ikiimarishe na kukiboresha Kitengo cha Idara ya Pensheni. Lugha chafu sana kwa wastaafu kama wametenda kosa kustaafu kazi. Wastaafu walipwe mara tu wanapostaafu. Ucheleweshaji malipo ni kujenga hisia ya kudaiwa rushwa.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zinazopelekwa mikoani, ziwe wazi. Viwepo vigezo vya utoaji fedha mikoani. Bila vigezo, bado kutakuwa na wasiwasi wa

namna ya ugawaji huo na kuona mikoa mingine kuwa Serikali haiwatendei vema. Aidha, majibu ya kusema fedha zingine zimejificha mahali, ni jibu la watu wasiojua chochote. Siyo jibu la kitaalam.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kama kuna fedha za miradi katika mikoa fulani, basi Serikali iweke wazi fedha zake. Siyo kutoa jibu la kusema fedha zingine zimejificha mahali, wakati Bunge hili huja wakati wa bajeti kuruhusu mafungu yatumike. Kila mkoa una fedha za maendeleo na miradi pia. Hivyo basi, mafungu yote yawekwe wazi kuondoa hisia za upendeleo kwa baadhi ya mikoa hasa ile ya Kanda ya wakubwa wanakotoka.

Malipo ya pensheni kwa miezi sita, sita, ni vema malipo ya miezi ya toka Julai hadi Desemba. Wastaafu walipwe mwezi Januari kwa lengo la kumsaidia mstaafu kulipa karo kwa watoto wa shule na hata kilimo. Kwani wanapolipwa mwezi Februari mwishoni, huwa wamekwisha pata matatizo ya kutumia fedha hizo; kwani Shule nyingi za Msingi na Sekondari, hufunguliwa mapema mwezi Januari ya kila mwaka. Wakati huo malipo ya pensheni bado kutolewa. Naishauri Serikali ilifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, Wahasibu nchini waongezewa maslahi yao. Hii itawafanya Wahasibu wazuri watulie katika kulitumikia Taifa lao kuliko hivi sasa Wahasibu wengi walio wazuri hukimbilia kwenye Mashirika yaliyo na maslahi bora. Kutunza mali nyingi, yahitaji moyo na maslahi bora pia. Hapo Wahasibu wengi watafaidika na kutulia. Ahsante.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia hoja hiyo hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyounga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha kwenye ufunguzi wa kikao hiki cha bajeti kwa asilimia mia moja, naunga mkono maombi ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwenye mchango wangu wa awali, nilitambua mkoroganyo uliojitokeza kwenye mapato ya ndani, hususan kwenye ukusanyaji wa kodi wa kujikadiria mwenyewe mtu binafsi. Ambacho kilichojitokeza ni kuwa yule mwenye kumbukumbu sahihi alipaswa kulipa zaidi kuliko yule asiye na kumbukumbu. Lakini nashukuru kuwa hilo sasa limesahihishwa na Mheshimiwa Waziri vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, hivi leo sina budi pia nirejee tena kwenye eneo hilo hilo la mapato ya ndani, ingawa kwenye mazingira tofauti, lakini kwenye dosari ya msingi ile ile. Kumwajibisha mwenye kufuata taratibu za kulipa kodi zaidi kuliko yule ambaye mwenye taratibu hafifu. Hili ni eneo la pato la pango la nyumba *(Rental Income).* Mwenye nyumba moja, tozo lake la *withholding tax* ni 10%. Yule mwenye nyumba nyingi, huwajibishwa tena kwenye *final assessment.* Kwa kampuni hii ina maana ya kuwajibishwa tena kodi kwa 30%.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa hili litaleta mianya ya kukwepa kodi? Je, kwa sababu gani mtu kutobadilisha umilikaji wa nyumba kwa ndugu, marafiki na wabia wengine ili kubakiza kwake umilikaji wa nyumba moja? Gazeti la *Financial Times* la Julai 9, 2004 lilielezea hili vizuri. Nashauri Wizara ya Fedha ilitazame hili upya ili tuimarishe mapato kamili ya nchi bila mabadiliko ya kimbinu ya walipakodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Makatibu Wakuu, Ndugu Gray Mgonja na Ndugu Peniel Lyimo, Manaibu Katibu Wakuu, Ndugu Ramadhan Khijjah na Ndugu Wilfred Nyachia na viongozi wa Taasisi chini ya Wizara ya Fedha, kwa kazi nzuri wanazofanya kuifanya Wizara ya Fedha kuwa moja ya asasi chache Serikalini, ambazo ni kitovu cha ufanisi *(Centre of Excellence).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mengine, ningependa kutambua Mapinduzi mahsusi yanayofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* katika kuboresha mapato. Rekodi ya mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi, kutoka wastani wa shilingi bilioni 25 kwa mwezi, mwaka 1995, yanayopatikana sana na kwa mwezi Juni, 2004 mapato hayo yalifikia kiwango kipya cha juu kabisa cha shilingi bilioni 136.8, hayakupatikana hivi hivi tu. Wahenga walisema, usione vyaelea, vimeundwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania imefanya kazi kufikisha mapato yalipo sasa. *TRA* wamekuwa wabunifu kweli kuongeza mapato. Pamoja na kujiimarisha kimuundo kama kuanzisha Idara za *VAT,* walipa kodi wakubwa, uchunguzi, mawasiliano ya kisasa na kuanzisha *One Shop Center* kwa malipo ya kodi zote na kuwawezesha watumishi kuwa na ujuzi wa kodi zote, Mamlaka ya Mapato imefanya yafuatayo:-

(a)Kuainisha walipa kodi kimaeneo *(block system)* kwa madhumuni ya kusimamia vizuri zaidi ulipaji wa kodi.

(b) Kuweka *TV monitor* katika sehemu nyeti za kulipia kodi, kama *long room* na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam.

(c) Kuweka *X-ray Scanner* bandarini ili kurahisisha usimamizi wa bidhaa ziingizwazo nchini kutoka nchi za nje.

(d) Kuweka *flow meters* katika bandari zetu za kupima mafuta yaingizwayo nchini.

(e) Kuanzisha utaratibu mpya wa kusajili magari.

Mheshimiwa Spika, mikakati hii na mingine mingi, imekuwa ya kimapinduzi kweli kweli, kwani imelenga kuziba mianya ya wakwepa kodi na kuongeza mapato. Matokeo yake ndiyo hayo ya kiwango cha shilingi bilioni 136.8 zilizopatikana mwezi Juni, 2004 kiwango ambacho ni cha juu kabisa tangu *TRA* ianzishwe. Hiki ni kiwango ambacho ni zaidi ya mara tano ya shilingi bilioni 25 zilizokuwa zinakusanywa hadi mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, lazima tutambue mchango huu mkubwa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kuchangia na kuimarisha maendeleo ya wananchi wetu na katika utawala bora. Sasa hivi nchi yetu imejijengea heshima kubwa mbele ya mataifa kwa kujizatiti katika kujitegemea. Sasa hivi tunaweza kubuni, kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa kutumia fedha zetu tu kama ujenzi wa barabara za Kitaifa, za Kanda ya Kati, mradi wa maji ya Ziwa Victoria kupelekwa Miji ya Kahama na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu una uwezo wa kutupatia mapato mengi zaidi. Ni matumaini yangu kwamba upo uwezekano wa kufikia viwango vya shilingi bilioni 150 mpaka shilingi bilioni 200 kwa mwezi, vya makusanyo ya kodi. Kwa mikakati na ari ambayo Mamlaka ya Mapato inayo, naamini ipo siku watafikia viwango hivyo. Nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha juu ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali na Watendaji wote walioko chini yake.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naomba tu mambo yafuatayo yatekelezwe na pia nipewe taarifa ya utekelezaji umefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri anifahamishe wakati wa majumuisho yake, amefikia wapi wa kupitishia mishahara ya Walimu na Watumishi wengine *NMB*. Zoezi hili limechukua muda mrefu na wafanyakazi wanazidi kuumia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie kutokana na malalamiko ya wananchi, ni sababu zipi zinafanya bei ya saruji, mabati na kadhalika kutofautiana kati ya Dar es Salaam na mikoani. Mbona bia na soda zinazozalishwa Dar es Salaam, bei ni moja nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Mheshimiwa Waziri aliahidi na kutamka Bungeni ya kwamba Mikoa kame ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Tabora na kadhalika itaingizwa kwenye mpango maalum utakaofadhiliwa na *ADB* kwa ajili ya kuboresha kilimo, mawasiliano, afya, elimu na kadhalika. Mpango huu ambao ulikuwa unashughulikiwa na Hazina wakishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, umefikia

wapi? Mbona tunasikia sasa hivi unatekelezwa Mikoa ya Kagera na Kigoma tu? Wizara yake sasa hivi ina mpango gani wa kuisaidia hii mikoa kame?

Mheshimiwa Spika, naupongeza sana uongozi unaosimamia Mfuko wa *Tanzania/Japan Counter Party Fund,* kwa kazi nzuri wanayofanya. Huu ndiyo mfuko pekee unaowagusa wananchi vijijini na tunaomba uendelee. Kuna tetesi ya kwamba fedha za mfuko huu zinataka kubadilishwa na zifanye kazi nyingine. Nashauri Mheshimiwa Waziri msifanye makosa hayo kwa sababu mtakuwa mmewanyika huduma wananchi wetu kupata maji, kilimo, elimu, afya, mawasiliano na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu unalegalega kwa ajili ya Wizara ya Kilimo na Chakula, kutousimamia vizuri. Naleta pendekezo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba mfuko huu sasa uwe chini ya Hazina moja kwa moja ili usimamizi uwe imara na mzuri. Pia napendekeza mifuko yote inayohusu fedha iwekwe chini ya Hazina mara moja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kusikitisha ni madeni yaliyoachwa na *ATC.* Nyumba zilizokuwa mali ya *ATC,* Shirika lililoanzishwa kisheria, zilichukuliwa na Serikali kienyeji badala ya kuuzwa na kulipa madeni. Kwa sababu Serikali ilikwisha zichukua, basi itoe fedha ili wanaoidai *ATC* walipwe.

Mheshimiwa Spika, ndege zetu zilikamatwa Nairobi na Afrika Kusini. Madeni yaliyokuwa yanadaiwa na nchi hizo, yalilipwa haraka sana.

Mheshimiwa Waziri, nakushauri utumie busara zako ili madeni haya yalipwe haraka, kwani wananchi hawana uwezo wa kukamata mali za *ATC* (Serikali), bali wanasubiri huruma yako. Kwaheri.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ubinafsishaji na timu zao za utendaji, zikiongozwa na Makatibu Wakuu, kwa hotuba zao za bajeti na hasa uendeshaji wa Wizara zao kwa ufanisi wa mifano. Napenda kuchangia kwenye suala la *excess liquidity* kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa zisizo rasmi kwamba ilipofika Machi, 2004 *excess liquidity* ilikuwa imefikia shilingi bilioni 960. Kati ya hizo,shilingi bilioni 600 ni fedha za Kitanzania nashilingi bilioni 360 ni fedha za kigeni *(foreign currency).*

Je, kuna ukweli wa kiasi gani kwenye hili? Asilimia 90 ya *local currency component* inasemekana inaenda kwenye Benki tatu, *NMB* shilingi bilioni 283, *CRDB* shilingi bilioni 169 na *NBC* shilingi bilioni 84. Benki hizi huwekeza kwenye *Government Securities.* Kwa hiyo, kwa sehemu kubwa, fedha ya *excess liquidity* hazileti faida kubwa kwenye uzalishaji. Changamoto kubwa ni jinsi gani *excess liquidity* ilete maendeleo kwenye uzalishaji na Serikali bado iwe na fursa ya kudhibiti *inflation* bila ku-*recycle liquidity.*

Mheshimiwa Spika, kuna mawazo na dhana ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Viwanda. Haya mawazo ni mazuri na yanastahili kufanyiwa kazi. Kuna mawazo mengine mazuri ya kuanzisha *deposit instruments* kwa ajili ya sekta ya kilimo. *Non-Bank Financial Institutions* zingehamasishwa kuwekeza kwenye *instruments* hizi. Hili pia linaweza kufanyiwa kazi na Wizara na wadau wa taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, *discount rate* ya Banki Kuu *(BOT)* ni kubwa *at 13 + %.* Hii ndiyo inakuwa kigezo cha *rates* zingine. *BOT* wanaombwa wafikirie kupunguza hii *rate.* Lakini pia *T-bill rate* nayo itabidi ishuke kwa sababu nayo ni kigezo muhimu cha *rate* zingine *commercial.*

Mheshimiwa Spika, naunga miono hoja hii.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali. Wizara imefanya kazi nzuri ya kukusanya fedha za kodi kukidhi mahitaji ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa matumizi ya fedha hizi ni dhaifu sana, hususan katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Hii kwa kiwango kikubwa inasababishwa na kutokuwepo kabisa kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani *(Internal Audit)* au pengine vitengo hivyo havina watendaji wenye uwezo wa kitaaluma.

Aidha, naunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi ya kuundwa kwa *Expenditure Authority* ambayo itawajibika moja kwa moja Bungeni. Serikali iifanyie kazi rai hii kupitia Wizara ya Fedha na kuona uwezekano wa kuunda Mamlaka hiyo ili kuboresha matumizi ya fedha za Serikali kwa kuwawajibisha kwa karibu *Accounting Officers* wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Procurement Account.* Kumekuwepo ukiukwaji wa hapa na pale wa sheria hii, na aidha utekelezaji wa vipengele vingine, unaleta ucheleweshwaji mkubwa katika kufanya manunuzi, hususan kwa Mashirika ya Umma ambayo yanatakiwa kufanya kazi kibiashara na kwa ushindani, hali ambayo inahitaji kufanywa maamuzi ya haraka bila kukiuka utaratibu wa kanuni kwa mujibu wa sheria. Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika hayo hufanya tu *post moterm* wakati kama wangalihusishwa tangu awali, makosa mengine yangeliweza kuzuiwa kabla hayajatendwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisema wanafanya mapitio ya sheria hii ili kufanya marekebisho na kuiboresha sheria hii na kwamba Wizara ingelileta marekebisho hayo mara moja. Lakini muda unayoyoma na ukiukwaji unafanywa huku hamna dalili ya kuleta *amendments* ambazo ziliahidiwa. Je, ni lini Wizara italeta *amendment* ya Sheria ya *Procurement Account* ili kusiba mianya iliyojitokeza?

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Mabenki umeendelea kuboreka kwa maana ya kuongezeka kwa *profitability.* Lakini hii peke yake haiwezi kuwa kigezo cha utendaji wa Mabenki katika nchi inayoendelea na ambayo imepania kuleta Mapinduzi ya kiuchumi

kwa haraka, kama inavyotaka Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Mabenki ni lazima yajihusishe katika upunguzaji wa umaskini uliokithiri kwa kutenga sehemu ya mapato yao na kuwekeza katika sekta inayowaajiri Watanzania wengi (zaidi ya asilimia 80%) yaani sekta ya kilimo na hapa siyo kutoa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa mazao tu, bali pia kwa kuzalisha *(primary production)* mazao hayo kwa kutoa mikopo ya kununulia pembejeo na usindikaji wa mazao ya kilimo. Kufanya hivyo kutaongeza kasi ya kutekeleaza mchakato wa Serikali wa kupunguza makali ya umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, aidha, ulipaji wa riba duni kwa amana wakati zikitoza riba kubwa kwa mikopo itolewayo na Mabenki hayo, hakusaidii kuhamasisha azma ya Serikali ya kuongeza uwekaji wa akiba *(mobilization of savings)* kwa maendeleo ya nchi. Benki Kuu imekuwa bubu mno katika suala hili. Wakati umefika kwa Benki Kuu ku-*play a more aggressive role* katika kuhamasisha Mabenki ya Biashara kuwa chachu za maendeleo ili faida wanayopata haitokani na kuwabana wenye amana kwa kuwalipa faida kidogo, bali itokane na kuwekeza au kukopesha kwa miradi ya uzalishaji pamoja na biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Nyumba, nini kinachelewesha uanzishwaji wa Benki ya kuwakopesha watu wanaotaka kujenga nyumba za makazi? Hali ya sasa ya kukosekana kwa taasisi kama hiyo, kunapelekea utumiaji wa fedha taslimu ambazo hazipo. Badala yake, wizi wa fedha umeongezeka ili kukidhi mahitaji ya fedha zinazohitajika na wale wanaotaka kujenga, hasa ukizingatia kuwa wengi wao ni watendaji Serikalini au katika Mashirika ya Umma, ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, napendekeza tena kwamba Serikali ianzishe mara moja Benki ya Nyumba kwa kushirikiana na Makampuni ya Nje ambayo yana uzoefu wa shughuli za mikopo ya nyumba. Wakati ni huu na kuchelewa zaidi ni kuwafanya Watanzania waendelee kuishi katika nyumba duni ambazo ni kielelezo wazi kabisa na kukithiri kwa umaskini. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha utekeleze hili kabla ya kumaliza kipindi chako.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza kwenye sekta muhimu ya fedha ambayo mpaka sasa haijawekewa mkakati bayana wa kuifufua, nayo ni *Mortgage or Housing Finance.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amewahi kuelezea nia ya Serikali kubadilisha *(to convert)* mitaji mfu *(dead assets)* kuwa mitaji hai *(active assets)* ili kuwasaidia wananchi kupambana na umaskini. Njia moja kuu ambayo hutumika ni *Mortgage Market* ambayo hubadilisha mitaji iliyowekezwa kwenye *concretes and motors in form of* majumba kuwa *liquid assets.*

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi ambazo Serikali inaweza kusaidia katika suala hili bila ya kujiingiza moja kwa moja katika biashara. Serikali inapanga katika bajeti yake kujenga majumba kama tulivyoshhudia katika uwekaji wa jiwe la msingi, wa majumba 300 na Mheshimiwa Rais. Mitaji hii kama ipo ndani ya Serikali, ingeweza

kuunganishwa na sekta binafsi kuwa kianzio tosha cha kuanza *Mortgage Market.* Mpango wa kujenga majumba ambayo hayakuzingatia mahitaji ya soko, ni kuelekeza pesa za Serikali vibaya bila ya kuwa na mpango endelevu kama ambavyo ingekuwa katika kuwekeza kwenye *Mortgage Market.*

Mheshimiwa Spika, Serikali imewaanzia wafanyakazi majumba ambayo mengi yako katika hali mbaya *(rehabilitation form).* Kuweka kiwango cha kutoyabadilisha hati kwa miaka 25, kinapingana na sera ya Waziri aliyoitangaza ya kutofanya sekta ya nyumba idumae kwa kuwa ni mitaji mikubwa sana ambayo ni mfu. *Concept* ya *securitization of assets* ni muhimu, izingatiwe kama kweli tuna nia ya kuondokana na mitaji mfu.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri, Watumishi wote na hasa watumishi wa Mapato, kwa kazi yao nzuri wanayoendelea kuifanya ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukusanyaji mzuri wa mapato, bado ukwepaji wa kulipa mapato ni mkubwa. Wizara ingeweza kukusanya mapato hata mara mbili ya sasa, kama usimamizi zaidi utawekwa. Naomba nionyeshe sehemu moja tu ambayo ina fedha nyingi kama zingeweza kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, *VAT* katika uuzaji wa mafuta na Petroli, ni mara chache sana katika vituo vya uuzaji wa mafuta wanatoa risiti. Mafuta mengi yanatumika sana kila siku. Kama kila lita inayonunuliwa italipiwa *VAT,* Serikali ingeweza kukusanya fedha nyingi. Hivi Wizara haioni hili?

Mheshimiwa Spika, kwa nini kituo kisidaiwe *VAT* kwa mafuta waliyoyaleta hapo kituoni yaani *Petrol Station* ikiagiza mafuta na kuyaleta, basi iyalipie *VAT* na wao baadaye wadai kurudisha fedha wanapouza? Kwa namna hiyo hawataacha kutoa *receipt.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kufikiria kufanya marekebisho ya sheria ya manunuzi ya umma. Naomba marekebisho hayo yafanyike haraka ili miradi iliyocheleweshwa na sheria hii, iweze kukwamuliwa haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake wawili na Wizara kwa kazi nzuri mnayofanya ya kudhibiti na kukusanya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifikirie kuanzisha kodi mpya ya Uandikishaji Magari Nchini (Kodi ya Kifahali - *Luxury).* Hii itakuwa kwa wale wenye uwezo na kupenda fahari ya kujulikana, waweze kupewa namba maalum za magari

binafsi zenye kuonyesha majina yao kwenye *plate number* za magari. Mfumo huu unatumika nchini Uganda na umesaidia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiwango kikubwa. Ni kwamba gari badala ya kuwa na namba hizi zinazotumika, yenyewe baada ya kulipiwa ada maalum ya kiwango cha juu, *plate number* inaandikwa jina la mwenye gari. Mfano, gari ya Nyaburi, *plate number* isomeke Nyaburi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iweke ada kati ya shilingi 500,000/= hadi shilingi 1,000,000/= kwa atakayependa kuweka namba hii maalum kwenye gari yake na mmiliki akiwa na gari zaidi ya moja na zote anapenda kuwa na namba ya aina hii, basi iwe kwa jina hilohilo, labda Nyaburi 1, Nyaburi 2 na kuendelea. Kwa jinsi ninavyoona, Watanzania wengi wenye uwezo wataweka namba hizi maalum na hivyo kuchangia fedha nyingi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili lifanyiwe kazi hata ikibidi kutuma wataalam Uganda kuangalia mfumo huu unavyofanya kazi. Nadhani ni mpango mzuri kwa kuzingatia pia kwamba sote tuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na tunafanya kazi kwa kujifunza mafanikio mazuri ya nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Asante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria ya *The Public Procurement Act, 2001* ina kasoro hasa katika Halmashauri za Wilaya, Bodi ya Zabuni *(Tender Board)* ina Wajumbe wachache, akiwemo *DED* (Mwenyekiti), ndio wanaoamua zabuni zote katika Wilaya. Pia hata katika Serikali Kuu, utekelezaji wa miradi kutangaza (zabuni) ni siku 45, je, Serikali ina mpango gani wa kuleta marekebisho ya Sheria hiyo Bungeni ili kuirekebisha na kuondoa kazoro zilizopo?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi ya *TRA* Wilayani Mpwapwa? Tayari Wilaya imekwisha tafuta kiwanja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kodi ya *VAT* katika miradi ya maendeleo? Kwa mfano Mkoa wa Dodoma ulitengewa shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kutengeneza barabara kwa bajeti ya mwaka 2003/2004. Kati ya fedha hizo,shilingi milioni 258 zilikatwa kodi ya *VAT.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kukwepa kulipa kodi ni kosa la jinai na kuinyima mapato Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kutunga sheria kali ya kudhibiti hali hiyo ya ukwepaji kodi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mawaziri wote wawili, Naibu Mawazili, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara mbili za Mipango/Ubinafsishaji na Fedha, kwa kazi nzuri ya maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kwanza nauelekeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Mchango huu unahusu kudumaa kwa uchumi na mipango ya maendeleo ya Wilaya ya Same, Mkoani Kilimanjaro. Wilaya ya Same ndiyo Wilaya yenye eneo kubwa kiutawala. Eneo lake ni zaidi ya kilometa za mraba 5,700,000. Ukubwa huu ni mara mbili ya eneo la Wilaya ya Mwanga au Rombo au eneo la Wilaya ya Same linalingana na eneo la Wilaya ya Mwanga na Rombo au Rombo na Hai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukubwa huo wa eneo la Wilaya ya Same, lipo tatizo la kijiografia la Kanda ya Milima ya Mashariki ya Same na Magharibi ya Same. Hali hii ya kijiografia ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya Wilaya ya Same. Ili kukabiliana na vikazwo hivi viwili na kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, Halmashauri ya Wilaya ya Same na Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Kilimanjaro *(RCC)* imeomba Wilaya hii igawanywe kulingana na majimbo ya uchaguzi ya sasa, Same Magharibi na Same Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo huo utatupatia Wilaya mbili, ambapo Mji wa Same utaendelea kuwa Mji Mkuu wa Wilaya kongwe ya Same na Mji wa Ndungu utakuwa Mji wa Wilaya mpya ya Same Mashariki. Mgawanyo huu utaweza kuboresha programu inayohusu dira ya Taifa ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 na mpango wa muda wa kati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa mwaka 2004/2005 hadi mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, swali kwa Mheshimiwa Waziri ni kuwa mkakati huu wa kugawa Wilaya ya Same hautafanyika juhudi za Wilaya hii (kama zinginezo Tanzania) za kukuza uchumi na kupunguza umaskini, zitawanyima wananchi wa Same haki yao ya uchumi wao kukua na kuondokana na umaskini? Naomba hili lipatiwe majibu ili wananchi wa Wilaya ya Same wajue ni lini wilaya yao hii itagawanywa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili unahusu Wizara ya Fedha. Kule katika Wilaya yangu ya Same, kuna fedha za uhamisho za Walimu ambazo zimeletwa Wilayani, lakini Walimu hao hawakulipwa. Kule katika Wilaya ya Same, fedha ya uhamisho wa Walimu wa Shule za Msingi, ambazo hawakulipwa, lakini ilitumwa shilingi 94,600,000/= wakati ukiichanganya na ile ya mishahara, matibabu na masomo ni shilingi milioni 162.

Mheshimiwa Spika, inasemekana fedha hiyo imetumwa Wilayani, lakini Walimu hao hawakulipwa. Hesabu hii ni tofauti ya ile ya Walimu wa Shule za Sekondari. Agizo la Waziri Mkuu limekuwa ni faraja kwa Walimu, lakini halikuhusisha eneo lile la fedha

iliyotumwa kwa Wilaya husika, lakini Walimu hawakulipwa. Naiomba Wizara ihakikishe inafanyia kazi madai haya ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja zote mbili na kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha, iliyotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba hii kwa umahiri na ufanisi mkubwa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utendaji mzuri wa Wizara ya Fedha, naunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia moja. Sambamba na kuunga mkono hoja hiyo, napenda tena nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwahakikishia wanahisa wa Benki ya Wananchi ya Mbinga *(MCB)* kuwa Benki hiyo ni mtoto halali wa sera sahihi ya Chama cha Mapinduzi ya kupeleka huduma za fedha kwa wale walioikosa. Wakati wa uzinduzi rasmi wa Benki hiyo, Mheshimiwa Waziri aliwakilishwa na Naibu Katibu Mkuu ambaye aliiwakilisha Wizara vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo linalofanya Wilaya ya Mbinga isiendelee ni kukosekana kwa umeme. Gharama za uzalishaji na utoaji huduma mbalimbali ni kubwa sana, pamoja na huduma za Benki. Wananchi wa Mbinga wamenituma nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha akope fedha mahali popote duniani ili Wilaya ya Mbinga ipate umeme. Wajukuu zetu wataridhika na kuwa tayari kulipa deni hilo pale watakapoambiwa deni hilo lililenga kuleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri hasa kutokana na mtazamo wake wa kutumia fedha kwa lengo la kuzalisha fedha zaidi. Naomba atupe kipaumbele ili wazalishaji wa Wilaya ya Mbinga waweze kuzalisha zaidi.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa mara nyingine unahusu zao la korosho ambalo hulimwa katika mikoa zaidi ya minane ya Tanzania. Zao hilo ndiyo tegemeo kubwa kiuchumi kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Wilaya ya Tunduru, Mkoani Ruvuma. Suala lililopo kwa zao la korosho hivi sasa si upanuzi wa kilimo cha korosho, bali uboreshaji wake; kwani nchi hii ina idadi kubwa ya mikorosho ambayo inazaa korosho.

Mheshimiwa Spika, utafiti mkubwa umefanywa juu ya zao la korosho kupitia vituo mbalimbali vya utafiti, vikiongozwa na Kituo cha Utafiti wa Mazao cha Naliendele, Mtwara. Nachukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Kituo cha Utafiti cha Naliendele, Mtwara, chini ya Mkurugenzi wake Dr. Shomari, kwa kazi nzuri ya utafiti wa zao la korosho. Kazi kubwa imefanywa kuanzia ya utafiti wa mbegu bora, magonjwa mbalimbali na dawa za kutibu magonjwa. Aidha, napongeza juhudi za kituo hicho za

kueneza elimu ya uendelezaji wa zao la korosho katika maeneo mbalimbali kupitia Vituo vya Uendelezaji wa zao hilo *(CDC's).* Matokeo yake ni wananchi wengi sasa kudai dawa za kutibu magonjwa ya mikorosho.

Mheshimiwa Spika, licha ya hali hiyo, inaonekana Serikali haijatekeleza ahadi zake nyingi za kuendeleza zao la korosho nchini. Pamoja na Serikali kutumia fedha nyingi kwenye utafiti wa zao la korosho, bado haijatoa fedha za kutosha ili kufufua kwa kasi kubwa zao la korosho. Sasa tunajua kuwa tunahitaji pembejeo za kutosha kwa ajili ya zao la korosho, lakini hatuna mipango thabiti ya kuhakikisha kuwa pembejeo hizo zinapatikana kwa wingi, ubora na wakati unaotakiwa. Bado Serikali inawategemea wafanyabiashara binafsi katika usambazaji wa pembejeo na dawa za zao la korodho, kitu ambacho siyo sahihi kabisa. Ikiwa wafanyabiashara hao watafanya uzambe wa kutoagiza pembejeo hizo au kuagiza kidogo sana kuliko mahitaji, ni kuua zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma niliwahi kusema humu Bungeni kuwa mkorosho mmoja ambao umetunzwa vizuri na umepata pembejeo za kutosha, una uwezo wa kutoa kilo 50 za korosho. Kwa bei yashilingi 500/= kwa kilo moja ya korosho ghafi, mkorosho huo humpmatia mkulima shilingi 25,000/=. Kwa Wilaya kama ya Masasi ambayo inayo mikorosho milioni tano, mapato ambayo yanaweza yakapatikana kutokana na korosho ni shilingi bilioni 125 za Tanzania. Je, kwa Tanzania nzima, mapato si yatakuwa makubwa zaidi?

Naomba Serikali basi ichukue hatua za dhati katika kulifufua zao la korosho, kwani ndiyo njia ya haraka au ya muda mfupi ya kuleta maendeleo kwa wananchi wengi wanaolima zao hilo na wengi zaidi ambao wameajiriwa na kujiajiri na kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba, wanaelewa umuhimu wa zao la korosho. Hivyo nina imani kubwa kwao kuwa haya yote watayavalia njuga na kuyapangia mipango mizuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine muhimu juu ya zao la korosho ni la ubanguaji wa zao hilo. Serikali imeeleza mara nyingi juu ya wawekezaji kukosekana kwenye Viwanda vya kubangua Korosho. Kwa nini tungoje muda wote huo kusubiri wawekezaji wa nje kuja kuwekeza katika viwanda hivyo? Kwa nini Serikali isiwasaidie Watanzania wenye utaalam wa kuviendesha viwanda hivyo, lakini wamekosa mitaji ili waviendeshe? Watanzania wengi sasa wanajua kuviendesha viwanda, kinyume na huko nyuma wakati wa Azimio la Arusha. Naomba Serikali iwaamini Watanzania kwa kuviendesha viwanda vya korosho hivyo, iwasaidie tu kupata mitaji na masoko.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, mimi sina maneno mengi sana maana hata nikisema vipi tayari mmeshapanga mipango yenu na fedha mmeshaelekeza katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, labda niwapeni maeneo ya kutilia maanani bajeti ijayo ya mwaka 2005/2006, bila kujali kama nitarudi Bungeni. Lakini nikirudi nitakukumbusha na kusimamia maombi yangu haya. Maeneo ninayoomba yatiliwe maanani katika Jimbo la Mtwara Vijini na kupeleka fedha zaidi ni kuhusu tatizo sugu la maji.

Kuna maradi wa uchimbaji mabwawa, Bwawa la Nyundo na Mbamba Kofi, hayajakamilika. Linahitaji mipango ya kukamilishwa na fedha za kutosha. Mabwawa tunayotaka yatengewe fedha za kuchimba ni Bwawa la Maramba, Maranje, Mtiniko, Kiromba, Nachuma, Mbemba, Magomeni, Njengwa, Mangopachanne, Mnima, Madimba, Naumbu na Kawawa. Tunaomba iingizwe katika mipango ya ujenzi wake. Licha ya hayo, kuna mradi wa maji ya bomba kutoa maji Kitere kupeleka Kara ya Mnima, Njengwa, Nitekela, Nanyamba na Mtiniko. Aidha, kuimarisha mradi wa maji Chikodoli, Mnyawi, mradi wa maji Mbuo Mkunwa na wa Naumbu una matatizo ya kusimama sana kutoa huduma. Uimarishwe.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu umeme Nanyamba na vijiji vya Mbuo, Msijute, Hiyari, Ndumbwe na Mpapura, wawekwe kwenye mipango ya kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, tatu ni mipango ya ujenzi wa barabara za Hiyari - Dihimba - Njengwa - Nanyamba, Mtwara - Nanyamba - Newala - Masasi, Mangamba - Kitinya - Mnongodi - Chikwaya, Madimba - Msimbati, Mpapura - Kitere - Chemchem na Mbuo - Muungano - Malohi - Dihimba.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu mpango wa ujenzi wa Shule za Sekondari za Serikali. Naiomba Wilaya ya mwanzo Mtwara Vijijini iwe miongoni mwa Wilaya za kwanza maana tuna Sekondari moja tu.

Mheshimiwa Spika, tano, ni kuhusu uchimbaji wa gesi ya *Mnazi Bay.* Mipango iharakishwe na sita ni kuhusu mipango ya ubanguaji korosho, kutafuta masoko zaidi na ujenzi wa Kiwanda cha *Surphur,* Mtwara kiharakishwe.

Mheshimiwa Spika, saba ni kuhusu mipango ya kututafutia soko la muhogo ni muhimu na nane ni kuhusu mikopo kwa wakulima na wazee. Mipango iharakishwe.

Mheshimiwa Spika, tisa ni kuhusu mikopo ya wavuvi. Kuwe na mpango mahsusi wa kuanzisha mfuko wa mikopo kwa wavuvi ili wavuvi wanufaike, pia kuwe na mipango sahihi ya Serikali ili Watumishi Walimu na Watumishi katika Zahanati zetu waongezwe pamoja na kuongeza madawa.

Mheshimiwa Spika, kuwe na mipango ya kuboresha Wizara ya Maliasili ili waweze kuajiri *Game Scouts* kila Kata Mtwara Vijijini, ili kudhibiti wanyama wakali na waharibifu wa mazao ya biashara na chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa kivuko vya kudumu cha Kilambo, kinachovusha toka Tanzania kwenda Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu mipango ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mtwara ili kupunguza adha ya kufuata huduma hii Dar es Salaam, Mbeya au Moshi hasa ukilinganisha na uwezo wa kiuchumi kwa walio wengi, hauruhusu kuuguzana mbali ya makazi ya mgonjwa au muuguzaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nazipongeza hotuba zote mbili za Waheshimiwa Mawaziri. Kazi kubwa iliyo mbele yao ni kusimamia ipasavyo yote yaliyowasilishwa. Hata hivyo, ninayo maoni machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Wizara zote mbili ni kuweka mipango thabiti na endelevu itakayosaidia kuwaondolea Watanzania walio wengi umaskini uliokithiri. Kwa mpango uliowekwa na Serikali wa kuweka sehemu moja ya kuingizia mafuta toka nje (Dar es Salaam) pamoja na njia hiyo kusaidia kudhibiti mapato ya Serikali, lakini kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera ambao hapo awali tulikuwa tukiingiziwa mafuta kupitia Kisumu na hivyo bei ya mafuta kuwa nafuu kutokana na gharama ndogo za usafirishaji, mpango huu sasa utatuweka kwenye umaskini zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa bei ya petroli Mjini Bukoba imefikia shilingi 1,200/= kwa lita na kama inavyoeleweka, bei ya mafuta ikishapanda, bidhaa nyingine zote na huduma gharama zake hupanda mara moja. Kama Serikali imenuia kweli kuwasaidia wananchi wa Kagera waondokane na umaskini, jambo hili liangaliwe kwa umaskini. Tusiumie kwa sababu ya kukaa mbali na Dar es Salaam. Vinginevyo iangaliwe njia mbadala ya kutusaidia kwa kuangalia mambo tunayoweza kunufaika nayo kutokana na huduma tunayoipata kwa eneo tulilopo. Kwa mfano, bei ya umeme kwa Kagera iwe pungufu kutokana na ukweli kwamba umeme tunaoupata toka Uganda, ni nafuu kuliko ule wa *TANESCO* ambao umewekewa pia gharama za *IPTL.* Vinginevyo, Serikali ituwekee ruzuku ili kuleta ulinganisho sahihi na maeneo mengine kwa huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kukitolewa taarifa za upungufu wa Wahasibu ndani ya Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi nyinginezo. Jambo hili limekuwa likiisababishia Serikali upotevu mkubwa wa fedha kwa kisingizio cha kutokuwa na Wahasibu wa kutosha. Ni vema Serikali ikaangalia namna na taratibu zinazotumika kuwasajili Wahasibu.

Mheshimiwa Spika, chombo pekee ambacho kimekuwa kikitambuliwa katika kuwasajili na kuwatambua Wahasibu ni *NBAA.* Kwa taratibu walizojiwekea, ni chombo hicho tu kinachotoa na kuwatambua Wahasibu hata kama kuna watu wamesomea taalum hiyo katika nchi nyingine au taasisi nyingine. Ni vema ili kuondoa ukiritimba na wakati mwingine mazingira ya rushwa na kukomoana taasisi zetu nyingine kama Vyuo Vikuu, ni vema pindi mhitimu katika field ya Uhasibu anapokuwa ameshinda vizuri mitihani yake, akatambuliwa moja kwa moja badala ya utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo ni vyema Serikali ikatupia jicho nini kinaendelea huko *NBAA,* kinachosababisha Wahasibu wengi washindwe kufaulu na kusajiliwa, lakini wakati huo huo nchi za Kenya na Uganda zinasajili Wahasibu wengi kwa mwaka. Nawasilisha.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha kwa kuamua kusomesha Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri hapa nchini. Hii ni muhimu, kwani sasa ruzuku kwa Halmashauri toka Serikali Kuu ni kubwa. Hali hii imewezesha sasa Halmashauri zilizopata hati safi kuongezeka. Nawapongeza sana kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu baadhi ya Wabunge wamekuwa wakilalamikia mgawanyo usioridhisha wa rasilimali za Taifa kwa mipango ya maendeleo, ambapo baadhi ya mikoa ilionekana kupendelewa na mingine kudumazwa na kupunjwa. Mikoa iliyoonekana kupewa mgao kidogo ilikuwa Kigoma, Shinyanga, Tabora, Singida na Rukwa na mikoa iliyoonekana kupendelewa ikiwa ni Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kufanyia kazi malalamiko hayo na kuja na utaratibu mpya wa kugawa rasilimali kwa mikoa. Nashukuru kuwa Serikali imekiri hivyo na sasa Mkoa wa Shinyanga mgao umeongezeka, wakati ule wa Arusha unaonekana kupungua.

Mheshimiwa Spika, nashauri mambo mawili katika mgao huu. Moja, wananchi wasiadhibiwe kwa vigezo ambavyo hawana *control* navyo. Kwa mfano, kutotoa mgao kwa sababu Halmashauri haina hati safi, si sahihi, kwani Serikali ndiyo inatakiwa kupeleka watendaji wazuri kwenye Halmashauri na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ili kuwa na *fair playground,* juhudi za makusudi lazima zifanywe na Serikali kuhakikisha kuwa mikoa iliyo nyuma kimaendeleo, inainuliwa na kupewa nyenzo wakati huu wa mpito, badala ya kuondelea kuelekeza rasilimali katika mikoa iliyoendelea kwa kisingizio cha kukamilisha miradi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, wakati akichangia hotuba ya bajeti tarehe 16 Juni, 2004, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa alisema, nanukuu: "Tuwe na Mamlaka ambayo ina sura ya Kitaifa, tusiwe na Mamlaka ambayo inaonyesha kwamba kuna kundi fulani ndilo lenye nafasi ya kupewa pale hayo Mamlaka ... Kwa hiyo, mimi naliomba hilo aliangalie, maana hatuwezi kuweka mkate wa Serikali hii kwenye kundi fulani tu na tukasema kwamba linakuwa salama." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kauli hii ilimuudhi sana Waziri wa Fedha na alikasirika sana wakati anafanya majumuisho. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kuwa yeye ni mtu wa dini, lakini hata Kanisani kuna ufisadi. Kwani wote tu mashahidi wa kesi ya wizi wa sadaka katika Kanisa moja Jijini Dar es Salaam, wakati wa Pasaka. Nakubali pia kuwa ni mwana CCM safi na kada mzuri, lakini hata CCM kuna sera ya kujikosoa na kujisahihisha. Inawezekana yale yaliyoko katika Wizara yake na Sekta ya Fedha,

hayaoni kwa sababu hakuyaunda yeye au labda tu hataki kuyaona. Sitaki kuwa na *innuendo* kama alivyosema, nitafafanua ili afumbue macho na kama kuna tatizo, alifanyie kazi. Najua yeye si mkabila, lakini sura ya Wizara na asasi huonyesha hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Fedha, kuna Maafisa Waandamizi 15 ambao wote wanatoka Mkoa wa Kilimanjaro. Naomba niwataje kwa vyeo Waziri, Katibu Mkuu - Hazina, Katibu Mkuu - Fedha, Kamishna - Fedha za Nje, Kamishna Msaidizi - Fedha za Nje *(Multilateral),* Mkurugenzi - *Project Audit,* Kamishna Msaidizi - *Fiscal Policy,* Mkurugenzi Msaidizi - Uhakikimali, Wasajili wa Hazina Wasaidizi wawili, *Assistant Accountant General, Financial Coordinator - Union Matters, Coordinator - European Union, Executive Secretary - Anti-Money Laundering* na *National Secretary - Anti-Money Laundering.*

Mheshimiwa Spika, hawa ndio wenye maamuzi katika Wizara na wote wanatoka mkoa mmoja! Lakini pia watumishi wa ngazi za kati wengi wanatoka mkoa huo huo! Kwa mfano, 91% ya wafanyakazi wa Idara ya Fedha za Nje, hutoka huko huko Kilimanjaro. Hii ni hatari hasa kama mdudu rushwa ataingia katika Wizara hii. Lakini pia ni hatari kwani kutatokea kurithishana kama tutaangalia mle mle ndani, kwani itakuwa *automatic promotion!*

Mheshimiwa Spika, naomba nitofautiane na Mheshimiwa Waziri aliyesema suala liwe je, *is he performing?* Nadhani ni wengi wanaoweza ku-*perform,* wakati huu ambapo wengi wamesoma. Suala ni kupewa nafasi ili uonekane una-*perform,* kwani Kiongozi Mkuu eneo fulani siyo lazima awe na akili au busara kuliko wengine. Yeye ni msimamizi tu! Napendekeza Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi hili.

Mheshimiwa Spika, sina mengi sana kuhusu *TRA,* lakini Mheshimiwa Waziri mwenyewe kasema, nanukuu *Hansard* ya tarehe 18 Juni, 2004: "Wakuu wale wa Mikoa ni 15% ndio wametoka Mkoa wa Kilimanjaro, ingiza Wapare wote na Wachaga na wengine wanaotoka mkoa ule pamoja na Wahindi na Waarabu wanaoishi mkoa ule ..."

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa tuna mikoa 21, kama mkoa mmoja tu una 15%, ni dhahiri mingine iliyobaki inagawana 85% iliyobaki! Huu ni upendeleo wa mkoa huo mmoja ama kwa makusudi au bila kujua! Lakini pia 80% ya Makamishna katika *TRA* wanatoka pia mkoa huo huo, hawa ni pamoja na Kamishna Mkuu, Kamishna wa Forodha, Kamishna wa *VAT* na Kamishna wa Elimu kwa walipakodi! Mapato mengi ya *TRA* yanatoka Dar es Salaam na hata hapa *RRO Customs Long Room, RRO* Ilala na *RRO VAT,* Dar es Salaam, wote wanatoka mkoa huo huo. Siamini kuwa mambo haya yalipangwa. Lakini kama yalipangwa, basi lazima kuna mtandao unaoashiria rushwa katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, narudia wito alioutoa Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, kuwa Wizara ya Fedha na *TRA* ziwe na sura ya Kitaifa katika kuajiri. Lakini pia natoa wito kwa Mamlaka za uteuzi wa watendaji wasielekeze macho yao tu kaskazini, kwani wasomi sasa wako kila mkoa. Si vema mkoa mmoja kuwa na Mawaziri sita wakati

mikoa mingine haina. Kwa makusudi turekebishe hali hii, tusijenge chuki miongoni mwa watu wetu kwa kuwaona wachache ndiyo wateule.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja kama nitapata maelezo ya kina kuhusu bei ya mbolea na ruzuku inayotolewa kwenye mbolea.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2003/2004, Serikali ilitoa ruzuku ya kufidia gharama ya kusafirisha mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yaani Mikoa yua Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma. Pamoja na kutoa ruzuku hiyo, bei ya mbolea ilipanda zaidi badala ya kupungua.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua orodha ya wasafirishaji waliolipwa fidia ya kusafirisha mbolea. Aidha, naomba pia kujua sababu zilizopelekea bei ya mbolea kuzidi kupanda badala ya kupungua.

Mheshimiwa Spika, naomba nijue kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha bei ya mbolea inazidi kupungua ili tuweze kuzalisha chakula kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono baada ya kupata maelezo ya hoja nilizotoa hapo juu.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa uhodari na umakini wake wa kufanya kazi ya kuendesha Wizara ya Fedha kwa kiwango kikubwa cha ufanisi mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kumlipa Mheshimiwa Mbunge posho ya mafuta ya lita 100 kulingana na bei ya mafuta ya sasa. Ieleweke kuwa posho ya mafuta tunalipwa shilingi 700,000/= kwa bei ya shilingi 700/= kwa lita. Sasa mafuta yamepanda kwa kiwango kikubwa na yapo maeneo ya nchi hii ambako yanafikia kwa shilingi 1,000/= kwa lita ya mafuta ya *Super.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kumlipa Mbunge shilingi 700,000/= kama posho ya mafuta, ina maana ya kumkwamisha Mbunge ashindwe kufanya kazi zake za Jimboni kama ipasavyo, kwani hawezi kununua lita 100 za mafuta.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wanaingia katika wakati wa uchaguzi na watashindwa kununua lita 100 za kuwahamasisha wananchi wao wajue wajibu wao wa kujiandikisha kupiga kura. Kwa hili, nashauri posho ya mafuta irekebishwe kufikia shilingi 1,000,000/= ambayo ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2003/2004 ilitaja kuwepo kwa Mabenki ya Wakulima na wavuvi, je, Mabenki hayo yako wapi na katika mikoa ipi?

Mheshimiwa Spika, kuna kundi kubwa sana la vijana wasio na ajira na hata sisi watawala tunatoa maneno yasiyo na uhakika wa mitaji. Hivyo, mfuko wa vijana uongezewe nguvu, na wala siyo hivyo vipesa vidogo vidogo; haviwezi kuondoa tatizo lililopo.

Mheshimiwa Spika, naomba upendeleo maalum kwa Mkoa wa Kigoma kwa suala la uvuvi na njia ya kuwapatia mikopo ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika ambalo lina uvuvi ule ule usio na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, miundombinu mingi imekosekana kwa sababu sehemu nyingi zinategemea hisani ya wafadhili na ndipo sehemu zikaweza kupata mafanikio na zile sehemu ambazo hazina wahisani, hubakia vile vile bila ya maendeleo kama vile barabara, umeme na viwanda.

Mheshimiwa Spika, ni vema Wizara ya Fedha izijue sehemu hizo, kama vile hakuna barabara ya Dodoma - Itigi - Tabora mpaka Kigoma. Hivyo wananchi wa Kigoma hawajui ni lini watapata barabara ya lami, au hata ya changarawe kwa kisa hakuna pesa.

Pia hakuna umeme kwa sababu hakuna pesa. Hivi katika bajeti zote za Serikali, suala la miundombinu kwa mikoa duni wataendelea kubakia nyuma bila msaada.

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara ya lami na umeme kwa mkoa wa Kigoma.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara zote mbili. Hata hivyo, naomba Wizara ya Fedha isaidie suala la upelekaji umeme Songea hadi Wilayani - Mjini Namtumbo, pia Songea hadi Mbinga.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Ruvuma watashukuru sana iwapo Wizara ya Fedha ikatafuta fedha za kigeni ili wakati Sweden inajenga umeme *(extension)* kutoka Makambako hadi Njombe, mradi uendelezwe hadi Ruvuma, umbali upatao kilometa 100 tu. Sisi Wabunge wa Ruvuma tutafarijika sana iwapo kilio chetu mkikipa sikio. Tunategemea tutetee kero hii ya kukosa umeme wa grid toka Makambako. Ninaamini hiyo yawezekana, maana kutoka Njombe kuelekea Ruvuma siyo mbali (kilometa 100). Wananchi Kijijini na Mjini Namtumbo pia Mjini Mbinga, watafurahiwa mno! Hicho ni kilio chao tangu mwaka 1980.

Mheshimiwa Spika, umeme wa gridi ukifika Namtumbo, utasukuma zaidi usindikaji wa tumbaku. Huko Mbinga, utaongeza usindikaji wa kahawa. Tayari

*TANESCO* imekamilisha *feasibility study* toka Makambako kupitia Njombe hadi Mjini Namtumbo na Mjini Mbinga.

Aidha, Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, aliniahidi kuwa akipata barua ya Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini na kuiwasilisha kwake (Wizara ya Fedha), fedha zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, barua ya Waziri Mheshimiwa Daniel Yona, ametekeleza kuiomba Wizara ya Fedha itusaidie *Grid Electricity.* Hivyo tunaimani kubwa utekelezaji utakuwa wakati wa mwaka 2004/2005, ili Wabunge tupate *milage* ya kisiasa 2005.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, katika mipango ya kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025 na malengo ya milenia, kwa nini hakuna muda maalum *(time frame)* wa kuondoa jembe la mkono? Asilimia 80 ya wananchi ni wakulima na wanatumia jembe la mkono ambalo limetudumaza na kuongeza umaskini. Ni lini hatua kwa hatua tutaondokana na jembe la mkono?

Mheshimiwa Spika, uko wapi mpango wa maendeleo wa miaka mitano, mitano? Zamani mipango ilieleweka hasa ile ya Kitaifa kama barabara, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, imejielekeza mno kwenye ubinafsishaji kuliko mipango na hata huo ubinafsishaji bado hatua zinasuasua. Kwa mfano, juu ya *Tabora Textile, MOPROCO, CANVAS* na kadhalika, ambapo *failure* yake imefanya soko la masoko, mfano pamba imezorota. Wizara (Mipango) iwe ni *think tank* kusimamia uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Michezo ya kubahatisha ambapo Serikali inaipa *BMT* fedha kwa ajili ya kuimarisha michezo. Kwa nini bado hawajaanza kukusanya hizo fedha na kuipa *BMT?* Je, kwa kuwa Rais alisha-*sign,* Wizara italipa fidia?

Mheshimiwa Spika, bado tunaweza kupata mapato zaidi ya fedha kila mwezi hasa kama tungejipanga vema zaidi kwenye mipango. Kuwe na tathmini ya mara kwa mara kuelekea mwenendo wetu.

Mheshimiwa Spika, fedha za wastaafu ingefaa iwe kila baada ya miezi mitatu, mitatu, badala ya miezi sita, sita.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kheri na baraka katika kazi zao.

**MHE: ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha kwa umahiri na umakini wa kuongoza Wizara ya Fedha. Vile vile nampongeza Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, najua anavyoimudu Wizara hii kwa umahiri wa pekee.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Fedha iwe makini katika kujali na kuthamini wale watu wanaoitegemea Wizara ya Fedha, hasa kwa kuangalia upandaji wa gharama za maisha mfano hai posho ya mafuta ya Wabunge shilingi 700,000/= kwa bei ya shilingi 700/= *per litre* wakati Biharamulo lita moja swa na shilingi 1,100/= huku ni kumkwamisha Mbunge kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliangalie swala hili kwa hekima, busara na wataalamu wa uchumi walione kama wanaojua kupanda kwa gharama za maisha. Wasiwe wageni katika Israel . Afanya kweli kutokana na ujuzi alionao.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Waziri kwa nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji katika ukurasa wa 23 mikoa ni mingapi iliyofanyiwa uchambuzi wa kubaini kuanzisha fursa mbalimbali ya maeneo maalumu ya kuendelezwa kwa ajili ya kuvutia uwekezaji rasilimali wa ndani na nje (*special economic zones)* na ni vigezo vipi vilitumika kubaini mikoa hii. Kwa nini zisitumike takrimu mbalimbali na taarifa zilizomo nchini ili kuwezesha nchi kuwa moja Taifa moja kwa ajili ya manufaa na watu wake wote.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa *TRC* uende haraka, hali ya Shirika inazidi kudidimia, isipowezekana wafunguliwe mikono waweze kukopa kuboresha reli.

Mheshimiwa Spika, zile fedha za *World Bank* zitolewe zote sasa ili ziboreshe reli kabla ya ubinafsishaji na siyo baada ya ubinafsishaji. Nia si kukodisha kwa bei poa kutokana na hali ya reli ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizira ya Fedha, hivi bado hawaoni umuhimu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika kuboresha na kuendeleza sekta nyingine na pia kuondoa umaskini? Wakati umefika sasa wa Wizara hii kuingizwa katika *priority list.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha itoe umuhimu wa kusaidia kutatua matatizo muhimu ya kijamii pale sekta fulani inapowasilisha rasmi na siyo majibu ya haraka haraka ya kuwa eneo hili au lile linaloombewa sio *priority.* Je, katika maisha ya watu wetu *priority* ni nini?

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na makubaliano yanapofanywa huwa ni ahadi ambayo waungwana hupaswa kutimiza. Sasa ahadi ikitolewa ni vyema kutimizwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha, sasa ni wakati wa *priority* kwa sekta ambazo zitakusaidia kuchangia fedha katika mfuko mkuu kwa Hazina kwa *Airports,* Reli, *Telecommunications* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nampa hongera Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wake na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya kukusanya kodi na kuboresha makusanyo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya mapato na kufanikisha maendeleo. Juhudi za Wizara ndiyo iliwezesha mafanikio mengi kwenye Wizara mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufanisi huo bado kuna mambo ambayo Wizara inabidi kuangalia.

Kwanza, Kodi ya *VAT* . Kodi hii ni kubwa mno hasa ukijua walipaji ni walalahoi ndiyo wanaolipia kodi na kusababisha maisha yao kuwa magumu sana, kodi hizo zipunguzwe.

Pili, upangaji wa bei ya mafuta uangaliwe kwani bei ya sasa ni ya juu sana na imesababishwa mfumuko wa bei. Wakulima wanashindwa kulima kwa ajili ya gharama ya mafuta.

Tatu, utaratibu wa wananchi kutopata mikopo kutokana na masharti magumu ambayo wananchi wa hali ya chini wanashindwa kukopa. Wananchi wawekewe mazingira mazuri ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kama nilivyoeleza makusanyo kuwa mazuri sana ukilinganisha na miaka ya nyuma, bado kuna maeneo ambayo wananchi wanapata shida sana kwenye maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu naelekeza kituo cha Namanga mpakani mwa Tanzania na Kenya. Kuna kero zifuatazo:-

Kwanza, kucheleweshwa kwa wananchi wanaposafiri na kulipia vifaa vyao huchukua muda mrefu wakizungushwa na kusababisha wananchi kwenda kulipia kwenye maeneo ya mipaka mingine kama Holili au Arusha na kuleta stakabadhi. Usumbufu huo ni mkubwa sana.

Pili, usumbufu wa kuwakamata wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanajitafutia riziki kusumbuliwa na kudaiwa ushuru mkubwa kuliko bei aliyonunulia mzigo wake. Namanga kuna unyanyasaji sana wa wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri aende Namanga kuangalia usumbufu huo na kuelezea utaratibu wa ushuru ili wananchi wasinyanyaswe na walipie kulingana na sheria. Kwani wanashindwa kuelewa kodi ambazo zimefutwa kwani mabadiliko hayaonekani. Asante na naunga mkono hoja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa yote mazuri waliyoyafanya katika mwaka 2003/2004. Bila shaka mwaka huu 2004/2005 wataendelea kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba Wizara izingatie yafuatayo:-

Kwanza, Mkoa wa Kigoma kutokuwa na Maafisa Mipango wa kutosha. Naomba Wizara hii ikishirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi, ipeleke Maafisa Mipango wa kutosha katika Mkoa wa Kigoma kwani Mkoa huu una upungufu mkubwa sana wa kada hii ya watumishi na hivyo unaathirika sana kimipango.

Pili, uanzishwaji wa *SUMATRA* na *EWURA,* sheria za kuanzisha *regulatory authorities* kama *SUMATRA* na *EWURA* zilipitishwa na Bunge hili Tukufu zaidi ya miaka miwili iliyopita lakini Mamlaka zenyewe hazijaanza. Mamlaka zinatakiwa zianze mara moja ili malengo yaliyotegemewa yafikiwe.

Tatu, ubinafsishaji wa *TRC* na *TANESCO,* naiomba Wizara isifanye haraka kubinafsisha au kukodisha Mashirika ya *TRC* na *TANESCO,* bali wafanye uchambuzi na utafiti wa kutosha kuepusha uwezekano wa kukwamisha kabisa huduma hizi muhimu kiusalama na kiuchumi. Ningeishauri Serikali ifanye kila inavyoweza kujenga upya njia ya reli na kununua vifaa kwa ajili ya *TRC* kwani vilivyopo ni vikuu kuu (karibuni miaka mia moja).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa kazi nzuri na hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi namwomba Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa vya Morogoro hususan kiwanda cha *Morogoro Shoe.* Hiki kiwanda kilikuwa na mwekezaji ambaye ameondoka baada ya kiwanda kuungua moto.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na hisa katika kiwanda hiki, je, hisa hizi zililipwaje na Bima? Ilikuwa shilingi ngapi? Aidha, kiwanda kilikuwa kimeajiri wafanyakazi wengi wakiwemo wanawake, je, ni nini hatma ya malipo yao?

Mheshimiwa Spika, je, ni nini hatma ya malipo yao? Sasa hatma ya kiwanda hiki ni nini? Bado tunahitaji viatu na wakazi wa Morogoro wanataka ajira. Mheshimiwa Waziri tunaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kingine ni *Morogoro Leather Goods,* hiki kiwanda kwa nini hakifanyi kazi ikizingatiwa kwamba kiwanda hiki kilikuwa kimeajiri wanawake wengi na sasa hawa akinamama hawana kipato pamoja na kwamba wengine wao hawajalipwa mafao yao mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, siyo vizuri hawa akinamama wakaendelea kuishtaki *PSRC* kwa kutumia ahela za mikopo. Hali hii inawaongezea umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba lifanyike kila liwezekanalo ili kiwanda hiki kiweze kupata mwekezaji madhubuti *(reliable)* ili wananchi wapate ajira na Serikali ipate mapato.

Mheshimiwa Spika, hali ya mashine inazidi kuwa mbaya na wizi umekithiri. Mheshimiwa Waziri akinusuru kiwanda hiki muhimu kwa wanawake wa Morogoro na Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ili mipango mizuri ya nchi izae matunda, lazima suala la rushwa liwekewe mikakati ya kupambana nao na kuhakikisha mikakati hiyo inatekelezwa.

Katika moja ya mipango ya kupambana na rushwa ni kuwa na kila sekta katika nguzo tatu za dola zinakuwa na *action plan* ya kupambana na rushwa. Je, Bunge lina mikakati/au limetengenezwa *action plan* ya kupambana na rushwa? Kama haina je, huoni mipango mizuri ya Serikali itakosa usimamizi/ushauri mzuri na Bunge kwa kuwa haitakuwa na vigezo/dira ya kupambana na rushwa hasa pale idara fulani fulani za Serikali zinapojiingiza na rushwa?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna maeneo yanasemwa kuwa yanahusika na matumizi mabaya ya fedha za Serikali au mipango ya Serikali, je, Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji ili mipango yake isiathirike, inafuatiliaje suala hili la rushwa? Je, katika mikakati yake kisekta ya kupambana na rushwa, inalifuatiliaje swala hili Bunge kupitia *PAC* imeonyesha wasiwasi wake katika mipango mbalimbali ya Serikali kwa mfano *TACAIDS, TVT, TANSORT,* Mradi na bomba la Mafuta kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, *IPTL, Mtibwa Sugar Company* (Kamati ya Fedha).

Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je anaonaje kufuatilia kwa makini masuala ya rushwa kama moja ya *secterial plan of action* ya Wizara yake?

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetolewa asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri na namtakia kila la kheri na fanaka katika kutekeleza majukumu tuliyojiwekea katika Wizara hii. Pamoja na kwamba natambua kuwa hotuba ya Waziri inaangalia masuala ya kifundi zaidi *(Technical issues)* bado naikumbushia Wizara hii ahadi yake ya kuhakikisha kuwa mashamba ya *West Kilimanjaro* yanapimwa kwanza kwa ajili ya Maskota kabla ya kubinafsishwa ili waweze kupata makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, aidha, namkumbushia Mheshimiwa Waziri kwa ahadi yake ya kulitembelea jimbo langu la Siha. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachangia katika maeneo yafuatayo, hisa, viwanda vinavyobinafsishwa, mafanikio kwa wafanyakazi na tofauti za bei.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hisa, suala la hisa ni suala la faida kwa kila mkoa na kwa maana hizo. Naomba Wizara itoe elimu kwa wananchi kuhusu hisa na isambae mikoa yote hadi vijijini ili wanawake wafaidike na hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vinavyobinafsishwa, ubinafsishaji tumeona matunda yake na umekomboa wananchi/Watanzania na faida yake inaonekana. Ila kuna tatizo la wafanyakazi ambao waliokuwa wakifanya kazi maeneo mengi wanapunguzwa na kuwaacha bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri atoe nafasi kwa wafanyakazi na wawekezaji wawatendee haki wafanyakazi. Mfano *Tanga Cement,* imeandaa utaratibu mzuri kwa wafanyakazi. Nachukua nafasi hii kupongeza kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, tatizo la tofauti za bei kimkoa, napata tabu sana kuona viwanda hivi vinauza mfano, *cement,* kila mkoa na bei yake na kuna sababu ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, tujifunze kutoka *TBL* mbona bia za Kilimanjaro, Safari, bei ya Dar es Salaam, Tabora na Morogoro ni hiyo hiyo? Pia hata soda, kwa nini Wizara haijifunzi hilo kwa vitu vingine, wale wanafanya nini na wao wawekezaji wengine waige hayo.

**MHE. DR. RAPHAEL CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda, kwa hotuba yake nzuri na kwa ufanisi mkubwa ambao ametuonyesha katika kutekeleza majukumu katika Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, sambamba na pongezi hizi pia nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na watendaji wote kwa kumsaidia Waziri katika kutekeleza majukumu na kuifanya Wizara hii kuwa chachu kwa mafanikio ya mabadiliko ya kiuchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kusisitiza yafuatayo:-

Kwanza, hoja kubwa ya kuunda chombo au *(think tank)* Tume ya Mipango ili isaidie kuongoza mikakati ya kupanga na kuchambua masuala muhimu ya uchumi. Pia kuratibu sera mbalimbali za uchumi na kufuatilia ili kuhakikisha malengo ya mipango ya nchi yanafikiwa.

Pili, Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo sera ya kuendeleza rasilimali watu ili iendane sambasamba na dira ya Taifa ya maendeleo.

Tatu, haja ya Wizara hii kutengewa fedha za kutosha ili itekeleze vema majukumu yake makubwa na mazito kuhusu kupanua na kuboresha uchumi jumla.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Katibu Mkuu Dr. Enos Bukuku, pamoja na wataalam wote waliohusika katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza masuala mawili tu, kwanza, kwa kuwa kuna baadhi ya Mashirika na viwanda vilivyobinafsishwa yamefilisika kabisa au tangu yanunuliwe yameendelea kufungwa, nadhani ni muda muafaka kuchukua hatua ya kuyafanya Mashirika au viwanda hivyo vifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana tokea zoezi hili lianze nasisitiza kuwa Wizara ikamilishe mapema iwezekanavyo sera ya kuendeleza rasilimali watu ili iendane sambamba na dira ya Taifa ya maendeleo 2005. Ahsante. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na timu nzima ya wataalam wake ikiongozwa na Katibu Mkuu Dr. Enos Bukuku, kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya Wizara na kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu zao la Chai ili Serikali iweze kutafakari dukuduku zangu kwa ni ya kuzitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kama unavyoelewa zao la chai linalimwa na wakulima wadogo na wakubwa. Mashamba makubwa *(Estates)* yanamilikiwa na wawekezaji toka nje ya nchi. Mmoja wa wamiliki hao anaitwa *SHAMJI,* yeye ndiye aliyenunua mashamba ya chai ya Tukuyu (Rungwe) na Ambangulu, Balangai na Dindira yaliyoko Korogwe, tangu anayanunue mashamba haya mwaka 1995 kumekuwa na matatizo makubwa ya kuyaendesha mashamba hayo pamoja na viwanda.

Mheshimiwa Spika, mbolea na madawa hayawekwi, uzalishaji umepungua na mashamba hayana sura. Matokeo yake ni kwamba mishahara, posho, mafao na haki mbalimbali za wafanyakazi hazijalipwa kwa muda mrefu. Kwa mfano hadi kufikia Machi, 2004 watumishi wa mashamba ya Tukuyu wanadai kiasi cha shilingi milioni 860.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi sasa wamegeuka ombaomba, wana madeni kibao na wanashinmdwa kuwapeleka watoto wao shule au Zahanati. Huyo mmiliki *SHAMJI* anaishi Uingereza na anaendesha shughuli za mashamba *by remote control,* anakula kivulini. Haji Tanzania na hajawekeza chochote tangu anunue mashamba na viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wamechoka kuvumilia. Kumekuwa na migomo, baadhi ya mashamba yamechomwa moto na hivi karibuni watumishi wenye hasira waliezua majengo na kukata mabomba kiwandani Musekera, Rungwe.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Chai ina uwezo wa kisheria kuchukua hatua *up to a point.* Hivi sasa bodi imesimamisha leseni ya kampuni kuuza chai nje ya nchi kwa mategemeo kwamba ikiuzwa ndani ya nchi bodi inaweza ku-*keep track* ya mauzo na kuangalia uwezekano wa mapato kupunguza madeni.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Serikali iingilie kati kero hii. Nahisi *SHAMJI* amejenga hisia kwamba Serikali yetu haina meno kwani malalamiko juu yake yamefikishwa Serikalini mara nyingi. Ni mnyanyasaji huyu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 27 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri unazungumzia Sera ya Uwekezaji Rasilimali. Kifungu cha 47 kinaelezea juhudi za kueneza huduma za uwekezaji na kwamba Kituo kitafungua Ofisi za Kanda, Mjini Moshi na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aone kuwa katika masuala ya maendeleo kama hili Taasisi zilizo chini ya Wizara yake zijaribu ku-*balance* Kaskazini na Kusini, Magharibi na Mashariki na kadhalika ili maeneo yote yaende sambamba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri na namtakia utekelezaji mwema.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Waheshimiwa wote wawili yaani Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Manaibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalamu wao wote kwa kuweza kukaa pamoja na kuandaa hotuba hii nzuri ambayo inaonesha ufanisi wa hali ya juu na yenye kuleta matumaini katika kutekeleza ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo sote tunatakiwa kuitekeleleza kwa asilimia mia moja ili kurahisisha na kuweka bayana nguvu ya utendaji wetu kama chama Tawala. Hongera.

Mheshimiwa Spika, Wizara hizi mbili ndiyo Wizara mama katika Serikali yetu na macho ya Wizara zote yako katika Wizara hizi, kwa hiyo, ni muhimu kufanya kazi zao kwa uangalifu zaidi kwa kuelewa thamani yao hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo ambalo kila siku tunajitahidi kulipigia kelele hapa Bungeni, lakini hadi hii leo ufumbuzi wake ni kitendawili, kwani usumbufu kila siku zinaposonga mbele basi ndiyo matatizo yanapozidi badala ya kupungua na si jingine ni hali ya Biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, ugumu wa biashara katika usafirishaji umekuwa na usumbufu kila siku zinapoendelea kwani kutokana na Zanzibara kuwa ni kisiwa inalazimika kufanya biashara zake na Tanzania Bara kwa 70% na nchi ya Comoro nayo kwa 20% na 10% tu hio kwa ajili ya watu wa Zanzibar kwa hiyo utaona hali gani ilioko katika kuendeleza biashara.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwa Serikali yetu iangalie zaidi kuhusu mfumo mzima wa usafirishaji wa mzigo yote inayotoka Zanzibar kupewa kipaumbele katika kufanikisha zoezi zima la uendeshaji wa shughuli za *TRA*.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii japo kwa kiasi kidogo niweze kuwazungumzia wastaafu hasa wale wanaotoka Zanzibar kwani inawawia vigumu sana kufuatilia mafao yao kutokana na Wizara kutokuwa na uhakika kkatika kuwapatia mafao yao wastaafu kwani haina mipango iliyokuwa wazi ya kuelewa inafanya nini katika kuwapatia mafao yao na wala Wizara haielewi watendaji wangapi wataacha kazi katika mwaka husika, hilo ni tatizo na Wizara lazima iwe na takwimu sahihi za watumishi ili tuondokane na kuwasumbua hawa wazee wetu ambao wanastaafu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kutoa salaam za pole kwa familia na wananchi wa Ulanga Mashariki kwa kufiwa na Mbunge wao Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi *Amin.*

Baada ya rambirambi hiyo nianze kwa kuunga mkono hotuba zote mbili kwa asilimia mia moja. Pia niwapongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na wataalam wote wa Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia sehemu kubwa mbili, nazo ni uwekezaji/ubinafsishaji. Suala la kiwanda cha Nyuzi, mafao ya waliokuwa watumishi wa kiwanda hicho kwa zaidi ya miaka kumi na tano sasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ucheleweshaji wa uuzaji na ukosekanaji wa mnunuzi wa kiwanda hicho tangu mwaka 1997, kumesababisha matatizo makubwa kwa wakazi wa Tabora kwa kuzidi kuwa maskini zaidi. Wafanyakazi hao wamekuwa mara kwa mara wakileta madai au malalamiko yao bila mafanikio yoyote pamoja na uongozi wa Mkoa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ofisi za Chama Tawala Mkoa bila mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watumishi hao wameleta kwangu *EMS* ili nifuatilie kwa kina majibu toka kwa Waziri husika, wakimwandikia Waziri wa Utawala Bora kama nitakavyokabidhi kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nimeomba wakati wa kujibu anisaidie kwa maelezo ya kina ili tufikie muafaka.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza, ningeshauri Wizara husika ikutane na viongozi wa kiwanda hicho, pili, Serikali ikubali kulipa kiasi hicho cha fedha, ili kuondoa usumbufu huo na tatu, Serikali hapa nchini ipitie tena maeneo ambayo yana matatizo kama hayo ili kulinda utulivu na amani ya nchi yetu, kwani hivi karibuni kumetokea matatizo makubwa kwa watumishi wa kiwanda cha chai nchini huko Mbeya Wilaya ya Rungwe, wakidai shilingi milioni 500,000,000/= na wakaamua kuvunja na kubomoa mali mbalimbali za viwanda hivyo. Tuwe makini sana kwani hilo tatizo linaigusa jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo/nyumba, Serikali ifanye utaratibu wa kupangisha wafanyakazi kwenye nyumba ya viwanda ili ziendelee kuwa katika hali nzuri kuliko ilivyo sasa, kwani kiwanda cha nyuzi kilijenga majengo nje ya kiwanda ambayo thamani yake ni kubwa na hivi sasa baadhi ya nyumba hizo wameanza kuiba vifaa. Nyumba hizo zikabidhiwe ofisi za Mikoa kwa utunzaji zaidi kabla ya kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali imalize migogoro kabla ya kupata wawekezaji kwenye maeneo husika ili tusiwaogopeshe na kuifanya Tanzania ieleweke vibaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nikabidhi nakala ya madai ya watumishi hao na pia ningeomba Waziri wakati wa kujibu nipewe matumaini zaidi ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, mara nyingi nikichangia ndani ya Bunge lako Tukufu nimezungumza kwa uchungu mkubwa namna ambavyo wafanyakazi wa zamani na wa sasa katika shamba la Katani la Mnazi wanavyonyanyasika kwa kutolipwa mishahara na marupurupu yao kwa muda mrefu. Baada ya kubinafsishwa kwa shamba hilo nyaraka nyingi zinazowahusu wafanyakazi zilipotea au kufichwa.

Mheshimiwa Spika, ni siku mbili tu zilizopita nililetewa baadhi ya nyaraka husika ambazo tangu mwaka 1997 wafanyakazi katika nyaraka nilizoletewa wanadai jumla ya shilingi 25,907,469.50. Nyaraka nyingine bado hazijapatikana. Naomba Waziri mhusika atusaidie ili wafanyakazi hao waweze kulipwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji aliyepewa shamba la Katani la Mnazi haonekani kuwa na nia hasa ya kuendeleza kilimo cha Mkonge. Tangu apewe shamba hilo mwaka 1997 hadi leo bado anavuna Mkonge wa zamani na wala haonekani kuongeza jitihada za

upandaji katani mpya.  Zaidi ya hayo ameuza zana nyingi za kilimo katika shamba hivyo, kwa sababu hizo napendekeza anyang'wanywe shamba hilo na wapewe wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda vya mbao, viko viwanda vya mbao vingi katika Kanda ya Kaskazini yaani mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha likiwemo Jimbo la Uchaguzi la Mlalo.  Katika mikoa hiyo viwanda vikubwa kama vile *Tembo Chipboard, Fibreboard (20000 Ltd.* na *Kilitimber,* vilibinafsishwa.  Hivi karibuni zimeonekana mbinu na jitihada kubwa za wazi za viwanda  hivyo vikubwa kuviua viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, mbinu hizo ni pamoja na kuwapunguzia mgao wa magogo (mashamba ya miti), kuwa magumu kama vile milimani au katika makorongo ambapo gharama ya uvunaji huko ni kubwa, hupewa miti myembamba badala ya ile minene na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, viwanda vidogo vidogo vya mbao vimeunda umoja wao uitwao *Northern Forestry Industries Association (NOFIA).*  Viwanda vidogo vya mbao kwangu ni muhimu sana.  Hawa kule Mlalo ndio Wahisani wakubwa wa shughuli za kijamii za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tumejenga shule za  sekondari nyingi kwa mfano Rangwi, Kwemaramba, Lukozi, Mnazi, Mng'aro, Sunga na pia tunajenga pale Manolo, Mtae, Mlalo, Mkunki na Mbarama.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wa viwanda vidogo vidogo vya mbao ndiyo wahisani wakubwa katika shughuli kama hizo.  Kwangu mimi hawa ni sehemu muhimu kwa maendeleo ya Jimbo langu.  Pia hawa hutoa ajira kwa kina mama wengi pamoja na vijana.  Napendekeza wasibughudhiwe na pia na wao wapewe mikataba kama wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashamba ya miti, ziko habari kuwa mashamba ya miti ya Serikali kyako njiani kuuzwa.  Kama habari hizo ni za kweli basi naomba mashamba hayo wapewe wananchi badala ya wawekezaji hasa wageni.  Eneo hili la mashamba na kwa kweli hata viwanda vya mbao vikubwa ni muafaka sana kwa kuhudumiwa na wananchi wanao uwezo kwa maeneo haya wanachotaka ni mbegu na msaada wa utaalam.

Mheshimiwa Spika, wananchi ndiyo wanaolimia miti katika mashamba hayo. Kwa sababu hizo na nyingine nyingi ambazo hazijatajwa ni haki wakati ukifika mashamba hayo kama ilivyokuwa kwa mashamba ya mifugo wapewe wananchi. Aksante.  Naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:**  Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizo mbili, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazofanya kusaidia kujenga uchumi wa Tanzania.  Naomba sasa kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kuhusu takwimu za Sensa ya watu na makazi. Natoa pongezi kwa upeo wa juu uliofanyika katika kuchambua na kutoa mchanganuo wa takwimu za Sensa kujibu hoja mbalimbali na kubaini tafsiri mbali mbali kwa lengo la kusaidia kuboresha mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kwamba Tume ya Sensa ikamilishe takwimu za hali ya kiuchumi za Mikoa na Wilaya ili kusaidia kuondoa malalamiko ya kutokuwa na vigezo katika kupanga mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali kwa uwiano kimkoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Mipango. Elimu kutoka Chuo hiki ni muhimu sana katika kuwezesha vitongoji, vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa kuwa na mipango mizuri ya maendeleo ya kiuchumi. Mahitaji ya Chuo ni makubwa Kitaifa na pia kwa Mataifa ya nje yanayothamini elimu hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, je, kuna mpango gani wa kukifanya Chuo hicho kuwa Chuo Kikuu cha Mipango? Ni vema tukajenga mwelekeo huo katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya mafao ya wafanyakazi shamba la Mpira Kihuhwi, Muheza, wakati wa kujibu swali lililokuwa linahusu madai ya wafanyakazi hao Wizara husika ilionyesha uwezekano wa Serikali kuwalipa wafanyakazi hao. Kutokana na madai hayo kuwa ya muda mrefu na kutokana na nia nzuri ya Serikali kujenga mahusiano mazuri na wananchi wake na pia haki ya Serikali kulinda haki na mali za wananchi wake, je ni maandalizi gani yameanza kufanywa ili kuwalipa wafanyakazi hao?

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa *Kibaranga Estate* (wafanyakazi 23). Madai ya wafanyakazi hao yaliyowekwa chini ya Mfilisi *(Mnguto Advocate)* kwa miaka mingi sasa hayajalipwa kikamilifu. Inafahamika wazi kwa maana kwamba Serikali inajua kuwa fedha zilizotengwa kuwalipa wafanyakazi hao hazikulipwa kikamilifu kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, pia zipo kumbukumbu za maandishi kati ya mfilisi na *PSRC* ambapo mfilisi anatupa lawama za ucheleweshaji na uwajibikaji kwa *PSRC* huku wafanyakazi wakikosa haki zao. Hivi ni lini Serikali itatambua kwamba jukumu la kumuwajibisha mfilisi ni la Serikali na siyo la wafanyakazi husika? Na kwa msingi huo kwa nini *PSRC* na Serikali inakwepa wajibu wa kuwalipa wafanyakazi haki zao. Ni busara Serikali ikamaliza mgogoro huo ambao wala hauhusu fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Fedha kwa kuwa tayari kulipa wastaafu wa pensheni waliowahi kulipwa kwa mkupuo. Uchambuzi uliofanywa juu ya utaratibu wa kuanza kuwalipa wastaafu hao kwa mpango wa kwanza kulipwa kwanza na wa mwisho kulipwa mwisho unaonyesha kwamba sasa Wizara inao wataalamu wenye uwezo wa kutafakari kubuni na kupanga mambo *(think tanks),* nawapongeza sana. Njia hiyo ndiyo pekee itakayofanya haki itendeke kwa usawa kwa wote badala ya wachache kuachiwa kunufaika na mabadiliko ya sheria.

Mheshimiwa Spika, malipo ya leseni za biashara mwaka wa fedha 2004/2005. Kama ilivyogusiwa wakati wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara malipo ya leseni za biashara yataendelea hadi hapo sheria ya biashara itakapofanyiwa mabadiliko. Uamuzi huu utaleta utata mkubwa kwa sababu wananchi/wafanyabiashara wengi walijua kufutwa kwa malipo ya leseni za biashara yangeanza Julai, 2004. Hata Wizara ya Fedha katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kinaonyesha mapato kutokana na leseni za biashara kuwa katika mabano ( ) kuonyesha pungufu la pato kutokana na kodi hiyo kuondolewa. Je, ni vipi Wizara ya Fedha iachie mgongano kama huu kuendelezwa?

Mheshimiwa Spika, njia iliyopo ni Wizara ya Viwanda na Biashara kuendelea kutoa leseni kama inataka kufanya hivyo, lakini bila kutoza ada za leseni na kwamba Wizara ya Fedha kisheria imekwisha ashiria kutokuwepo na mapato ya kutokana na kodi za leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Fedha ilitoa maelezo hapa Bungeni wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara juu ya leseni za biashara kuwa hakuna lililoharibika juu ya kuelewa kwa wananchi kwamba ada za leseni za biashara zinakuwa hazipo kuanzia Julai, 2004, basi ni vizuri wananchi wakawekwe sawa juu ya hali halisi kuondoa utata unaoweza kujitokeza kutokana na Kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Biashara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nawapongeza kwa dhati Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa hiyo, naunga mkono hoja hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja (hotuba) hizi mbili nitauelekeza kwenye maeneo yafuatayo kama ushauri na ombi kuleta mabadiliko na kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naishauri Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, kuona umuhimu wa kuanzisha utayarishaji wa ramani ya Taifa ya rasilimali za Uchumi na Jamii za Maendeleo *(National Economic Resources Development Potentialities Zoning).* Katika ramani hii itakuwa kama kioo ambapo pataonyeshwa kwa kina rasilimali zote *(resources potential)* katika kila Wilaya/Mkoa yaani Wilaya au mkoa una uwezo gani kuzalisha na kwa gharama gani ukilinganisha na Wilaya/mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, zoezi kama hili litapunguza hoja za wananchi kung'ang'ania kuendelea kuzalisha au kufanya shughuli ambazo hazina faida kibiashara na Kijamii. Ramani hii pia itaelekeza misingi ya kuendeleza miundombinu katika Mikoa/Wilaya husika kusudi kuwezesha kuendeleza miundombinu kama barabara, umeme au mabwawa ya maji kuelekeza kwenye maeneo/vijiji vya uzalishaji. Mfano mzuri ni Wilaya ya

Iramba ambapo Bonde la Wembere lina rasilimali nzuri kwa kuzalisha mazao ya chakula na ya biashara kama pamba kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, udongo una rutuba nzuri, kinachotakiwa ni kuvuna maji katika milima ya Sekenke kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji, mradi huu umebuniwa na umepekewa kwa Wizara hizi mbili kutafutia fedha za kufanyia *feasibility studies.* Suala la umeme kupelekwa kwenye maeneo ya Ziwa la Kitangiri utasaidia uvuvi. Ramani kama hii itaaelekeza vizuri wawekezaji mbalimbali kwa miradi mbalimbali kwenye Wilaya/Mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu nini tumejifunza kutokana na njaa iliyolitikisa Taifa zima mwaka jana na sasa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji imeandaa tahadhari kukabiliana na janga hili Kitaifa kwa miaka ijayo. Hili ni suala la mipango ya muda mrefu na siyo suala la bajeti ya mwaka. Kwa miaka ijayo kama Taifa hili litakumbwa na njaa, itakuwa ni suala la kichekesho na uzembe kwani nchi hii inayo rasilimali nyingi za kujitosheleza kwa chakula na kulisha hata nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tatu ni kuomba Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, kurudi kwenye utaratibu wa kutayarisha mipango ya miaka mitano ya maendeleo *(five years development plans)* na kwa utaratibu huu itawezesha kuona maendeleo ya utekelezaji wa miradi muhimu na mikubwa ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Fedha natoa ushauri kuhusu kutazama upya Halmashauri na matumizi ya ruzuku kutoka Serikali Kuu. Wizara lazima ifanye tathimini ya kina kuona kama malengo yaliyokusudiwa yamefanikiwa. Suala la kuimarisha uwezo wa Halmashauri ni muhimu sana *(capacity building).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Halmashauri zote nchini, natoa ombi kwa Serikali kuwa sasa ione umuhimu wa kujenga miundo mbinu muhimu katika Wilaya zote kama barabara vijijini, mabwawa ya maji kwa kilimo cha umwagiliaji na kupeleka umeme vijijini kwa usindikaji mazao, uvuvi na mifugo. Suala la miundombinu hizi muhimu haliwezi kuachiwa Halmashauri kwani zenyewe hazina uwezo kifedha, kiutalaamu na kivifaa kuweza kujenga au kuendeleza miundo mbinu hizi tatu (barabara, mabwawa, umeme na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali kujenga/kuendeleza miundombinu hii muhimu inaweza pia kuwavutia wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi katika Wilaya/Mikoa mbalimbali. Baada ya kuendeleza miundombinu kama hii basi Serikali inaweza kukabidhi Halmashauri kuzimiliki na kuziwezesha kwa kuzipa ruzuku kama inavyofanywa sasa. Kwa kufanya hivyo ruzuku katika sekta mbalimbali zinazotolewa na Serikali kuu zitafanikisha malengo ya kuleta maendeleo na kuboresha maisha katika Wilaya/Mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi Afrika na pengine duniani Serikali Kuu zinafanya zoezi la kujenga miundombinu msingi katika Wilaya na baada ya hapo kukabidhi Halmashauri kumiliki na kwa kutumia ruzuku.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, suala la kuleta utawala bora *(Good Governance)* utaleta maana kama Serikali italeta uwiano wa wazi wa maendeleo kiuchumi, kijamii, kimiundombinu kwa kutoa upendeleo maalumu kwa mikoa/Wilaya zilizo nyuma kimaendeleo kama wilaya za mikoa ya Singida, Dodoma, Shinyanga. Kuendelea kuelekeza maendeleo kwenye Mikoa/Wilaya iliyokwisha endelea ni kuvuruga amani na utulivu wa Taifa.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba za Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nimesha changia zaidi ya mara mbili sasa kwa maandishi kwenye Wizara mbalimbali baada ya maafa yaliyotupata hivi karibuni, nimekwisha toa pole kwa wote wanaohusika kwa hiyo, sitataja majina hapa ila tu naomba nitoe pole ya jumla kuhusiana na matukio haya.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niwapongeze Wizara ya Fedha kwa ufanisi unaojitokeza wazi wa utendaji kazi. Kwa hiyo, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri ya Wizara kuhusu Bajeti ya mwaka 2004/2005. Pongezi hizo hizo ziwafikie Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu ambao kwa ushiriki wao wamewezesha hotuba hii ya Wizara kuwa bora na yenye kueleweka na ya kina.

Mheshimiwa Spika, pongezi hizo hizo ziwafikie Makatibu Wakuu wa Wizara, Manaibu Katibu wa Wizara, Wakurugenzi wote na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa ujumla wao kwa ushirikiano wao unaonekana wazi wazi kwa kutayarisha hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, kama mchango wangu kwa Wizara ya Fedha, naomba nitoe maoni hayo kwa utaratibu ufuatao:-

Kwanza, nimefurahishwa sana na juhudi za Wizara ya Fedha kwa uongozi wa mambo ya vyombo vya fedha na hatimaye kuiwezesha kampuni ya Mgodi wa Mererani *(AFGEM)* kutoa hisa zake *( to float shares)* kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam kama utafuatilia mijadala ndani ya Bunge. Nilitoa hoja kwamba sasa Migodi ya Madini ya dhahabu na almasi, hisa ziuze kupitia soko la Hisa la Dar es Salaam pia hapa natoa hongera kubwa kwa Wizara kufanikisha hili.

Pili, makusanyo ya kodi kila mwezi yamepanda kutoka shilingi bilioni 1.1 na kufikia zaidi ya shilingi bilioni 1.6 kwa mwezi. Naipongeza sana Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi naomba Wizara ya Fedha, izingatie yafuatayo:-

Kwanza, kuhusiana na mpango wa kuingilia mafuta ya Petroli *(petroleum products)* usiamliwe kwa haraka kwamba iwe Dar es Salaam kwa kuweka *Flow metres*

huko. Kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa, hasa Mkoa wa Mwanza, kuna uwekezaji hapo Jijini Mwanza wa vyombo vya kubebea mafuta yaani meli kwenye ziwa ambavyo vinabeba mafuta kutoka Kisumu Kenya. Pia kuna magari ya aina ya Tankers mengi kwa ajili ya mafuta kuja Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara na kadhalika zitaharibikiwa kama uamuzi wa kutumia tu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha atoe maelezo juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Fedha kusimamia shughuli muhimu kama vile maagizo yanayotolewa na Waziri wa Fedha kupitia hotuba ya Bajeti, ihakikishe wazi kwamba maagizo yanaanza na yanatekelezwa kama ilivyoagizwa. Kwa mfano, utekelezaji wa agizo la kutoza ada za leseni kwa ngazi kama ilivyopangwa agizo hilo. Halmashauri za Wilaya/Miji/Jiji wanalalamika sana kutokana na usumbufu wa Halmashauri hizi pia agizo la kutotoza kodi mazao zaidi mara moja halijatekelezwa. Mazao bado yanatozwa kodi kule yanakokwenda pia yaani mazao yanayotozwa kwenye Wilaya yalikozalishwa na pia kwenye Wilaya yanakopelekwa kwenye masoko au kufikia. Wakati mwingine Halmashauri zinatumia mbinu ya kuita majina mbalimbali ya kodi lakini kinachotozwa kodi hiyo ni mazao na zaidi ya 5%.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Fedha isimamie kwa karibu sana matumizi ya fedha kwenye Serikali. Kama inawezekana, basi kiundwe chombo maalum cha kusimamia matumizi zaidi ya *cash budget arrangement.* Ninayo imani kwamba usimamizi wa matumizi ukifanikiwa pesa zetu zitatusaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mipango ya nchi, kwa vile sensa ya mwaka 2002 sasa imekamilika angalau imetoa mwanga wa pa kuanzia kufanya mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza hatuna Hospitali ya Mkoa watu ni milioni 2.9. Hospitali ya Sekou Toure ya Mwanza haina sifa na kuwa hospitali ya Mkoa. Tatizo hili ni kubwa kwa Mkoa wa Mwanza ndiyo maana wananchi wa Mkoa wenyewe wameamua kufanya upanuzi wa hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, atoe maelezo ya namna gani ataipangia Hospitali ya Sekou Toure, Mwanza ataiwekea utaratibu wa kujengwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha Kikao cha leo. Uzoefu wa Wizara zilizotangulia umetuonyesha kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wanafaidika kuuliza maswali na kupata ufafanuzi katika Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, kwa hali ya leo pengine ni vizuri tukatoa nafasi kubwa zaidi kwenye Kamati ya Matumizi ili wengi waweze kupata ufafanuzi. Kwa ajili hiyo, mara tukirudi saa 11.00 jioni nitawaomba watoa hoja wahitimishe hoja zao. Halafu twende kwenye Kamati ya Matumizi. Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hasi saa 11.00 jioni.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo. Uzoefu wa Wizara zilizotangulia umetuonyesha kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wanafaidika kuuliza maswali na kupata ufafanuzi katika Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, kwa hali ya leo pengine ni vizuri tukatoa nafasi kubwa zaidi kwenye Kamati ya Matumizi ili wengi waweze kupata ufafanuzi. Kwa ajili hiyo mara tukirudi saa 11.00 jioni nitawaomba watoa hoja wahitimishe hoja zao. Halafu twende kwenye Kamati ya Matumizi.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kutoa shukrani nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia.

Napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya maandishi, kwanza ni Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Chegeni Masunga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Ibrahimu Marwa. Nawashukuru sana kwa michango yao ya maandishi. *(Makofi)*

Vile vile napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kauli hapa ndani ya Bunge, kwanza ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Emmanuel Kipole na Mheshimiwa Paschal Degera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuwa kusema kwamba viongozi wa Kamati ambao wametoa mapendekezo yao katika maandishi mbele ya Bunge lako Tukufu hapa nikimaanisha Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda kusema kwamba maoni waliyoyatoa katika nyaraka zile zikiwakilisha Kamati mbalimbali pamoja na Kambi ya Upinzani tutazifanyia kazi kwa kina na ushauri waliotupa tutauchukua na hata katika taarifa hizo wamekiri

kabisa Kamati zilipokaa wakati zikizungumzia masuala ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji maagizo yote waliyokuwa wakitupa tunayatimiza. Kwa hiyo, hilo tutalifanyia kazi na nina hakika kwamba itabidi kuboresha Ofisi yetu ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Rostam Aziz, aliyoitoa hapa Bungeni. Nilivyomwelewa Mheshimiwa Rostam Aziz hoja yake ilikuwa na maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza lilikuwa ni masuala ya kiuchumi na eneo la pili alikuwa akiulizia muundo wa Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Ningependa kusema kwamba katika nchi ambayo inatafuta mafanikio ya kukuza uchumi wake, mwaka 2002 Tanzania ilikuwa ni nchi ya tatu katika nchi za *SADC.* Mwaka huu Tanzania imekuwa nchi ya kwanza katika nchi za Afrika Mashariki katika kukuza uchumi wake. Hali hiyo inadhihirisha wazi kwamba mipango ipo. Hakuna nchi ambayo inaweza kuendelea katika hatua namna hiyo kama mipango haipo.

Sasa tunaweza tukazungumzia tatizo la utekelezaji wa kutokufikia malengo yetu hasa nchi kama Tanzania ambayo ni nchi mojawapo iliyo katika kundi la nchi zinazoendelea. Sasa kutofikia malengo ya utekelezaji kwa kweli maana yake si ubabaishaji. Tunaangalia tu zile *constraints* ambazo tunazo katika kutekeleza malengo yale tuliyojiwekea. Tunaelewa kwamba katika nchi zetu tuna upungufu mkubwa wa kuibua rasilimali zetu, uwezo wetu ni mdogo. Tuna utegemezi mkubwa wa hali ya hewa, mwaka jana sekta ya kilimo ilituangusha kidogo kwa sababu ya hali ya hewa. Tunayo teknolojia duni, mazao yetu yamekuwa ni mhanga mkubwa wa kupata bei ndogo katika soko la dunia na hili tumekuwa tukilizungumza mara kwa mara. Sasa haya tu ni baadhi ya matatizo tuliyonayo na haya ndiyo tunayapangia mipango ili kuweza kutatua matatizo haya.

Napenda kumsisitizia Mheshimiwa Rostam Aziz, kwamba suala la mipango ya maendeleo, anapozungumzia mipango ya maendeleo narudia tena hatuzungumzii tukio, tunazungumzia *process.* Hatuwezi tukazungumzia maendeleo leo na kesho tukajikuta tumepiga hatua. Lazima twende kwa mchakato ambao tumeuweka. *(Makofi)*

Mimi napenda kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba takwimu zinazotolewa na ofisi yangu kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa kwa kweli si za ubabaishaji. Katika hotuba yangu leo nimeelezea orodha ya tafiti tunazozifanya katika nchi hii. Tafiti zinazokwenda mpaka Vijijini kutafuta ukweli wa takwimu hizi. Sasa takwimu hizi tunapozileta hapa haziwezi kuwa zimekaa kusoma magazeti tu zinafanyiwa kazi na tuna wataalamu wa Kitanzania na sasa tunaboresha zaidi Ofisi ya Takwimu kwa hiyo takwimu zetu ni nzuri.

Tunaambiwa kwamba kukua kwetu kwa uchumi mara tunapanda, mara tunateremka, mara tunapanda. Mimi sifahamu nchi duniani ambayo uchumi wake unakuwa unapanda moja kwa moja. Maana yake sasa hiyo ndiyo ambayo inaleta ile *concept* ya uchumi ya ku-*hit up* uchumi wa nchi. Nafikiri wote hawa Waheshimiwa

Wabunge mnafahamu hata Uchina juzi ilipata matatizo kwa sababu uchumi wake ulikuwa unakua kwa kasi sana. Kwa hiyo, *economy* ikaanza ku-*heat up.* Kwa hiyo, ilibidi watumie *macro economic fundamentals* kwa maana ya *inflation rates* wameangalia *revenue visas GDP Gross rates* ili kuutuliza uchumi usikue. Lakini mbona tuna maneno yanaitwa *depression* kwenye uchumi. Hata uchumi wa Marekani unaingia kwenye *depression,* unashuka, unapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako Makampuni makubwa kama Enron, Yucco sasa hivi yameshuka na yamefikia kiwango cha kufilisiwa. Sasa kukua kwetu kwa uchumi kwa kweli kunatakiwa kuwe ni moja ya eneo ambalo sisi Waheshimiwa Wabunge lazima tujivunie kwamba tunafanya kazi vizuri ya kuhamasisha wananchi, wakulima na wafanyakazi wanafanya kazi kubwa katika maeneo yao kulima na kadhalika ili kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia pia kwamba uchumi wetu unakua. Mheshimiwa Rostam Aziz, anasema uchumi wetu unakua kwa kutegemea mikopo ya kutoka nje. Nadhani tukizungumzia hii hatufanyi *justice* kwa sababu kwa kweli wakulima wanafanya kazi kubwa sana, wakulima wetu nchini wanafanya kazi kubwa sana. Wakulima wanalima pamba, kahawa, mahindi na kadhalika. Yote haya tukiyaweka pamoja yanasaidia katika kukuza uchumi wetu.

Bei ya mafuta inapanda, ni kweli. Wiki moja iliyopita bei ya mafuta Marekani ilikuwa ni dola za Kimarekani 43 kwa pipa na katika historia ya soko la dunia la mafuta Marekani pia imekuwa ikisumbuliwa sana na kupanda kwa bei ya mafuta. Sasa kama nchi zilizoendelea zinasumbuliwa na upandaji wa bei za mafuta kwa kweli lazima tukiri kwamba nchi kama zetu kutakapotokea tu uhaba wa uzalishaji wa mafuta hasa kutokana na vita vinavyoendelea sasa hivi lazima uchumi wetu utaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia thamani ya shilingi kushuka bei hata tukichukua nadharia gani thamani ya kushuka kwa fedha yetu inapungua kwa sababu tunahitaji kuzalisha zaidi na kuuza katika soko la nje. Tunapouza katika soko la nje ni lazima tusisitize suala zima la usindikaji wa mazao yetu ili tupate *value addition.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi mlikuwa mnafahamu kwamba kulikuwa na mkutano hivi karibuni Geneva wa *WTO* moja ya eneo lilikuwa ni hilo nchi zinazoendelea litafaidika vipi katika kupata bei nzuri katika soko la dunia.

Kwa hiyo, tunapozungumzia hata kama tuna urari wa mapato ya nje na ndani ambako sawa sawa hizi *reserves* wakati mwingine zinaweza kuwa *resources* ambazo tunazipata kwa njia nyingine kama misaada na kadhalika. Lakini la msingi ni kwamba lazima tujenge sekta yetu ya kuzalisha nje kwa bidii kubwa sana. Nchi ambayo thamani ya shilingi inashuka si Tanzania peke yake. Kuna wakati tunakaa tunasikia *Japanese Yen* inashuka thamani, dola inashuka thamani, hivi karibuni dola ilishuka thamani kweli kweli kulinganisha na *Euro.*

Kwa hiyo, yote hii haimaanishi kwamba hakuna mipango, ni zile *dynamics* na *operations* za kuendesha uchumi hasa katika nchi zetu hizi zinazoendelea. Kwa hiyo, mimi ningemwomba Mheshimiwa Rostam Aziz, ambaye ni rafiki yangu sana aelewe tu kwamba kwa kweli hizi ni *dynamics* tu za uchumi lakini mipango tunayo. Alitaja hapa katika hoja yake mipango ya kupunguza umaskini, tuna mipango ya muda mrefu, mipango ya muda wa kati. Tuna mipango ya kisekta na kadhalika.

Lakini la pili, vile vile pia alizungumzia muundo wa Wizara akasema anataka kujua kwamba Wizara inaelekea wapi. Mimi nashukuru Mheshimiwa Rostam Aziz, alikwishatoa jibu. Jibu ambalo na mimi huwa nalitoa siku zote hapa. Ni kweli kabisa ubinafsishaji ni urekebishaji ambao ni wa mpito tu ni wa mpito kabisa, ni *transitional* na nilikuwa nasema hapa katika nyanja zote za kurekebisha uchumi, ubinafsishaji labda inachukua asilimia mbili tu maana tunafanya marekebisho kwenye sheria, masoko, barabara, huduma za jamii lakini hili la ubinafsishaji tumeona tufanye marekebisho yetu ili viwanda vyetu vianze kufanya kazi. Hakuna nchi duniani itakayoendelea ikiwa ina *gross rate* ya *negative one* na viwanda havifanyi kazi. Lakini sasa viwanda vinafanya kazi. *(Makofi)*

Vile vile hata hili suala la Wizara ya Mipango inaelekea wapi. Wala hilo sio tatizo kwa sababu hili linatokana na *instrument* ambayo amepewa Mheshimiwa Rais. Sisi tunafuata tamko tu la Mheshimiwa Rais kwamba Wizara ya Mipango itashughulika na Mipango na Ubinafsishaji. Lakini mimi nina hakika kabisa kutokana na Ilani za Chama cha Mapinduzi na taratibu tunazoziweka hapa, baada ya masuala ya mipango ambayo ni ya kudumu nadhani suala litakalofuatia ni suala la mipango na uwezeshaji. Kuwawezesha wananchi hivi sasa wapate fursa zao za uchumi ili kukuza maisha yao. Tutakapofanya hivyo maana yake ni kwamba sasa tunatumia *principles* za uchumi. Uchumi jumla tunaupeleka kwa wananchi. *Filtering from the macro level to the micro level.* Kwa sababu nchi zote zinafanya hivyo, hili tumeshalianza. Tumelianza katika kupunguza *non income poverty.* Tuna shule, barabara, maji yanafanyiwa *improvement,* miundombinu na kadhalika.

Kwa hiyo, mimi nina uhakika kabisa jinsi tunavyokwenda tutakwenda na jitihada za kupunguza *income poverty,* mwananchi aweze kupata fedha kule anakofanya kazi yake. Hizi sera ambazo tumeziendesha hapa kufuta kodi, sera za kufuta ada, sera za kufuta leseni, sera za kuwezesha kila mwananchi aweze kusoma mwaka kesho. Tunaingia katika utaratibu wa Shule za Sekondari yote haya ni maeneo ya uwezeshaji ambayo mimi nafikiri yatafanyiwa kazi vizuri zaidi hapo baadaye. Lakini vile vile inaweza kuwa ni mipango na uwezeshaji lakini na pia vile vile mipango na kuendeleza sekta binafsi. Kwa sababu sasa hivi tumeamua kwamba sekta binafsi ndiyo eneo ambalo litaendesha uchumi wetu.

Kwa hiyo, mimi namalizia kwa kusema kwa hoja hiyo ya kwanza kwamba Mheshimiwa Rostam Aziz, rafiki yangu, mimi naona uunge mkono hoja. Nakuomba uunge mkono hoja hii kwa sababu wewe kama Mheshimiwa Mbunge una mchango mkubwa kwenye hoja hii. Lakini vile vile Waheshimiwa Wabunge nao wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo. Nafikiri tukifanya hivi tutaondoa lile tatizo la

kukwama utekelezaji wa mipango ambayo imeainishwa vizuri katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rostam Aziz, nakuomba uunge hoja mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kwa kuzungumzia taratibu nzuri za ubinafsishaji. Ametoa mfano wa *Kilimanjaro Hotel* na *Embassy Hotel.* Ninachotaka kumweleza ni kuhusu *Embassy Hotel* ni kwamba Serikali tuna hisa ndogo sana, sisi ni *minority shareholders.* Wawekezaji binafsi ndio wana *share* kubwa zaidi. Kwa hiyo, suala la ubinafsishaji inabidi tuongee vizuri kati ya wawekezaji hawa ambao wana share kubwa zaidi kuliko Serikali.

Mimi napenda kumhakikishia Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kwamba ubinafsishaji wa Shirika la Reli tunataka tuufanye kwa makini sana, hatutaki kukurupuka tu. Kwa sababu tayari tuna uzoefu kwa nchi kubwa kama *New Zealand, Britain* ambapo zilibinafsisha Reli bila ya kuwa makini baadaye kwa sababu hii inahudumia watu wengi inairudia tena Serikali wakati ikiwa na hali mbaya zaidi. Kwa hiyo, tutaifanya kwa utaratibu mzuri tu. *(Makofi)*

Nakushukuru Mheshimiwa Abdullatif Esmail, kwamba na wewe unaipa nguvu sekta binafsi na kwa hiyo, kwa kweli ndiyo sera yetu sasa kwamba sekta binafsi lazima itiliwe kipaumbele na ile *smart dialogue* ambayo Serikali inaifanya sasa hivi. Niseme tu Waheshimiwa Wabunge katika Afrika Tanzania ndiyo nchi ya kwanza ambayo wakati inapopanga bajeti yake inahusisha Serikali na sekta binafsi ili kupunguza kero za kuongeza uwezeshaji katika Taifa. Kwa hiyo, nashukuru kwa mchango wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala, rafiki yangu leo kidogo amenishangaza, maana yake wakati anachangia anasema sisi Wabunge hatushirikishwi. Sasa ukisema sisi Wabunge hamshirikishwi kwenye hoja yangu mimi maana yake na mimi umenitoa nje sio Mbunge, mimi vile vile ni Mbunge. Namwambia rafiki yangu Mheshimiwa Emmanuel Kipole na mimi vile vile ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi na nina hakika yote tunayoya-*discuss* hapa tunayazungumza kwa maslahi ya Bunge letu.

Sasa hilo napenda likae sawa sawa, sisi sote ni Wabunge. Huu Uwaziri ni matokeo tu lakini wote tutakimbia tena Handeni, Msalala, kutafuta nafasi hii. Kwa hiyo, naomba hilo aone kwamba tuko pamoja asinitenganishe mimi na yeye. Kwanza mimi na yeye ni marafiki sana. Lakini napenda kumwambia Mheshimiwa Emmanuel Kipole kwamba ushirikishwaji wa hii mikataba, kuna mikataba ya dunia na ya Kimataifa ambayo na sisi hapa tunairidhia. Lakini mikataba mingine ni mikataba ya kisekta, ipo mingi sana. Sekta ya afya ina mikataba na sekta ya barabara ina mikataba. Sasa mikataba yote hii ije hapa Bungeni tuje kuifanyia maamuzi na iko katika eneo la utendaji, nadhani uchumi wetu utalala sana. Lakini ninachosema ni kwamba pamoja na kwamba sekta hizo tunazozifanyia hivyo ni suala la kisekta haizuii Waheshimiwa Wabunge kuhoji na kuuliza mikataba fulani inakwendaje.

Sasa ninachosema ni kwamba ushauri wake alioutoa pamoja na kuunga hoja mkono sisi Serikali tuko tayari kuchukua ushauri huo na kuona tunaufanyia kazi kwa

taratibu gani. Tukielewa kwamba mikataba ya kisekta ni *operational.* Lakini vile vile kuna *separation of powers.* Kikatiba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halikupewa kazi ya kujadili kila siku sekta kwa sekta mikataba inayoingia humo lazima kuwe na *executive,* sisi tunatengeneza sheria kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Lephy Gembe, nakubaliana naye kwamba rasilimali watu lazima tuifanyie kazi. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali nakubaliana na wewe kwamba utaratibu wa kununua hisa usambazwe hadi Vijijini. Tuangalie mafanikio ya viwanda vinavyobinafsishwa. Lakini vile vile nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Gama kwamba lazima kuwe na *action plan* ya kupambana na rushwa. *Action Plan* hizo zipo za kisekta na vile vile sasa hivi tunahusisha moja kwa moja Mashirika yasiyo ya Kiserikali kuingia katika utaratibu wa kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, amezungumzia Wizara itengewe fedha za kutosha. Tunapenda sana Wizara itengewe fedha za kutosha, lakini tuna upungufu wa *resources* na nakubaliana naye kwamba tuendeleze rasilimali watu. Mheshimiwa George Lubeleje, anatushauri tuendelee na jitihada za kupata wanamipango wengi kutoka Chuo chetu cha Mipango haps Dodoma. Hilo nakubaliana nalo asilimia mia moja kwamba kwa kweli tunahitaji tupate wanamipango wengi kuwapeleka mpaka ngazi za chini katika maeneo yetu. Imefikia wakati Mheshimwia Herbert Mntangi, ameshauri vile vile kwamba ni afadhali sasa Chuo cha Mipango cha Dodoma tukifanye Chuo Kikuu. Hilo ni eneo ambalo tunaweza tukaliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Frank Mussati, nakubaliana na wewe kwamba kuna upungufu wa Maafisa Mipango, Kigoma na jana nimeongea na Kanali Mahawa hata Afisa Mipango wa Mkoa hamna. Nilimwambia kwamba nitaongea na Katibu Mkuu Dr. Enos Bukuku, tuone ni utaratibu gani wa kupeleka Afisa Mipango wa Mkoa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka za udhibiti zimeshaanza kufanya kazi kama *TCRA* na ile ya *Tanzania Broadcasting Corporation* kwa sababu zile tayari zimekuwa zimerithi mali zilizokuwepo. Lakini niseme kwamba kwa hizi zingine zinahitaji rasilimali na fedha nyingi lakini nina hakika kwamba maandalizi ya kuanza tayari tumeshasema yataanza kuanza mwaka wa fedha hiki tulichonacho sasa hivi.

Mheshimiwa Semindu Pawa, ameuliza wawekezaji walioingia ni wangapi nchini mpaka hivi sasa. Mpaka sasa Mheshimiwa Semindu Pawa, kuanzia mwaka wa 1990 tuna miradi 2,527 ambayo ina thamani ya shilingi 12 na imeshaleta ajira ya takriban watu 500,000. Ile ya wazalishaji wa Magunia na kadhalika baadaye wanatoa vibali vya kununua nje, ule ni utaratibu wa kisera ambao tuliukosea, lakini tumeshaanza kufanya marekebisho hasa katika zao la ngozi kwa kuweka kodi kubwa kwa wale wanaosafirisha wanatoa nje ngozi ghafi badala ya zile zilizosindikwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwanne Mchemba,amezungumzia suala la wafanyakazi wa *TABOTEX.* Wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Nyuzi cha *Tabora Textiles* wamelipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria na kufuatana na kumbukumbu zao walizozileta. Malalamiko yanatokana yanahusu aidha, kukataa ukweli wa kumbukumbu hizo zao au

kutaka malipo zaidi ya yale waliyolipwa au kutaka walipwe sawa sawa na ile menejimenti ambayo ilichukua fedha na ikajilipa mafao makubwa zaidi kuliko wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili sasa hivi linashughulikiwa na vyombo vya dola. Malalamiko yao ya pensheni tumeshayafanyia kazi. Kutokana na madeni makubwa ilibidi Serikali kutoka kwenye mkakati wa ubinafsishaji na kuingia mkakati wa kufilisi Kiwanda cha *TABOTEX* na wakati huo *PSRC* ilikuwa haikuhusika kwa namna yoyote kwa sababu wizi wa fedha zile zitafanyika na menejimenti ile ulitokea baada ya kiwanda kukabidhiwa kwa mfilisi.

Sasa napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kwamba Mungu akijalia wiki ijayo nitakuwa Tabora tutaweza kufika katika eneo hilo na kuona tunalitatuaje hili tatizo kwa sababu naelewa kwamba limehusisha viongozi wa Mkoa na vile vile limemhusisha Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini. Tukikutana pamoja tunaweza kuona tunaendelea vipi.

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, nakubaliana na wewe kwamba yule mwekezaji Shamji ni tatizo kwa sababu yeye ni *land load* wa *remote control.* Suala hilo nimekwenda mwenyewe Rungwe nimeliona, tumeliwasilisha kwa Wizara ya Kilimo na Chakula na tunaangalia taratibu za umiliki wa hati za umiliki wa ardhi ili tuweze kuona ikiwezekana mashamba haya kwa kweli wapewe wananchi au wawekezaji wenye nguvu zaidi kulikohawa ambao wapo sasa hivi.

Mheshimiwa Alhaj Shawej Abdallah, napenda nikuhakikishie kwamba *Katani Limited* mpaka tunavyozungumza sasa hivi hawajarudisha yale mashamba nane. Lakini utaratibu wa Serikali unaendelea kuhakikisha kwamba wanayarudisha mashamba hayo nane. Kwa hiyo, baada ya mashamba hayo nane kurudishwa tutazungumzia huu utaratibu ambao umeulizia.

Mheshimiwa Charles Kagonji, nakubaliana na wewe kwamba mwekezaji wa shamba la Katani kwa kweli ameendelea kuonekana suala lile hatalimudu, kazi ile hawezi kuimudu na kutokana na hali hiyo tutafanya juhudi zile zile za kuona kwamba kama *Katani Limited* ambayo wameshindwa ku-*invest* kwenye mashamba yote, shamba hilo tulipeleke kwa mwekezaji mwenye uwezo.

Mheshimiwa John Singo, nakubaliana na wewe kwamba Wilaya ya Same igawanywe lakini inategemea *availability of resources.* Mheshimiwa Aridi Uledi, amezungumzia masuala ya ubanguaji wa korosho, baada ya ziara yangu ya Mikoa ya Kusini, nina furaha kukuarifu kwamba kwa sasa hivi karibu viwanda vyote vya korosho vimeshapata wawekezaji na vingine vitaanza kazi ya ubanguaji katika msimu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucas Selelii, amesema tutaondokana lini na jembe la mkono? Namhakikishia kwamba hatua kwa hatua taratibu zitakazofanya sasa hivi tutaondokana na jembe la mkono. Mheshimiwa Aggrey Mwanri, nakubaliana na wewe mashamba ya

*West Kilimanjaro* yatapimwa na *Mascoutah* watapewa kabla ya kubinafsisha ili kuondoa hilo tatizo. Nakuhakikishia bado nitatembelea Siha kuja kuona hali halisi jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tumepata michango mingi. Michango hii tutaiboresha na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwamba utaratibu wa kubinafsisha *NMB* kwa sababu umepitishwa kisheria na Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatuwezi kwenda tofauti na utaratibu wa Bunge. Kwa sababu itakuwa ni ajabu sana Serikali kufanya ubinafsishaji tofauti na taratibu tulizozifikisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, matatizo ya *Tanzania Elimu Supplies, TRC* kama tulivyoyasikia siku zote na migogoro ya *TTCL.* Serikali inafanya utaratibu mzuri wa kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi kuona kama matatizo haya tutayamaliza namna gani. Tatizo la *Tanzania Elimu Supplies* wanahitaji mkono wa kheri. Sasa mafao yao yapo kisheria. Sasa suala la mkono wa kheri hilo ni suala ambalo linabidi majadiliano yazidi kuendelea kuona kwamba wataupataje mkono wa kheri kutoka Shirika ambalo walilifilisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wakubaliane nasi kwamba katika yale maeneo ambayo hatukuyagusa tutayafanyia kazi na kama kawaida yetu tutawaletea majibu ya kina zaidi tutakapopata wasaa ambao tunaweza kuyaaandika kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru wachangiaji walioshiriki kwenye hotuba yangu ya leo asubuhi.

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Irenius Ngwatura, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Dr. Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Semindu Pawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa majadiliano ni Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Emmanuel Kipole na Mheshimiwa Paschal Degera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna jina ambalo nimelisahau naomba msamaha, lakini nikiwahi kulipata, nitalitambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nawatambua Wenyeviti wawili, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Hawa nimewataja mwisho kwa sababu nataka kuwajibu kwa undani zaidi kwa kuamini kwamba nikimjibu Mwenyekiti, nimejibu Kamati yake yote na wale wote wenye fikra kama hizo na nikimjibu Msemaji wa Upinzani, nimejibu Kambi yote na wale wengine wenye fikra kama hizo kama wapo. Nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, alizungumzia kwamba bado kuna ukwepaji kodi. Mimi nasema hiyo ni kweli na hakuna nchi duniani iliyofanikiwa mia kwa mia kuondoa wakwepa kodi. Hakuna! Maana kwenye kodi kuna njia mbili za kukwepa, kuna moja inayoitwa *tax evasion,* kukwepa kodi. Hilo ni kosa hasa na lina sheria zake, watu wanaweza wakafungwa au wakafainishwa.

Pia kuna kitu kinaitwa *tax avoidance,* hujakosea wala hujafanya vizuri, upo hapo katikati. Kwa mfano, badala ya kufanya shughuli zako hapa Tanzania, badala ya kuandikisha Kampuni yako hapa Tanzania ili ilipe kodi za Tanzania, unakwenda kwenye nchi kule *West Indies* ambako ndiko kwenye nchi nyingi za namna hii, unaandikisha Kampuni yako huko, kwa hiyo mapato yake na faida zake zinakwenda kule, unakwenda kulia huko *West Indies,* hulipi hapa. Kwa hiyo, hiyo inaitwa *tax avoidance.* Nimeweka hivyo tu kwa sababu hapa kodi ni kubwa mno, kule hakuna kodi, kwa hiyo, unapata mapato zaidi, zikiwa kule unaweza ukahamishia hapa kama vile mwekezaji anavyohamishia. Hiyo ni ya pili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya tatu, kuna hili nililotaja kwenye hotuba yangu leo, la fedha haramu. Fedha haramu kwa hulka hazipiti hadharani, hakuna mtu anaziona. Maana Bwana Kodi akiona fedha haramu atazipiga kodi kweli kweli na mnavyojua jinsi zilivyo nyingi ndivyo zinavyotakiwa kodi yake iwe kubwa zaidi. Kwa hiyo, hela haramu zinazotembea ni nyingi sana. Tanzania sisi sio maarufu kwa fedha haramu, lakini hakuna nchi ambayo haina fedha haramu. Kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba anayekwenda kule kwa namna fulani haendi au unamfanya asiende au akienda unamkamata. Mwenye fedha haramu vile vile unazifuatilia, ziko kwenye madawa ya kulevya, ziko kwenye wizi, ziko kwenye njia za aina mbalimbali na kadhalika. La maana, kila Serikali itambue kwamba jambo hilo lipo na itafute namna ya kupambana nalo na ndivyo tunavyofanya kama nilivyosema kwenye hotuba yangu hapa na nchi tofauti zina mafanikio ya aina tofauti.

Kwa hiyo, nafurahi na kama kuna Wabunge wowote pamoja na Kamati ambao wanataka kunisaidia hata kwa kutoa habari tu, sisi tutafurahi na tutafuatilia.

La pili ni kupanua wigo wa walipakodi ili watu wengi zaidi wawe wanalipa kodi. Hili nasi tumeliona, ni jambo muhimu na ndio maana kwenye hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka huu tumelizungumzia sana wazo hilo la wigo wa kulipa kodi. Kwa mfano, kama tungeweza tukafanikiwa wale watu wote wadogo ambao tumewawekea *schedule* kwenye hotuba yangu ya Bajeti, wale wa kuanza kulipa shilingi 35,000/= wanaendelea mpaka shilingi 500,000/=. Kama wale wote wa aina ile wangekuwa wanalipa kodi, basi tungekuwa tumepata mafanikio makubwa sana. Kama watu ambao ni wakwepa kodi wa kweli kweli, wale wakubwa wanaokwepa kodi, nao tungewafikisha mahali wote wakalipa kodi, kama mlivyosikia tukijibu swali juzi, walipakodi wa nchi sio wengi ni 236,000 nadhani. Sio wengi sana. Lakini hawa kumbe ndio wanaotubeba.

Kwa hiyo, hili tatizo lipo, tunalifahamu na tunaanza kulishughulikia kwa makundi. Kundi hili tulitumbukize, baadaye kundi lingine na ndio maana kwa mfano tumekuwa tukishughulikia hili kundi la wanaofanya biashara za mafuta ya petroli. Hilo ndio somo langu la pili katika hoja ya Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwamba ni kweli bado mapendekezo ya wale waliofanya utafiti wa kujua jinsi wakwepa kodi wa eneo hili wanavyokwepa, tumeanza kuyatekeleza. Tumeanza kwanza kwa hatua tulizochukua mwaka 2003 kama nilivyotangaza ambapo ukusanyaji wa mapato kutoka sekta hii ya mafuta ya petroli ulipanda kutoka shilingi bilioni 12 hadi 18, 19, 20. Hilo lenyewe tu lilikuwa ni mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisha tukasema hatua ya pili kubwa zaidi, tufunge mita ile inayoitwa *flowmeter.* Nafurahi kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba ile *flow meter* imefika, sasa iko katika hatua za kufungwa na hatua tuliyofika sasa ni kwamba tumekwishakamilisha jengo, kitu wanachoita *mechanical works* kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichobakia sasa ni mambo matatu, kwanza kuingiza kitu kinachoitwa *software* kwenye mitambo iliyokuja, kuwafunza watumishi wa Mamlaka ili waweze kutumia chombo hicho au utaratibu huo, kufanya kitu wanaita *test run* yaani kujaribu kama kweli kitafanya kazi au namna gani na mwisho kuikabidhi Serikali ya Tanzania kwa sababu huu ulikuwa ni mkataba wa watu ambao waliajiriwa kufanya kazi hiyo. Kazi hiyo itaendelea na tumaini letu ni kwamba ikifika mwisho wa mwezi huu, kila kitu kitakuwa kimekamilika na kwa hiyo *flometer* zitaanza kufanya kazi na hapo tutaona tena matokeo yake ambayo tunatumaini yatakuwa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kitu ambacho wala Waheshimiwa Wabunge walikuwa hawajakipigia kelele sana, nacho ni kwamba, kwenye mitambo hii iliyokuja, imekuja 14. Kati ya hiyo, 12 itakuwa kwa ajili ya kudhibiti mafuta ya petroli na miwili kwa ajili ya kudhibiti mafuta ya kupikia. Maana kuna watu pia wanaingiza mafuta ya kupikia kana kwamba ni petroli. Kwa hiyo, kwa mpigo mafuta ya kupikia na mafuta ya petroli yatadhibitiwa kwa utaratibu huu wa *flow meter* na tutaona pia matokeo makubwa sana kwenye kodi. *(Kicheko/Makofi)*

Kwenye eneo hili kuna mambo mengine yalikuwa yamependekezwa kwamba Serikali iyatekeleze kama mtiririko wa kupambana na ukwepaji kodi na nafurahi

kuwaambia kwamba Mamlaka ya Mapato ikishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini na shahidi yangu ni Waziri mwenyewe anaingia hapa ananisikiliza, vyombo hivyo viwili vinatekeleza sasa hivi yale mapendekezo mengine yaliyokuwepo kwenye taarifa hiyo. Kwa hiyo, mimi sina wasiwasi, nafikiri tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilikuwa na mapendekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi ni lile la kuhusiana na Benki ya Viwanda na Benki ya Kilimo. Hii nilikwishalieleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti kwamba tunaendelea kulifanyia kazi na ningependa niseme hivyo tu bila kusema zaidi mpaka hapo tutakapofika mahali tukafanya uamuzi, lakini Serikali ina nia ya kufika mahali na kuamua kama nilivyosema wakati wa hotuba yangu ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu riba, ushahidi tulionao sasa hivi ni kwamba riba za amana zinapanda, zimefikia sasa kwa kutegemea aina ya mteja mpaka asilimia nane. Hivi leo ziko asilimia tatu, nne, tano, sita, saba, nane, hata tisa kwa kutegemea aina ya mteja na uaminifu wa mteja. Riba za mikopo nazo zinateremka. Sasa hivi ziko hadi asilimia 12. Mwaka 2003 zilikuwa zaidi ya 12%, zilikuwa kwenye ishirini na kitu. Sasa zinateremka ziko asilimia 12. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jambo la tatu limetokea jipya nalo ni kwamba Benki zenyewe zimeunda kitu kinachoitwa *Credit Information Bureau. Credit Information Bureau* ni utaratibu wa kuwa na kumbukumbu za wakopaji ili ndani ya kumbukumbu hizo wajulikane wakopaji wabaya. Kama mimi ni mkopaji mbaya yaani yule asiyelipa madeni, kwa kawaida mkopaji mbaya anatoka kwenye Benki hii, anakwenda kukopa kwenye Benki nyingine, anatoka hapa anakwenda nyingine, baada ya muda kila Benki ameshakopa na kila Benki hajalipa. Sasa utaratibu huu wa *Credit Information* ni kwamba nikishashindwa kurudisha mkopo kwenye Benki moja, Benki nyingine zote zinaambizana kwamba huyu sio mwaminifu. Sasa kila nikienda sipati mkopo ili kusudi wakope watu waaminifu zaidi.

Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba kwa njia hizo, Benki zitapata imani kwamba maadam huyu hayuko kwenye orodha yetu, basi tumwamini na tumkopeshe. Kwa hiyo, zitakopesha zaidi na zinavyozidi kukopesha zaidi masharti yatakuwa nafuu zaidi kwa sababu ushindani utaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mabenki mengi kulundikana, kwa bahati mbaya hizi sio zama za Serikali kuziambia Benki wapi zifungue matawi. Benki zina uhuru wa wapi zifungue matawi na ni kweli kwa sababu ni Benki za biashara, zinakwenda Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, lakini hapa karibuni zimeanza pia kwenda kwenye Miji mingine ya Mikoa kama Mtwara, Lindi, Moshi, Tanga, zinaanza kuhamia kwenye Miji midogo. Miji mingine kwa mfano Kahama zikifuatilia madini na kadhalika. Kwa hiyo, kidogo kidogo mradi huko kuwe na biashara yaani wawekaji na wakopaji na biashara za namna hiyo, Benki zitaamua zenyewe kibiashara. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa tatizo la kukosa Wahasibu, nimelieleza kwenye hotuba yangu kwamba ni kweli Wahasibu hawatoshi, lakini zaidi ni

wale wenye sifa za juu *CPA*. Wale wenye sifa za kati, *Diploma* na kadhalika hali sio mbaya kama wale wenye sifa za juu. Hao ndio tunawasomesha kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, ndio tunawasomesha kwa viwango mbalimbali katika Vyuo vyetu vya Uhasibu.

Ningependa tu kusema na nilisema kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba tatizo kubwa tulilonalo ni kulipa mishahara mizuri ili hawa wanapoingia Serikalini wabaki humo. Mwaka 2004, Waziri wa Utumishi amewapa Wahasibu hawa mshahara mzuri wakati wakiongeza mishahara. Hawa wamefikiriwa kwa kiwango cha juu zaidi kuliko wengine, lakini bado ushindani ni mkubwa kwa sababu kuna upungufu mkubwa nchini na ndiyo maana tunaendelea kufundisha na kusomesha Wahasibu.

Kule kwenye Chuo cha Uhasibu cha Dar es Salaam, Kurasini, tatizo ni kweli lilikuwepo kama alivyosema Mwenyekiti, lakini hivi ninavyozungumza, Wakuu wa Idara watatu ambao ndio walikuwa hawajaajiriwa wamekwishaajiriwa, majengo yamekarabatiwa na sasa kinaonekana kama Chuo. *(Makofi)*

Kuhusu madeni ya ndani, nashukuru kwa hoja hii ya Mheshimiwa Njelu Kasaka. Mwezi Mei, wakati Kamati ya Fedha na Uchumi wakizungumza nasi, tulikuwa hatuna jibu. Hivi leo tuna jibu nalo ni kwamba baada ya madeni haya kuhakikiwa, tumethibitisha kwamba watumishi katika Serikali za Mitaa wanaidai Serikali shilingi bilioni 12 zilizohakikiwa. Hawa wengi wao ni Walimu na wasio Walimu, jumla ni shilingi bilioni 12.

Sasa kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, ndani ya miezi miwili ijayo, fedha hizi zitakuwa zimelipwa kwa utaratibu ambao tumekubaliana kati ya Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha na Waziri Mkuu mwenyewe ambaye kama alivyotoa hotuba hapa, yeye ndiye alikuwa kinara wa jambo hili na sisi ndio tunafanya ile kazi kule jikoni na chakula kimeshaiva ni mpangilio tu wa kupanga sahani na vijiko mambo yaweze kujipa. Kwa hiyo, naomba muamini kwamba tuko kazini kushughulikia tatizo hilo na kutekeleza agizo la Waziri Mkuu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ningependa nieleze tu kwamba Serikali yenyewe katika ngazi ya Baraza la Mawaziri ilikwishaamua mwezi uliopita kwamba tuanze mazungumzo upya na hawa wahusika kwa sababu kama mnavyoelewa watu hawa wako Mahakamani na kwa utaratibu ukishaenda Mahakamani basi, tunasubiri uamuzi wa Mahakama ndio maana Serikali haikujigusa. Lakini maadam sasa wao wenyewe wameonyesha nia ya kutaka kuzungumza na Serikali, basi taratibu za kisheria zitafuata na sisi tumeshajiandaa kuzungumza nao. Iko Kamati maalum ambayo imeundwa ya kuzungumza nao ili tuweze kumaliza jambo hili kindugu, labda na kwa haraka zaidi kuliko kusubiri Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumtambua Mheshimiwa Nimrod Mkono, ambaye sikumtaja hapa kama alichangia kwa maandishi, naona anaondoka, kwa hiyo, nilitaka kumtambua na vile vile Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, ambaye naye alichangia kwa maandishi na nilikuwa sijamtambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la wafanyakazi kutozwa kodi kubwa mno, naomba kesho mnisikilize wakati wa hotuba yangu nikiwasilisha Muswada wa Fedha. Kesho nitasema mambo marefu kidogo juu ya jambo hili ili kuondoa maneno yote. Kwa hiyo, msisite kunisikiliza, lakini maneno yote ni mazuri. Nataka niwahakikishieni nitasema maneno mazuri kesho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato ya Serikali, mambo yote yanayohusu misamaha ya kodi yako kwenye Tovuti ya Wizara ya Fedha. Naomba mtu yeyote anayetaka kujua ni nani amepata msamaha, kiasi gani na kwa muda gani, aende kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha atapata kila kitu pale. Lakini utaratibu wenyewe unajulikana na ni wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Njelu Kasaka kwamba tukipata habari za maana kwenye ukaguzi wa migodi ya dhahabu tutatoa taarifa na vile vile *by the way* hii habari ya kesho, hata lile la wigo wa kodi pia nitalisemea kwenye Muswada nitakaokuwa nawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza wigo maana yake ni kuongeza mchango wa kodi kwenye Pato la Taifa. Asilimia 15 ni nzuri na sisi tunatarajia kwamba ikifika mwaka 2007/2008 tutakuwa tumefika ngazi hiyo ya asilimia 15 ya *contribution* kwa upande wa kodi.

Hili la *VAT* kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya Bajeti, hata Serikali yenyewe kweli ina nia lakini kama nilivyosema tulikubaliana kwamba mwaka huu tufikirie kwanza vile viwango vya juu *threshold,* tukasema iwe shilingi milioni 40 badala ya shilingi milioni 20. Mwaka ujao tutafikiria viwango kama vitakuwa chini ya 20 na kama ni ndiyo, ni kiasi gani na maana yake ni nini. Kwa hiyo, naomba mtupe muda, pengine mwakani tutakuwa na la kusema juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya Wilaya na Halmashauri na vifaa vya kizamani na nini, kwa kweli hayo ni ya Halmashauri na kuna mpango wa kuboresha Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, huko ndiko mambo yanakofanyika na tumaini letu ni kwamba mambo haya yatarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *National Microfinance Bank,* kama alivyojibu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ubinafsishaji huu unaendelea kama tulivyoelewana na kwa mujibu wa taratibu za *PSRC,* hakuna jipya la kusema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa haya nimetoa madukuduku makubwa yaliyokuwa yanaikera Kamati ya Fedha na Uchumi, nadhani nimemaliza yote, labda kama baadaye kutatokea swali la ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maelezo kuhusiana na hoja alizotoa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Leo mimi lazima nimsifu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwamba amezungumza ki-*executive* kabisa, kwa utulivu na kwa

heshima na taadhima na mimi kwa heshima na taadhima lazima nimjibu, maana ndio kazi yetu hapa kuheshimiana na kujibizana kwa heshima na taadhima. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la kutaka kujua hisa za Serikali ndani ya Mashirika mbalimbali pia lipo kwenye Tovuti ya Hazina. Mambo ya kileo ndio yanaingia huko kama hayo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge asome kwa sababu ni mengi na muda hauruhusu.

Kuhusu Benki Kuu kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ndivyo. Hadi sasa Benki Kuu ilikuwa inakaguliwa na *Tanzania Audit Corporation.* Baada ya Shirika lile kukabidhiwa watumishi, kuanzia mwezi Julai, 2004 Benki Kuu itakuwa inakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hilo halina migogoro. Hili la madeni, namna ya ku-*treat* madeni na kadhalika, tunalichukua, tulifanyie kazi kwa sababu ni jambo la kitaalam kidogo, lote lile linalohusiana na madeni, *point* kama nne hivi tutazifanyia kazi, ni *point* nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na wadai wa madeni wasio wanachama wa *Paris Club* au wanachama lakini wasiwe *G8* (sio wale matajiri), ni kweli hawa wapo na kama alivyopendekeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, sisi tunafanya hivyo hivyo alivyopendekeza, kwamba tunazungumza nao kwa masharti ambayo sio mia kwa mia ya *Paris Club,* lakini yanakubalika ndani ya *Paris Club.* Ndivyo tunavyoifanya, kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo, tunakubaliana naye.

Kuna suala la namna Mashirika yetu ya pensheni yanavyoweza kubuni mbinu za kuwasaidia wanachama wake. Najua kwamba *PPF* kama alivyosema mwenyewe Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wanafanya kazi hiyo vizuri, wameanza vizuri fikra za kimapinduzi, najua kwamba *NSSF* wana mipango yao vile vile, kwa hiyo, hili tuliachie Bodi za Mashirika hayo ziendelee kubuni. Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kubuni kama ni mikopo, sawa lakini waangalie. Ila kwa hulka, mifuko ya namna hii ina namna zake, ina mambo ambayo yanakubalika ya kutumia fedha zake na mambo mengine hayakubaliki. Hili tutalipeleka kwenye Bodi hizo ziweze kufikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la wanaodai pensheni zao, usumbufu uliopo sasa, tumeamua kama nilivyosema kwenye hotuba yangu mwaka huu kwamba kuanzia sasa mwajiri mwenyewe ndiye atamshughulikia mtumishi kuleta zile kumbukumbu zilizokosekana na kuzitafuta mpaka atuletee sisi Hazina *full file.* Badala ya mtumishi kuzungukazunguka mwajiri wake wa mwisho ndiye atazunguka hadi atakapofikisha *file* ndani ya *Treasury.* Kwa hiyo, nakubalina na Mheshimiwa Mbunge kwamba nalo ni wazo zuri.

Mwisho katika mapendekezo, yale mambo ambayo yanahusu Tume ya Pamoja, tutaendelea kutumia Tume ya Pamoja. Kwa bahati mbaya bado wako kwenye hatua za mwanzo za kujizatiti na hakuna mapya sana, isipokuwa mwaka 2004/2005 ndio kweli utakuwa mwaka wao wa kazi.

Kuna Mheshimiwa mmoja alisema, sasa itakuwaje hii miezi sita, sita ya pensheni? Mimi niseme tu kwamba jambo hili tulipe muda, maana kuna gharama zake, ukilipa kila mwezi au miezi fulani kuna gharama zake. Tupeni muda tuweze kulichunguza tuone litakuwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nimrod Mkono, alikuwa na dukuduku hapa na lazima nijibu hili dukuduku, kwamba kwa nini wananchi wa kawaida wanapochangia mifuko yao ya maendeleo wasipewe misamaha ya kodi kama wanavyochangia wengine? Nimeeleza hapa wiki iliyopita juu ya utaratibu kwa wanaochangia maendeleo yao Vijijini, Shule, Zahanati na kadhalika, nilipotoa kauli ya Serikali hapa. Ile ilihusu watu wanaolipa kodi za mapato, lakini kwa miradi ya maendeleo ya kawaida Vijijini, hii ya *TASAF* ya Elimu na kadhalika kwa kweli kitu ambacho kinaweza kikasamehewa ni *VAT*. Kama kuna Taasisi ambayo inashughulika, *VAT* inaweza ikasamehewa kwa kupitia *NGO* inayoshughulika na mradi huo. Lakini sisi tunaogopa kwamba tatizo kubwa kwenye jambo hili kwanza ni kupunguza sana kodi inayopatikana na *VAT,* hatari iliyopo na ya pili ni usimamizi wake unakuwa mgumu sana. Ni vigumu sana kusimamia utaratibu wa kusema ukinunua mabati, misumari na saruji usilipe *VAT*. Kusimamia miradi hiyo midogo midogo toka Zahanati mpaka Shule na mambo mengi Kijijini inakuwa ni tabu sana, hakuna uwezekano. Kwa hiyo, wajanja wanaweza wakaiba na Serikali ikapoteza sana mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama Kijijini kunaingia kitu kama *windmill,* Mheshimiwa Nimrod Mkono, alitaja hapa, *windmill* ni mtambo, hata kama umekuja lakini bado haijakamilika, sio mzima lakini ni vipande vya kuunganisha. Ule ni mtambo na una msamaha wake wa kodi na ushuru. Kwa hiyo, hilo ni suala tu ambalo nimelitaja hata kesho nitalizungumzia kwenye Sheria ya *Finance Bill.* Kwa hiyo, hilo lisitie tabu, lakini ningependa tu kumhakikisha Mheshimiwa Nimrod Mkono kwamba ukweli wetu ndio huo, lakini kama ana mawazo zaidi tutayapokea na kuyaingiza kwenye sheria. Mimi nilipopata hili la *windmill* mara moja nimeliingiza. Kama kuna namna nyingine mpya tutaendelea hivyo ilimradi tufanye mambo kisheria. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wale ambao wamechangia, tutayachukua yote hayo, labda niseme tu kwamba hili la fidia kwa Halmashauri zenyewe zile ambazo zimepoteza fedha kutokana na kufuta zile kodi za kero, fidia iliyotoka ni ile ambayo tulikubaliana na Wizara ya Serikali za Mitaa. Lakini tunaangalia upya tena kama kuna mahali tulifanya makosa ili turekebishe tukishirikiana na Serikali za Mitaa. Kama kutatokea hali hiyo ya kwamba pengine mahali fulani watu walipunjwa au hesabu zilikwenda vibaya, kuna uwezekano wa kurekebisha hapa na pale. Lakini hatuwezi kufidia tu kwa sababu vyanzo vile vilitoweka. Hilo litakuwa jambo jipya na litahitaji *study* mpya, kwa sababu utaanzia wapi na utamalizia wapi! Lakini kurejea kama tulifanya makosa, hilo nina uhakika ni jambo linaloweza kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwahakikisha Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla na Waheshimiwa Wajumbe wa Kambi ya Upinzani, kwamba kama mtakavyoona wenyewe, Wizara ya Fedha ni Wizara inayotumia fedha nyingi kwa mambo mengi. Kama nilivyosema hapa wakati

mmoja, hata siku moja sisi hatuwezi kusema kwamba mambo yetu yote ni sawa, safi, kwa sababu tunashughulika na binadamu. Lakini yeyote anayetaka kutupima aangalie *graph*. *Graph* inapanda au inateremka? Mimi natoa hoja kwenu kwamba maadam *graph* inapanda, *zigzag* kidogo hapa na pale tutaendelea kusahihishana na kupitisha Bajeti ili tuendelee kufanya hizi *zigzag* zilizobaki tufukie mashimo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana hoja imetolewa. Uongozi wa Spika.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo tuna Wizara mbili ambazo zimesoma kwa pamoja na tunakwenda katika Kamati ya Matumizi. Hivi taratibu zetu zinasemaje kama Wizara moja ikikwamishwa itakuwaje? Naomba mwongozo wako. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benedict Losurutia, ameuliza jambo zuri na pengine alikuwa anataka kujua *procedure* itakayotumika.

Sasa tutafanya hivi tutakapoingia kwenye Kamati ya Matumizi, tutaipitisha hoja moja moja. Tutaanza na hoja ya Waziri wa Mipango na ubinafsishaji, tutamaliza na vifungu vyake. Halafu tutaingia hoja ya Waziri wa Fedha tutamaliza vifungu vyake halafu tutakuja hapa, taarifa itatolewa kwenu yale ambayo tunayapitisha na kila hoja itahojiwa peke yake.

Kwa hiyo, wala usiwe na wasi wasi, *procedure* iko *under control* mambo yatakwenda vizuri. Baada ya maelezo hayo hatua inayofuata, Katibu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ..5,856,385,000/=

**MWENYEKITI:** Naona wale ambao mnakaa tu mkae ili nione nani wanasimama hasa. Kwa hiyo, nawaona moja, mbili, tatu, nne. Nawaona Waheshimiwa Wabunge wanne na tunaanza na Mheshimiwa Lucas Selelii, tunakwenda hivi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kifungu 1001, kifungu kidogo 250100, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Nahitaji maelezo, wakati nachangia kwa maandishi nimezungumzia mkakati wa kuondoa umaskini hasa *vision 2025* nimezungumzia ni namna gani Serikali au katika mkakati huo tumejipanga kama tulivyojipanga katika elimu. Katika elimu au maji au barabara au

sehemu zingine zote tumejipanga kwamba ifikapo mwaka kadhaa tunajenga madarasa kadhaa. Tumejipanga sasa hivi katika MMES kwamba ifikapo mwaka 2009 tutakuwa tumejenga madarasa ya sekondari au shule za sekondari kadhaa.

Lakini kwa upande wa wakulima ambacho ninaamini kama tungejipanga vizuri katika sekta hii ya kilimo kwa sababu mipango ingekuwa mizuri kwa sekta ya kilimo tungeweka lengo au muda wa kufikia kuondoa hasa jembe la mkono ambalo naona ni kikwazo kikubwa sana katika kuondosha umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hapa amesema tu kwamba litaondoka kwa taratibu, hatua kwa hatua. Lakini hatua kwa hatua ni namna gani? Ningemwelewa kama angeweka mwaka 2000-2010 au 2015 wakulima kadhaa wangeondokana na jembe la mkono au kadhaa. Lakini kusema hatua kwa hatua, ni vipi?

Nahitaji maelezo kwa sababu mwaka 2003 Serikali imeagiza matrekta 23 tu. Sasa kama kweli tumedhamiria kuondoa umaskini kwa kuagiza matrekta 23 bila kuondoa jembe la mkono kwa kweli bado mimi sijaridhika na kwamba kweli tutaondoa umaskini. Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucas Selelii kama ifuatavyo:-

Wakati tunapopanga katika sekta ya kilimo tuna mipango mingi, kuna mipango ya maendeleo vijijini ambayo inalenga katika kuboresha kilimo. Tunao mpango wa mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo yenyewe na katika mkakati huo tumesema tutatoa umuhimu mkubwa katika kuboresha kwanza miundo mbinu yenyewe ya kilimo, teknolojia ya kilimo kwa maana ya pembejeo, utaratibu wa masoko na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema kwamba jembe la mkono litakwisha mwaka gani. Hili jembe la mkono nimezaliwa, nimelikuta, sasa naelekea kwenye kuzeeka, nitaliacha. Sasa kutoa muda *perfect* kwamba mwaka 2005 jembe la mkono litaondoka, kwa kweli kwangu itakuwa ni suala gumu sana. Lakini ninachosema ni kwamba kwa mikakati hii iliyowekwa na Serikali, majembe ya *plough* tunaendeleza, tunavyoendeleza utaratibu wa pembejeo, mimi nina hakika pole pole hizi *bottle neck beraking technology* tutaingiza katika kilimo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri hajajibu swali langu. Basi kwa sababu hana jibu, angejibu hivi, hakuna mpango kwenye mpango wa *vision 2025* ya kuondosha jembe la mkono. Mimi ningeridhika. *(Makofi)*

Lakini kweli inapanga mpango Wizara ya Mipango ipo. Kama unaweza kupanga madarasa, kama unaweza kupanga shule za sekondari, unashindwaje kupanga kuondoa jembe la mkono? Jibu ni kwamba hakuna mpango. Mimi sina tatizo la mshahara wake.

Ningeridhika, tutakaa hapa tutapanga kwamba ifikapo mwaka 2020 tutaondoa jembe la mkono basi. Ajibu tu kwamba hakuna mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unajibu hivyo kwamba hamna mpango? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu suala la nyongeza la Mheshimiwa Lucas Selelii, kama ifuatavyo:-

Mehsimiwa Mwenyekiti, utaratibu wetu wa kupanga sasa hivi siyo *Central Planning.* Hatuwezi ukilinganisha suala la jembe na madarasa. Tunachozungumzia ni *Sectoral Planning,* mipango ipo na ndio maana tunasema kwamba tunataka turekebishe teknolojia na kuboresha teknolojia katika sekta ya kilimo. Lakini ninachosema pamoja na mipango hiyo nikisema kwamba jembe la mkono tutaliondoa mwaka 2007 kwa kweli nitakuwa nasema uongo na kwenye mipango huwezi kusema uongo na mimi nafikiri kutokana na dira yetu ya mwaka 2025 tutakapofika huko kwa hatua kubwa sana sekta ya kilimo wakulima wetu watakuwa wanatumia zana za kisasa badala ya majembe ya mkono. *(Makofi)*

**MHE. ROSTAM AZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub-Vote 1001* mshahara wa Waziri. Wakati nikichangia asubuhi nilizungumza hoja ya msingi ambayo ilikuwa inasema kwamba Wizara hii ya Mipango na Ubinafsishaji, haina mipango, ni ubinafsishaji tu. Haya ndiyo niliyoyasema wakati nikichangia asubuhi na Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu hapa alitumia muda mrefu sana kutushawishi kwamba kuna mipango. Lakini kwa bahati mbaya jitihada zake hazikunishawishi kwamba kuna mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara hivi sasa haina Makamishna. Tume ya Mipango hivi sasa haina Makamishna. Bajeti zake tunazisoma, zaidi ya takwimu ambazo zinatoka Wizara mbalimbali pamoja na Benki Kuu kuhusu ukuaji wa uchumi na kadhalika. Hamna kingine chochote ambacho kinaashiria kwamba kuna mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa maelezo ya ziada ya kukiri kwamba kweli hakuna mipango na hatua gani wanachukua ili kurekebisha hali hiyo? La kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilizungumzia habari ya kuporomoka kwa thamani ya shilingi na nikasema kwamba kutokana na *balance of payments* na *inflation rate* yetu ukilinganisha na nchi ambazo tunafanya nazo biashara sikuona sababu kwa nini shilingi inaendelea kuporomoka siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri katika majibu yake alijaribu kunishawishi kwamba hiyo ilikuwa ni ya lazima na kwamba ilikuwa ikisaidia katika mauzo ya nje katika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Waziri anajua kwamba toka waanze muda mrefu toka waanze kuporosha hii shilingi, mapato ya mazao yanayosafirishwa nchi za nje hayajapanda kabisa na kwa maana hiyo, huku kuporomoka kwa shilingi hakujasaidia kabisa katika kuuza mazao yetu nchi za nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya uhakika zaidi na ya ukweli zaidi, halafu tutamwachia aendelee baada ya kupata hayo maelezo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya nyongeza ya Mheshimiwa Rostam Aziz, kama ifuatavyo:-

Katika kutoa maelezo yangu nimesema kwamba haiwezekani kwa nchi yoyote ambayo katika vigezo vyote inaambiwa ni nchi ya tatu katika kukuza uchumi wake katika nchi za *SADC* na mwaka 2004 kuwa nchi ya kwanza katika nchi ya Afrika za Mashariki katika kukuza uchumi wake. Nchi hiyo iwe isiwe na mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hata kidogo na hizo takwimu ziko wazi tu na wala sio za kificho. Ninachosema ni kwamba tunapozungumzia kuzorota kwa uchumi wetu inawezekana tukazungumzia eneo la utekelezaji. Sasa tukishazungumzia eneo la utekelezaji tujue kwamba matatizo ya utekelezaji hayo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mpango wa kupunguza umaskini. Tunao mpango wa muda wa kati na wa muda mrefu. Tunayo dira ya maendeleo ya mwaka 2025 ambayo imefanyiwa kazi na vyombo vyote na taasisi zote. Ninachosema bado nazidi kusisitiza kwamba kwa kweli nchi ya Tanzania ina mipango mizuri sana. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge tuangalie taratibu za kufikia malengo ya utekelezaji kwa yale tunayoyaweka sisi wenyewe. Lakini mipango tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna la pili la shilingi. Nakubaliana na Mheshimiwa Rostam Aziz, kwamba thamani yetu ya shilingi inashuka na mimi katika maelezo yangu nimesema hivi, kama tunataka kuboresha nguvu ya shilingi yetu ni lazima tukazane, ni lazima tujitahidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujitahidi kukuza uzalishaji wa mazao yetu tunayouza nje. Tunajitahidi sana kwa kweli kukuza mazao yetu tunayouza nje. Lakini kwa bahati mbaya mazao haya tunayauza yakiwa ghafi. Tuingie katika utaratibu wa kuyasindika. Lakini vile vile tutakapoingia katika utaratibu wa kuyasindika siku hizi kumekuja *concept* mpya hata *branding* pia inaongeza thamani ya bidhaa hizo. Nadhani tukifikia hapo na ndiyo mkakati ambao tumesema tutaweka katika hii *Tanzania Min Tiger* katika kipindi hiki kijacho. Nina hakika kwamba tutazidi kuimarisha shilingi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa thamani ya shilingi si Tanzania peke yake. *Japanese Yen* inashuka nimesema, *British Pound* inashuka. Hivi karibuni dola ilishuka uki-*compare* na *Euro.* Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Rostam Aziz,

kwamba lazima tukuze uzalishaji nje, uuzaji wa mazao yetu nje. Ahsante Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. ROSTAM AZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusema kwamba uchumi wetu haukui. Sikusema kwamba nchi yetu haina mipango. Nilichosema ni kwamba Wizara hii ya Mipango haifanyi kazi ambazo zimekusudiwa kufanywa na Wizara hii. Mipango, huu uchumi unavyokua hivi sasa ni kila Wizara inafanya kazi yake na siyo kwamba huu uchumi umepangwa na Wizara ya Mipango au tuseme miradi ya kipaumbele imepangwa na Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nikisema ni kwamba hii Wizara ingesaidia sana kama na yenyewe ingejihusisha na kupanga na kuweza kutusaidia kuweka miradi ya kipaumbele ili uchumi kama unakua kwa asilimia tano basi ukue kwa asilimia 8. Hilo ndilo nililolisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la shilingi nimesema kwamba mauzo yetu ya bidhaa hayajaongezeka pamoja na kuporomoka kwa shilingi na Waziri nimefurahi hapa amesema kwamba labda tungejitahidi kuanza kusindika haya mazao kabla hatujauza nje. Lakini kusindika mazao maana yake ni kuweka viwanda na kuweka viwanda ni pamoja na ku-*import machinery* na ku-*import machinery* maana yake ni kwamba shilingi ikizidi kuporomoka namna hii mashine hizo zinakuwa ghali zaidi. Nadhani tuna-*defend* hoja hii ya kujaribu kusaidia kukuza kilimo na kukuza biashara hii ya kuuza mazao nje kama tukiendelea kuporomosha shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya ziada kidogo, je, Wizara hii ina mpango gani wa kujirejesha katika majukumu ambayo yaliwekwa wakati ikiundwa. Iliundwa kisheria na sheria ile bado ipo na Makamishna lini watarudishwa ili waweze kutusaidia katika kuweka mipango yetu sawa? Nashukuru sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rostam Aziz, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba katika mgawanyo wa majukumu katika nchi, tamko la kuunda Wizara Kikatiba na kwa mujibu wa madaraka yaliyopo linatoka kwa Mheshimiwa Rais.

Kwa hiyo, Wizara yote inapoundwa ni *prerogative* ya Mheshimiwa Rais na wakati Mheshimiwa Rostam Aziz, akichangia leo asubuhi hapa amesema vizuri kwamba Mipango tunaangalia *stability* au ku-*economic fundamentals,* mipango maana yake ni kutathmini na kubuni mipango, kuratibu. Tukichukua orodha ya mipango ambayo tumeitayarisha kama Wizara ya Mipango, uko mpango wa muda mrefu tunautayarisha tunausambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dira ya maendeleo ya mwaka 2025 tumetayarisha, tumepeleka Mikoani mpaka Wilayani mpaka kwa Waheshimiwa Wabunge. Kuna

*medium term planning* tumeifanyia kazi Wizara yetu tumepeleka mpaka ikafika kwa Waheshimiwa Wabunge. Kuna mipango ya mwaka ambayo tunaitoa mara kwa mara. *(Kicheko/Makofi)*

Kuna mkakati wa kupunguza umaskini *(Poverty Reduction Strategy)* tumetayarisha, tumesambaza kila mahali. Lakini vile vile tumefanya mpango mmoja mkubwa sana miaka miwili iliyopita, kuhesabu watu wote Tanzania nzima kupitia *census.* Ule ni mpango na umesimamiwa na Wizara yangu, mipango ipo. Labda Mheshimiwa Rostam Aziz, tukubaliane kwamba mipango ipo. Sasa tuzungumzie utekelezaji, hapo tutakubaliana. *(Makofi)*

Lakini hili la kwamba thamani ya bei yetu itapungua na tununue viwanda kutoka nje na mitambo ndiyo maana shilingi yetu inashuka. Thamani bado tunarudi pale pale, kwamba lazima tufanye kazi kwa bidii tuongeze *export sector gross* tuweze ku-*export* nje. Sasa hili mimi sioni kama lina ubishi mkubwa sana na kama nilivyosema mwanzoni Mheshimiwa Rostam Aziz, unga hoja hii tutekeleze Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi niko katika fungu hilo la *Vote 66 programme 10, Sub-Vote 1001* na kifungu kidogo 25100 mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri anisaidie baada ya Waheshimiwa Wabunge kupata nafasi katika Kamati zao kuzunguka waliweza kugundua mambo mengi. Moja walikuta kiwanda cha Sukari Mtibwa *share 25* iliacha kwa ajili ya Serikali ili iwape wananchi, *share 20* amerudishiwa *investor* yule yule, tano ndio zimebaki. Je, Waziri hayo ndiyo makubaliano yetu? Nataka anisaidie hilo.

La pili, naomba anisaidie mimi naamini kuna kitu kinaitwa *Strategic Long Term Planning* ama *Strategic Implementation* angalau Waziri alikubali *implementation* ndiyo tatizo. Naamini kabisa katika Wizara ya *Good Governance* ili wakamisheni sekta zote kupanga mipango ya kupambana na rushwa. Kwa hiyo na yeye yuko katika ile *Sectoral Anti-Corruption Action Plan* kama nimeikosea lakini anaijua maana yangu.

Lakini imejitokeza *plan,* zikikutana na rushwa, zikikutana na utekelezaji mbaya, *plan* zako nzuri ambazo unazo ambazo nimesema *ever strategic thinking, long term planning with diffidence in implementation* kwa maana isikutane na rushwa na utekelezaji mbaya. Serikali mipango yake inaathirika, je, pale inapojitokeza sehemu mbalimbali zinaonekana zimeingiliwa na rushwa au matumizi mabaya, mfano *PAC* ilishagundua kuna kitu *TVT,* Maafa, kuna suala la *TANSORT* kuna suala la *package.* Je, Wizara yake ambayo inapanga mipango ili isaidie nchi na mipango mizuri tu na ninasema ni mizuri, inafanya mkakati gani katika suala zima la wajibu aliopewa ya *Sectoral Action Plan on such corruption?* Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya nyongeza kutokana na hoja za Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Serikali inapoamua kuuza hisa zake tunajaribu kuepuka taratibu za kuingia gharama ambazo inaona kwamba ni mzigo. Sasa ikiwa kama kwenye mradi fulani yupo *strategic investor* na *investor* yule anaweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaweza ikauza hisa zake. Sasa katika utaratibu huu wa Serikali inapoamua hivyo, kwa kweli hatuwezi kusema kwamba labda kuna tatizo la rushwa limepitika. Serikali inauza hisa zake inanunua hisa zake, kwa utaratibu na kanuni zilizowekwa kisheria kabisa.

Kwa hiyo, hilo tuliondolee wasiwasi. Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, nakubaliana na wewe kwamba tunapozungumzia masuala ya *strategic thinking, strategic planning* na hata *strategic implementation* suala la rushwa linapoingia, mipango haiwezi kwenda vizuri. Nakubaliana na wewe asilimia mia moja. Lakini nadhani unaelewa jitihada za Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi katika kuona ni jinsi gani tunapambana na suala la rushwa. Katika nchi yetu suala la kupambana na rushwa limewekewa mkakati unaotekelezwa katika ngazi mbalimbali.

Kwanza ngazi ya Taifa, kuna mkakati wa Taifa kupambana na rushwa, mkakati huu unatekelezwa na Serikali kwa kushinikisha sekta binafsi, jumuiya za kiraia, *media,* mashirika yasiyo ya kiserikali na madhehebu ya dini. Lakini vile vile kuna ngazi za Wizara kila Wizara iliagizwa kutayarishwa *action plan* ya kudhibiti rushwa katika Taasisi zao au asasi zao na hilo linafanyika.

Kwa hiyo, sisi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji vile vile tumetayarisha *action plan* ya kuona kwamba sekta zote zinadhibiti rushwa. Lakini vile vile kwa ujumla wake utekelezaji wa ratiba ya kudhibiti rushwa umepunguza urasimu katika maeneo mengi sana. Lakini kwa mara ya kwanza vile vile iko Wizara maalum ya kuhusika na mambo ya rushwa ambayo ni Wizara inayoendeshwa na Mheshimiwa Wilson Masilingi.

Lakini vile vile kuna *PCB* ambayo nayo inafuatilia suala hilo. Nina hakika kwamba kiwango cha rushwa kinachoongelewa hapo nyuma na sasa kidogo kinapungua na tutaendelea kuwa katika hali hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 50 (4), mzungumzaji aliyetoka kusema sasa hivi Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, anasema *PAC* imebaini rushwa katika Kamati yakem *TVT,* Maafa na *TANSORT* na *TACAIDS.*

Nafahamu kwamba *PAC* waliunda Kamati ndogo ndogo kuchambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kwa tabia kwa Kanuni hii watakuja kuwasilisha ile ripoti hapa. Sasa Kanuni nataka kumsomea hapa inasema ni marufuku

kwa Mbunge yoyote kuzungumzia shughuli yoyote ya Kamati ya Bunge mpaka shughuli hiyo iwe imeshawasilishwa Bungeni kama Taarifa au ripoti ya Kamati juu ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, naona ulisimama ulitaka kusemaje?

Naendelea bado ametoa hoja. Sasa katoa utaratibu ambao lazima ufafanuliwe kwanza ndipo utapata nafasi. Sasa kifungu hicho kinasema kweli kama iliundwa Kamati ya kushughulikia hilo jambo, tunangoja *vote* yake ndipo tuijadili. Sasa inawezekana wenzetu hiyo ripoti uliipata pata sisi hatuijui. Kwa hiyo, si vizuri kulizungumzia jambo ambalo tuna uhakika kuna Kamati na itawasilishwa hapa Bungeni ili ijadiliwe. Kwa hiyo, endelea.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hebu subiri kwanza Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Mheshimiwa Mbunge ulitaka kuongelea.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako rasmi kwamba taarifa hiyo ya Kamati bado haijafikishwa kwenye Bunge na bado hata hatujamwambia Mheshimiwa Spika, kwamba ni lini tutaiwasilisha. Kwa hiyo, taarifa haijatoka kwa mtu yeyote ukiacha Wajumbe wa Kamati yenyewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hii inaimarisha ile hoja kwamba Kamati haijawasilisha. Kwanza hoja kwamba ilikuwepo Kamati, kweli ilikuwepo. Hoja hiyo haijawasilishwa bado ni kweli. Kwa hiyo, kufuatana na Kanuni hii hairuhusiwi, ni marufuku kuijadili hiyo Kamati. Kwa hiyo, naomba uondoe hiyo hoja kwamba iligundua rushwa.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hili sijasema, kwanza sikujua kwamba wameunda Kamati. Lakini kitu ninachokifahamu walionyesha *queries* zao kwa matumizi yao ndicho nilichosema. Ninachofahamu walionyesha, kama waliunda Kamati hawajaniambia mimi. Mimi nasema imeonyeshwa kwamba kuna wasiwasi wa rushwa au matumizi mabaya. Kwa hiyo, mimi sijazungumzia ripoti yao na sijui wala sina. Hilo nilitaka nili-*clear.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, naomba ukae. Uliposimama ulisema kuna Kamati imegundua kwamba kuna hilo, hilo, hilo. Sasa unageuka kwamba hukusema hivyo. *(Makofi)*

Ni kwamba basi ulikuwa hujui hilo ni kweli limeundiwa Kamati, haijatoa taarifa. Kwa hiyo, uliondoe. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana na nashukuru kusikia *PAC* imeunda Kamati. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, nisiendeleze, nitaliendeleza baadaye baada ya ripoti ikitoka. Lakini narudi kwenye suala la Mtibwa. Sisi wote hapa Wabunge tulikaa tukakubaliana .......

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Eee.

**MWENYEKITI:** Sijui kwa nini tuna, mimi nimetoa maelekezo kwamba ufute huo usemi kwamba umegundua rushwa, halafu tuendelee.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana nawe na nimesema kwamba, hilo nimelifuta, nitalizungumza likiletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naendelea na la Mtibwa ambalo halipo kwenye *PAC.*

**MWENYEKITI:** Enhee.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Kwamba sisi wote tulikubaliana na suala la ubinafsishaji, *investor* pamoja na wananchi na katika *share* tunazosema za wananchi ni ile *share* ya Serikali, *share 25* iliyobaki kwenye Serikali, wafanyakazi wa Mtibwa walitaka kununua, wamekataliwa na sisi tumesema hawa angalau wapewe *priority* kwa sababu ndio wafanyakazi lakini leo Serikali inasema ahaa si lazima wapewe wananchi. Tulibishana hapa kwenye suala la *Microfinance* kwenye *share,* kwa hiyo, kwa tamko hili inaonyesha hata *Microfinance* baadaye itapewa huyo atakayepewa kwa sababu ile ya Serikali anaweza kuwa mtu yeyote, inanitisha. Isipokuwa nataka kusema kwamba ni kweli kabisa Serikali haikuwatendea haki wafanyakazi wa Mtibwa waliotaka kununua.

**MWENYEKITI:** Ngoja ajibu kwanza hilo unalolisema kama ni kweli, akishajibu kama ni kweli basi utaendelea. Mheshimiwa Waziri hoja yake nadhani umeisikia kulikuwa na hisa ziliachwa pembeni 25, zimeuzwa 20 bado tano. Kwa hiyo, ni kweli na kwa nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema hapo awali, mkiwa ninyi ni wawekezaji ambao mna *shares* kwa utaratibu huu ni kati ya Serikali na *strategic investor,* Serikali ikaona kwamba haiwezi kuhudumia *share* zake zile, inao uwezo kisheria kabisa kuuza hisa zake ili kuondokana na tatizo la kutokuweza kuhudumia *share* hizo kwa maana ya uwekezaji. Lakini vile vile tunaposema tunasikitika *share* za Serikali zimeuzwa bila kupewa wafanyakazi, Serikali hiyo hiyo inayomiliki *share* inamiliki kwa niaba ya wananchi wote Tanzania ambao ni pamoja na wafanyakazi hao. Sasa tunachosema ni kwamba hata wale

wafanyakazi wangepewa *share* asilimia 25 wasingeweza kuzimudu *share* zile katika uendeshaji wa kiwanda kile wakati ambapo Serikali ilikuwa imeshashindwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Naomba nipate tu ufafanuzi kidogo *Vote 66, programme 10, subvote 1001,* mshahara wa Waziri.

Kwanza nchi hii ina mipango mizuri, mambo tunayoyaona yanayofanyika katika barabara, elimu, afya ni kutokana na mipango mizuri. Bila kuwa na mipango mizuri naona leo hapa tungekuwa katika hali mbaya sana. Kwa hiyo, kwa ujumla mimi naipongeza Serikali kwa mipango yake mizuri na mafanikio makubwa tuliyopata, uchumi wetu unakua, *inflation rate* imeshuka, mapato ya Serikali yameongezeka, hayo yote ni kutokana na mipango mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango wowote mzuri una kasoro ama matatizo, hilo ndilo nataka kuzungumza. Mimi nazungumzia jinsi ya kutafuta mkodishaji wa *TRC*. *TRC* itakodishwa, atakodisha ili afanye biashara sio aweke tu pesa zakek lakini tunavyofahamu miundombinu ya *TRC* ipo katika hali mbaya, mabehewa, reli na mambo mengi tu yapo katika hali isiyoridhisha. Kwa hiyo, nataka nifahamu Serikali ina mpango gani wa kuiweka miundombinu ya *TRC* katika hali nzuri ili mkodishaji atakayekuja kukodi hiyo *TRC* aweze kufanya biashara siyo kutoa sadaka? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, inafahamika wazi kwamba, Serikali imejiondoa katika mambo ya uchumi lakini wawekezaji tunaowapata wote wanawekeza katika *light industries,* hakuna mwekezaji yoyote anayewekeza katika *heavy industries* ili mtaji wake urudi baada ya miaka mingi. Sasa katika hali hii nchi hii tutaendelea bila kuwa na *heavy industries* kama kiwanda cha Chuma ya Liganga na viwanda vingine vya *chemicals* yaani viwanda mama. Je, Serikali ina mpango gani katika mpango wa *heavy industries? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga kama ifuatavyo:-

Nilijibu swali hapa Bungeni kuhusu kuboresha *TRC* kabla ya ubinafsishaji, nilisema kwamba *World Bank* imekubali kutoa takriban dola milioni 30 kuendeleza uboreshaji wa miundombinu ya *TRC* ambayo kwa sasa hivi ipo katika hali mbaya sana. *TRC* inahitaji mabehewa kama mia tatu na tulizungumza hapa Bungeni na katika Kamati mbalimbali kwamba ili *TRC* iweze kuamka sasa hivi inahitaji zaidi ya dola milioni sabini. Sasa kutokana na hali hiyo tukasema Serikali haiwezi, njia nzuri ya kufanya ni kuibinafsisha *TRC* kwa njia ya ukodishaji, tukatangaza zabuni, tukapata wawekezaji sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji hao ni *Grate Rate Railways Company* ya Afrika Kusini, *Right Consosium* ya India, *Enely Pias Pour Neck* ya Afrika Kusini, *CANAC* ya Canada, *Dynamic Rail* na kadhalika, hizi sasa hivi zinatathminiwa, wanaangalia *bid* zao kuona kwamba ni mwekezaji gani mzuri ataweza kuiboresha reli. Lakini tunachosema katika ubinafsishaji huu hatutaki kukurupuka hasa katika kubinafsisha *TRC,* tunataka tufanye kwa makini zaidi. Tunaogopa tusije tukaingia katika uzoefu wa New Zealand au *Britain* nchi kubwa kama ile ilipata matatizo makubwa sana wakati wa kukodisha reli yake. Sasa nafikiri Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali ina mkakati wa kuona kwamba tunajaribu kuboresha *TRC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la *heavy industries* tumeanza sasa tunazungumzia *Mtwara Corridor* tumeanza kuingiza *Seamen* sasa katika mradi wa Mchuchuma. Kwa hiyo, naelewa tutaendelea na miradi mingine. Cha msingi kwetu sasa tunapoingia katika *heavy industries* tuweke sawasawa *mind set* na ku-*change attitude* kwamba tunatakiwa kujenga viwanda hivyo ili kukaribisha wawekezaji wengine popote pale ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza bila kufikiria kwamba tunauza nchi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... ... ... ... ... ... ...202,821,900/=
Kifungu 1003 - *Policy Information Development*... ... ... ... ...386,728,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Macro Economy*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 425,028,900/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipochangia kwa maandishi nilieleza kuwa pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara ya Mipango, Taifa hili linahitaji kupata taarifa kamili kuhusu rasilimali katika kila maeneo ambazo zinaweza kuendelezwa. Hii nilisema kuwa itasaidia kama tutajua rasilimali zipo wapi na zinawezekana kuzalishwa kwa gharama gani na hii itasaidia pia kuelekeza miundombinu ya msingi katika maeneo hayo kusudi kuwaelekeza hawa wawekezaji na wananchi katika kuzalisha rasilimali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliulizia kuwa, je, kama kweli tuna mipango mizuri ambayo inaweza kutufikisha mbali baada ya Taifa hili kutikiswa na njaa mwaka jana na juzi, je, Wizara ya Mipango ina mipango gani kukabiliana na tatizo hili kama litatokea tena? Kwa kuwa suala la njaa lilijitokeza katika Taifa hili, huenda ni suala ambalo lilisababishwa na kutokuwa na mipango mizuri. Tuna uwezo wa kuzalisha chakula cha kutosha na kukigawa kwa kila mwananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nikasema kuwa Mheshimiwa Waziri ameongelea vizuri sana kuwa kuongeza thamani ya mazao yetu tunayopeleka nje lazima usindikaji wa mazao ukazaniwe. Sasa swali ni kuwa kama mazao haya yanazalishwa Vijijini, itakuwa

bora zaidi yasindikwe huko huko Vijijini, je, yatasindikwaje kama hatutaweza kupeleka umeme kule ili waweza kusindika? Kwa maana hiyo mpaka yapelekwe Dar es Salaam, Mwanza au Dodoma, itakuwa kilometa ngapi kuleta haya mazao ghafi kutoka Vijijini kwenda kusindikwa?

Naomba maelezo kamili kama tutaweza kusindika mazao yetu pasipokuwa na miundombinu ya kutosha kama barabara mahali yanapozalishwa mazao hayo, umeme na pia kusaidia kuongeza uzalishaji kwa kuchimba mabwawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu au kutoa maelezo ya hoja ya Mheshimiwa Leonard Shango kama ifuatavyo:-

Nakubali kweli alichangia kwa maandish,i lakini kwa sababu ya *constraint* ya muda labda hatukuweza kumjibu, lakini nakubaliana naye kwamba ni lazima tuwe na ramani ya maliasili yetu tuliyonayo ili tujue wapi tunaweza kuwekeza nini na wapi tunaweza kufanya nini. Ndio maana sasa hivi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ikishirikiana na Mikoa mbalimbali tunaanza kutengeneza *regional economic profiles* ambazo zinatuonyesha *investment opportunities,* rasilimali zilizopo katika maeneo kadhaa. Kwa hiyo, hilo tunakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la njaa, Wizara ya Mipango itafanya nini ili kuzuia njaa? Tunachofanya ni kuzidi kuisisitiza Wizara ya Kilimo na Chakula, maagizo tuliyotoa ya kipaumbele katika kuendeleza chakula yaliyopitishwa na Bunge hili, sisi kama Serikali tusimamie na wananchi wenyewe kwa ujumla wao wafanye kazi kwa bidii walime, wapate chakula ili tusitegemee kulishwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho aliloulizia, nadhani lilikuwa la itakuwaje tusindike Vijijini wakati umeme hakuna. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekwishatoa taarifa kwamba inaanzisha Mfuko wa *Rural Energy Fund* na Mfuko huu uta-*focus* zaidi kupeleka umeme katika maeneo ya Vijijini. Mimi nina hakika kwa Mheshimiwa Leonard Shango, umeme upo tayari kwa sababu tulisaidiana sana kuzungumzia mradi wake wa umwagiliaji wa Wembere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Leonard Shango, anipe fedha, vihela vyenyewe vidogo, ili nikafanye hiyo kazi. Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *External Sector*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... … … 291,359,200/=
Kifungu 3001 - *Social Services and Human Resources Development*…260,663,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Public Investment Planning* ... ... ... ... ... ... 203,784,400/=

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme 50, subvote 5001, Public Investment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwa sababu niko kwenye Kamati ya Biashara na Uwekezaji, katika zoezi zima la ubinafsishaji tumeona kwamba viwanda vingi wameuziwa *indigenous* au wenyeji, wazawa na viwanda hivyo kwa muda mrefu vimekuwa vinatelekezwa. Tunapotaka kuzungumzia masuala ya kujenga uchumi ulio kweli hivi ni kweli tunaweza kufanya mambo kama haya na tukategemea uchumi wetu utakua? Ningeomba kidogo Mheshimiwa Waziri anifafanulie hilo jambo. Nashukuru sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwa hoja aliyotoa Mheshimiwa Omar Chubi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya viwanda tulivyovibinafsisha kwa wananchi wa Tanzania bado havijaanza kufanya kazi. Suala hili aliliuliza vizuri sana Mheshimiwa Bernard Membe na lilijibiwa hapa hapa Bungeni. Tuna matatizo kwanza ya madeni makubwa katika viwanda hivyo, tuna matatizo ya ukosefu wa mitaji kwa waliochukua viwanda hivyo, kuna matatizo ya kupitwa na wakati kwa teknolojia ambapo inahitaji kubadilishwa kwa gharama kubwa sana ikilinganishwa na uwezo wa kifedha wa wawekezaji hao na vile vile kuna madeni makubwa ambayo yapo katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo Serikali inachukua hatua mbalimbali kuona kwamba inatoa vivutio kwa wawekezaji wananchi hawa wa Kitanzania ili kuweza kuvianzisha viwanda hivyo. Natoa mfano mara nyingi hapa, kuna wawekezaji wengine wanachukua maeneo makubwa, tunawashauri wapunguze. Kuna wawekezaji wengine wanachukua viwanda vingi, tunawashauri wapunguze vingine.

Kwa hiyo, tunaendelea na nina hakika kwamba baada ya muda hata Watanzania wataendelea vizuri kuendesha viwanda hivi. Lakini tukumbuke pia kumiliki viwanda kwa Watanzania ni utamaduni mpya, sio utamaduni ambao tumeuzoea, kwa hiyo lazima matatizo haya tupambane nayo hapa mwanzoni, lakini mwishoni tutaendelea vizuri.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu baadhi ya wawekezaji waliokuja Tanzania waliwezeshwa na Serikali ili wafanye kazi kwa ufanisi mkubwa. Sasa je, hawa wawekezaji ambao tunawajua wamekwama hamwezi kuwapiga jeki ili haya mambo yaende kwa sababu viwanda sasa hivi vinaoza na mitambo inaoza, sasa hiyo itakuwakuwaje kwa hilo jambo?

**MWENYEKITI:** Unaweza kufafanua waliwezeshwaje hao waliokuja?

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waliwezeshwa, kwa mfano, *NetGroup Solutions* waliwezeshwa kwa kupewa fedha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kwa mfano, mimi shirika langu linakufa, lakini *TANESCO* ambao walikuwa taabani walipewa pesa na wakabadilisha *management* kidogo, sasa hivi ndio wanafanya kazi asilimia tisini na kitu. Sasa hawa wawekezaji ambao mlitiliana saini Mikataba na sasa hivi wamekwama, si muwafanyie mpango ili mambo yaende kwa sababu mitambo inaoza? Hilo mimi ndilo nilitaka Mheshimiwa Waziri anisaidie. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Omar Chubi, kama ifuatavyo:-

Kwanza tumshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa kuzindua Sera ya Uwezeshaji hapa hapa Bungeni ambayo ilituhusisha sisi wote. Katika sera hii moja ya maeneo ni kwa wawekezaji wa Kitanzania ku-*access banking facilities,* kuandika *feasibility studies,* kuwafutia baadhi ya madeni ili kuendeleza entities zile za kujenga uchumi ili uchumi wetu ukue, tusiache viwanda hivi vinazorota na kuoza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5002 - *Growth Strategies* ... ... ... ... ... .. .. .. .. .. .. … …325,962,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ...9,467,237,800/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... ... ... ... ... ... 344,000,000/=
Kifungu 2001 - *Macro Economy* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 10,000,000/=
Kifungu 3001 - *Social Services and Human Resources Dev.* ..276,530,000/=
Kifungu 5001 - *Public Investment Planning*... ... ... ... ... ... ...35,000,000/=
Kifungu 5002 - *Growth Strategies*... ... ... ... ... ... ... ... ... 4,565,530,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi tutakwenda kwenye Wizara ya Fedha.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... 4,694,350,600/=

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Benedict Losurutia, alipokuwa anauliza...

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu kifungu gani?

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Benedict Losurutia, aliposimama kuomba utaratibu wa leo utakuwa namna gani ni kwa sababu ya suala la muda kwa sababu Wizara zipo mbili, je, Wizara ya Fedha nayo itapata muda wa kutosha ili Wabunge waweze kuulizia maswali?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sijui tufanyeje kwa sababu sisi hapa kiutawala tulijipangia nusu kwa nusu, dakika 45 Mipango na 45 Wizara ya Fedha. Lakini mtu akishasimama huwezi kumzuia, hiyo moja.

Lakini la pili, tunazo dakika karibu hamsini kumaliza, kwa hiyo, tunadhani inatosha ni kama tulivyofanya kwa Wizara nyingine tulikuwa na muda kama huo, kwa hiyo, unatosha kabisa. Sasa kwa sababu wamesimama wengi na kanuni zipo tutaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sikutaka kufika kote huko lakini naona nimelazimika. Kuna Kanuni humu mkitaka leo tukeshe tunaweza kukesha, tunaweza kuongeza dakika thelathini. Sasa hilo huna haja hata ya kuliuliza. Lakini tunaendelea tuone tutafikia hatua gani. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 50, programme* ya 10, *subvote 1001,* Kasma 250100. Naomba nipate maelezo tu. Wakati nilipochangia hapa kwa kuzungumza nilibaini matatizo mawili ambayo niliomba Waziri ama Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, katika hatua ile ya kufuta kodi za kero ambazo wananchi na Wabunge tunashukuru kwa Serikali kufanya hivyo, kumejitokeza upungufu mkubwa katika mapato ya Halmashauri. Lakini sambamba na kuondoa hizo kodi za kero, Serikali iliahidi kwamba itatoa fidia halisi ili Halmashauri zetu ziweze kufanya kazi zake.

Sasa mimi katika mchango wangu nilitoa mfano wa Wilaya ya Kondoa kwamba, sisi hatujafidiwa fidia halisi. Kwa hiyo, tuna matatizo makubwa ya kuendesha Halmashauri na nikasema kwamba kwa wastani tulitakiwa tufidiwe shilingi milioni 343.4, lakini sasa tunafidiwa shilingi milioni 264. Tunapunjwa karibu shilingi milioni 80 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja athari za mapunjo hayo kwamba vikao vya kisheria sasa hivi havikai, watumishi hawalipwi, miradi haitekelezwi. Sasa sijapata jibu, naomba kama sitapata jibu hapa basi waende wakafanyie kazi, inawezekana Halmashauri nyingine wanapata fidia halisi, sisi kwa kweli Kondoa tunaathirika vibaya sana, tunaomba mtusaidie.

Naomba jibu kama mtasaidia ili nikitoka hapa nifuatilie ili tuweze kupata hiyo fidia na tuweze kuwahudumia wananchi wetu. Naomba pia kwa sababu mwaka 2003 tulipata upungufu wa shilingi milioni 80 na tuna madeni, tunaomba hiyo shilingi milioni 80 tufidiwe ili tuweze kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pia nilizungumzia juu ya programu inayoitwa *Local Government Support Programme* ambayo imebuniwa na Serikali, lakini vigezo ambavyo vimetolewa ili Halmashauri iweze kupata pesa hiyo ni vigumu kweli kweli kiasi ambacho kwamba sasa hivi Halmashauri 47 tu ndizo zimeweza kufikia vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukifanya hivi ni kwamba kuna Halmashauri nafikiri zaidi ya 77 ama kwenye sabini na kitu hivi hawapati kabisa pesa hizo. Pesa hizo ni nyingi kidogo ni shilingi bilioni 12.4, sasa tusipopata maana yake ni kwamba tunaathirika. Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ni mojawapo na tatizo ni nini ama vigezo ni nini?

Kwanza unatakiwa uwe na Mkurugenzi na vigezo mbalimbali ambavyo nimekwishaorodhesha. Mimi ombi langu ni kwamba kama tulitereza katika kuweka mkataba twende tukarejee huo mkataba ili kila Halmashauri iweze kupata hiyo *support.* Mimi naomba majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilijaribu kumjibu Mheshimiwa Paschal Degera, hili la kwanza la kupunjwa kwa Halmashauri na jibu ambalo ni la kila Wilaya ni kwamba Wizara ya Fedha baada ya ule uamuzi wa kufuta kodi za kero ilishirikiana na Wizara ya TAMISEMI kubaini tofauti kwa kila Halmashauri iliyojitokeza juu ya uamuzi huo.

Vilevile tulikubaliana juu ya utaratibu wa kutumika kwa kila Halmashauri kwa sababu zote ziliathirika. Sasa ni kweli katika picha ya mwisho kuna Halmashauri ambazo ziliona sawa, kuna Halmashauri ambazo ziliona zimepunjwa sana. Mojawapo ni Halmashauri ya Rombo na mimi kama Mbunge kule nina matatizo hayo hayo ya Mheshimiwa Paschal Degera. Kwa hiyo, zile Halmashauri ambazo zimetuandikia kama Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Halmashauri ya Masasi kadhaa kadhaa za namna ile

tumezichukua barua hizo na kuona kiini cha malalamiko yao kama labda ni hesabu zimefanywa vibaya au nini. Lakini kama hesabu hazikufanywa vibaya hatuwezi kuziongezea Halmashauri ambazo zinadai zimepunjwa bila kuleta ushahidi wa namna zilivyopunjwa. Kwa sababu tutakuwa tena tumeleta tofauti ya mapato kati ya Halmashauri na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jibu langu mimi ni kwamba kama Halmashauri ya Kondoa ina matatizo hayo ni juu yao kupeleka barua waeleze matatizo hayo yako namna gani na barua yao itachambuliwa pamoja na barua za Halmashauri nyingine kama Rombo na kadhalika kama nilivyoeleza hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naona Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kuhusu *Local Government Support Programme.* Ni kweli Halmashauri za Wilaya na Miji zimegawanyika katika mafungu. Kuna fungu la Halmashauri 47 hizi ndizo zile ambazo zimetimiza vigezo vyote. Fungu la pili ni Halmashauri ambazo zinapata misaada kutoka kwa Wahisani. Kuna baadhi ya Wahisani wanasaidia Halmashauri hao wako kwenye kundi lingine isingewezekana na wao wapewe fedha hizi hizi tena na wengine wakati hawajapata na kundi la tatu ni zile Halmashauri ambazo zimepata hati chafu, zina matatizo, hizo zimewekewa utaratibu maalum nazo zitasaidiwa ili ziweze kuingia katika vigezo hivyo.

Kwa hiyo, siyo kweli kwamba hizi fedha za *Local Government Support Programme* zimetolewa kwa ajili ya hizi Halmashauri 47 tu kama Mheshimiwa Mbunge ana matatizo au hajanielewa basi anaweza kuja kuniona kesho nitampa maelezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwingine ambaye angependa kuhoji. Ningependa tu kumwambia kwamba kwa leo naomba mnivumilie sana. Mtu awe *specific* ili tuweze kumaliza. Lakini mifano na labda, naomba hiyo mngeipunguza sana. Kuwe na *specific question* ya kutaka kupata ufafanuzi ili tuendelee. Sasa Mheshimiwa George Lubeleje. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho mshahara wa Waziri. Wilaya ya Mpwapwa ni Wilaya ya zamani sana, lakini hakuna jengo la *TRA*. Niliwahi kuuliza swali hapa Bungeni kwamba je, Serikali itajenga lini jengo la *TRA* katika Wilaya ya Mpwapwa na Serikali ilinipa matumaini. Sasa swali langu ni kwamba je, mwaka huu wametenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida ya utendaji ni vigumu sana Waziri wa Fedha kujua jengo lipi limejengwa wapi kwenye Shirika lake moja. Lakini ninachoweza kusema ni kwamba kuna Mpango wa miaka mitano ijayo wa kuboresha miundombinu ya *TRA* na kwa kuanzia tumeanza na majengo

kwenye Mikoa ya mipakani ili kuleta heshima kidogo huko mipakani kuwa na majengo mazuri.

Baada ya hapo tutaelekea Mikaoni hadi Wilayani kule ambako kuna majengo yasiyofaa au hakuna jengo kabisa, kwa hiyo, tutakwenda kwa umuhimu wake. Inawezekana katika utaratibu huo Wilaya ya Mpwapwa ikawepo. Lakini mimi naogopa sana kuanza kuwambia sasa kwa sababu Mbunge amesema anzeni Mpwapwa muache Kibondo, itakuwa naingilia kati mambo ya Bodi. Mimi nitaiarifu Bodi kwamba kuna kilio kutoka Mpwapwa sitaki kuahidi, lakini naahidi kuiarifu Bodi kwamba kuna kilio kutoka Mpwapwa. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme 10 Subvote 1001.* Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala la kero kubwa ambayo wananchi wa Mkoa wa Kagera na Kanda ya Ziwa kwa ujumla tunayoipata kutokana na kupanda kwa bei ya petroli kutokana na umbali wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri kabisa wakati ana-*wind up.* Amezungumza kwamba ameleta mitambo ya *flow meter 14* ambayo naamini itaziba mianya mingi ya wakwepa kodi na nampongeza kwa hilo. Sasa jibu linaloliomba tu fupi. Ni kwamba anieleze iwapo kati ya hizo *flow meter 14* kuna mpango wa kutenga baadhi ya *flow meter* hizo zikafungwa Bukoba, Mwanza, Musoma kama maeneo mojawapo ambayo huwa yanapokea mafuta kutokea Kisumu ambayo bei yake huwa ni nafuu kuliko hivi sasa mafuta yanayotoka Dar es Salaam na kama anavyofahamu mafuta yakishapanda na tukiwa na chanzo kimoja cha kutokea Dar es Salaam, matokeo yake ndiyo bei ya petroli ni shilingi 1,200/= na bei ya mfuko wa *cement* ni shilingi 15,000/=. Sasa kama tutafungiwa *flow meter* pale Bukoba mimi naamini bei inaweza ikawa ya chini na bidhaa zikawa na bei ya chini. Ni hilo tu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi tu kumweleza Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kwamba tukiwa hapa hapa Dodoma chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu tumezungumza suala hilo na mengineyo yanayoendana nalo. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amepewa kazi ya kuleta mapendekezo haraka Serikalini ili tuweze kuliamua kwa ujumla, kwa sababu kuna Mikoa inayozunguka Ziwa Victoria, kuna Mikoa ya Kusini Mtwara, kuna Tanga, kuna njia za barabara, Horohoro, Holili, Tarakea, Namanga na kadhalika na kadhalika ili tuweze kuamua kwa ujumla wake kumalizia maeneo ambayo hayajashughulikiwa. Vile vile tuwe tumepata uzoefu kwa sababu kama *flometer* hii itafanikiwa kwa kiasi gani pia hatujajua. Kwa hiyo, yote hayo tutayachukua kwa pamoja ili tuweze kuamua ndani ya Serikali.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi niko kwa *Vote 50* kwenye *Basic Salaries Pensionable Posts* pale pale. Nataka nipate ufafanuzi tu kuhusu *VAT* inayolipwa na wananchi wanaojenga shule kwa nguvu zao. Wanaojenga shule hao ni vijiji ambavyo vimeandikishwa na Serikali ya Vijiji, wanajenga shule za msingi ama shule za sekondari. Wanapomaliza kujenga hiyo mali kwa kweli ni ya kijiji lakini iko *Local Government.* Kwa hiyo, wanasaidia Serikali siyo mali ya *NGO*

ama ya mtu binafsi. Hawa watu ni wawekezaji ama siyo wawekezaji hawa wanaojenga hizo shule. Maana ukichukua mfano wanaowekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge imeishaeleweka, sasa mifano naomba uipunguze.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Pili, kama wao ni wawekezaji, je, kwa nini wasipewe angalau *certificate* kuonyesha kwamba wao ni *investors* na watafanya vitu vyao bila kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema utekelezaji wake ni mgumu utakuwaje mgumu ambapo vile ni vijiji vya Serikali vimeandikishwa na vinatambulika Kiserikali kama vile wawekezaji wanatambulika. Kwa nini wao wasipewe *exemption by simply gazette.* Unawa-*gazette* tu hawa wanajenga shule unaiona. *Twenty percent off* ama asilimia 20 wanazokatwa waweze angalau kuongeza juhudi yao ya kujenga shule zao. Kwa nini iwe ngumu? *(Makofi)*

La tatu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kusema analifikiria suala la *windmills* kwamba anatoa *exemption* kwenye Muswada unaokuja kesho sijauona *details* zake. Nataka anihakikishie na wananchi wangu kule wananisikiliza wanataka kujua je, *windmill* yao ya Rwamisanga italipa kodi ama haitalipa kodi? Je, *windmill* ya Kasoma italipa kodi ama haitalipa kodi? Je, wao ni wawekezaji ama la?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la mwisho nafikiri ni heshima zaidi kwa Bunge kuniagiza kesho. Mimi naleta tu pendekezo kesho Bunge linaweza likakataa. Mimi nikitanguliza kimbelembele kusema ndiyo na Bunge likanikatalia kesho nitapata matatizo hapa.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Nimrod Mkono, kesho aungane na Waheshimiwa Wabunge kupiga kura ya ndiyo ili niweze kutekeleza mara moja. Lakini mimi nitalileta hilo pendekezo na linahusiana na kilimo, lakini pia ni mtambo si *windmill* ni mtambo kwa ajili ya maji na yote hii imekuwa ikisamehewa ushuru. *Customs duty.*

La pili, kuhusiana na *VAT,* narudia hili kwa Waheshimiwa Wabunge ni vizuri mlifahamu kwa sababu naelewa kwamba, Waheshimiwa Wabunge wengi wana Taasisi zao zisizo za Kiserikali kwenye Majimbo yao zinazojenga shule na mambo mbalimbali ya namna ile. Nichukue mfano wa *Chunya Development Trust* wanataka kujenga shule ya wananchi, maana yake wao wanawajengea wananchi siyo zao ni za wananchi wakishirikiana na wananchi. *CHUDET* kwa niaba ya wananchi wa eneo lile inaweza kuomba msamaha wa *VAT* kwa shule maalum siyo ya kijumla kwa kusema tunajenga shule kwenye kijiji fulani labda Kanga na mabati yote tunaomba tusamehewa *VAT* au *cement* yote au nini au vitu vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha anaweza akasemehe kwa kupitia hiyo *CHUDET* kwa sababu gani? Kwa sababu naweza nikaikagua *CHUDET* lakini mkisema tu wanakijiji wote wa Kanga wasamehewe kodi kwa sababu wanajenga shule

nani mwanakijiji wa Kanga hasa na yule Mwenyekiti wa kijiji anaweza akadhibiti namna gani na akanihakikisha kwamba ana utaratibu wa kuthibitisha kwamba mabati 100 yalikwenda kwenye shule ile na hayakwenda kwenye shule na vitu vingine.

Kwa hiyo, ili kudhibiti pande zote mbili Serikali isipoteze mapato mengi mno na wananchi waweze kujenga shule zao ambalo ndiyo lengo lao basi tunaweka utaratibu huo wa kutumia vyombo visivyo vya Kiserikali katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili lingine la kutoa *certificate* sheria ile ya kutoa *certificate* haipo mkononi mwangu, lakini nina hakika Waziri wa *Tanzania Investment Centre (TIC)* amelisikia na nafikiri anaweza akalifanyia kazi na mimi nitashirikiana naye tuone uwezekano huo. Nafikiri itabidi lifanyiwe utafiti kidogo ili tujue mwananchi anapojenga shule anakuwa mwekezaji au anakuwa mwana maendeleo au anakuwa nani hasa na kama ni hivyo, haki ya bwana maendeleo ni ipi, haki ya mwekezaji ni ipi na haki ya mwekezaji wa ndani ni ipi.

Mwekezaji wa ndani sasa hivi anapewa *certificate* ya *TIC* kama anawekeza kwa viwango fulani sheria ndivyo inavyosema siyo chini ya milioni 500. Lakini kama sasa tutateremka tuseme milioni 5 pia anaweza akapewa *certificate* na msamaha wa kodi, ni jambo ambalo itabidi tulifanyie uchunguzi siwezi kulitamka hapa, lakini tutalifanyia uchunguzi.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nataka kupata ufafanuzi kuhusu *component* kama ni za *windmill. Windmill* inapokuja unaifunga kwenye bomba zina nati na vingine vitu mbalimbali. Je,huo Muswada unaokuja kesho sijui utaweka bayana kabisa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nadhani unaelewa tukubaliane alichosema Mheshimiwa Waziri, kesho tuna muda tunaweza kumkatalia au kumkubali kesho. Kwa hiyo, naomba uridhike tu kesho ujiandae. Mheshimiwa Maria Watondoha, alikuwa mwanamke pekee yake kwenye hili.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 50* kifungu 1001. Sitaki kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini naomba kupata ufafanuzi.

Kwa kuwa Serikali ilipobadilisha noti ilitoa matangazo na kusema noti hizi haziwezi kugushiwa. Lakini kwa kuwa hivi sasa noti za bandia ni nyingi. Moja ni hii hapa sisi tuliipata siku ya Mwanamke wa Kitanzania hapa walioingia, noti hii hapa ya bandia na kwa kuwa noti hizi zimezagaa na kila mara zinakamatwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hasa kwa wale wananchi wa vijijini kwamba hapewi noti bandia wakaingia mashakani. Mimi niliipeleka benki hii noti nilinusurika kwa sababu nilisema jamani niliipata mlangoni na siyo mimi walikuwa wanakusanya watu wengine pale. Lakini ingekuwa hivi hivi ningeingizwa ndani nikahojiwa nimeipataje? Je, mwananchi wa kawaida Serikali ina mpango gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama tulivyoeleza hapa katika nyakati tofauti tukijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge noti bandia bado ni tatizo, lakini mtakumbuka kwamba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mwenyewe alipokuwa anajibu swali hapa siku za karibuni alisema jambo hili Polisi wa Watanzania na wa nchi jirani na *Interpol* wanalivalia njuga kujaribu kutambua hivi nani hasa anayetengeneza hizo noti bandia na nani hasa anayezisambaza ndani ya nchi na je, zinatengenezwa ndani ya nchi au nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliwahi kutoa zawadi ya shilingi milioni 5 mwaka 2003 na kwa bahati mbaya hakuna hata mmoja aliyeniletea jina la mtu yeyote anayetengeneza noti bandia. Kwa hiyo, mpango wa kuwakamata upo, fedha za kuwapa watoa habari zipo, lakini bado naendelea kukazana kutafuta watu hao sijawapata. Lakini kama Mheshimiwa Maria Watondoha, ana fununu yoyote hata kama ni uvumi akitusaidia watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wako tayari kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa kwa kuwa noti za bandia zimezagaa na wananchi wa vijijini hawawezi kubaini tofauti na mimi nimeonyesha tu pale Bungeni tofauti, je, hao wananchi kule vijijini hawatapata matatizo wakipatikana na noti bandia hizi?

**MWENYEKITI:** Kwa mfano matatizo ya kushitakiwa.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Ndiyo kushitakiwa, kutiwa hatiani, maana mimi nilikuwa nachunguzwa nikawambia jamani niliipata mlangoni getini pale sijui na kwa sababu ni Mbunge niliachiwa, je, wananchi wa kawaida itakuwaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* ufafanuzi kuhusu hili la kushitakiwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukikamatwa na noti bandia haijali wewe kama ni *Attonery General* au ni Mbunge unaweza ukakamatwa. Lakini kama alivyopata hiyo fursa ya kutotiwa misukosuko mikubwa. Mwananchi ambaye amenunua kitu halafu akapewa chenji ya noti ambayo baadaye inagundulika kwamba ni ya bandia. Yeye atatoa maelezo hayo hayo kama aliyoyatoa Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi wakati napewa hii noti sikuwa nafahamu kweli kabisa kwamba hii ni noti bandia na kwa mazingira ambayo atakuwa ameelezea hiyo, mimi naamini Polisi na hata Mahakama wataliona hilo na kumwachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi ni kama Serikali ilivyosema humu Bungeni tufanye kila linalowezekana sisi wote kama tunawafahamu hao wanaojishughulisha na biashara hii haramu, kweli tujitokeze kuisaidia Serikali na kusema wako wapi. Mheshimiwa Waziri ametoa ile ahadi ya shilingi milioni 5 tulichangamkie.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Lakini kabla sijaanza kueleza niliyotaka kuyasema naomba kuhusu utaratibu kanuni namba 21(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wasemaji bado ni wengi na muda wa kuhairisha Bunge karibu unakaribia, ningeomba tutumie kanuni hii namba 21(4), Bunge liongezwe muda wa dakika 30 ili wasemaji wote waliopangwa waweze kusema na ikifika pale Bunge linaweza kuahirishwa. Naomba kutoa hoja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna hiyo Kanuni ya 21(4), kuna ile ya 81(6) yote haya yanataka kutupa nafasi ya kuongeza muda kama tunahitaji muda. Kwa sababu ameishatoa hoja. Mimi ndiyo nimekaa huku naona waliounga mkono. Kwa hiyo, nyie wenzangu mmeangalia huku hamuwaoni kule. *(Makofi)*

Lakini nataka kusema inatupa tatizo moja kwamba kama kweli mngependa ziongezwe dakika 30 na mimi naona bado dakika 30 ni kama hazitoshi maana leo kulikuwa na Wizara mbili. Lakini maadam mnataka basi Bunge litarudia tutafanya maamuzi hayo tutaongeza tena dakika 30. Halafu tuendelee.

Turudi kwenye Bunge tuje tena dakika 30. Sasa maadam mna hiari haina tatizo, kwa hiyo, hivi sasa maadam alitoa hoja ya kutaka kuongeza muda basi Bunge litarudia atatoa tena hoja itakuwa *supported,* ikikataliwa basi tutarudi kwenye *guillotine,* tunamaliza katika muda ule ule. Sasa Bunge linarudia. *(Makofi)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Bunge limerudia nampa nafasi Mheshimiwa Lucas Selelii, atoe hoja yake, nihoji sasa hivi.

**HOJA YA KUONGEZA MUDA WA BUNGE**

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa kutumia kanuni namba 21(4) ya kanuni za Bunge. Naomba Bunge lako Tukufu liongeze dakika 30 ya muda usiokuwa wa kawaida ili tuweze kuendelea na Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji. Hoja iliyopo mbele yetu ni kuongeza dakika 30 juu ya ule muda ambao huwa kawaida tunamaliza Bunge. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya kuongeza muda wa dakika 30 wa kukaa Bunge baada ya muda wa kawaida ilikataliwa na Bunge)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kura zihesabiwe. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sawasawa tunakwenda taratibu. Mheshimiwa Lucas Selelii, amesema kura zihesabiwe, haikuungwa mkono na Wabunge kwa kusimama sehemu yao.

Kwa hiyo, tunarudi kwenye Kamati ya Matumizi kuendelea na Kamati itakapofika bado dakika 10 tutaingia kwenye *guillotine* tunamaliza Bunge. Kamati inarudia *(Makofi)*

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Bunge kukataa kuongeza muda, tumebakiwa na dakika tano za mjadala, zinazobaki ni *guillotine.* Sasa namwita Mheshimiwa Lucas Selelii. Haya endelea na hoja yako.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza.

Nimechangia kwa maandishi kuhusu michezo ya kubahatisha, Bunge lako hili lilipitisha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Mheshimiwa Rais alishaitia saini, je, ni kwa nini Serikali haijaanza kutoa fedha kwenye Baraza la Michezo kwa ajili ya ku-*support* timu zetu za mipira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mwaka 2003 katika fedha za mafuta za Waheshimiwa Wabunge ziliwekwa kwa kulingana na bei ya mafuta ya dizeli ambayo ilikuwa shilingi 700/= sasa hivi ni shilingi 1,000/=, je, Serikali ipo tayari ku-*compensate* kufikia shilingi 1,000/= katika hizo fedha ambazo ziliwekwa?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Sheria ya Michezo ya Kubahatisha inataka kila mwaka Wizara ya Fedha irejeshe kwenye Baraza la Michezo fedha zilizotokana na michezo ya mwaka huo, lakini sio kila mchezo. Ni leseni ile ya Kitaifa.

Kwenye michezo hii kama nilivyosema kwenye hotuba mtaona kuna leseni nyingi zimetolewa. Lakini kuna moja tu tumesema imetolewa na hiyo ni ile ya michezo ya Kitaifa. Kwa bahati mbaya michezo ya Kitaifa haijachezwa. Tumaini langu ni kwamba ndani ya miezi miwili ijayo Michezo ya Taifa itaanzwa kuchezwa na kwa hiyo fedha zitapatikana mwaka mmoja baadaye kwa ajili ya Baraza la Michezo.

Hili la mafuta liko kwenye Wizara nyingine, sisi katika Wizara ya Fedha, hatujapata mapendekezo lakini nina hakika Mheshimiwa Daniel Yona, amelisikia na kama kuna hoja ataleta mapendekezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Yona, yupo ajibu?

**WAZIRI WA FEDHA:** Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fedha za ongezeko la *allowance* kwa namna bei ya mafuta ilivyoongezeka. Samahani nimelipata sasa. Hilo naomba nisaidiwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Lucas Selelii ambayo najua yanawagusa Waheshimiwa Wabunge wote. Bahati nzuri wewe ni Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Huduma za Bunge, umelisikia nafikiri wakati muafaka litazungumzwa kwenye Tume yetu. Si jambo ambalo mara nyingi linaamuliwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, litafika kwa Mwenyekiti pia. Huku nimekwenda wawili na sasa nakwenda huku wawili. Bado dakika zangu pale mbili. Dakika moja ya kwako dakika moja ya Waziri. Sawa.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi niliandika lakini sikujibiwa. Lakini naomba niulize moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipata shida sana wakati wa mkopo wa pembejeo. Kwa sababu Benki iliyotajwa hapa ya *EXIM* ni Benki ambayo haina mtandao. Kwa hiyo, haijulikani, ni wakati huo ndio tumeanza kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza hizo fedha zilizoko katika Benki ya *EXIM* haziwezi kutolewa ziende katika Mabenki ambayo tunayafahamu kama *NMB? (Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sifahamu kwa undani sana juu ya suala hili. Lakini ninachojua ni kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula imesaini mkataba na Benki ya *EXIM* ili iweze kutawala ule Mfuko wa Pembejeo. Sasa sielewi masharti ya Mkataba, lakini ninachoelewa katika Serikali hakuna ndoa yoyote kati ya Idara fulani ya Serikali na Benki yoyote, kuna mkataba tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hoja hii ilivyokuja nina hakika Waziri wa Kilimo na Chakula, anaifahamu na anaisikia kwa kufuata mkataba mwenyewe

natumaini ataweza kuona la kufanya na sisi Wizara ya Fedha tunaweza tukamkumbushia kwamba suala hili liangalie kwa utaratibuhuo kama tutakavyoshauriwa zaidi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwa vile sasa tumefika ile *time* ya *guillotine* sasa nitawahoji na utataja fungu zima zima.

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... 4,694,350,600/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... ...4,284,808,500/=
Kifungu 1004 - *Legal Services* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 425,681,400/=
Kifungu 1005 - *Information, Education and Communication* ... .... 300,000,000/=
Kifungu 2001 - *Government Budget* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...70,682,745,300/=
Kifungu 2002 - *Policy and Research*... ... ... ... ... ... ... ... ... ...45,772,171,800/=
Kifungu 2003 - *Treasury Registrar* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...2,741,602,300/=
Kifungu 4001 - *External Finance* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 8,986,554,800/=
Kifungu 5001 - *Stock Verification* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 3,207,973,200/=
Kifungu 5002 - *Central Tender Board* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 2,901,991,300/=
Kifungu 6001 - *Computer Services* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,520,601,200/=
Kifungu 6002 - *Tax Revenue Appeal Board* ... ... ... ... ... ... ... ...245,499,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 - Exchequer and Audit Department**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... 5,143,270,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001- *Public Debt Management*... ... ... ... ... ... ... ... 853,370,000/=
Kifungu 3002 - *Expenditure Management* ... ... ... ... ... ... ... ... 490,140,000/=
Kifungu 3003 - *Financial Management* ... ... ... ... ... ... ... 57,643,389,300/=
Kifungu 3004 - *System and Internal Audit* ... ... ... ... ... ... ... 7,915,460,700/=
Kifungu 3005 - *Sub Treasury Arusha* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 173,496,000/=
Kifungu 3006 - *Sub Treasury Coast* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 172,280,000/=
Kifungu 3007 - *Sub Treasury Dodoma* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 266,216,000/=
Kifungu 3008 - *Sub Treasury Iringa* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 194,636,000/=
Kifungu 3009 - *Sub Treasury Kagera* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 211,478,000/=
Kifungu 3010 - *Sub Treasury Kigoma* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 205,000,000/=
Kifungu 3011 - *Sub Treasury Kilimanjaro* ... ... ... ... ... ... ... ... 194,310,000/=
Kifungu 3012 - *Sub Treasury Lindi* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 190,796,000/=

Kifungu 3013 - *Sub Treasury Mara* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 214,096,000/=
Kifungu 3014 - *Sub Treasury Mbeya* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...236,000,000/=
Kifungu 3015 - *Sub Treasury Morogoro* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 246,806,000/=
Kifungu 3016 - *Sub Treasury Mtwara* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 189,726,000/=
Kifungu 3017 - *Sub Treasury Mwanza* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 204,646,000/=
Kifungu 3018 - *Sub Treasury Rukwa* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...216,916,000/=
Kifungu 3019 - *Sub Treasury Ruvuma* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 183,366,000/=
Kifungu 3020 - *Sub Treasury Shinyanga* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 229,166,000/=
Kifungu 3021 - *Sub Treasury Singida* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 208,916,000/=
Kifungu 3022 - *Sub Treasury Tabora*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...181,341,000/=
Kifungu 3023 - *Sub Treasury Tanga* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...221,536,000/=
Kifungu 3024 - *Sub Treasury Manyara*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 193,556,000/=
Kifungu 7001 -*Pension and Gratuity*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...246,106,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 22 - Deni la Taifa**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... 477,011,533,500/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... 1,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... ... ... ... ... ... ... ...650,000,000/=

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, anataka kufafanua hilo fungu.

**WABUNGE FULANI:** Hapana!!!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tuelewane hapo kwa sababu yeye ndiyo anaomba fedha na kama tukipitisha zile ambazo hakuomba si sahihi. Kwa hiyo, anataka *clarify* fungu hili ili tupitishe kwa ujumla.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 1001, *sub vote 1002 Finance and Accounts* ukurasa 64 kifungu kidogo 6206 kuna masahihisho kwamba, naomba nifanye masahihisho kwenye jinsi ilivyoandikwa. Pale imeandikwa *construction of IAA, Modern Library* na *Project* ikaishia pale.

Ukweli tunachotaka kuweka pale ni *construction of IAA* kama ilivyo, *TIA* hiyo ni mpya na *IFM. TIA* maana yake ni kile Chuo cha Uhasibu cha Kurasini na *IFM* tunaifahamu. *Vote* ile ambayo jumla ni shilingi 650,000,000/=. Fedha zile zimegawanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 200,000,000/= kwa *IAA,* shilingi 200,000,000/= kwa *IFM* na shilingi 250,000,000/= kwa *TIA.* Kwa hiyo, baada ya masahihisho hayo kwa hiyo, yale maneno *Modern Library* na *Project* yatafutika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu 2001 - *Government Budget* ... ..... ... ... ... ... ... ... ... ... 823,000,000/=
Kifungu 2002 - *Policy and Research*... ... ... ... ... ... ... ... ... 11,733,938,000/=
Kifungu 4001 - *External Finance*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 2,313,882,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 - Mkaguzi Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... ...1,617,904,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3003 - *Financial Management*... ... ... ... ... ... ... ... 11,299,849,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko.

Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2004/2005, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko madogo niliyofanya mwenyewe.

Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 5 Agosti, 2004 saa tatu asubuhi)*